

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA SABA

Kikao cha Kumi na Mbili – Tarehe 25 Aprili, 2017

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Mwenyekiti (Mhe. Andrew J. Chenge) Alisoma Dua

MWENYEKITI: Waheshimiwa tukae. Tunaendelea na shughuli zetu Mkutano wa Saba, Kikao cha Kumi na Mbili.

Katibu!

NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI.

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:

Hotuba ya bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

MHE. JORAM I. HONGOLI (k.n.y MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA):

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka wa fedha 2016/2017 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2017/18.

MHE. SUBIRA K. MGALU (k.n.y MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI):

Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Bajeti kuhusu Maoni ya Kamati hiyo juu ya Utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Mahakama kwa mwaka wa fedha 2016/2017 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

MHE. ABDALLAH A. MTOLEA (k.n.y MSEMADI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA):

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Katiba na Sheria juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria mwaka wa fedha 2017/2018.

MWENYEKITI: Ahsante, tunaendelea.

Katibu!

NDG. ZAINAB ISSA - KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

MWENYEKITI: Maswali na swali letu la kwanza, swali namba 95 linaulizwa na Mbunge wa Biharamulo Magharibi, Mheshimiwa Oscar Rwegasira Mukasa na linalekezwa Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

Na.95

Kuwawezesha Waendesha Bodaboda

MHE.OSCAR R. MUKASA aliuliza:-

Ibara ya 57(b) ya llani ya CCM inaahidi kuweka mfumo wa kuvitambua, kuvisajili na kuviwezesha vikundi vyote vyenye mwelekeo wa ushirika na ujasiriamali nchini. Kwa kuwa kundi la waendeshaji wa vyombo vya usafiri wa abiria maarufu kama bodaboda ni kundi la kijasiriamali, na inawezekana ndilo kundi lenye mwelekeo na fursa za kiushirika ambalo ni kubwa zaidi Wilayani Biharamulo na nchini kote kwa sasa.

Je, Serikali ina mpango gani mahususi juu ya kundi hilli?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Oscar Rwegasira Mukasa, Mbunge wa Biharamulo Magharibi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha Ibara ya 57(b) ya llani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015 inatekelezwa kikamilifu kuhusu uwezeshaji, Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo imeweza kuvitambua na kuvisajili jumla ya vikundi 1,940 vya wajasiriamali vikiwemo vikundi 34 vya vijana waendesha bodaboda. Aidha, waendesha bodaboda 2,000 wametambuliwa kwa jitihada kubwa za Mheshimiwa Mbunge kwa kushirikiana na Halmashauri na wakawekewa utaratibu wa utoaji huduma ya usafiri wa pikipiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi Wilaya ya Biharamulo imewezesha jumla ya waendesha bodaboda 410 kupata

mafunzo ya uendeshaji wa pikipiki na kupata leseni za kuendesha na kufanya biashara hiyo.

Natoa wito kwa Wakurugenzi wote wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhamasisha waendesha bodaboda wajunge kwenye vikundi na *SACCOS* ili watambulike kisheria na kupata fursa ya mikopo inayotolewa kuitia asilimia 10 ya vijana na wanawake pamoja na Baraza la Taifa la Uwezesaji Kiuchumi.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Mukasa.

MHE. OSCAR R. MUKASA: Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante, nakushukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, kwa mujibu wa takwimu tulizopewa kwenye majibu na Mheshimiwa Waziri, asilimia 80 ya waendesha bodaboda hawana leseni, jambo ambalo linawafanya waishi kwenye mzunguko wa kukimbizana na polisi badala ya kuzalisha mali kwa ajili kujenga uchumi wao na uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kumuuliza Mheshimiwa Waziri, je, Serikali iko tayari kuwasaidia kwa kuwawekea ruzuku ya kupunguza walau kwa mara moja kodi ya kulipia leseni angalau kwa nusu ili waweze kupata leseni kama hatua ya kwanza ya kuwasaidia ili tuweze kushirikiana nao kuongelea habari ya kuwahamisha kuapeleka kwenye ushirika wa *SACCOS* na mambo mengine?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili; Mheshimiwa Waziri yuko tayari kuambatana na mimi twende Biharamulo kuziona fursa nyingine zaidi ya kuwaomba tu wajunge kwenye *SACCOS* ambazo Serikali Kuu ikishirikiana na sisi tunaweza kuzumia kuwatoa kwenye yale waliyonayo ili Biharamulo iwe mfano wa kusambaza hatua kama hiyo maeneo mengine ili kundi kubwa la bodaboda nchini tulisaide liwe la ujasiriamali kweli kweli? Ahsante.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZAA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya Mheshimiwa Mbunge kama ikiwezekana Serikali ifanye uwezeshaji, naomba nikiri wazi kwamba hatuvezi kusema kama Serikali tufanye uwezeshaji kwa watu wote, lakini tunakuwa na mikakati mbalimbali ya kufanya uwezeshaji. Mimi niwapongeze Wabunge wengi humu ndani ambao wamefanya *initiatives* katika Majimbo yao kuhakikisha vikundi mbalimbali vinahamasishwa na wao wanasaidia *ku-chip in* humo kwa ajili ya kuwasaidia vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo mimi ninajua wazi kwamba kuna baadhi ya Halmashauri nyingine zina mipango mbalimbali yenye lengo la kuwasidia hawa vijana ili hatimaye, kama ulivyofanya Mheshimiwa Mbunge katika Jimbo lako ambapo na sisi tume-*recognise* shughuli na juhudii kubwa unazofanya katika Jimbo lako, nadhani tukifanya uhamasishaji sisi wengine tutafanya kwa kuangalia fursa zilizopo katika maeneo yetu na hivyo tutaweza kuwasaidia hao vijana kwasababu lengo letu ni kwamba vijana waweze kukomboka katika jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kikubwa zaidi kama hatufahamu; bahati nzuri Ofisi ya Mama Jenista Mhagama katika Baraza la Taifa la Uwezeshaji, hata jana nadhani walikuwa wanafunga mafunzo yao, wameona kwamba jinsi vijana wengi wanavyokosa fursa hizi kwa kutokuwa na ufahamu wa kutosha na ndiyo maana wamesema sasa hivi wanataka kuzifanya programu zao kupitia maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sehemu ya pili naomba nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba mimi nipo radhi, nilifika Biharamulo mara ya kwanza, lakini kama kuna jambo lingine mahususi tutakwenda tena ili kuwasaidia vijana wetu waweze kufika mbele katika suala zima la maendeleo.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa

Mwenyekiti, kwanza naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Jafo kwa majibu yake mazuri kwenye swali hili la msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge ametaka kuiuliza Serikali ni kwa kiasi gani inaweza ikajipanga kupeleka juhudzi za ziada ili kuhakikisha kwamba vijana wa Tanzania, hasa vijana wa kule Biharamulo wanaweza kufaidika na mikopo mbalimbali na kuweza kuwaboreshea shughuli za ujasiriamali wakiwemo vijana wa bodaboda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikuhakikishie kwamba, Mheshimiwa Mbunge ni kati ya Wabunge amba walihudhuria maonyesho ya mifuko ya uwezeshaji wananchi kiuchumi, na tumeshakubaliana na Mheshimia Mbunge kwamba baada ya shughuli hizi za Bunge kukamilika, Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na timu ya Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi pamoja na yeye Mheshimiwa Mbunge watakuwa na ziara maalum kule Biharamulo ili kuangalia Serikali inaweza ikafanya nini kwa ajili ya maendeleo ya vijana na sekta nydingine.

Nitoe wito kwa Waheshimiwa Wabunge wote, tumefunga maonesho ya mifuko ya uwezeshaji wananchi kiuchumi, tunaomba sana tuendelee kuwasiliana ili fursa zilizopo ndani ya Serikali ziweze kuwafikia Watanzania wengi hasa wakipato cha chini na kipato cha kati wakiwemo vijana na kuweza kuwainua kiuchumi. Nakushukuru.

MWENYEKITI: Ahsante, Waheshimiwa tunaendelea, swali letu linalofuata, swali namba 92 linaulizwa na Mheshimiwa Ezekiel Magolyo Maige Mbunge wa Msalala.

Na. 96

Mradi wa Maji Kutoka Ziwa Victoria Hadi Kahama

MHE. EZEKIEL M. MAIGE aliuliza:-

Mwaka 2014/2015 Serikali iliahidi kuongeza usambazaji maji katika viji 100 vilivyoko umbali wa kilometra 12 kutoka

bomba kuu la Ziwa Victoria hadi Kahama na Shinyanga. Serikali ilitenga na Bunge kuitisha shilingi bilioni nne ili kutekeleza mradi huo.

(a) Je, ni vijiji vingapi vimeshapatiwa maji katika hivyo vijiji 100 hadi sasa?

(b) Je, Serikali inafikisha lini maji ya Ziwa Victoria katika vijiji vya Mwakuzuka, Mwaningi, Kabondo, Ntundu, Busangi, Buchambaga, Nyamigege, Gula, Izuga, Buluma, Matinje na Bubungu?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ezekiel Magolyo Maige, Mbunge wa Msalala, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa kuunganisha vijiji vilivyopo umbali wa kilometra 12 kutoka bomba kuu la Ziwa Victoria hadi Kahama na Shinyanga unatekelezwa chini ya programu ya maendeleo ya sekta ya maji. Katika awamu ya kwanza ya utekelezaji vijiji 40 vilainishwa, kati ya hivyo vijiji 32 vimefanyiwa usanifu. Hadi sasa jumla ya vijiji 13 uunganishaji umekamilika na vijiji hivyo ni Nyashimbi, Magobeko, Kakulu na Butegwa, hilo ni Jimbo la Msalala. Ng'homango, Kadoto, Jimondoli, Mwajiji, Ichongo, Lyabusalu na Bukamba hili ni Jimbo la Shinyanga Mjini na Runere na Gatuli hii ni Kwimba; na vijiji viwili vilivyopo Shinyanga Vijijini ambavyo ni Mwakatola na Mwasekagi uunganishaji unaendelea. Hadi sasa kiasi cha shilingi bilioni 1.96 zimetumika kwa ajili ya kuunganisha maji kwa vijiji hivyo kutoka bomba kuu la Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijiji vya Mwakuzuka, Kabondo, Ntundu, Busangi, Nyamigenge na Gula vipo katika mpango wa awamu ya kwanza na usanifu wake umekamilika na ujenzi unatarajiwa kuanza mwaka wa fedha 2017/2018. Aidha, Serikali itaendelea kuunganisha vijiji

vilivyobaki vikiwemo vijiji vya Mwaningi, Buchamba, Izuga, Buluma, Matinje na Bubungu kulingana na upatikanaji wa fedha.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Maige

MHE. EZEKIEL M. MAIGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Pamoja na hayo naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika vijiji hivi ambavyo vimewekwa kwenye kundi la vijiji vilivyoko katika kilometa 12, *infact* viko vijiji vingine ambavyo viko ndani kabisa ya kilometra moja kwa maana kwamba vilisahaulika wakati wa usanifu wa mradi mwanzo hasa vijiji kama Matinje na Izuga. Kwa mfano pale Izuga lile bomba limepita kabisa kwenye uwanja wa shule ya msingi Izuga.

Sasa katika mazingira haya ambapo jibu linasema vitaunganishwa kutegemea upatikanaji wa fedha. Hivi ni sawa katika mazingira hayo ambayo bomba limepita pale pale kijijini halafu wanaendelea kukaa bila kujua? Nilitaka kujua Mheshimiwa Waziri atuambie ni lini hasa vijiji hivi ambavyo bomba limepita pale pale kijijini kama Izuga na Matinje vitafanyiwa angalau mpango wa dharura wa kuunganishwa badala ya kusubiri mpango au lugha ya kwamba fedha zitakapopatikana? Nilitaka kujua lini katika hali ya dharura.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii la pili; katika maeneo haya ambapo bomba kuu la Ziwa Victoria kutoka Mwanza kwenda Kahama na Shinyanga limepita hapakuwepo utaratibu wa kutengeneza mabirika ya kunyweshea mifugo (*water traps*); na mwaka 2014 tulikubaliana kwamba uwepo mpango wa kutengeneza *water traps* kwa ajili ya mifugo. (*Makofii*)

Je, ni lini Serikali sasa itafanya mpango huo ili maeneo haya pia mifugo iweze kupata maji?

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa kifupi tu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, amesema ndani ya kilometra 12 kuna baadhi ya vijiji ambavyo vimesahaulika. Nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba hatutaacha kijiji hata kimoja, tunachotaka ni ushirikiano na Halmashauri husika kama kuna kijiji ambacho kimesahaulika basi tunaomba tipeane taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia umependa kujua ni mpango gani wa haraka, kwa mfano kama kijiji cha Mitinje, kijiji cha Izuga ambacho kina kilometra moja tu kutoka kwenye bomba. Tushirikiane Mheshimiwa Mbunge, Wizara ya Maji na Umwagiliaji kila mwaka inatenga fedha kwa kila Halmashauri. Basi ningeomba Halmashauri husika ijaribu kuangalia uwezekano wa kuunganisha kutokana na fedha tuliyotenga Wizara ya Maji na kama wanaona hawawezi basi wawasiliane na Wizara ili tufanye hiyo kazi haraka kuhakikisha kwamba wananchi wanapata huduma ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kuhusu mabirika. Mimi tu niseme Mheshimiwa Mbunge kwamba haya Mabirika tumepokea hii tutalifanyia kazi ili kuona ni namna gani tunaweza tukatumia maji haya ili kuweza pia kusaidia mifugo ilio karibu na hilo bomba.

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa, tuone wanaotoka ukanda huo, Mheshimiwa Kwandikwa.

MHE. ELIAS J. KWANDIKWA: Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante sana kwa kuniona ili na mimi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mahitaji ya Jimbo la Msalala yanafanana kabisa na mahitaji ya Jimbo la Ushetu, na kwa kuwa maji haya ya Ziwa Victoria yamefikishwa Kahama Mjini na hayajawafikia kabisa wananchi wa Jimbo

la Ushetu, je, Serikali inawaambia nini wananchi hawa ambao wanayasubiria maji haya?

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, Injinia Isaac Kamwelwe.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari tuna bomba, na juzi tumesaini mkataba tarehe 22 Aprili kwa ajili ya kufikisha maji Nzega, Igunga na Tabora. Kama bomba limeshapita karibu na eneo lako, tutaendelea, na kama *topography* inaruhusu tutaendelea kuweka fedha ili kuhakikisha kwamba na maeneo kama haya ya Ushetu na nikuhakikishie tu kwamba bado *capacity* ipo kubwa, yapo maji ya kutosha, tutaendelea kutenga fedha kuhakikisha kwamba na hili eneno la Ushetu tuhakikishe tunalipatia maji. Na nikuombe Mheshimiwa Mbunge kwamba naomba tuwasillane ili tuweze kupanga tuone namna gani tunaweza tukahakikisha kwamba maji yanafika haraka Ushetu.

MHE. STEPHEN H. NGONYANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kazi nzuri anayofanya. Mimi nilikuwa nataka kujua ule Mradi wa Vuga - Mlembule - Mombo ambao yeye ameutelelea kwa muda mrefu sana na kuona matatizo yake na kuwaahidi wananchi wa Mombo kwamba ikifika mwezi wa sita watapata maji. Ni lini Mradi huu utakuwa umekamilika na wananchi wale wafurahie mradi ule mkubwa wa maji ambao unaghanimu zaidi ya shilingi 900,000,000?

MWENYEKITI: Ahsante! Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri Maji na Umwagiliaji.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuhakikishie kwamba wananchi wa Mombo watapata maji. Nilifanya ziara nimeenda Vuga, nimeongea nao na tumekubaliana kwamba sasa tuongeze fedha pamoja na hiyo milioni mia tisa, tunaongeza fedha katika bajeti ya 2017/2018. Na tumeweka utaratibu, eneo lolote lenye chanzo tunapofanya mradi lazima tuhakikishe

kwamba wananchi wanaozunguka hilo eneo wapate maji kabla ya kupeleka Kijiji cha mbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tunatenga fedha itakayohakikisha kwamba wananchi wa Vuga wanapata maji, na bomba lingine linakuja moja kwa moja mpaka eneo la Mombo na maeneo mengine yatakayopitiwa na hilo bomba. Kwa hiyo nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tunaendelea na juhudini kuhakikisha kwamba wananchi wa Mombo wanapata maji kutoka Vuga.

MWENYEKITI: Ahsante, Waheshimiwa Wabunge kwa sababu ya muda tunaendelea. Swali linalofuata, swali namba 97 linaulizwa na Mheshimiwa Innocent Lugha Bashungwa, Mbunge wa Karagwe, na linaelekezwa Wizara ya Maji na Umwagiliaji. Mheshimiwa Bashughwa.

Na. 97

Ujenzi wa Mabwawa ya Maji

MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA aliuliza:-

Serikali imeahidi kujenga mabwawa ya maji katika Kata za Kanoni, Igarwa, Ihanda na Chenyoyo ili kuwapatia wananchi wa kata hizo maji.

(a) Je, Serikali imefikia hatua gani katika kutekeleza kazi hiyo?

(b) Je, Serikali inawahakikishajie wananchi wa vijiji vya Kafunjo, Kijumbura na Bweranyange kwamba mradi wa maji wa Lyakajunju utakapotekelezwa utawaachia wananchi miundombinu ya maji ili kuwanusuru kuliwa na mamba wanapofuata maji ziwani?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Innocent

Lugha Bashungwa, Mbunge wa Jimbo la Karagwe, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza ujenzi wa mabwawa, Serikali kupitia Wizara ya Maji na Umwagiliaji imeziagiza Halmashauri zote nchini kuainisha maeneo yanayoweza kujengwa mabwawa na kutenga fedha kwenye bajeti zao za kujenga angalau bwawa moja kila mwaka. Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe imeweza kuainisha maeneo yanayofaa kujengwa mabwawa kama ifuatavyo:-

Kata ya Kanoni eneo la Kabare na Omukigongo, Kata ya Igurwa eneo la Omukalinzi (Kabulala A) na Kata ya Nyakahanga eneo la Kashanda (Karazi). Mabwawa katika maeneo hayo yatajengwa kulingana na upatikanaji wa fedha baada ya kazi za usanifu, kuandaa michoro, kuainisha gharama na nyaraka za zabuni kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ipo katika hatua za usanifu wa kina wa utekelezaji wa Mradi wa Maji wa Bwawa la Lwakajunju ambao kutekelezwa kwake kutavipatia huduma ya maji vijiji vyote vitakavyopitiwa na bomba kuu la maji katika umbali usiozidi kilometra 12 kutoka eneo la bomba kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya usanifu kukamilika itaainisha iwapo vijiji vya Kafunjo, Kijumbura na Bweranyange vitakuwa ndani ya kilometra 12 kutoka eneo la Bomba Kuu. Mradi huo utavipatia maji na endapo havitakuwepo basi Halmashauri iweke kwenye vipaumbele vijiji hivyo katika bajeti inayotengwa na Wizara kila mwaka.

MWENYEKITI: Ahsante! Mheshimiwa Bashungwa.

MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza. Kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri na Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri wanayofanya katika utendaji wao wa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maswali yangu mawili ya nyongeza ni kama yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa Lwakajunju, imekuwa ni ahadi ya muda mrefu sana zaidi ya miaka 15. Kwa maana hiyo tumewaaahidi sana akina mama wa Karagwe na wananchi kuwatua ndoo kichwani kwa muda mrefu sana. Kama unavyojuu akina mama ule muda ambaa wanautumia kwenda kuchota maji umbali mrefu ndio muda huo huo ungeutumia kufanya kazi za maendeleo. Sasa swalii la kwanza, Mheshimiwa Naibu Waziri naomba unipe *comfort*, je, huu mradi wa Lwakajunju utatekelezwa lini? Ni lini wananchi wa Karagwe watapata hii huduma ya maji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na changamoto za kibajeti za Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe, je, Wizara ipo tayari kushirikianan na Halmashauri kuhakikisha fedha ambapo tunahitaji kwa ajili ya kuchimba mabwawa katika Kata za Kanoni, Igulwa lhanda, Chonyonyo na Nyakahanga zinapatikana ili wananchi wapate huduma ya maji?

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji kwa kifupi, muda si rafiki.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kuhusiana na Mradi wa Lwakajunju, ameomba apate *confort* na wananchi wake pia. *Comfort* ya kwanza ni kwamba mradi huu umetengewa dola milioni 30 kutokana na mkopo wa India, ni mkopo wenye uhakika na sasa hivi tupo kwenye taratibu za kukamilisha usanifu ili tutangaze *tender*. Kwa hiyo, nikuhakikishie kwamba mradi huu unatekelezwa kwasababu tayari una fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swalii la pili linalohusiana na ushirikiano na Halmashauri, Mheshimiwa Mbunge nikuhakikishie kwamba tutaendelea kushiriakana na Halmashauri zote kuhakikisha kwamba miradi ya maji inatekelezwa, mabwawa, mserereko, visima na mingine ili kuhakikisha kwamba wananchi wanapata maji. Kuhusu

suala la fedha upungufu wa fedha tutaenda nalo sabamba, lakini suala la msingi ni kuhakikishe kwamba wananchi wanapata maji. (*Makofii*)

MHE. MOSHI S. KAKOSO: Mheshimiwa Mwenyekiti nashukuru kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Katavi kuna miradi ya umwagiliaji ambayo imeanzishwa na Serikali na imetumia fedha nyingi sana. Miradi hiyo ni mradi wa Karema, Kabage na Mwamkulu. Miradi hii ya Serikali imetolewa fedha nyingi, bahati mbaya sana Serikali inapoanzisha haiwezi kuikamilisha hiyo miradi. Nilikuwa nataka kujua ni lini Serikali itakamilisha hiyo miradi ya Karema, Kabage na Mwamkulu ili iweze kuwanufaisha wananchi?

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri Maji na Umwagiliaji majibu, anauliza lini.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi hiyo ilianza, ni kweli ilichelewa kukamilishwa lakini sasa hivi tumeandaa timu ambayo inakwenda kupitia ili kuainisha changamoto ambazo zimefanya isikalimike ili tuweze kutoa fedha tuhakikishe kwamba miradi hiyo yote mitatu Karema, Kabage na Mwamkulu inakamilika.

Kwa hiyo, nikuhakikishie kwamba tayari, na mimi mwenyewe nimeshakwenda kutembelea Mradi mmojawapo pale na huo mradi sasa hivi tayari kazi inaendelea mkandarasi amerudi *site* ili kuhakikisha kwamba miradi yote hii inakamilika.

MHE. RHODA E. KUNCHELA: Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nilitaka nimuulize Mheshimiwa Waziri. Imekuwa ni kero kubwa kwa wananchi wa Manispaa ya Mpanda kuendelea kusubiri miradi ambayo haitekelezeki, lakini pia ni wiki sasa maji hayatoki. Sasa ni nini tamko la Serikali ili kuhakikisha wananchi hao wanapata maji lakini pia wasiendelee kulipa bili ambazo hawapati maji? (*Makofii*)

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, Mji wa Mpanda mahitaji ya maji ni lita 10,200,000 kwa siku. Hadi sasa kwa mradi uliopo unatoa maji lita 3,150,000 kwa siku. Sasa hivi kuna miradi miwili ambayo wakati wowote itasainiwa, miradi hiyo ikikamilika basi itaongeza kiwango cha maji hadi kufikia lita 6,000,000. Kwa hiyo, nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba utekelezaji unaendelea. Changamoto kama maji hayajapatikana, kwanza tufahamu kwamba maji yaliyopo yanatosheleza kwa asilimia 30 tu. Kwa hiyo, si suala kwamba maji hayapo, hapana, ni kidogo. Serikali inaendelea kujitahidi kuhakikisha kwamba yale mahitaji ya lita 10,200,000 yanafikiwa na tatizo la maji kutokupatikana halitakuwepo tena.

Na. 98

Kupunguza Ajali za Barabarani

MHE. SABREENA H. SUNGURA aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kupunguza ajali za barabarani?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Sabreena Hamza Sungura, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeandaa mkakati wa kudhibiti makosa yanayosababisha madhara makubwa ambayo hupelekea ajali za barabarani kuongezeka. Mambo yaliyolengwa katika mkakati pamoja na mambo mengine ni:-

(1) Udhibiti wa madereva walevi na kuendesha kwa uzembe;

(2) Udhibiti wa mwendokasi kwa madereva na wamiliki wa magari , kuwa na madereva wenza kwa mabasi ya safari za zaidi ya masaa manane;

(3) Kuthibiti uendeshaji magari bila sifa/leseni za udereva ama Bima;

(4) Kudhibiti usafirishaji wa abiria kutumia magari madogo yenye muundo wa tairi moja nyuma;

(5) Kusimamia matumizi ya barabara kwa Makundi Maalum mfano watoto, wazee, walemauvu na wasiotumia vyombo vyaa moto ikiwemo mikokoteni na balskeli;

(6) Kudhibiti ajali za pikipiki za magurudumu mawili (bodaboda) na magurudumu dumumatatu (bajaji);

(7) Kuzishauri mamlaka husika kuweka alama za kudumu za utambulisho kwenye maeneo hatarishi ya ajali;

(8) Kusimamia utaratibu wa nukta (*Point System*) kwenye leseni za udereva;

(9) Marekebisho ya Sheria za Usalama Barabarani;

(10) Abiria kufunga mikanda ya usalama wanapotumia vyombo vyaa usafiri;

(11) Kubaini maeneo tete na hatarishi ya ajali za barabarani;

(12) Kuthibiti utoaji na upokeaji rushwa barabarani;

(13) Motisha kwa askari wanaosimamia vizuri majukumu yao; na

(14) Kuwajengea uwezo wa kiutendaji askari wa usalama barabarani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nidhahiri kwamba suala la usalama barabaran siyo la kundi au taasisi moja tu ila ni letu sote. Wabunge ni miongan mwa wahusika wa suala la usalama barabaran, kwa maana kuwa nafasi yao kubwa ni katika kuelimisha umma na kusaidia katika ujenzi wa utamaduni wa kuheshimu alama za usalama barabaran nchini. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Sabreena.

MHE. SABREENA H. SUNGURA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri lakini bado kuna mambo ya msingi ambayo yanapelekea ajali za barabaran kuendelea kutokea ambayo hayajakuwa *mentioned* katika majibu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hususani njia inayoelekea Kigoma, kuanzia Itigi kwenda Tabora mpaka Kigoma, tumekuwa na *railway cross* nydingi sana katika eneo hilo, lakini nydingi katika hizo hazijawekewa alama kiasi kwamba msafiri anapokuwa anaendesha ama madereva wanapokuwa wanaendesha wanashindwa kutambua. Ni kwa mita chache sana alama hizo zipo na maeneo mengine alama hizo hakuna kabisa, kitu ambacho kinaweza kikapelekea sasa magari yetu na treni zije zisababishe ajali kubwa hapo baadaye. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kwamba wana-*fix* vibao vinavyoonesha *railway cross* barabaran katika njia hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kwa kuwa kumekuwa na shida kubwa sana hasa ya wafugaji, hususani wafugaji wa ng'ombe, hufuga maeneo ambayo ni pembezoni mwa barabara na wakati mwingine ng'ombe wale hupelekea ajili zisizokuwa za msingi na kwa kuwa kumekuwa na *tendency* ya *traffic* hasa katibu miji mikubwa kama Mwanza, Dar es Salaam, Dodoma na kadhalika, hususani Dar es Salaam ambapo taa za barabaran zinafanya kazi, hapo hapo na *traffic* wanafanya kazi, kitu ambacho kinapelekea ku-*confuse* madereva barabaran na kuweza kusababisha ajali.

Je, Serikali inatoa kauli gani juu ya mambo haya mawili?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tumekuwa tukikabiliana na changamoto za kukosekana katika baadhi ya maeneo alama za barabaranzi zinazotakiwa kuelekeza madereva kuona maeneo ambayo ni hatarishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kulitambua hilo ndiyo maana katika jibu langu la msingi nilieleza kati ya mikakati 14 moja katika eneo tulilokuwa tulifanyia kazi ni eneo hilo na kwamba tumejaribu kwa kiasi kikubwa sana kuweza kuwasiliana na kufanya kazi kwa karibu na mamlaka husika ili kuweza kudhibiti na kuweka hizo alama ambazo anasema kuwa zimekosekama. Bahati nzuri Makamu Mwenyekiti wa Baraza letu la Usalama Barabani ni Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uchukuzi, kwa hiyo tumelifanya hili kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo kubwa ambalo linasababisha alama hizi kupotea. Mara nyangi ni kutokana na tabia mbaya za baadhi ya wananchi ambao wamekuwa waking'oa kwa makusudi alama za barabaranzi na kuvitumia vyuma hivi kama vyumba chakavu. Naomba nitoe wito kwa wananchi kuacha tabia hiyo na kwamba mamlaka husika ziko macho kwa wale wote ambao watakiuka sheria za nchi, kwa kung'oa vibao vya alama hizi tutawachukulia hatua za kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili lilikuwa linahusiana na askari wa barabaranzi pamoja na taa za barabaranzi. Mara nyangi askari wa barabaranzi wanakaa wakati ambao kuna msongamano wa magari barabaranzi, hasa wakati wa asubuhi wakati watu wanakwenda kazini na wakati wa jioni wanapokuwa watoka kazini. Hii ni kwa sababu taa za barabaranzi zilipowekwa haziwezi kukidhi mahitaji ya nyakati husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo kuna wakati ambao kuna msafara mwingu unatokea katika

upande mmoja, kwa hiyo kutegemea taa za barabarani peke yake kunaweza kusababisha msongamano mkubwa. Kwa maana hiyo hao *traffic police* wanakaa pale kwa lengo la kudhibiti na kuzuia msongamano huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutaendelea kuhakikisha kwamba askari hao wanaendelea kutumika kusaidia kupunguza msongamano wa magari hasa katika nyakati hizo za watu ambao wanakwenda kazini na kurudi kazini asubuhi na jioni. (*Makofii*)

MHE. RICHARD P.MBOGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nina swali dogo kuhusiana na makazi ya Katumba, yaliyokuwa makazi ya wakimbizi. Makazi haya ya Katumba yana barabara takribani nne ambazo zinaingia kwenye eneo hilo. Tuna barabara kuu ya kijiji cha Msaginya ambako kuna geti ambalo limekuwa ni usumbufu mkubwa kwa wananchi wa Katumba hususani kuanzia saa 12.00 jioni kutokana na sheria za wakimbizi. Sasa kwa kuwa wananchi wa eneo hilo takribani asilimia 90 wameshapewa uraia na wengine hawaishi ndani ya eneo hilo.

Je, Serikali haioni sasa ni muda muafaka kwa lile geti la Msaginya kuendolewa au muda kuongezwa hata ikawa saa 24?

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake tumelichukua na tutalitafakari tuone jinsi gani tutalifanyia kazi.

MWENYEKITI: Ahsante, Waheshimiwa tunaendelea na swali namba 99 linaloulizwa na Mheshimiwa Hamida Mohamed Abdallah, Mbunge wa Viti Maalum na linalekezwa kwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo.

Na. 99

Kuboresha Uwanja wa Mpira wa Miguu Lindi

MHE. HAMIIDA M. ABDALLAH aliuliza:-

Uwanja wa mpira wa miguu Lindi ulijengwa tangu mwaka 1957 wakati wa ukoloni wa Gavana Sir Edward Twining na mpaka leo haujafanyiwa maboresho.

Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka wa kuukarabati na kuwa wa kisasa ukizingatiwa kwamba uwanja huo ulikuwa ukitumika kwa ajili ya michezo ya Afrika Mashariki?

NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANA NA MICHEZO aliibuu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hamida Mohamed Abdallah, Mbunge Viti Maalum. kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwezi uwanja wa mpira wa miguu wa Lindi (Ilula) ni mkongwe ulijengwa wakati wa ukoloni wa Mwingereza na unahitaji ukarabati ili kuufanya kuwa wa kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ya Maendeleo ya Michezo inahimiza kila taasisi yenye kiwanja au viwanja vya michezo kuvitunza viwanja hivyo ili viweze kudumu. Uwanja huu upo chini ya Halmashauri ya Lindi kama ilivyo kwa viwanja vingine vingi vilivyoko chini ya Halmashauri hapa nchini. Wizara yangu inashauri Halmashauri ya Lindi kuangalia uwezekano wa kuufanya ukarabati uwanja huo kwa kuwashirikisha wadau mbalimbali pamoja na wananchi wa Lindi wakiongozwa na Waheshimiwa Wabunge.

Aidha, Wizara yangu itakuwa tayari kutoa ushauri wa kitaalamu ili kusaidia kukarabati uwanja huo na kuufanya

kuwa wa kisasa na kutumiwa na wanamichezo wengi zaidi wa Mkoa huo na Taifa kwa ujumla.

MHE. HAMIDA M. ABDALLAH: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nimshukuru Mheshimiwa Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri yenye matumaini. Ninashukuru Serikali inatambua kwamba uwanja ule unahitaji kukarabatiwa na kuwa uwanja wa kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwanja wa Lindi usifananishwe na viwanjwa vingine vilivyojengwa na Halmashauri. Uwanja wa Lindi ni mionganini mwa viwanja vitatu bora vilivyojengwa na wakoloni mana yake ni kwamba tumerithi kutoka mikononi mwa wakoloni ikiwemo kiwanja cha Mkwakwani - Tanga, kiwanja cha Dar es salaam na kiwanja cha Lindi Manispaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwanja ule umewahi kutumika kwa michezo ya Afrika Mashariki, kwa hiyo uwanja unahistoria ya kipekee kwamba timu za Afrika Mashariki zimechezwa katika uwanja wa Lindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wana-Lindi sasa tunahitaji kuona uwanja ule unabadijika na kuwa uwanja wa kisasa, tunaiomba Serikali ituambie itatusaidiaje kukarabati uwanja ule? Ninajua kwamba Halmashauri haina uwezo wa fedha wa kukarabati uwanja ule na kuwa uwanja wa kisasa, kwa hiyo ninaiomba Serikali ituambie ni namna gani itaweza ikatusaidia kukarabati uwanja na kuwa uwanja wa kisasa?

NAIBU WAZIRI, HABARI UTAMADUNI SANAA NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Hamida kwa jinsi alivyokuwa mstari wa mbele kufuatilia suala la ukarabati wa uwanja huu wa mpira wa miguu wa Ilula (Lindi), kwa kweli hii imekuwa ni chachu kubwa sana katika maendeleo ya ukuaji wa soka katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niishauri Halmashauri ya Lindi kwamba iweke kipaumbele katika

kutenga bajeti kwa ajili ya ukarabati wa uwanja huu. Pili, napenda kuchukua nafasi hii kumjulisha Mheshimiwa Hamida kwamba Serikali inalitambua hili na kutokana na hilo imekuwa ikitoa ushauri kwa *TFF* kuzisaidia Halmashauri kufanya ukarabati wa viwanja kwa kutumia wadau mbalimbali au wafadhili wa ndani na nje ya nchi, na kwa namna hiyo basi *TFF* imekuwa ikiweka katika orodha kila mwaka walau viwanja katika Halmashauri mbili hadi tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kumtaarifu kwamba uwanja wa llula upo mionganoni mwa orodha ambayo imewekwa na *TFF* kwa ajili ya ukarabati. Niseme tu kwamba *TFF* watakapotaka kufanya ukarabati itabidi waweke mkataba na Halmashauri ya Lindi na mkataba huo unasharti kwamba ni lazima kipaumbele cha matumizi kiwe katika mchezo wa mpira, ahsante sana.

MHE. KHATIB SAID HAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa kuwa Chama cha Mapinduzi kirithi viwanja vilivyokuwa mali ya Watanzania kutoka kwa wakoloni wakati sasa nchi imekuwa ya mfumo wa vyama vingi; na kwa vile Chama cha Mapinduzi kimeshindwa kuitunza mali hii ya mayatima, ni lini Chama cha Mapinduzi kitarudisha viwanja hivi kwa Halmashauri au Serikali ili irudi mikononi kwa Watanzania wote badala ya kuendelea *kudhulumu* haki hii ya watanzania? (*Makofii*) **[Neno kudhulumu siyo sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

MWENYEKITI: Mheshimiwa Haji, naomba ili neno dhulumu uliondoe halafu lijibiwe.

MHE. KHATIB SAID HAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima napenda kuondoa neno kudhulumu na badala yake liwe kuirejesha haki hii kwa Watanzania wote. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Habari Utamaduni Sanaa na Michezo majibu.

NAIBU WAZIRI, HABARI UTAMADUNI SANAA NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa hakuna

hati yoyote inayoonekana kwamba Chama cha Mapinduzi kimechukua viwanja kutoka kwa mmiliki yoyote, hati zote zinaonyesha ni miliki ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo basi napaenda kulithibitisha Bunge lako Tufu kwamba Chama cha Mapinduzi kinavifanyia ukarabati viwanja vyake kama zinavyofanya Halmashauri; kwa mfano uwanja wa Singida. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Singida Mheshimiwa Martha Mlata anasimamia zoezi hili, upo uwanja wa Mbeya na wenyewe unafanyiwa ukarabati na Chama cha Mapinduzi kwa kushirikiana na wadau. Ahsante.

MHE. RICHARD M. NDASSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa sababu tunao uwanja wetu wa Taifa (Dar es Salaam) ambao ni wa kimataifa na ili kuutangaza uwanja huo, na ili kutangaza utalii na kuongeza ajira kwa nini Serikali sasa isije na mpango wa kuziomba Balozi zetu nje ili timu zao za Taifa huko ziliko zije kuutumia uwanja wetu wa mpira wa uwanja wa Taifa, na wakimaliza kucheza mpira au baada ya kucheza mpira wachezaji hao waende kwenye hifadhi zetu ili watangaze utalii wa nchi yetu kupitia uwanja wa Taifa?

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri wa Habari Utamaduni Sanaa na Michezo jibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI, HABARI UTAMADUNI SANAA NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, wazo lake ni zuri, tumelichukua na tutakwenda kulifanyia kazi na tutarejesha majibu, ahsante sana.

MWENYEKITI: Asante tunaendelea, swalı letu namba 100 linaulizwa na Mheshimiwa Albert Obama Ntabaliba, Mbunge wetu wa Buhingwe linaulizwa kwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

Na. 100

Ujenzi wa Barabara ya Kasulu – Manyovu Kilometra 48.7

MHE. ALBERT O. NTABALIBA aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga kwa kiwango cha lami baraba Mnanila – Manyovu – Kasulu ili kuwasaidia wananchi wa maeneo hayo?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Albert Obama Ntabaliba, Mbunge wa Buhigwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Kasulu hadi Manyovu yenye urefu wa kilometra 48.7 ni barabara ya kiwango cha changarawe na inahudumiwa na Wakala wa Barabara (*TANROADS*) Mkoa wa Kigoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya Kasulu hadi Manyovu ni sehemu ya mradi wa kikanda wa Barabara ya Kibondo - Kasulu hadi Manyovu yenye urefu wa kilometra 250 inayofanyiwa mapitio ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kupitia mpango wa *NEPAD* yaani *New Partnership for Africa's Development* kwa ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Afrika chini ya uratibu wa Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa kiwango cha lami wa barabara hii unatarajiwa kuanza baada ya kukamilika kwa mapitio ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina.

MHE. ALBERT O. NTABALIBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwanza niipongeze Wizara kwa majibu mazuri, baada ya hapo nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii ya Manyovu - Kasulu imekuwa ni kero kubwa sana hasa wakati huu wa mvua na sasa hivi nauli ya kutoka Manyovu - Kasulu imefikia mpaka shilingi 10,000; na tunayo barabara nyngi ya lami ya kutoka Kigoma mpaka Manyovu yenyeye urefu wa kilometa 60 ambayo nauli yake ni shilingi 3,000. Kwa hiyo, umuhimu wa kujenga barabara hii na kuianza mapema inajionyesha kwa vigezo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kujua, Wizara imekiri kwamba inafanya upembuzi yakifu, wananchi wa Buhigwe wanataka kujua upembuzi yakinifu unaisha lini na ujenzi unaanza lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Mheshimiwa Rais alipokuwa akijinadi tuliita vijiji vya Mlela, Buhigwe, Kavomo, Nyankoloko, Bwelanka na akaahidi kwamba atajenga barabara ya kilometra tano katika Wilaya ya Buhigwe, je, ni lini ahadi hiyo itatimizwa?

MWNEYEKITI: Ahsante, Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba kumpongeza sana Mheshimiwa Ntabaliba kwa kazi kubwa anayofanya ya kufuatilia miradi mbalimbali ya Miundombinu katika Wilaya yake na Jimbo lake, nikupongeze sana. Mimi ninakuhakikisha kama ambavyo tumekuwa tukiwahakikisha katika ofisi zetu mimi na Waziri wangu, kwamba tutashirikiana na wewe kuhakikisha mambo yote ambayo tuliyaahidi katika Wilaya yako yanatekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema katika jibu la msingi, ujenzi utaanza baada ya kukamilika upembuzi na usanifu wa kina, kwa maana unaofanywa na kufuatiliwa na wenzetu wa *AfDB*. Nikuombe tu kwa kuwa anayefanya si Serikali, kazi hii inafanya na *AfDB* chini ya Afrika Mashariki suala la lini ni gumu kukueleza isije ikaonekana tunasema uongo hapa Bungeni. Nikuhakikishie suala hili litakamilika katika

kipindi kifupi kijacho na baada ya hapo shughuli za ujenzi zitaanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa swali lake la pili, nimuhakikishie, kama ambavyo tulimuhakikishia ofisini, kwamba kilometra zake tano ambazo Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tano aliahidi zitatekelezwa mara baada ya masuala haya ya miradi ambayo ni kiporo yatakapokamilika; na uzuri wake sehemu kubwa za viforo zinakamilika mwaka huu ujao wa fedha baada ya hapo tutakamilisha ahadi zingine zote ambazo Mheshimiwa Rais alizahidi hasa za kilometra tano, kilometra sita katika sehemu mbalimbali za Miji ya Tanzania hii.

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, keshokutwa uwanja ni mpana kwa Wizara hii, leo kidogo, Mheshimiwa Msukuma.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Wananchi wa Jimbo la Geita Vijijini hususan Jimbo la Geita Vijijini ndilo Jimbo pekee linaloongoza kwa kupata chakula kingi kila mwaka kwenye Kanda ya Ziwa; wamekuwa na kilio cha barabara yao kutoka Senga - Sungusila - Lubanga mpaka Iseni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge watatu walionitangulia wote wamekuwa wakiomba Serikali barabara hii ichukuliwe angalau tu kwa kiwango changalawe siolami na Serikali imekuwa ikitoa ahadi kila siku tunafanya tunafanya, na mipango yote sisi kwenye RCC tumeshabariki. Sasa nataka kujua Waziri ni lini barabara hii unaichukua na kuiweka kwenye angalau kiwango cha molami tu?

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri Ujenzi, Uchukuzi Mawasiliano ni lini utaichukua.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana Mheshimiwa Musukuma kwanza kwa kutukumbusha kuhusu

barabara hii. Aliiongelea muda mrefu, kuanzia miaka ya nyuma na sasa tunamuhakikishi kwamba hii barabara itachukuliwa na *TANROADS*, kwa maana ya kukasimiwa. Barabara hii haijakidhi vigezo vya kupandishwa hadhi, lakini Waziri ameshakubali na ameshaikasimu barabara hii ili iweze kutekelezwa na *TANROADS* Mkoa wa Geita.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Paresto.

MHE. MUSSA B. MBAROUK: Mheshimiwa nashukuru kwa kuniona Mheshimiwa kwa kuwa barabara ya Tanga - Pangani hadi Bagamoyo

MWENYEKITI: Mheshimiwa Paresto. (*Kicheko*)

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa sera ya masuala ya ujenzi ni kuunganisha barabara ya mkoa mmoja na mwingine kwa kiwango cha lami, na kumekuwa na ahadi ya muda mrefu ya ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya Njiapanda - Karatu - Mang'ola mpaka Lalago, ambayo inaunganisha Mkoa wa Arusha na Mkoa wa Simiyu, je, ni lini barabara hii itajengwa kwa kiwango cha lami?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuombe Mheshimiwa Paresto asubiri, ni keshokutwa tu bajeti yetu inakuja, na ramani yote ya shughuli za ujenzi wa barabara zote itakuwa imeanikwa wazi. Nisinge penda kwenda kwa undani kwa sababu ni sehemu ambayo Waziri wangu ataishughulikia keshokutwa.

MWENYEKITI: Ahsante tunaendelea Waheshimiwa Wabunge swali namba 101 linaulizwa na Mheshimiwa Gimbi Dotto Masaba, Mbunge wa Viti Maalum na linalekezwa kwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji. Mheshimiwa Gimbi.

Na. 101

Hitaji la Viwanda Mkoa wa Simiyu

MHE. GIMBI D. MASABA aliuliza:-

Mkoa wa Simiyu ni miongoni mwa mikoa ambayo haina viwanda licha ya wananchi wake kuwa wakulima na wafugaji.

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga viwanda vingi Mkoani Simiyu wikiwemo viwanda vyta kusindika nyama, matunda, maziwa, ngozi, mafuta ya kula na nguo ili kuharakisha ukuaji wa uchumi na ongezeko la ajira kwa vijana?

WAZIRI WA VIWANDA, BIASARA NA UWEKEZAJI
alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Gimbi Dotto Masaba, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, azma ya Serikali ya ujenzi wa uchumi wa viwanda imeainishwa vyema katika Mpango wa Pilli wa Maendeleo wa Miaka Mitano wa mwaka 2016/2017 mpaka 2020/2021 wenye dhima ya kujenga uchumi wa viwanda ili kuleta mageuzi ya kiuchumi na maendeleo ya watu. Ili kufikia azma hiyo, ushiriki wa mchango wa mtu mmoja mmoja, makundi ya watu, taasisi za umma na taasisi binafsi unahitajika. Aidha, Serikali kwa kushirikiana na wadau wengine tumeanza kutekeleza mikakati minne ya ngozi, mafuta ya kula, nguo na mazao jamii ya kunde. Wakati huo huo mapango wa wilaya moja, zao moja na uhamasishaji wa ujenzi wa viwanda chini ya *SIDO* unaendelea nchini kote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu na Watanzania kwa ujumla kuwa Mkoa wa Simiyu chini ya uongozi wa Komredi Anthony Mtaka umekuwa kinara wa kutekeleza mpango wa *one district one product*. Wilaya

tano za Bariadi, Busega, Itilima, Maswa na Meatu katika Mkoa wa Simiyu zimepangiwa kuzalisha mafuta ya alizeti. Vilevile Mkoa wa Simiyu una viwanda ambavyo vinaanzishwa kwa kuzingatia upatikanaji wa malighafi, teknolojia na soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya ya Maswa Kimejengwa kiwanda cha chaki, Wilaya ya Bariadi na Itilima Kitajengwa kiwandacha nyama na Wilaya ya Meatu Kimejengwa kiwanda cha Maziwa. Hizi ni kazi ya mwaka mmoja na naweza kusema ni mwanzo mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa taasisi, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (*NHIF*) unakamilisha taratibu za kuwekeza kwenye kiwanda cha kuzalisha vifaa tiba vitokanavyo na pamba na bidhaa za maji (*drip*). Gharama za miradi hiyo inakadiriwa kufikia dola za kimarekani 36.5 na kutoa ajira za moja kwa moja 1,600 na zisizo kuwa moja kwa moja 5,000. Mradi huo unakadiriwa kutumia pamba tani 50,000 kwa mwaka. Aidha, Serikali ya Mkoa inaendelea na jitihada za kutenga maeneo ya uwekezaji kwa kuwalenga wajasiriamali wadogo, wa kati mpaka wakubwa bila kujali kwamba wanatoka ndani ya nchi au nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshauri Mheshimiwa Mbunge tushirikiane katika kuhamasisha wawekezaji wa ndani na nje kuanzisha viwanda na kusindika mazao ya kilimo katika Mkoa wa Simiyu ili kuhakikisha ukuaji wa uchumi na kuongeza ajira kwa vijana.

MHE. GIMBI D. MASABA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri, wakati Serikali inahamasisha wadau na jamii kujenga viwanda hivi, je, Serikali inatoa kauli gani kwa viwanda ambavyo ilivianzisha na imevitekeleza, kama vile kiwanda cha *Nasai Ginnery, Ngasamwa Ginnery, Rugulu Ginnery, Malampaka Ginnery* na Solwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kukosekana kwa bei nzuri ya ng'ombe na wananchi wa Mkoa wa Simiyu

kulazimika kusafirisha ng'ombe wao kupeleka Jiji la Dar es Salaam, je, Serikali inatoa kauli gani na mkakati madhubuti wa kuhakikisha kwamba wanajenga viwanda vyta nyama kama alivyojibu kwenye swali lake la msingi, kwamba watajenga Bariadi na Itilima. Ni lini mkakati wa makusudi wa kuharakisha kujenga viwanda hivyo? (*Makof*)

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na hili la pili, sehemu ya Mkoa wa Simiyu ni maarufu kwa ufugaji wa ng'ombe na zao la pamba. Juzi Mkuu wa Mkoa, Mheshimiwa Anthony Mtaka alikutana na wataalam wangu wa uwekezaji katika jitihada za kusaidiana kutafuta wawekezaji. Wawekezaji wanatafutwa, kwa hiyo, tunachofanya ni sekta binafsi itakayowekezwa kwa hiyo tunatafuta wawekezaji waje wawekeze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swali langu la pili nilikuomba Mheshimiwa Mbunge na wewe uingie kwenye boti hiyo hiyo ya kuwatafuta wawekezaji. Tunatafuta wawekezaji ili wawekeze, ndiyo namna ya kupata wawekezaji. Nitumie fursa hii, kuwashukuru Wabunge ambaa mmekwenda maili moja zaidi na kuwatafuta wawekezaji, ambapo mimi kazi yangu ni kuwaondolea vikwazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali la kwanza, kwamba vipo viwanda ambavyo vilibinafsishwa, vipo viwanda ambavyo vimekwama, kauli ya Serikali ni kwamba wale waliokuwa na viwanda vile, walio vinunua au vyta kwao wavirudishe katika shughuli vifanye kazi. Tunachofanya sasa chini ya *Treasure Registrar* Wizara yangu na Wizara za kisekta zinazohusika tunawafuata wale kuwashawishi kutumia nguvu zote ili warudi katika shughuli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuhusu viwanda vyta pamba naomba niwatoe hofu watu wanaolima pamba, chini ya mkakati wa pamba mpaka mavazi tuna imani kwamba uzalishaji wa pamba kwa tija utalazimisha viwanda vile vifufuke kwa sababu *the supply* itakuwa nyingi na viwanda vitafanya kazi, tuwe na subira. (*Makof*)

MWENYEKITI: Asante Mheshimiwa Stanslaus Nyongo na mwingine ni Mheshimiwa Halima.

MHE. STANSLAUS H. NYONGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi nimuulize Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Maswa imekwisha kutenga eneo kwa ajili ya uwekezaji (*EPZA*) zaidi ya heka 110, na Mheshimiwa Waziri tulishakuja kuleta barua na *EPZA* walishakubali kuwekeza hapo, lakini mpaka sasa hivi hakuna mkakati wowote unaoendelea. Naomba kauli yako na *commitment* ya Serikali, je, ni lini Serikali sasa au *EPZA* watacaa na Halmashauri ya Maswa na kuweza kuanzisha mradi huu katika maeneo haya? Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa kifupi tu.

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu Mheshimiwa Nyongo kuhusu eneo la uwekezaji la Maswa na tunashukuru tumelipata eneo la Maswa na Mheshimiwa Nyongo nimshukuru ni mionganini mwa Wabunge ambao wamejasiria kutafuta maeneo ya uwekezaji bila vikwazo. Kuna wengine maeneo yao yanakuwa na vikwazo vikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kitakachofuata, kama nilivyofanya kwa Bunda, Bunda nimeishaitangaza kuwa *special economic zone*; nitaitangaza Maswa halafu sasa tutaanza kutafuta wawekezaji.

Nirudie Waheshimiwa Wabunge Wawekezaji wanatafutwa dunia nzima na Tanzania si *destination* peke yake, *wana-move* kutoka Asia kuja Afrika, Afrika si Tanzania peke yake. Kwa hiyo, tuweke mazingira wezeshi tuwe wakalimu waje kusudi tutengeneze ajira.

MWENYEKITI: Ahsante, swalii la mwisho Mheshimiwa Halima.

MHE. HALIMA ALI MOHAMMED Mheshimiwa
Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimuulize Mheshimiwa Waziri, je, Serikali ina mkakati gani mahsuswi wa kuhakikisha kwamba Sera ya Tanzania ya viwanda inamkomboa kweli mwanamke wa Kitanzania?

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji tumkomboe mwanamke kupitia Viwanda.

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:
Mheshimiwa Mwenyekiti, unapozungumzia uwekezaji katika viwanda unazungumzia akina mama; na nguvu kubwa ya ujenzi wa uchumi wa viwanda, viwanda ambavyo ni *sustainable*, viwanda ambavyo ni darasa, ni viwanda vidogo sana, viwanda vidogo na vya kati. Katika shughuli za kuhamasisha viwanda hivi mimi ninaokutana nao watupu ni akina mama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna shirika la akina mama la *Food Processing* liko Dar es Salaam, Binti Nasibu ndiye Mwenyekiti wake. Tunawatafuta akina mama tunawahamasisha kusudi muanze viwanda vidogo na vya kati ili kusudi mkue mfundishe na wazazi wenu. Mama akipata kiwanda na wajukuu wanapata kiwanda, na mama zao wanapata viwanda nchi yote inakuwa ya viwanda. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante, tunaendelea.

MWENYEKITI: Swali linalofuata 102 linaulizwa na Mheshimiwa Zuberi Mohamed Kuchauka Mbunge wa Liwale na linalekezwa kwa Waziri wa Fedha na Mipango.

Na. 102

**Kuhusu Kubinafsifishwa kwa Shirika la Usagaji la Taifa
(NMC)**

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA aliuliza:-

Shirika la Usagishaji la Taifa (NMC) liliokwua na matawi karibu nchi nzima na *assets* mbalimbali lilibinafsishwa kutokana na sera ya ubinasfishaji.

(a) Je, ni matawi mangapi yamebinafsishwa na mangapi yamebaki mikononi mwa Serikali?

(b) Je, Serikali imepata fedha kiasi gani kutokana na ubinafsishaji huo?

(c) Kati ya matawi yaliyobinafsishwa ni mangapi yanaendeshwa kwa ubia wa Serikali?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango napenda kujibu swali la Mheshimiwa Zuberi Mohamed Kuchauka, Mbunge wa Liwale, lenye vipengele (a) (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Idadi ya matawi ya Shirika la Taifa la Usagishaji yaliyobinafsishwa ni 22 na yaliyobaki mikononi mwa Serikali ni matano;

(b) Katika kubinafsisha mali za NMC Serikali imepata fedha kiasi cha shilingi 7,491,611,000; na

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, katika matawi yaliyobaki hakuna tawi linaloendeshwa kwa ubia kati ya Serikali na mwekezaji. Matawi hayo kwa sasa yanasmamiwa na Bodi ya Nafaka na Mazao mchanganyiko. Hata hivyo, tawi la NMC - Arusha maarufu kama *Unga Limited* limekodishwa kwa Kampuni ya *Monaban Trading Company Limited*.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Zuberi.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Niseme tu nasikitika kwa majibu ambayo ni rahisi, majibu mafupi, majibu ambayo hayaoneshi matumaini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo
Mheshimiwa Naibu Waziri...

MWENYEKITI: Uliza swali.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: ...anasema ubinafsishaji wa matawi 22 yaliyokuwa *National Milling* tumepata shilingi bilioni 7.4, ni masikitiko makubwa sana; na hii inaonyesha moja kwa moja kwamba sisi huu umasikini umetuandama. kwa sababu kama tunaweza tukatupa...

MWENYEKITI: Uliza swali Mheshimiwa.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: ...ni masikitiko makubwa sana. Msheshimiwa Mwenyekiti, najenga hoja. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Muda.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna matawi kama *Plot 33, Plot 5, Tangold* yale matawi sasa hivi yote ni ma-godawn. Watu walionunua matawi ya *National Milling* ambayo yanafanya kazi ni Bakheresa na *Mohamed Enterprises* speke yake, lakini matawi mengine yote yaliyobaki yamekuwa ma-godawn na ninyi mnasema mnaenda kwenye viwanda, mimi hapa sijapata kuelewa. Nini hatima ya hayo mashirika ambayo sasa hivi ni ma-godawn badala ya kuwa viwanda? (*Makofii*)

(b) Kwanza niseme wazi kwamba na mimi ni mmoja kwenye taaluma hii ya usindikaji wa nafaka. Nimefanya kazi *National Milling* si chini ya miaka 10. Kwa upande wa Kurasini mnamo tarehe 31 Aprili, 2005 waliletewa barua aliyekuwa Meneja pale kwamba kiwanda hicho akabidhiwe *Mohamed*

Enterprises anayekaribia kununua, alikabidhiwa tu kwa sababu anakaribia kununua. Si hivyo tu, wafanyakazi waliokuwepo pale mpaka leo hii wanaidai Serikali hii zaidi ya shilingi milioni 234.3, bado hatima yao haieleweki na kesi imekwisha. Vilevile si hivyo tu, tarehe 20...Hazina wameitwa mahakamani hawataki kwenda, nini hatima ya wafanyakazi wale? (Makofi)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa kifupi tu, maswali haya mawili.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la kwanza nini hatima ya hayo Mashirika ambayo yalikodishiwa na sasa sio viwanda ni magodown. Naomba kumkumbusha Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali ilishaanza mchakato wa kufanya tathimini ya viwanda vyote vilivyouzwa na ambavyo vimegeuzwa matumizi.

Mheshimiwa Waziri wa Viwanda alishasimama hapa na kusema na ndiyo kauli ya Serikali, kwamba vyote hivyo vitarejeshwa Serikalini na vitaendelea kufanya kazi, na vitatafutiwa wawekezaji na wataendelea kuviendesha viwanda hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali la pili linalohusu hatima ya wafanyakazi, ameshasema kesi iko mahakamani, ikishakuwa mahakamani naomba nisilionelee hapa na ni imani yangu kwamba kesi hiyo itaendeshwa na itafika mwisho mzuri. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante, Waheshimiwa tunaendela. Swali linalofuata swali namba 103 linaulizwa na Mheshimiwa Yahaya Massare, Mbunge wa Manyoni na linaelekezwa kwa Waziri wa Maliasili na Utalii.

Na. 103

Sheria ya Usafirishaji wa Mazao ya Misitu

MHE. YAHAYA O. MASSARE aliuliza:-

Tanzania ni nchi yenye misitu mingi na Sheria ya Usafirishaji wa Mazao ya Misitu inazuia kusafirisha zaidi ya sentimeta 15 au inchi sita.

Je, Serikali imepata hasara kiasi gani kwa kuruhusu usafirishaji wa sentimeta 20 sawa na inchi nane ili kujenga uwezo wa kiushindani na nchi nyingine katika soko?

MWENYEKITI: Ahsante, majibu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii *Engineer Ramo Makani*.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swalı la Mheshimiwa Yahaya Omari Massarem, Mbunge wa Manyoni Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 50 cha Kanuni za Sheria ya Misitu kinakataza kusafirisha magogo nje ya nchi. Sheria hiyo pia hairuhusu kuuza nje ya nchi mbao zote zenye unene unaozidi inchi sita, uamuzi ambao azma yake kubwa ni kutoa fursa ya kukuza viwanda ndani ya nchi na kupanua wigo wa ajira kwa vijana nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kwa mujibu wa sheria, Serikali hairuhusu usafirishaji wa mbao zenye unene wa sentimeta 20 sawa na inchi nane ni dhahiri kwamba haiwezi kuwa na takwimu za hasara iliyopata kwa kuruhusu usafirishaji wa mbao za unene huo.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Massare.

MHE. YAHAYA O. MASSARE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii, pia nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Lakini pamoja na majibu hayo mazuri nina maswali madogo tu ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ya Maliasili kupitia TFS imekuwa ikitoa vibali vya kuvuna mazao ya misitu. Mvunaji anaanzia vijijini, Wilayani kwenye kanda na hadi Wizara, lakini kabla ya kuruhusiwa kuvuna mazao ya misitu, Serikali imekuwa ikiwasajili wadau hawa na kuwatoza pesa kila mwaka. Vilevile kumekuwepo na tatizo kubwa la Wizara hii kuwa ikishatoa vibali hivi inachukua muda mfupi tu kuvifuta kama ilivyokuwa mwaka huu ambapo vilitolewa vibali zikiwemo *approval* za...

MWENYEKITI: Swali.

MHE. YAHAYA O. MASSARE: ... kutoka nchi za nje na baadae vilifutwa na Mheshimiwa Waziri, sasa swali.

(a) Je, ni lini Serikali itaacha utaratibu huu mbaya na ambaao unawatia hasara wadau wao?

(b) Serikali haioni sasa ni vyema isitoe *approval* hizi hadi ijiridhishe kwamba wananchi na wadau hawa wakipewa vibali hivyo watafanya kazi kwa mwaka mzima kuliko kama hivi wanatoa na kufanya kazi kwa miezi miwili tu na kuwasimamisha?

MWENYEKITI: Ahsante, Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ufupi suala la uvunaji wa maliasili linatokana na ukweli kwamba nia na dhamira ya Serikali ni kuliwezesha Taifa hili kuweza kutekeleza mipango yake yote ya maendeleo kwa kutumia rasilimali za Taifa hili ikiwemo maliasili. Jambo la msingi ni kwamba tunatakiwa kutumia maliasili hizo kwa namna ambayo ni endelevu. Kwa hiyo, udhibiti haumaanishi kwamba rasilimali hizo au maliasili hizo

zisitumike kabisa, hapana, nia ya Serikali ni kuhakikisha kwamba tunafanya matumizi endelevu ili tuweze kuendana hata na malengo ya Umoja wa Mataifa ya Maendeleo Endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kuhusu swali lake moja kwa moja la utaratibu wa utoaji wa vibali, huo ni utaratibu ambao utatuwezesha kutoa fursa kwa kila mwananchi ya kuweza kushiriki katika uvunaji wa rasimili hiso. Lakini ikiwa kwamba, utaratibu huo unaonekana pengine una kasoro basi kwa kuwa ulikuwepo kwa mujibu wa sheria basi...

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, naomba utulivu Bungeni.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge anayo fursa ya kufuata utaratibu wa kawaida wa kuleta maoni ili tuweze kuititia upya sheria hiyo.

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea na swali letu la mwisho, swali namba 104 linaulizwa na Mheshimiwa Joseph George Kakunda, Mbunge wa Sikonge kwa Wizara hiyo hiyo ya Maliasili na Utalii.

Na. 104

Kumega Sehemu ya Hifadhi kuwapa Wananchi – Sikonge

MHE. JOSEPH G. KAKUNDA aliuliza:-

Kati ya mwaka 1954 na 1957 kulifanyika zoezi la upimaji wa maeneo ya Hifadhi za Misitu, Mapori ya Akiba na Hifadhi katika Wilaya ya Sikonge ambapo kulikuwa na wakazi takribani 16,000 na ng'ombe wapataao 2500. Kwa sasa wakazi wameongezeka hadi kufikia takribani 300,000 na ng'ombe wapo takribani 200,000 lakini eneo la kuishi, kulima na malisho ya mifugo na shughuli nyingine za kiuchumi ni lile lile la asilimia 3.7 ya eneo lote la Wilaya huku eneo la Hifadhi

likibaki asilimia 96.3 na hali hii inasababisha migogoro kati ya wakulima, wafugaji na warina asali dhidi ya Maafisa Maliasili.

(a) Je, ni lini Serikali itawaongeza wakazi wa Wilaya ya Sikunge eneo la kuisha, kulima na kulishia mifugo kutoka asilimia 3.7 hadi angalau asilimia 25 ya eneo lote la Wilaya?

(b) Je, Serikali haioni kuwa kuongeza eneo la Wilaya hiyo kwa asilimia 25 kutaepusha migogoro iliyopo sasa na hivyo wananchi watatekeleza shughuli zao kwa amani na utulivu huku wakilinda mazingira pamoja na hifadhi?

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri Maliasili na Utalii, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joseph George Kakunda, Mbunge wa Sikunge, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulingana na takwimu za Taasisi ya Takwimu ya Taifa (*The National Bureau of Statistics*) na Sensa ya mwaka 2012, Wilaya ya Sikunge ina ukubwa wa kilometa za mraba 27,873 na idadi ya watu wapatao 179,883. Aidha, maeneo ya hifadhi za misitu na wanyamapori yana ukubwa kilometa za mraba 20,056.94 sawa na asilimia 72 ya eneo lote la Wilaya, hivyo kufanya eneo la makazi na shughuli nyiningine za binadamu kuwa sawa na asilimia 28.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hifadhi za misitu na mapori ya akiba katika Wilaya ya Sikunge ni muhimu kwa uhifadhi na maendeleo ya sekta nyiningine, ikiwa ni pamoja na kuwa vyanzo vya mto Ugalla, ziwa Sagara, Nyamagoma na ardhi oevu ya Malagarasi - Moyowosi. Kwa mantiki hiyo, kugawa maeneo haya na kuruhusu shughuli za kibinadamu kutahatarisha upatikanaji wa rasilimali za maji kwa ajili ya shughuli za uvuvi, kilimo, ufugaji, matumizi ya nyumbani na

mengineyo kwa kiasi kikubwa. Muhimu zaidi ni mchango mkubwa wa misitu hiyo katika hali ya hewa na udhibiti wa mabadiliko hasi ya tabianchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imethibitika kwamba kilimo cha kuhama hama, ikiwa ni pamoja na utumiaji wa maeneo makubwa ya ardhi; ufugaji wa kuhama hama ukijumuisha uingizaji wa mifugo katika maeneo yaliyohifadhiwa, ni matumizi mabaya ya rasilimali ardhi na yasiyo na tija kwa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi nitumie nafasi hii kuwakumbusha na kuwaomba wananchi kwa kushirikiana na uongozi wa Halmashauri za Wilaya husika, kuchukua hatua za makusudi kuandaa na kutekeleza mipango ya matumizi bora ya ardhi; hatua ambazo zitasaidia kuondoa changamoto za mahitaji ya ardhi katika Wilaya zote nchini ikiwa ni pamoja na Wilaya ya Sikunge iliyoko Mkoani Tabora.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Joseph Kakunda swali la nyongeza.

MHE. JOSEPH G. KAKUNDA: Mheshimiwa Mwenyekiti nashukuru kunipa nafasi. Niseme wazi kabla sijauliza maswali mawili ya nyongeza kwamba wananchi wa Sikunge wemesikitishwa sana na majibu ya Serikali. Ninayo maswali mawili ya nyongeza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kutumia takwimu za Ofisi ya Takwimu ya Taifa (*NBS*) za mwaka 2012 kama zilivyo ni sahihi, lakini je, Serikali haioni kuwa kutumia takwimu hizo bila kufanya *projections* kwa kutumia *formular* rasmi iliyo kwenye taarifa ya uchambuzi ya *NBS* inaweza kusababisha takwimu zisizo sahihi kwa mwaka 2017 na hivyo kusababisha Bunge hili pamoja na wananchi kuamini kuwa Serikali imelidanganya Bunge pamoja na wananchi? Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, kwa kuwa takwimu rasmi zilizoko kwenye Halmashauri yetu ya Wilaya ya Sikunge pamoja na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya, ambazo pia ndizo

alizonazo Mkuu wa Idara ya Maliasili wa Halmashauri inaonyesha kwamba kati ya kilometa za mraba 27,873 za Wilaya ya Sikonge, kilometa za mraba 26,834 ambayo ni sawa sawa na asilimia 96.3 ni hifadhi za misitu, wanyamapori, mapori ya akiba na maeneo mengine ya hifadhi ambayo yote hayo yako chini ya udhibiti na dhamana ya Kisheria ya Wizara ya Maliasili na Utalii. Je, wananchi tumebaki na kilometa za mraba elfu moja na thelathini na...

(Hapa sauti ilikatika)

MHE. JOSEPH G. KAKUNDA: ...hili la pili, Serikali itateua lini timu yake ije kufanya kazi na timu yetu Sikonge, ili kusudi tupate suluhisho la kudumu kuhusu takwimu hizo?

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tuwe tunaenda moja kwa moja kwenye maswali. Mheshimiwa Naibu Waziri Majibu.

NAIBU WAZIRI MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza, takwimu huwa zina chanzo, na mara nyingi unapokuwa unataka kunukuu takwimu ni lazima useme chanzo cha takwimu hizo yaani hizo takwimu ni kwa mujibu wa nani aliyezifanya. Takwimu zina mwenyewe na mwenye takwimu ni lazima awe ni mtu mwenye mamlaka na kwa Taifa hili takwimu ni mali ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali. Kwa hiyo, takwimu nilizozitumia kwa kuwa ni za Mtakwimu Mkuu wa Serikali sina shaka kwamba takwimu hizi ni sahihi na hizi ndizo takwimu zinazotakiwa kutumika

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kufanya *projections* kwamba ilitakiwa kuzitoa kutoka mwaka 2012 kuzileta leo, hiyo inaweza kuwa ni hoja, lakini ingekuwa ni hoja tu kama kweli hoja ya takwimu ingekuwa ni ya msingi kutoptana na swali la msingi lilitoloulizwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ifahamike kabisa kwamba nchi yetu ndio nchi inayoongoza duniani kwa kuwa na eneo kubwa lilitengwa kwa ajili ya uhifadhi kwa ajili ya wanyamapori, misitu na hifadhi nyingine. Sisi tumetenga

asilimia 25 ya eneo zima la nchi yetu, hiyo inatosha kutuma ujumbe kwamba ni kweli tumehifadhi maeneo makubwa. Lakini hatukufanya hivyo kwa makosa, tulifanya hivyo kwa sababu za msingi ambazo ndio zimekuwa zikitupa faida nyingi sana zinazotokana na uhifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, tunapozungumzia uhifadhi kwenye eneo la Sikunge ifahamike kabisa kwamba uhifadhi huo sio kwa ajili ya Sikunge. Kila eneo lilitohifadhiwa hapa nchini limehifadhiwa kwa maslahi ya Taifa. Eneo hilo litaweza kupitiwa pale ambapo kama Taifa tutaona kwamba kweli kuna haja ya kufanya mapitio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba nimuombe Mheshimiwa Mbunge, pamoja na kumpongeza kwamba yuko hodari wa kufuatilia masuala yanayohusu wananchi wake, na yeye atakumbuka vizuri kabisa kwamba mwanzoni mwa mwaka huu tulikuwa wote Sikunge, tumepita kwenye maeneo yake, nami napenda wananchi wa Sikunge wajue kabisa kwamba wanao jembe, Mbunge wao ni mfuatiliaji sana wa masuala yanayohusu wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini wakati huo huo nataka nimuombe kwamba atumie fursa hiyo ya kuwakilisha wananchi kwa kuwaambia ukweli kwamba akiba ni akiba na tunatakiwa kuyahifadhi maeneo yale kama akiba. Tutaweza kuyatumia pale tu itakapotokea kwamba kuna ulazima wa kuweza kufanya vinginevyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la Serikali kuteua timu, nirudie tu kwamba tayari timu ipo na iko kazini na inaendelea na kazi hiyo, kinachosubiriwa sasa hivi ni wao na ile kazi yao kukamilika na kuweza kuleta mrejesho Serikalini kwa ajili ya kuweza kupiga hatua kutekeleza masuala haya yanayohusiana na upitiaji upya wa kile ambacho tunacho hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la mwisho kabisa niseme kwamba kamwe Serikali haitaweza kufikia mahali ikaamua tu haraka haraka kuweza kuyaondoa maeneo

yaliyohifadhiwa kwa matumizi mengine bila kufanya tathmini ya kuangalia kwamba maeneo yasiyohifadhiwa yametumika kwa tija. Kwa hiyo, jambo la msingi ni kuhakikisha kwamba maeneo ambayo hatujahifadhi yanatumika kwa tija kwanza ndipo tuenze kugusa maeneo ambayo yamehifadhiwa kwa ajili ya akiba ya Taifa hili kwa ajili ya kizazi kijacho.

MWENYEKITI: Ahsante.

Waheshimiwa Wabunge maswali na majibu yetu yamekula muda mwangi wa shughuli nyingine za Bunge letu. Ninyi ni watu wazima mnanielewa ninachokisema. Ombi langu la kwanza, utulivu Bungeni. Leo kidogo Waheshimiwa Wabunge mnamashauriano, sijui yanahu nini. Mshauriane lakini kwa staha, hilo ndilo ombi langu.

Tangazo la wageni tulio nao hapa Bungeni, kwenye Jukwaa la Spika tuna wageni tisa ambaao ni Waheshimiwa Wabunge kutoka Bunge la Zambia. *Please be up standing, ambaao pia ni Wajumbe wa Kamati ya Miundombinu kutoka Bunge hilo. Walikuja kujuana na kufanya majadiliano na wenzetu wa Kamati yetu ya Miundombinu. (Makof)*

Niwatambue sasa Wabunge hao ni Mheshimiwa Douglas Syakalima, Mwenyekiti wa Kamati na kiongozi wa msafara, Mheshimiwa Robert Lihefu, Mbunge, Mheshimiwa Given Kituta, Mbunge, Mheshimiwa Anthony Mumba, Mbunge, Mheshimiwa Gift Sialubalo, Mbunge, Mheshimiwa Yizukanji Siwanzi, Mbunge, Mheshimiwa Gerald Zimba, Mbunge, Mheshimiwa Peter Daka, Mbunge na Ndugu Chitachu Mumba, Katibu wa msafara. Karibuni sana, *we are great to have you with us from our sister Parliament of the Republic of Zambia. (Makof)*

Wageni wengine wanne ambaao tunao hapa ni wageni wa Mheshimiwa Profesa Palamagamba Kabudi, Waziri wa Katiba na Sheria, ni wageni wanne ambaao ni Ndugu Amon Mpanju, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria, Jaji Kiongozi Mheshimiwa Jaji Ferdinand Wambali, karibuni sana. *(Makof)*

Pia tuna Jaji Mfawidhi Mheshimiwa Jaji Mwanaisha Kwariko, Jaji wa Mahakama Kuu, Jaji Latifah Mansoor; Mtendaji Mkuu wa Mahakama si mwingine ni ndugu yetu Hussein Katanga. Karibuni sana, tunajua leo mpo hapa kwa ajili ya shughuli kubwa. Hawa wameongozana na wakuu wa taasisi zilizo chini ya Wizara ya Katiba na Sheria ambao ni Wakurugenzi na Maafisa mbalimbali katika Wizara ya Katiba na Sheria. (*Makofi*)

Tuna mgeni wa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo ambaye ni Bi. Asha Ally Mabula, ambaye ni mshindi wa kwanza wa *Tanzania Miss Super Model* mwaka 2017 ambaye ataiwakilisha nchi yetu Tanzania katika mashindano ya *World Super Model* yatakayofanyika Mjini Macau, China tarehe 21 hadi 28 Mei, 2017. Yuko wapi? Huyo hapo! Tunakutakia kila la kheri katika jukumu hili kwako, lakini ni kwa Tanzania lakini pia. (*Makofi*)

Tuna wageni mbalimbali wa Waheshimiwa Wabunge na pia waliokuja kwa shughuli za mafunzo, hilo ni kundi la kwanza. Pia mkiangalia upande huu wa jukwaa la wageni mnaona lilivyopendeza leo. (*Makofi*)

Sasa hawa vijana ni askari polisi, mnaona sura mpya ya Jeshi sasa hivi, vijana *succession plan* inaanza namna hiyo na tutaendelea. Lakini ni wageni wa Mheshimiwa Waziri wetu wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Mwigulu Nchemba. Napenda tu ni wahakikishieni vijana, simameni mko Bungeni. (*Makofi*)

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Lissu pigi makofi!

MWENYEKITI: Tunashukuru, karibuni sana. Tutambua na tunathamini kazi nzuri mnayoifanya kwa niaba ya Taifa hili, endeleeni, kazeni buti. Waziri wenu ni Waziri mahiri sana na Waziri timamu sana. Karibuni, kaeni.

Nina matangazo, nianze na tangazo linatoka kwa Mheshimiwa Mwenyekiti Anna Lupembe, Mwenyekiti wa Ibada, anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kwa

Imani ya Kikristu kuhudhuria Ibada katika *chape*/iliyopo jengo la Pius Msekwa, ghorofa ya pili, leo siku ya Jumanne, tarehe 25 Aprili mara baada ya kusitisha shughuli za Bunge saa saba mchana. Aidha, wanamaombi ya Mkoa wa Dodoma na kwaya ya *New Jerusalem* watahudhuria ibada hiyo.

Tangazo la pili linatoka kwa Mheshimiwa William Ngeleja, Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club*. Anaomba awatangaziwe Waheshimiwa Wabunge kuwa kesho Jumatano tarehe 26 Aprili, 2016 kutakuwa na mechi ya kirafiki ya mpira wa miguu (*football*) na mpira wa pete (*netball*) kati ya Waheshimiwa Wabunge na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwenye uwanja wa Jamhuri hapa Dodoma katika sherehe za kutimiza miaka 53 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar.

Mechi hiyo ya Waheshimiwa Wabunge na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi itakayofanyika saa tisa alasiri itakuwa ni utangulizi kabla ya mechi kati ya timu ya Yanga na timu ya Polisi Dodoma. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge wote na wananchi mnaombwa kuhudhuria. (*Makofi*)

Tangazo la tatu, Mheshimiwa Mwenyekiti wa Umoja wa Wabunge Wanawake Tanzania (*TWPG*) Mheshimiwa Margret Sitta (Mbunge) anaomba niwatangazie Wabunge wanawake wote kuwa kesho tarehe 26 Aprili, 2017 kutakuwa na semina kwa ajili ya Wabunge wanawake wote itakayofanyika katika ukumbi wa zahanati ya zamani ya Bunge (*the old dispensary*). Semina hiyo itafanyika saa nane mchana, kwa hiyo mnakaribishwa.

Waheshimiwa Wabunge, hayo ndiyo matangazo tulio nayo. Baada ya hapo sasa tuanze mambo yetu.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiri, Mwongozo.

MBUNGE FULANI: Mwongozo.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiri, Mwongozo wa Spika.

MWENYEKITI: Si mniruhusu nikae.

MBUNGE FULANI: Si ndiyo tumekuruhusu Mheshimiwa.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)

MWENYEKITI: Mwongozo, naanza na Mheshimiwa Sitta.

MHE. MARGARET S. SITTA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi...

MWENYEKITI: Ngoja niorodheshe kwanzia! Mheshimiwa Chumi.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Msigwa.

MWENYEKITI: Huku wametosha mnaonaje tukichukua wawili wawili tu.

MHE. PASCAL Y. HAONGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Haonga.

MWENYEKITI: Ndiyo.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Msigwa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Msigwa.

MHE. PASCAL Y. HAONGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Haonga.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mheshimiwa Kuchauka.

MHE. PASCAL Y. HAONGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Haonga.

MWENYEKITI: Unajisemea tu wewe! Wawili wawili inatosha kwa leo. (*Kicheko*)

MHE. RAPHAEL J. MICHAEL: Mwongozo Mheshimiwa.

MWENYEKITI: Haya.

MHE. RAPHAEL J. MICHAEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Japhary.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)

MWENYEKITI: Basi kama ni hivyo tutende haki tu, Haonga.

MBUNGE FULANI: Eeh tenda haki tu, eeh Haonga eeh!

MHE. RAPHAEL J. MICHAEL: Japhary tayari!

MWONGOZO WA SPIKA

MWENYEKITI: Sasa tunaanza na Mheshimiwa Margaret Sitta. (*Makofi*)

MHE. MARGARET S. SITTA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi yakutoa mwongozo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, natumia kifungu 68, wakati huo nikielewa kwamba inawezekana mwongozo ninaotaka kutoa hauhusiani pengine na kanuni mojawapo maalum na wakati huo inawezekana pengine haihusiki moja kwa moja na matukio ya leo, lakini naomba mwongozo wako kuhusu Binti yetu Asha Ally Mabula aliyesimama hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba mwongozo kuhusu kumpongeza kwa dhati kwa nafasi

aliyopata, lakini kwa la pili ni kwamba, mwongozo wako utusaidie, binti amefanya vizuri, tuna haja ya kumpongeza kwanza; lakini la pili kumuwezesha aweze kusafiri ashiriki katika mashindano mengine. Kwanza atangaze jina la Tanzania, lakini pili ajiendeleze naye mwenywewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako ili wapendwa Waheshimiwa Wabunge kutokana na moyo waliounesha kwa *Serengeti Boys* tunaomba pia wamwoneshe huyu binti kwa kumchangia angalau si chini ya shilingi 30,000. Naomba mwongozo wako Mheshimiwa Mwenyekiti. Naomba kutoa hoja wenzangu mniunge mkono upande wote. (*Makof*)

MWENYEKITI: Haya, kaeni tu. Tunaendelea, Mheshimiwa Haonga.

MHE. PASCHAL Y. HAONGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba mwongozo wako kwa Kanuni ya 68(7) kuhusu jambo lilitokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, gazeti la leo la Mtanzania toleo namba 8526 limeeleza habari za kufukuzwa kwa Mkurugenzi Mkazi wa *UNDP* ambaye aliletwa na *UN*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkurugenzi huyu amefukuzwa ndani ya saa 24 na ameambiwa aondoke chini ya ulinzi mkali sana, na wanadai kwamba anaingilia mambo ya ndani ya Serikali ikiwa ni pamoja na suala la uchaguzi wa Zanzibar. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili naona linaweza kuleta shida kubwa sana. Watanzania ambao nchi yetu ni wanachama wa *UN*na suala hili la kumuondoa chini ya ulinzi mkali tumemu-harasssana. Suala hili linaweza kutuletea shida sana kidiplomasia. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kauli ya Serikali kuhusu suala hili ambalo limejitokeza kwa sababu binafsi nalionia kama litatuletea shida kama nchi yetu, na kwa kweli

linapokuwa linaharibika jambo ninaamini kabisa kwamba wanaoathirika ni nchi nzima, ni sisi Watanzania wote kwa ujumla. Ninaomba kauli ya Serikali kuhusu jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Mwongozo wako. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Japhary Michael.

MHE. RAPHAEL J. MICHAEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo wako kupitia Kanuni ya 68(7) ikienda na Kanuni ya 64(1)(d), kuhusu jambo ambalo linalotamkwa linaloweza likadhalilisha nafasi ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana wakati Mheshimiwa Waziri Ofisi ya Rais, TAMISEMI anajaribu kujibu Mwongozo uliotolewa na Mheshimiwa Kubenea kuhusu tatizo la Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya kujichukulia maamuzi dhidi ya watumishi walio katika ngazi zao katika Halmashauri na maeneo mengine yaliyo chini yao, Mheshimiwa Waziri alisema kwamba Wakuu wa Mikoa na Wilaya ni Marais wa Mikoa na Wilaya zile. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba Mwongozo wako, iwapo ni jambo sahihi kwa Wakuu wa Mikoa kuitwa Marais wa Mikoa yao, na kwamba ni sahihi kuvunja Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Mwongozo wako katika hili, na kama ni kosa, basi Mheshimiwa Waziri aombe radhi na ajirekebishe na asifanyie mzaha kitu cha Rais. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Chumi.

MHE. COSATO D. CHUMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mwongozo wangu Mheshimiwa Mama Sitta ameshaufilisi. Nakushukuru sana.

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Msigwa.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru. Mwongozo wangu nauomba kuitia Kanuni ya 64, lakini nitaisoma na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; 64.-{(1) Bila kuathiri masharti ya Ibara ya 100 ya Katiba yanayolinda na kuhifadhi uhuru wa mawazo na majadiliano katika Bunge, Mbunge:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 100 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania moja inasema; 100.-{(1) Kutakuwa na uhuru wa mawazo, majadiliano na utaratibu katika Bunge na uhuru huo hautavunjwa wala kuhojiwa na chombo chochote katika Jamhuri ya Muungano au katika Mahakama au mahali penginepo nje ya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na Ibara ya 59(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inasema kutakuwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, inaeleza pale. Namba 59(2) Mwanasheria Mkuu atateuliwa kutoka miongoni mwa watumishi wa umma wenye sifa ya kufanya kazi za uwakili au watu wenye sifa ya kusajiliwa kuwa wakili na amekuwa na sifa hizo mfululizo kwa muda usiopungua miaka kumi na tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namba mbili, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaainisha majukumu ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, na inasema; 59(3) Mwanasheria Mkuu atakuwa ndiye mshauri wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano juu ya mambo ya sheria na, kwa ajili hiyo, atawajibika kutoa ushauri kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano kuhusu mambo yote ya kisheria, na kutekeleza shughuli nyinginezo zozote zenye asili au kuhusiana na sheria zitakazopelekwa kwake au atakazoagizwa na Mheshimiwa Rais, na inamalizia pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni kumekuwa na mazoea au na utamaduni ambao Mwanasheria Mkuu wa Serikali ambaye namheshimu sana amekuwa akifanya kazi za *Chief Whip*. Katiba ya Jamhuri ya Muungano inamuelekeza kabisa majukumu yake ni yapi. Mwanasheria Mkuu wa Serikali hauwezi kutofautisha amesimama kama Waziri wa Sheria

au ni *Chief Whip*. Anaingilia hata mambo ya lugha, kwa mfano jana kisu cha ngariba nalo anataka tafsiri, hii sio kazi ya mwansheria! (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na ningekuomba wewe ni mtu uliyebobea katika sheria, una *authority* katika nchi hii na ulikuwa Mwanasheria Mkuu na Katiba inasema huyu Mwanasheria Mkuu anateuliwa kwa sababu anakuwa na uzoefu. Amekuwa mzoefu, Mabunge matatu yamepita, amewaona wanasheria wengine walivyokuwa wanafanya kazi hapa, ameyaona haya mambo yanavyofanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kitendo anachokifanya Mwanasheria katika Bunge hili; kwanza ye ye ni mshauri wa Serikali, anapaswa aishauri Serikali inapokosea inaleta miswada, kwanza anaishushia heshima ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ameaminiwa na Rais, sasa anafika mahali anashughulika mpaka na lugha, namna za uandishi. Kitendo anachokifanya Mwanasheria kina *cripple* Bunge na Bunge tunashindwa kujadili mambo ya msingi. Siku moja uliwahi kusema wewe mwenyewe Mheshimiwa Mwenyekiti kwamba tunatakiwa tuwe na wivu wa kulilinda Bunge letu, hapa ni mahali ambapo tunatakiwa tutoe mijadala, sisi kama wapinzani lakini matokeo yake anafanya kazi za *Chief Whip*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Mwongozo wangu, je, Serikali ina *Chief whip* wawili? Ili tujue *Chief Whip* ni yupi kwa sababu Mwanasheria hafanyi kazi ya Mwanasheria. Nimuombe Profesa Kabudi, anaheshima yake, ni mwanasheria aliyebobea katika nchi hii. Hebu tulinde heshima ya Bunge, mhimili huu tuulinde. Sheria zitungwe, zifanyike vizuri badala ya kufanya kazi kama anavyofanya kazi mwanasheria. (*Makofi*)

(*Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio*)

MWENYEKITI: Umeeleweka.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, mnapiga kelele huko *most of you are not bookish, you don't read, that's why you are making noise.* Haya mambo ni ya msingi, ya kulinda Bunge letu. Naomba Mwongozo wako.

MBUNGE FULANI: Inatosha.

(*Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Msigwa, mimi nimekupa nafasi, sasa unaanza kujibzana huko. Hapana, *please always address the chair.* Mheshimiwa Zuberi Kuchauka.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii...

MWENYEKITI: Kwani nimekosea jina lako?

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Nasimama kwa Kanuni ya 68(7) ikisomwa pamoja na 46(1) inayohusu kujibu maswali kwa ukamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nimejibiwa swalilangu hapa, swalilangu nyongeza namba (b) halikujibiwa kwa ukamilifu. Nilichokisema ni kwamba kesi hii imeisha 2007 na hukumu ikatolewa, wafanyakazi wale walipwe shilingi milioni 234.3, kwa hiyo kesi hii imeisha. Mheshimiwa Wazri anasema kwamba kesi hii iko mahakamani hawezikuongelea hapa, si kweli kwamba hii kesi iko mahakamani, kesi hii imekwisha mwaka 2007. Naomba Mwongozo wako. (*Makof*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru sana kwa maombi yenu ya Miongozo. Nianze na hili la Mheshimiwa Zuberi Kuchauka.

Majibu ya Serikali, mimi haya ninayo na ninyi mmeyasikia na yamechukuliwa vizuri na *Hansard*. Nadhani hoja hapa ndogo ni kwamba muuliza swalilangu anaamini kwamba kesi iliyokuwepo mahakamani ilikwisha. Serikali wanasema hawawezi kulisemea suala hilo kwa sababu lipo

mahakamani. Sasa tunataka tuupate huo ukweli. Nilikuwa nakutegemea wewe ungeenda zaidi kwa sababu ndiye mwenye swali, ndiye mwenye *data*. Ile hukumu ungekuwa nanakala yake ingesadia sana Serikali, kwamba ndiyo hii hapa, kesi ilishaisha, wananchi hawa waliokuwa watumishi wa *National Milling* wanastahili haki zao stahiki. Ndiyo hivyo hoja hiyo.

Mwongozo wangu ili tuokoe muda ni kwamba ipate basi hiyo nakala ya hukumu uikabidhi kwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango ili waone na tuanzie hapo sasa, maana tunatafuta haki za watumishi waliokuwa wa *National Milling*. Huo ndio Mwongozo wangu kwa hilo. Tusaidie tuipate kwa uhakika.

Mheshimiwa Msigwa, umetumia kifungu cha 64(1) na kukiunganisha na Katiba kwenye vifungu vyatuzi ya nafasi ya Mwanasheria Mkuu. Umevisema na ndiyo Katiba inavyosema. Nianze na hili la 64(1), maneno yale bila kuathiri masharti ya Katiba ambayo inasema uhuru wa mawazo na majadiliano.

Waheshimiwa Wabunge, unakisoma hicho kwanza, lbara ya 101 ya Katiba halafu unashuka kwenye lbara ndogo ya pili. Ninachotaka kuwaambia ni hivi; 64(1) inasema mna uhuru wote mpana kabisa wa kufanya majadiliano, kutoa kile ulichonacho ulichotumwa na wananchi humu Bungeni, lakini bila ya kuathiri Katiba. Katiba ile unakuta imekuwekea mipaka ile, lakini uhuru wako ni kwamba hayo uliyoyasema humu ndani huwezi ukaenda ukahojiwa au ukafikishwa mahakamani au kwenye chombo kingine kile. Huo ndio msingi wa maneno hayo.

Waheshimiwa Wabunge, lakini ukienda nje na ndiyo maana sasa nakuja; humu ndani lbara ya 89 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaliruhusu Bunge hili kutunga Kanuni na Bunge hili limeshatunga Kanuni hizo. Kuna makatazo fulani ukiwa ndani ya Bunge hili huwezi ukatumia kugha ambayo sio ya Kibunge. Huwezi ukatumia lugha ya kuudhi wenzako. Makatazo hayo yote yanatokana na Katiba. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, sasa tutumie vizuri vifungu hivi tunavyovisemea lakini nikija sasa kwa nafasi ya Mwanasheria Mkuu, mimi najua *Chief Whip* wa Serikali ni mmoja, lakini hakuna kinachomzuia Mwanasheria Mkuu, Waziri mwingine yejote wa Serikali kusimama na kutoa ufanuzi au maelezo kwa masuala yaliyo mbele ya Bunge wakati huo. Kwa hiyo, ndugu zangu, Mheshimiwa Msigwa mimi nakusihi sana, wewe ni Mbunge wa siku nydingi sasa humu. Kidogo tusiletie hisia kwa ofisi kama hii.

Mimi nakubali nimewahi kuwa kwenye nafasi hiyo kwa kipindi kirefu, tumefanya kazi na Bunge, lakini jamani tuwe na staha tunapo *address office* ya Mwanasheria Mkuu. Mwongozo wangu ni huo, anaweza akasimama wakati wowote kusaidia Serikali na hiyo haimfanyi kuwa *Chief Whip*. Tunachotaka ni sisi tuwe na uelewa mzuri wa Kanuni au Sheria za nchi kwa suala linalosemwa kwa wakati huo (*Makofii*)

Mheshimiwa Japhary Michael, najua umeniomba tu msamaha kwamba AG Mstaafu nisaidie maana yale ya jana yamepita. Lakini unasema kwa huruma yako. Mimi nasema Kanuni ya 68(7) ni jambo ambalo limetokea mapema siku hiyo, linaruhusiwa na Kanuni au haliruhusiwi. Sasa mimi nisingependa sana Bunge hili tulilingize katika hayo ambayo unayatafuta. Mimi naamini kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa madaraka ambayo ma-RC na ma-DC wamekasimiwa na Rais kwenye maeneo yao ya kiutendaji na ya kiusalama ni kamili, wanamwakilisha Rais katika eneo hilo. (*Makofii*)

Sasa yawezekana mtu akajifikiria kwamba yeje kwa sababu anamwakilisha Mheshimiwa Rais hapo kwa kipindi hicho yeje ni Rais, haiwezekani. Rais ni mmoja tu, lakini anatekeleza majukumu ambayo yamekasimiwa kwake na Rais. (*Makofii*)

Mheshimiwa Haonga, kwa heshima zote huu ni mhimili kamili, Bunge na Serikali ni mhimili kamili kama ilivyo Mahakama. Mhimili wa Serikali (Utawala) umeshaamua kuhusiana na huyu uliyemtaja kwa sababu inazofahamu

mhimili huo. Sisi hatuwezi tena kama mhimili kwenda kuanza kuhoji ni nini kifanyike, hatuendi hivyo. Haya masuala yatasimamia mahusiano yetu ya klimataifa, diplomasia itatumika kama kuna mtu atalalamika huo ndiyo utaratibu ambao utatumika, sisi hatufiki huko. Halafu nimalizie kwa kusema hivi, taarifa za magazeti sisi huwa hatutumii kufanya maamuzi, hapana; hatutumii magazeti kufanya maamuzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Sitta amelisemea vizuri sana suala la binti yetu Asha Ally Mabula. Hapa mezani nililetewa moja ya mionganoni mwa wageni alikuwepo amesimama, tumemtambua, mmepiga makofi sana. Sasa nilivyomuelewa Mheshimiwa Sitta, Mwongozo wake anaoniomba niufikishe kwenu kwa sababu ni tukio kubwa linalohusu nchi yetu kwenda kujitangaza nje kupitia binti huyu, amependekeza tumsaidie kumsafirisha anakoenda akaitangaze nchi yetu lakini na ye ye pia amependekeza iwapendeze Waheshimiwa Wabunge kama tulivyofanya huko siku za nyuma tuchangie. Amependekeza shilingi 30,000...

MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wana mafuriko majimboni kwao.

MWENYEKITI: ... mimi nilikuwa naomba... Ngoja nimalize basi. Tujenge heshima kidogo.

MBUNGE FULANI: Mnatuonea.

MWENYEKITI: Sasa mimi nilikuwa nasema, hebu tuwe na kamjadala dakika mbili, tatu tu kidogo. Mheshimiwa Sitta wewe ndiye ulianzisha hii. Dakika moja, unapendekeza shilingi ngapi?

MBUNGE FULANI: Michango imezidi jamani ah!

MHE. MARGARET S. SITTA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nisimame? Ahsante.

MWENYEKITI: Tuchukue watatu huku, na huku watatu. Hoja hapa iko wazi. Ngoja basi twende vizuri jamani.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, twende vizuri.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Tunahamia huku, Khatibu. Lissu...

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)

MWENYEKITI: Ally Saleh. Imetosha! Waheshimiwa Wabunge, Margaret Sitta anza.

MHE. MARGARET S. SITTA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima nawaomba Waheshimiwa Wabunge, najua tuna majukumu mengi sana lakini nimewaomba angalau si chini ya shilingi 30,000, sikusema nyingi. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge, tumpe nafasi binti ya kueneza na kutangaza jina la Tanzania.

MBUNGE FULANI: Hatutoi!

MHE. MARGARET S. SITTA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaomba pande zote mbili tuungane, si chini ya shilingi 30,000. Ahsante sana.

MBUNGE FULANI: Tuna mafuriko.

MBUNGE FULANI: Tupige kura.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, lazima tuliamue suala hili, nilitegemea ninyi sasa msimame muunge mkono hoja hii.

MHE. MARTHA M. MLATA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(Hoja ilitolewa lamuliwe)

MWENYEKITI: Eeh, imeungwa mkono. Tunaendelea Mheshimiwa Chumi.

MHE. COSATO D. CHUMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwanza kwa kuniona, naomba kuungana na Mheshimiwa Mama Margaret Sitta, walikuja hapa vijana wa *Serengeti Boys* ambao wamefuzu kwenda kwenye *AFC CON ya under 17* kule Gabon na tulikubaliana tukawachangia. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, juzi Ndugu Alphonse Simbu amekuwa namba tano katika *London Marathon*, hivi karibuni kwa jitihada zake binafsi alikuwa pia mshindi *Mumbai Marathon*. Mambo kama haya siyo kwamba tumemsaidia *individual*, mtu huyu anapokwenda kule anatuwakilisha kama Taifa, pia anatangaza Taifa na kwa kufanya hivyo anatusaidia kuvutia watalii ambao ni chanzo cha mapato ya Taifa. (*Makofi*)

MBUNGE FULANI: Hatutoi.

MHE. COSATO D. CHUMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tumuunge mkono Mama Sitta ni utamaduni wa kawaida kama tulivyofanya katika *football* na hiki pia ni kitu ambacho kinatangaza Taifa.

MBUNGE FULANI: Serikali itoe hela.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Martha Mlata. Waheshimiwa Wabunge, naomba utulivu.

MHE. MARTHA M. MLATA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niunge mkono hoja ya Mama Sitta, lakini naomba niseme jambo moja. Tuko hapa Bungeni, tumepata kadi nyingi na vikao vingi vya watu ambao wanahitaji tuwachangie kwenye harusi na watoto wao na mambo mengine na tunachanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili ambalo binti yetu anaenda kuliwakilisha Taifa, kwanza mimi kama Mama

ninajisikia vibaya sana kuona wanawake ndiyo wanaoongoza kупinga jambo la kumchangia binti yetu, ninasikitika sana. Naomba nitoe ushauri wale ambao hawahitaji kuchanga wanyamaze, wanaotaka kuchanga watachanga. Ahsante sana.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Tunachanga wote.

MBUNGE FULAN: CCM tutachanga wote.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Keissy.

MHE. ALLY K. MOHAMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, namuunga mkono moja kwa moja Dada yangu Mwenyekiti wa Mkoa wa Singida. Amesema kuchanga ni hiari, mwenye kutaka kuchanga achange, asiyetaka kuchanga asichange. Mchango ni hiari siyo lazima. Kwa hiyo, ndugu zangu hakuna mjadala zaidi, anayetaka kuchanga achange, asiyetaka asichange. siyo kulazimishana hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, anayetaka kuchanga achange na asiyetaka asichange. Mmojawapo ni mimi mwenyewe sichangi. (*Makofi/Kicheko*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, naomba utulivu. Kwanza muda siyo rafiki, Mheshimiwa Lissu.

MHE. JAMAL KASSIM ALI: Mheshimiwa Jamal.

MHE. TUNDU A. LISSU: Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni jambo jema sana, isipokuwa wananchi wa Jimbo langu wanakabiliwa na njaa kweli kweli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali hii imekataa katakata kutoa msaada wa chakula. Sasa kama kuna jambo linalohitaji kutolewa mchango ni suala la kuponesha watu wetu njaa. Haya mambo ya walimbwende yasubiri wakati wake na kama kuna watu wanafikiri ni jambo jema kuna Waziri ambaye amekabidhiwa mambo haya, mwalimu wangu wa sheria afanye kazi hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, binafsi sitakubali kukatwa hata senti kumi kwa ajili hii. (*Makof*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ally Saleh.

MHE. ALLY SALEH ALLY: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza nataka kuanza na mwenzetu mmoja hapa aliyesema kwamba yeze kama mzazi wa kike amesikia uchungu, imekuja *issue* ya Ben Saanane hapa uchungu mbona... (*Makof*)

(*Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa hebu jielekeze tu kwenye hoja tuliyonayo hapa.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Sipokei taarifa kutoka upande wowote.

MHE. JUMA S. NKAMIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa kidogo tu.....

MWENYEKITI: Hapana nimekataa, kaa chini tu.

MHE. ALLY SALEH ALLY: Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili tuna utamaduni mbaya sana hapa, kama alivyosema Mheshimiwa Lissu hili ni jambo jema, lakini hatuna *insafu* tukileta mambo mema mbona upande huu hatuangwi mkono! Kwa hiyo, nahisi kwamba *this is a cooperate world*, mkinipa mimi tu *challenge* ya siku moja tu *I can raise millions* kutoka kwenye mashirika ambayo yanafanya kazi ya ulimbwende, waachenii Wabunge washughulikie na mambo mengine. Ahsante. (*Makof*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Khatib wa mwisho.

MHE. KHATIB SAID HAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Namuunga mkono Mheshimiwa Keissy moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulishuhudia hapa timu yetu ya Bunge ilivyokwenda Mombasa ilivyorudi kwa dhiki na malori na Bunge hili halikufikiria kuichangia. Bunge hili halikufikiria kuichangia timu ile walirudi Mombasa kwa malori ya *lift*. Tukirudi imani yangu huu ni mwezi wa Rajab mwezi unaokuja ni mwezi wa Ramadhan...

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MHE. KHATIB SAID HAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Zanzibar hakuna mashindano ya warembo. Serikali ya Zanzibar imelikataa na hili linalokuja sasa kwa imani yetu ya kidini ni dhambi kubwa kumchangia yule dada aende kuwakilisha hili.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MHE. KHATIB SAID HAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, dini yetu inatusuta na nafsi zetu zinatusuta. Aliposimama pale wengine tulianamia mivunguni, hatukuweza kumwangalia, kwa imani yetu ya kidini inavyotusuta. (*Makofi/Kicheko*)

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, tusaidie huku.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge lazima mheshimu...

MHE. JUMA S. NKAMIA: Hilo povu lote ni kwa sababu ya shilingi 30,000 tu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuhusu taarifa.

MWENYEKITI: Nimeshasema, sijakuruhusu kuongea Mheshimiwa.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Nkamia kaa chini.

MWENYEKITI: Nimeikataa sipokei taarifa.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Umenisahau kwenye...

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, huo ndio mjadala, kwa hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Margaret Sitta, kwa pendekazo la kumchangia huyu binti yetu

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwachangii walimbwende.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, sasa hoja yoyote lazima iamuliwe..

MBUNGE FULANI: Hatutaki.

MWENYEKITI: Ndio, lazima niitoe kwenu.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)

MBUNGE: Dhambi, dhambi.

MHE. ALLY K. MOHAMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, ukikata hela tutaenda mahakamani mzee.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, unataka kulazimisha.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, naomba tusikilizane, sitaki kuwataja ninaowaona sasa.

Mimi nimetumia Kanuni ili suala hili likae vizuri, haturuhusiwi kuanzisha mjadala, soma Kanuni ya 53, ndiyo maana nimemruhusu atoe hoja iungwe mkono. Sasa nawahoji wanaoafiki pendekazo la mtoa hoja kwamba kila Mbunge achangie si chini ya shilingi 30,000 waseme ndiyo.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, hatukubali.

(Hoja ilitolewa lamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, ninaamini walioafiki wameshinda.

(Hoja ya pendekezo la Mheshimiwa Margaret S. Sitta la kila Mbunge kuchangia shilingi 30,000 lilikubaliwa na Bunge)

MHE. ALLY K. MOHAMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango ni hiari, haikubaliki hata kidogo hiyo, tutakwenda mahakamani.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Wasanii mnawatumia kwenye kampeni hamtaki kuchanga. Profesa Jay unawaona wenzako?

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, naomba utulivu, tumeshaamua mengine ni utekelezaji. Katibu.

NDG. LAWRENCE MAKIGI-KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 - Wizara ya Katiba na Sheria

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamwita mtoa hoja, nimeletewa tangazo hapa na Mheshimiwa Ngeleja, Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club* akinifahamisha kwamba kwenye *gallery* ya Spika tutambue uwepo wa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, wachezaji wa *football*/*netball* ambao wameingia sasa, karibuni sana. Nadhani mmekuja kwa matumaini ya ushindi lakini michezo ni furaha, afya, pia hii timu ya Bunge ni kazi, karibuni sana. *(Makof)*

Waheshimiwa wabunge, tunaendelea na mtoa hoja Waziri wa Katiba na Sheria, Profesa Kabudi una saa moja.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia taarifa zilizowasilishwa leo katika Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako sasa likubali kupokea, kujadili na kupitisha mpango wa makadirio ya mapato na matumizi ya fedha ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniruzuku uhai na kunijalia afya njema kuweza kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha mpango na makadirio ya bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha napenda kutoa shukrani nydingi kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, kwa heshima kubwa aliyonipa kwa kunteua kuwa Mbunge na kushika wadhifa wa Waziri wa Katiba na Sheria. Kutokana na heshima hiyo, ninaahidi kuitumikia nafasi hii kwa hekima, uadilifu na uaminifu kwa kadri alivyonijalia Mwenyezi Mungu. Vivyo hivyo, ninaahidi kuwatumikia wananchi wote wa Tanzania bila kuwabagua kwa dini zao, rangi zao, kabilia zao, vyama vyao, itikadi zao kwa kuwa wao ndio msingi wa mamlaka yote ya Serikali kwa mujibu wa Katiba ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa masikitiko makubwa nakupa pole wewe na Bunge lako Tukufu kwa kuondokewa na Wabunge wenzetu waliotangulia mbele ya haki, ambao ni Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir aliyekuwa Mbunge wa Jimbo ka Dimani CCM na Mheshimiwa Dkt. Elly Marko Macha aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum - CHADEMA. Pia, natoa pole kwako na Watanzania wote, ndugu, jamaa na marafiki kutoka na kifo cha Mheshimiwa Samuel John Sitta aliyekuwa Spika wa Bunge la Kumi la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nitumie fursa hii kuwapa pole ndugu, jamaa na marafiki pamoja na wananchi walioguswa na misiba hii kwa namna moja au nyingine, Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi, Amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimpongeze Mheshimiwa Spika kwa uongozi wake mahiri wa kuliongoza Bunge letu na hivyo kudhihirisha uwezo na uzoefu alionao wa kuwatumikia Watanzania kuititia chombo hiki. Aidha, nitumie fursa hii kumpongeza Naibu Spika, Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson Mwansasu na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kuendelea kutekeleza majukumu yao vema kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nampongeza Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mbunge), kwa hotuba yake nzuri ambayo imetoa mwelekeo wa kisera katika utekelezaji wa shughuli za Serikali kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2017/2018. Vilevile nampongeza kwa uongozi wake thabiti katika kusimamia vema shughuli za Serikali ndani na nje ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niruhusu sasa niwapongeze Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Mohamed Omary Mchengerwa, Mbunge wa Rufiji na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia, Mbunge wa Mtwara Vijijini, kwa kuziongoza vema Kamati zao. Maoni na ushauri wao umekuwa ni msaada mkubwa kwa Wizara yangu katika kutekeleza majukumu yake na kuwashudumia Watanzania. Napenda niwahakikishie kuwa Wizara yangu inayo imani kubwa katika uongozi wao na itaendelea kuwapatia ushirikiano unaostahili katika kipindi watakachokuwa katika nyadhifa hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia natoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati hizo kwa kazi kubwa ya kuchambua mpango na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Mfuko wa Mahakama kwa mwaka wa fedha 2017/2018. Hakika tunatambua na kuthamini mchango wa Kamati hizi katika kuhakikisha kuwa sekta ya sheria inabaki kuwa kiungo muhimu kwa maendeleo ya nchi yetu kiuchumi, kijamii, kisiasa, kimazingira na kiteknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niruhusu sasa niwapongeze Wabunge wenzangu wote wa pande zote mbili za Bunge hili kwa heshima waliyopewa ya kuwa Wabunge wa Bunge lako Tukufu. Kwa namna ya pekee natoa pongezi zangu zadhati kwa Mheshimiwa Abdallah Majurah Bulembo (Mbunge), Mheshimiwa Anna Kilango Malecela (Mbunge), Mheshimiwa Juma Ali Juma (Mbunge), Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete (Mbunge) na Mheshimiwa Getrude Pangalile Rwakatare (Mbunge), kwa heshima kubwa waliyopewa ya kuitumikia Taifa letu kupitia chombo hiki kitukufu. Binafsi, ninawatachia heri na baraka za Mwenyezi Mungu katika kutekeleza majukumu yao ya Ubunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue pia fursa hii kwa sababu ni mara yangu ya kwanza nasimama katika Bunge hili kuwashukuru wazazi wangu, kuishukuru familia yangu, kuwashukuru walimu wangu na wahadhiri wote ambao wamenifikisha katika nafasi hii ambayo leo ninayo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, dira ya Wizara ya Katiba na Sheria ni kuwa na Katiba na sheria wezeshi, kwa maendeleo ya Taifa. Madhumuni ya dira hii ni kuweka mazingira rafiki kisera na kisheria ya kuwezesha utekelezaji wa mpango wa maendeleo ya Taifa, kudumisha hali ya amani, utulivu na utengamano wa Kitaifa ambavyo vimeendelea kuwepo nchini. Aidha, dhima ya Wizara ni kuwa na mfumo madhubuti wa Kikatiba na kisheria katika kufanikisha mipango ya maendeleo ya Taifa. Dhima hii inahimiza kufanya kazi kwa weledi na ubunifu katika kuhakikisha kunakuwepo mazingira rafiki ya upatikanaji wa huduma muhimu za kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Katiba na Sheria inajumuisha Mahakama ya Tanzania, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Tume ya Utumishi wa Mahakama, Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini, Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo na Chuo cha Uongozi wa Mahakama - Lushoto. Kwa pamoja tumeendelea kutekeleza majukumu yetu ya kuwahudumia wananchi kwa kutoa huduma mbalimbali za kisheria na kuhakikisha kuwa

wananchi wanaifikia na kupata haki kwa wakati wanapoitafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu inayo wajibu wa kuhakikisha kuwa nchi inaongozwa kwa kuzingatia Katiba, sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa na vyombo halali na kwamba haki inaendelea kutawala katika jamii wakati wote. Hivyo, kwa kutambua wajibu huo Wizara yangu imeendelea kutekeleza majukumu yake kama yalivyo kwenye hati ya mgawanyo wa majukumu kwa Mawaziri (*Instrument*), iliyotolewa kuititia Tangazo la Serikali Na. 144 la tarehe 22 Aprili, 2016 ambayo ni kama ifuatavyo:-

- i. Kuweka sera kuhusu masuala ya sheria na utekelezaji wake;
- ii. Kushughulikia masuala ya katiba;
- iii. Kusimamia haki na mfumo wa utoaji haki;
- iv. Uandishi wa sheria;
- v. Uendeshaji wa mashtaka;
- vi. Kushughulikia mashauri ya madai, usuluhishi, mikataba na sheria za kimataifa;
- vii. Kushughulikia masuala ya haki za binadamuna msaada wa kisheria;
- viii. Kusimamia na kufanya utafiti wa maboresho ya sheria;
- ix. Kushughulikia urejeshwaji wa wahaalifu na kuendeleza ushirikiano na mataifa mbalimbali kwenye makosa ya jinai;
- x. Kusajili matukio muhimu ya binadamu yanayohusu vizazi, vifo, ndoa, talaka, na uasili wa watoto; pamoja na kusimamia masuala ya ufilisi na udhamini;

xi. Kuboresha utendaji na maendeleo ya rasilimali watu katika Wizara; na

xii. Kuratibu shughuli za taasisi, mipango na miradi ya maendeleo chini ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2016/2017 Wizara yangu ilipanga na kutekeleza majukumu yake kwa kubainisha maeneo mahsus i ya kipaumbele yafuatayo:-

(i) Kuimarisha usimamizi na uratibu wa mfumo wa sheria;

(ii) Kuanzisha *Division* ya Mahakama Kuu ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi;

(iii) Kuimarisha mfumo wa haki na utoaji haki;

(iv) Kuimarisha usimamizi wa miradi ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya Mahakama na Taasisi nyingine zilizo chini ya Wizara yangu;

(v) Kuimarisha matumizi ya mfumo wa kielektroniki ya kutunza kumbukumbu na nyaraka muhimu pamoja na kutolea huduma;

(vi) Kuimarisha shughuli za utafiti na uboreshaji wa sheria nchini;

(vii) Kuimarisha uandishi na urekebu wa sheria za nchi;

(viii) Kuboresha mazingira ya kufanyia kazi, maendeleo na ustawi wa watumishi;

(ix) Kuimarisha mfumo wa mafunzo ya uwanasheria kwa vitendo kwa kuongza udahili wa wanafunzi na kupanua wigo wa utoaji wa huduma;

(x) Kuimarisha upatikanaji wa msaada wa kisheria kwa watu wasio na uwezo; na

(xi) Kuimarisha shughuli za usajili wa matukio muhimu ya binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia vipaumbele hivyo Wizara ilianda na kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Mpango na Bajeti na kuitishwa kwa utekelezaji. Kwa heshima na taadhima naomba sasa uniruhusu kuwasilisha mbele ya Bunge hili taarifa kuhusu hatua mbalimbali zilizochukuliwa katika kutekeleza mpango na bajeti kwa mwaka wa fedha 2016, mafanikio yaliyopatikana na changamoto mbalimbali ambazo Wizara ilikabiliananazo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, maandalizi ya Sera ya Taifa ya Sheria; Wizara iliendelea na juhudzi za kuandika sera mahsus kuhusu masuala ya sheria kwa kuandaa Rasimu ya Taifa ya Sheria ambayo kwa sasa inajadiliwa na makundi mbalimbali ya wadau ili kutoa fursa kwa Wizara kukusanya maoni yatakayofanya sera hiyo kukidhi mahitaji ya sasa ya sekta ya sheria na Taifa kwa ujumla. Ni matarajio yangu kwamba Serikali ikishapitisha sera hii na kuanza kutumika itakuwa ni hatua muhimu katika kuimarisha usimamizi na utekelezaji wa mfumo wa sheria nchini kwa maendeleo ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu tathmini ya hali ya utekelezaji wa sheria nchini; Wizara ya Katiba na Sheria inayo dhamana ya kuimarisha na kusimamia Mfumo wa Sheria Nchini. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2016/2017 Wizara ilifuatilia utekelezaji wa sheria mbalimbali kupitia Wizara, Idara, Wakala na Mamlaka nyingine za Serikali ili kutathmini hali ya utekelezaji wa sheria nchini. Kukamilika kwa zoezi hili kutaiwezesha Wizara kutoa mwongozo wa namna ya kuimarisha mfumo wa sheria nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sera na makubaliano ya kimataifa ya kikanda; kwa muda mrefu nchi yetu imekuwa mwanachama wa taasisi mbalimbali za Kikanda na

Kimataifa kupitia Umoja wa Mataifa, Umoja wa Afrika, Jumuiya ya Nchi za Kusini mwa Afrika (*SADC*), Jumuiya ya Afrika Mashariki na nyinginezo. Kupitia taasisi hizo Tanzania imeendelea kuridhia sera, malengo na mipango ya maendeleo inayopitishwa na taasisi husika ikiwemo:-

(a) Malengo ya Maendeleo Endelevu (*Sustainable Development Goals*):

(b) Mpango wa Maendeleo wa Afrika; na

(c) Mpango wa Kazi wa Afrika Kugharimia Shughuli za Maendeleo (*The Addis Ababa Action Agenda*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua wajibu ilio nao katika kufanikisha makubaliano hayo, Wizara yangu imefanya uchambuzi wa maeneo muhimu na kuweka mikakati ya kuiwezesha kutekeleza vyema wajibu huu wa wakimataifa sanjari na mipango ya ndani ya sekta. Kutohana na uchambuzi huo Wizara imebainisha maeneo lengwa (*thematic areas*) manne ambayo kwa namna moja au nyingine yanaakisi Malengo ya Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano na pia Mpango Mkakati wa Wizara. Maeneo hayo ni upatikanaji wa haki kwa wote na utawala wa sheria, amani na ushirikishwaji wananchi kwa maendeleo endelevu, usawa wa kijinsia na haki za binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu haki na mfumo wa utoaji haki; Katiba imeipa mamlaka Mahakama ya Tanzania kuwa ndicho chombo pekee cha utoaji haki nchini. Katika kuhakikisha kuwa chombo hiki kinatekeleza majukumu yake ipasavyo na kwa ufanisi, sheria zimeweka mfumo rasmi wa utatuzi wa migogoro unaojumuisha mfumo wa upelelezi wa makosa ya jinai, uendeshaji wa mashitaka, ushirikishaji wa mashauri pamoja na mifumo ya usuluhishi.

Hivyo, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2016/2017 Serikali ilichua hatua madhubuti za kuimarisha mfumo wa utoaji haki nchini kwa kuanzisha Divisheni ya Mahakama Kuu

ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi kuharakisha usikilizaji wa mashauri na ujenzi wa miundombinu muhimu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Divisheni ya Mahakama Kuu ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi. Katika kipindi hicho Wizara imetekeleza kwa vitendo azma ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, ya kupambana na rushwa na ujisadi nchini kwa nguvu zote kwa kuanzisha Divisheni ya Mahakama Kuu ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi. Divisheni imeanza kufanya kazi katika majengo yaliyopo kwenye Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo na kwamba kila Kanda ya Mahakama Kuu ni Masjala Ndogo ya Divisheni hiyo. Hatua muhimu zilizochukuliwani pamoja na kufanya marekebisho ya sheria na kuandaa kanuni za uendeshaji wa mahakama, kufanya ukarabati wa majengo, ununuzi wa vifaa, kuajiri na kutoa mafunzo kwa watumishi wa divisheni. Hadi sasa divisheni hiyo imeweza kusajili jumla ya maombi 25, kati ya hayo 20 yamesajiliwa Dar es Salaam, matatu Mtwara, moja Iringa na moja Tabora. Aidha, kati ya maombi 25 yaliyosajiliwa maombi 13 yametolewa uamuzi na mengine yanaendelea kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usikilizaji wa mashauri Mahakamani; mwaka 2016 Mahakama ya Tanzania ilianza na jumla ya mashauri 59,477 na kusajili mashauri mapya 276,147. Mashauri yaliyoamuliwa katika kipindi hicho yalikuwa 278,226 sawa na asilimia 83 ya wastani wa uwezo wa kumaliza mashauri yote yaliyokuwepo. Mafanikio hayo yalitokana na Mahakama kuendelea kubuni na kutekeleza mikakati mbalimbali ikiwemo kufanya kazi kwa malengo na kupima utendaji kazi wa Majaji na Mahakimu. Pia Mahakama ya Tanzania imeendelea kusisitiza matumizi ya njia mbadala za utatuzi wa migogoro na kuimarisha ushiriki wa wadau katika kubuni na kutekeleza mikakati ya kuharakisha usikilizaji wa mashauri. Maelezo ya ufanuzi kuhusu usikilizaji wa mashauri ni kama yaliyvo kwenye kiambatisho namba moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia matokeo ya

Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015 yalifunguliwa jumla ya mashauri 53 yaliyohusu nafasi ya Ubunge, mashauri 196 ya nafasi za Udiwani. Hadi kufikia mwezi Machi, 2017 mashauri 52 ya Ubunge yaliyamuliwa hivyo kubaki na shauri moja na kwamba hivi sasa kuna rufaa mbili katika Mahakama ya Rufani kupinga uamuzi wa Mahakama Kuu. Aidha, mashauri yote ya Udiwani yalisikilizwa na kuamuliwa katika kipindi kilichowekwa kwa mujibu wa sheria yaani mwaka mmoja kwa mashauri ya Ubunge na miezi sita kwa mashauri ya Udiwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ni mafanikio makubwa na ya kihistoria kuwahi kufikiwa kwa mashauri ya uchaguzi kusikilizwa na kutolewa uamuzi ndani ya muda uliowekwa kisheria. Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ilitoa mchango mkubwa kwa kusimamia uendeshaji wa mashauri hayo mahakamani ambapo katika mashauri yote isipokuwa shauri moja Serikali ilipata ushindi.

Aidha, katika kuhakikisha kuwa tunaimarisha uwezo wa Serikali kushughulikia kesi za uchaguzi, Mahakama ya Tanzania kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo (*UNDP*) ilitengeneza vitabu vitatu ambavyo ni kijitabu kinachoeleza utaratibu na mienendo iliyotumika katika kuendesha kesi za uchaguzi, ripoti kuhusu namna Mahakama zilivyoshughulikia kesi za uchaguzi na mafunzo yatokanayo na mkusanyiko wa sheria na kanuni za uchaguzi. Vitabu hivi vilikabidhiwa kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwa Mheshimiwa Spika tarehe 2 Februari, 2017 wakati wa maadhisho ya siku ya sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la miundombinu ya Mahakama; Mahakama ya Tanzania imeendelea na utekelezaji wa mikakati ya kuboresha huduma za Mahakama ikiwa ni pamoja na kufanya ujenzi na ukarabati wa Mahakama mbalimbali nchini. Hadi kufikia mwezi Machi 2017, Mahakama ya Tanzania ilikamilisha ukarabati wa majengo ya Mahakama Kuu Dar es Salaam na Tanga na kuendelea na ukarabati wa Mahakama Kuu Kanda ya Mbeya unaotarajiwaa kukamilika hivi karibuni.

Aidha, Mahakama ya Tanzania imekamilisha ujenzi wa Jengo la Mahakama ya Hakimu Mkazi Pwani na Mahakama ya Wilaya Kibaha na inaendelea na ujenzi wa Mahakama za Wilaya za Bagamoyo, Mkuranga, Kigamboni, Kinyerezi na Mahakama ya Mwanzo Kawe ambazo zipo katika hatua mbalimbali za ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukabiliana na changamoto ya miundombinu, Mahakama kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Ardhii na Baraza la Taifa la Ujenzi ilifanya utafiti wa teknolojia ya gharama nafuu ya ujenzi wa majengo ambapo teknolojia ya moladi imeonesha unaafuu wa gharama, kupunguza muda unaotumika kwenye ujenzi na ubora wa majengo. Kwa kutumia teknolojia hii Serikali imeweza kuokoa takribani asilimia 50 ya gharama za ujenzi ambazo zingetumika kwa kutumia teknolojia ya kawaida. Chini ya utafiti huu Mahakama za Mwanzo sita zimejengwa ambazo ni Mahakama ya Hakimu Mkazi Pwani na Hakimu ya Wilaya Kibaha, Mahakama za Wilaya za Bagamoyo, Kigamboni, Mkuranga na Kinyerezi pamoja na Mahakama ya Mwanzo Kawe. Ni dhahiri kuwa kutohana na uzoefu uliopatikana katika mradi huu, Wizara itaweza kutumia teknolojia hiyo ya moladi katika maeneo mengine ya nchi kwa gharama nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hatua nyingine Mahakama ya Tanzania imeanza kazi ya kukamilisha ujenzi wa Mahakama ya Mkoa wa Manyara na Mahakama za Mwanzo za Iguguno – Mkalama, Waso – Ngorongoro, Magoma – Korogwe, Bereko – Kondoa, Karatu Mjini – Karatu, Mvomero – Mvomero, *Old Korogwe* – Korogwe na Kilwa Masoko – Kilwa, ambazo ujenzi wake ulisimama kwa muda mrefu kutohana na ukosefu wa fedha. Aidha, Mahakama ya Tanzania imeendelea kuimarisha shughuli za usimamizi na ukaguzi wa Mahakama kwa kununua na kusambaza jumla ya nakala 650 za vitabu vya mwongozo wa ukaguzi katika Mahakama mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uandishi wa sheria, Wizara yangu imechukua hatua mbalimbali za kuhakikisha

kuwa sheria za nchi zinakuwa ni nyenzo ya kuharakisha maendeleo katika nyanja za kiuchumi, kijamii, kisiasa, kiutamaduni, kimazingira na kiteknolojia kupitia sera na mipango mbalimbali ya maendeleo. Hivyo, katika mwaka wa fedha 2016/2017, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali iliratibu maandalizi ya Miswada 12 ya sheria iliyowasilishwa na kujadiliwa Bungeni, kutokana na Miswada hiyo sheria mbalimbali zilitungwa ikiwa ni pamoja na Sheria ya Haki za Kupata Taarifa na Sheria ya Msaada wa Kisheria ambazo ziko chini ya usimamizi ya Wizara yangu pamoja na Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 03 ya mwaka 2016 na Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 04 ya mwaka 2016 na Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 01 ya mwaka 2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la uendeshaji wa mashtaka, Mkurugenzi wa Mashtaka aliendelea kuratibu shughuli za upelelezi wa makosa ya jinai, kufungua na kuendesha mashauri Mahakamani. Katika kipindi cha Julai 2016 hadi Machi 2017 kulikuwa na jumla ya mashauri ya jinai 31,723 yaliyoendeshwa katika Mahakama mbalimbali nchini. Kati ya hayo, mashauri 14,732 sawa na asilimia 46 yalitolewa uamuzi na Mahakama na mengine 16,991 yanaendelea kusikilizwa. Aidha, kulikuwa na mashauri matano yanayohusu urejeshaji wa mali zilizotokana na uhalifu yaliyokamilika kusikilizwa na fedha taslimu shilingi 439,628,000 kurejeshwa Serikalini ikiwa ni pamoja na nyumba nane, magari 25, pikipiki 10, boti nane na viwanja vinne. Aidha, jumla ya shilingi 1,110,893,995 zililipwa kama faini kutokana na mashauri hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi, 2017 kulikuwa na mashauri 463 ya ujangili, kati ya hayo mashauri 158 yalihitimishwa kwa wastani, kutiwa hatiani na kupewa adhabu za vifungo na kulipa faini ya shilingi milioni 811 taslimu. Aidha, kulikuwa na mashauri 9,813 ya dawa za kulevyaa yakiwemo mashauri 161 yanayohusu kiwango kikubwa cha dawa za kulevyaa ambapo mashauri tisa kati ya hayo yalihitimishwa. Katika mashauri yaliyohitimishwa washtakiwa 13 walihukumiwa vifungo vya kati ya miaka 20 na maisha jela.

Aidha, kilo 279 za dawa za aina ya *cocaine* na *herion* na kilo 21 za mirungi zilitketezwa kwa amri ya Mahakama. Pia Mkurugenzi wa Mashtaka alipokea jumla ya majalada 510 ya tuhuma za rushwa kutoka TAKUKURU yakiwemo majalada mapya 306 na 204 yaliyorejeshwa tena baada ya uchunguzi zaidi. Kati ya hayo, majalada 201 yaliandaliwa hatiza mashtaka, majalada 136 yalirejeshwa TAKUKURU kwa hatua zaidi za uchunguzi, majalada 168 yanaendelea kufanyiwa uchambuzi wa kisheria na mengine matano yalifungwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uendeshaji wa mashauri ya madai, Katiba na haki za binadamu; Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali iliendesha jumla ya mashauri 984 ya madai yanayohusisha Serikali katika Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufani yakiwemo mashauri 883 ya zamani na mashauri 101 mapya. Kati ya hayo, mashauri 11 yalitolewa uamuza na mashauri mengi 973 yanaendelea kusikilizwa. Serikali ilishinda katika mashauri tisa na kushindwa katika mashauri mawili. Kutokana na mafanikio hayo Serikali iliweza kuokoa takribani shilingi bilioni 23.75 sawa na asilimia 99.87 ya fedha zinazodaiwa katika mashauri yalioisha. Vilevile kulikuwa na maombi 48 mapya na 277 ya zamani na hivyo kufanya maombi yote kuwa 325. Kati ya hayo maombi 12 yamehitimishwa na maombi 313 yanaendelea kusikilizwa. Rufani za madai zilizokuwepo ni 59 ikiwemo rufani moja mpya na zote zinaendelea kusikilizwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na jumla ya mashauri mapya 32 ya Kikatiba yaliyofunguliwa kwenye Mahakama Kuu ya Tanzania na kufanya jumla ya mashauri yaliyokuwepo kuwa 164 yakiwemo mashauri 132 ya zamani ambapo mashauri 19 yalihitimishwa na kubaki mashauri 145. Katika Mahakama ya Rufani kulikuwa na rufaa saba ambazo zinaendelea. Aidha, katika Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu (*The African Court on Human and Peoples Rights*) kulifunguliwa jumla ya mashauri 104, kati ya hayo mashauri 40 ni mapya na 64 ni ya zamani na yanaendelea kusikilizwa, hali kadhalika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali iliendesha jumla ya mashauri sita katika Mahakama

ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (*The East African Court of Justice*), kati ya hayo, shauri moja lilmalizika na mashauri mengine matano bado yanaendelea kusikilizwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uhakiki wa mikataba na usimamizi wa sheria za kimataifa; Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali iliendelea kutoa ushauri wa kisheria kwenye mikataba na makubaliano mbalimbali ambapo katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi, 2017 ilifanya upekuzi na uhakiki wa jumla ya mikataba 1,473 yenye thamani ya shilingi triliioni 12.6, kati ya hizi ilihuisha mikataba ya ununuzi, ukarabati wa majengo, ujenzi wa barabara na hati za makubaliano (*MOU*) kutoka Wizara, Idara na Taasisi za Serikali na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Vilevile katika ngazi ya Kikanda na Kimataifa ofisi hii ilishiriki katika mikutano 86 ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, Jumiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika na Umoja wa Mataifa illyojadili masuala ya sheria na sera za sekta mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu haki za binadamu na msaada wa kisheria, usimamizi na hifadhi ya haki za binadamu; Wizara iliendelea kuimarisha na kusimamia utekelezaji wa haki za binadamu kama ilivyoainishwa na kuhifadhiwa katika Katiba na sheria za nchi. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2016/2017 Wizara iliandaa taarifa ya nchi kuhusu utekelezaji wa haki za binadamu iliyowasilishwa kwenye Baraza la Haki za Binadamu la Umoja wa Mataifa chini ya Mfumo wa Umoja wa Mataifa wa Mapitio kwa Kipindi Maalum (*The Universal Periodic Review Mechanism*). Taarifa hiyo ilijadiliwa kwenye vikao vya 25 na 33 vya Baraza la Haki za Binadamu vilivyofanyika Geneva, Uswis kati ya Mei na Oktoba, 2016. Kupitia taarifa hiyo Serikali ilipata fursa ya kufafanua mbele ya Jumuiya ya Kimataifa kuhusu hali ya utekelezaji wa haki za binadamu nchini na kutoa msimamo wa nchi kuhusiana na mapendekezo mbalimbali yaliyotolewa na Baraza la Haki za Binadamu wakati wa kujadiliwa kwa taarifa ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ilifuatilia na kutoa ushauri kwa Serikali na

taasisi zake kuhusu utekelezaji wa haki za binadamu na misingi ya utawala bora nchini. Hii ni pamoja na kufanya ufuatiliaji wa haki za binadamu kwa watu walio katika makundi yenye mahitaji maalum, haki za mahabusu na wafungwa, kufanya uchunguzi wa tuhuma za uvunjaji wa haki za binadamu na ukiukaji wa misingi ya utawala bora na kutoa elimu ya haki za binadamu na utawala bora kwa jamii. Katika kipindi hicho Tume ilitembelea jumla ya magereza 41 katika Mikoa 15 ya Arusha, Kilimanjaro, Mbeya, Dar es Salaam, Tanga, Mtwara, Lindi, Pwani, Manyara, Mara, Kigoma, Mwanza, Iringa, Singida na Dodoma. Pia Tume ilikagua vituo vya polisi 59, mahabusu za watoto tano na shule ya maadilisho ili kujiridhisha na utekelezaji wa haki za binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ilipokea na kufanya uchunguzi wa malalamiko 7,101 yanayohusu ukiukwaji wa haki za binadamu na kuhitimisha uchunguzi katika malalamiko 1,443 ambapo malalamiko mengine 5,658 yanaendelea kuchunguzwa. Baadhi ya malalamiko yalihusu kubambikiziwa kesi, ucheleweshaji wa upelelezi, uendeshaji wa mashauri mahakamani, utoaji wa nakala za hukumu na utekelezaji wa amri za Mahakama. Pia kulikuwe po malalamiko ya migogoro ya ardhi, rushwa katika vyombo vya utoaji haki na katika masuala ya mirathi. Aidha, Tume iliendelea na utekelezaji wa Mpango wa Kazi wa Taifa wa Haki za Binadamu (*NHRAP*) kwa kutoa mafunzo kwa maafisa wa Serikali kutoka katika mikoa mbalimbali, asasi za kiraia, watumishi wa mahakama pamoja na watumishi wa tume kwa lengo la kuwajengea uwezo kusimamia na kukuza haki za binadamu katika maeneo yao ya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu huduma ya msaada wa sheria; kwa kutambua umuhimu wa msaada wa kisheria katika kuimarisha upatikanaji wa haki nchini hususan kwa watu wasio na uwezo wa kumudu gharama za uwakili, Wizara ilichukua hatua ya kuzitambua na kuzisajili asasi zisizo za Kiserikali zinazojihusisha na utoaji wa msaada wa kisheria. Katika kipindi hicho, Wizara ilifanya utambuzi wa zaidi ya asasi 290 zinazotoa msaada wa kisheria nchini na

kuwasimamia wasaidizi wa kisheria (*paralegals*) zaidi ya 5,000. Pia ilichukua hatua ya kuweka mwongozo wa kisheria ambapo Bunge lako Tukufu Iilitunga Sheria ya Msaada wa Kisheria na hivyo kuweka mfumo rasmi wa kisheria kusimamia upatikanaji wa utoaji wa msaada wa kisheria kwa wananchi wasio na uwezo wa kugharamia huduma za kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utafiti wa kisheria; Wizara inatambua nafasi ya utafiti katika maendeleo ya sheria ili kuwa na mfumo wenye kuakisi mahitaji halisi ya nchi kwa maendeleo na ustawi wa watu. Hivyo kwa kutambua hilo, Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania imekamilisha utafiti wa mfumo wa sheria zinazohusu hifadhi ya taarifa binafsi (*review of legal framework on personal data protection in Tanzania*), mfumo wa sheria kuhusu haki za walaji na watumiaji wa bidhaa (*review of legal framework on consumers' protection*) na sheria zinazohusu masuala ya usajili wa matukio muhilmu ya binadamu (*review of the legal framework on civil registration and vital statistics*). Maendeleo ya kina kuhusu hali ya utafiti wa kisheria kwa mwaka wa fedha 2016/2017 yanapatikana katika kiambatisho namba mbili 2 A na 2 B.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu urejeshwaji wa wahalifu na ushirikiano na mataifa kwenye makosa ya jinai; Tanzania imeendelea kutekeleza wajibu wake Kimataifa kwa kushirikiana katika kupambana na uhalifu wa Kimataifa kwa kurejesha watuhumiwa wa uhalifu katika nchi walikofanya makosa. Katika kutekeleza wajibu huu Tanzania ilipokea maombi ya kuwarejesha watuhumiwa wanne katika nchi wanakotuhumiwa kutenda uhalifu. Maombi matatu yanaendelea kufanyiwa kazi na maombi mawili yalikataliwa kutokana na kutokidhi matakwa ya dheria. Pia kwa mujibu ya Sheria ya Ushikiriano katika Masuala ya Jinai (*Mutual Assistant Criminal Matters Act*) nchi yetu ilipokea jumla ya maombi 12 ya kukusanya ushahidi na vielelezo. Maombi manne yalishughulikiwa na mengine Nane yanaendelea kufanyiwa uchambuzi. Aidha Tanzania ilipeleka nje ya nchi maombi mawili ya kukusanya ushahidi na vielelezo ambavyo yanaendelea kushughulikiwa kushughulikia wahusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu usajili, ufilisi na udhamini; usajili wa matukio muhimu ya mwanadamu. Wakala wa usajili Ufilisi na Udhamini (*RITA*) kwa kipindi cha Julai 2016 mpaka Machi, 2017 umesajili matukio muhimu kama ifuatavyo:-

(i) Kusajili na kutoa vyeti kwa watoto 869,182 wa umri wa chini ya miaka mitano katika mikoa saba ya Iringa, Njombe, Mbeya, Songwe, Mwanza, Geita na Shinyanga.

(ii) Usajili wa watoto walioko shulen 28,554 katika shule za msingi zilizopo kwenye Halmashauri ya Manispaa ya Ilala, Temeke, Kinondoni na Iringa.

(iii) Kampeni ya Usajili ya katika Wilaya Nzega na Tunduru ambapo jumla ya watu 23,160 walisajiliwa na kupewa vyeti.

(iv) Kufanya usajili wa kawaida wa vizazi laki 348,544.

(v) Matukio ya vifo 5,213, ndoa 21,057 na talaka 85. Aidha jumla ya leseni mpya 2,477 za kufungisha ndoa zilizolewa na leseni 1,618 kuuhishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia *RITA* imeendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu masuala ya usajili kuhusu matukio muhimu ya binadamu kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu kupitia *RITA* imesajili jumla ya miunganisho 164 ya wadhamini vyama siasa, makanisa, misikiti, na mali za vikundi vya kijamii, Kuendelea kusimamia mali sizizokuwa na wenyewe pamoja na masuala ya mirathi kulingana na amri za Mahakama. Aidha, mapitio yamefanywa katika bodi za wadhamini za taasisi zilizosajiliwa ili kufahamu uhai wake, na jumla ya taasisi 181 zilifutiwa usajili wake. Pia jumla ya wosia 50 ziliandikwa na kuhifadhiwa na huduma ya Ushauri wa masuala ya wosia na mirathi imetolewa kwa wananchi kupitia kampeni maalum. Orodha ya Bodi za Wadhamini zilizofutwa inapatikana kwenye kiambatisho namba 3.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu taasisi za mafunzo mipango na miradi ya maendeleo; Chuo cha Uongozi wa Mahakama - Lushoto. Chuo cha Uongozi wa Makama Lushoto katika kutekeleza jukumu la kutoa elimu endelevu kwa watumishi wa Mahakama na sekta ya sheria imeendelea kutoa mafunzo ya Astashahada na Stashahada kwa watumishi wa Mahakama na jamii nzima kwa ujumla. Katika mwaka wa fedha katika 2016/2017 Chuo kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo, *UN Women* na Chama cha Majaji Wanawake Tanzania (*TAWJA*) kiliandaa kitabu cha kuratibu, kuendesha na kufundishia wakufunzi wa masuala ya haki za binadamu na mapambano dhidi ya ukatili kwa wanawake na watoto na hadi sasa kitabu hicho kimetumika kuendesha mafunzo kwa Majaji, Wasajili, Mahakimu, Askari Polisi, Askari Magereza pamoja na Wahadhiri wa Chuo hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2016/2017 Chuo kiliendesha mafunzo kwa watumishi wa Mahakama zaidi ya 400 ikiwemo mafunzo maalum kwa Majaji 24 waliojengewa uwezo na weledi wa namna ya kuendesha mashauri ya makosa ya rushwa na uhujumu uchumi. Vilevile kiliandaa na kuendesha mafunzo ya namna ya kufanya upelelezi na kuendesha namna ya kushughulikia mashauri ya ujangili kwa Mahakimu 30, Mawakili wa Serikali 10, Askari Polisi watano na Askari wa Wanyama pori watano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo; taasisi imeendelea kuongeza uwezo wake wa kudahili wanafunzi katika makundi yaani *cohorts* mbalimbali katika mwaka wa fedha 2016/2017 ilidahili jumla ya wanafunzi 1,680 katika makundi matatu kundi la 23, kundi la 22, kundi la 23 na kundi la 24. Kwa sasa taasisi ina jumla ya wanafunzi 2,234 ambao wamesajiliwa katika makundi manne yaliyo katika hatua tofauti za mafunzo. Taasisi hii imeendelea kujiimarisha katika masuala ya utafiti, kutoa huduma za udahili kwa njia za kieletroniki na kuendesha huduma za maktaba ya kisasa inayohifadhi zaidi ya nakala 7,000 za vitabu na machapisho ya aina mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maendeleo ya rasilimaliwateru; Wizara imeendelea kusimamia watumishi wake ili kuhakikisha wanatekeleza wajibu wao kwa mujibu wa sheria, kanuni, na taratibu za utumishi wa umma. Wizara imechukua hatua za kinidhamu dhidi ya watumishi waliokiuka maandili ya kazi kwa baadhi yao kupewa onyo kushushwa vyeo na wengine kufunzwa kazi. Aidha, Wizara illajiri, kuthibitishwa kazini na kupandishwa vyeo kwa watumishi wote waliostahili. Natoa wito kwa watumishi wote kuzingatia nidhamu ya kazi na kutekeleza majukumu yao kwa juhudzi maarifa na weledi ili kufanikisha malengo ya Wizara ya kuwatumikia wananchi kwa kutoa huduma zilizo bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mpango na miradi ya maendeleo; ni dhamira za Wizara yangu kusongeza huduma za kisheria karibu nawananchi kwa kubuni na kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo na kwa kuimarisha ushirikiano na wadau wa maendeleo. Katika mwaka wa fedha 2016/2017 Wizara imetekeleza miradi na programu mpya za maendeleo zikiwemo:-

- (a) Programu ya maboresho ya Mahakama.
- (b) Mradi wa kuimarisha mfumo wa upatikanaji haki nchini (*strength excess justice human rights protection Tanzania*).
- (c) Programu ya ulinzi na upatikanaji wa haki ya mtoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maboresho ya Mahakama ni program ya miaka mitano inayotekeliza na Serikali ya Tanzania kwa fedha kutoka Benki ya Dunia kwa madhumini ya kuimarisha mfumo wa Mahakama upatikanaji na ubora wa huduma za Mahakama nchini. Programu inahusu upatikanaji wa haki nchini ni sehemu ya mpango wa Maendeleo wa Umoja wa Mataifa unaojulikana kama *UNDAP II*. Wizara kwa kushirikiana na *UNDP*imeandaa andiko la mradi wa mpango kazi kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2017/2018 ambapo kupitia Programu ya *UNDAP II* Tanzania

inaendelea kutekeleza mradi wa usajili wa watoto wa umri chini ya miaka mitano, mradi wa kudhibiti vitendo vya ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto, kukuza na kulinda haki za binadamu pamoja na usimamizi wa mfumo wa utoaji haki nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafankio yaliyopatikana; mafanikio yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa vipaumbele vya Wizara kwa mwaka 2016/2017 ni pamoja na kuanzishwa kwa Divisheni ya Mahakama Kuu ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi, kukamilika kwa mfumo wa kisheria wa kusimamia na kuratibu utoaji wa msaada wa kisheria nchini, kutungwa kwa sheria ya upatikanaji wa taarifa, kuendelea kusimamia mashauri yote ya jinai na madai, kumalizika kwa mashauri yote ya uchaguzi yote wa Ubunge na Udiwani kwa wakati kama iliviotakwa la kisheria, kuweka mfumo wa usajili wa vizazi kwa watoto walio chini ya umri wa chini ya miaka mitano katika Mikoa saba ya Geita, Iringa, Mbeya Mwanza, Shinyanga na Songwe; ujenzi na ukarabati wa majengo ya Mahakama katika ngazi ya mbalimbali, kufanya utafiti na kuhuisha sheria mbalimbali ili kuakisi mahitaji halisi kwa maendeleo ya watu, kuongezeka kwa matumizi ya TEHAMA katika utoaji wa huduma katika utoaji wa huduma na ufuatilaji wa hali za wafungwa na mahabusu magerezani uliopelekea kufanyika kwa maboresho ya huduma kwa wafungwa na mahabusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio mengine ni pamoja na kukamilisha uhakiki wa watumishi wote wa Wizara, kuimarika kwa usimamizi wa rasilimaliwatu na huduma kwa watumishi ikiwa ni pamoja na kuboresha mazingira ya kazi. Kuendelea kusimamia maadili ya watumishi, kukamilika kwa rasimu ya mkakati wa Kitaifa wa usajili wa matukio muhimu ya binadamu na takwimu, ambayo ipo katika hatua za maamuzi Serikalini, kukamilika kwa mfumo wa TEHAMA utakaowezesha ubadilishanaji wa taarifa kati ya *RITA*, Tume ya Uchaguzi na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa, kukamilika kwa mfumo wa kisheria wa kusimamia na kuratibu huduma ya msaada wa kisheria na kuendelea kutoa mafunzo ya Uanasheria kwa vitendo.

Nipende kusizitiza kuwa Wizara inatambua kwamba pamoja na mafanikio yaliyopatikana yapo maeneleo bado yanahitaji kufanyiwa kazi ili kufikiwa malengo tuliyojiwekea. Hivyo Wizara yangu itahakikisha kuwa kazi mbalimbali zilizosalia zitakamilishwa sanjari na utekelezaji wa vipaumbele yya mwaka wa fedha 2017/2018.

Mtiririko wa mapato na maduhuli ya Serikali; katika mwaka wa fedha 2016/2017 Wizara ya Katiba na Sheria iliidhinishiwa jumla ya shilingi 155,192,263,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na ya maendeleo. Kati ya fedha hizo mishahara ni shilingi 67,328,697,000 na matumizi mengineyo (*OC*) ni shilingi 50,404,380,000. Fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo ni shilingi 37,459,186,000 Ambapo kati ya fedha hizo shilingi 13,919,000,000 ni fedha za ndani na shilingi 23,550,186,000 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia mwezi Septemba, 2017 Wizara ilipokeajumla ya shilingi 80,503,233,455 sawa na asilimia 52 ya fedha zilizoidhinishwa kati ya hizo shilingi 45,545,485,311 ni mishahara ya watumishi na shilingi 31,434,746,899 ni kwa matumizi mengineyo sawa na asilimia 62. Fedha za maendeleo ni shilingi 3,523,001,645 sawa na asilimia tisa ya bajeti ya miradi ambavyo fedha za ndani ni shilingi 246,882,000 na fedha za nje ni shilingi 3,276,119,645.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha katika mwaka wa fedha 2016/2017, Wizara ilipanga na kukusanya jumla ya shilingi 17,085,829,511 kama maduhuli ya Serikali kutoka vyanzo mbalimbali vinavyosimamiwa na Wizara. Kufikia mwezi Machi, 2017 Wizara ilikusanya jumla ya shilingi bilioni 10,976,126,511 sawa na asilimia 64 ya makadirio yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto na mikakati iliyopo; pamoja na mafanikio yaliyopatika katika utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2016/2017, kumekuwepo na changamoto mbalimbali ambazo ni pamoja na upungufu wa rasilimali muhimu ikiwemo fedha, watu na vitendea kazi, uchakavu na uhaba wa miundombinu ya Mahakama, mahitaji ya TEHAMA katika usimamizi wa mashauri, uelewa

mdogo wa jamii kuhusu haki na wajibu wa raia, kuwepo kwa uhalifu unaotumia teknolojia za kisasa na kuhusisha nchi zaidi ya moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kukabiliana na changamoto hizo Wizara yangu iliendelea kubuni na kutekeleza mikakati mbalimbali ya kukabiliana nazo katika kuhakikisha kuwa nchi inakuwa na mfumo imara wa kikatiba na kisheria ili kufanikisha mipango ya maendeleo ya Taifa mikakati hiyo ni pamoja na:-

(a) Kuendelea kushirikiana na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma katika kuyapatia ufumbuzi matatizo yanayohusiana na upungufu wa watumishi ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa vibali vya ajira, kujaza nafasi zilizoachwa wazi na kushughulikia maslahi ya watumishi.

(b) Kutafuta vyanzo vipyta vya mapato ili kufanikisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo ukiwepo mradi wa *e-justice* na programu ya maboresho ya mfumo wa mahakama.

(c) Kuendelea kubana matumizi na kuepukana na matumizi yasiyo ya lazima kufanyika kwa wakati uliopo.

(d) Kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika utoaji wa huduma za kisheria na ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali.

(e) Kuwajengea uwezo watumishi wa sekta ya sheria katika kukabiliana na aina mpya za uhalifu.

(f) Kuboresha huduma za mafunzo ya wanasheria kwa vitendo.

(g) Kutumia teknolojia ya gharama nafuu katika ujenzi wa miundombinu ya mahakama ili kukabiliana na ukubwa wa gharama za utekelezaji wa mradi wa maendeleo.

(h) Kuimarisha mfumo wa usimamizi, ufuatiliaji na tathmini ya kazi za Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Katiba ya Sheria yameweze kana kutokana na ushirikiano thabiti wa wadau wa maendeleo ambao wameendelea kutupatia katika utekelezaji wa programu na miradi mbalimbali ya maendeleo. Kwa namna ya pekee nichukue fursa hii kuwashukuru Benki ya Dunia, Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo (*UNDP*), Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (*UNICEF*), Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wanawake (*UN Women*), Shirika la Msaada wa Maendeleo ya Kimataifa la Uingereza (*DFID*) na Taasisi ya *Bloomberg Data for Health Initiative*. Napenda kuwashakikishia wote kwamba Wizara yangu inathamini sana mchango wao na tutaendelea kutoa ushirikiano wa kuhakikisha kwamba mipango na melengo ya Serikali kuhusu sekta ya sheria yanafanikiwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa mchoyo wa fadhila nisipotambua kazi iliyofanywa na Viongozi wenzangu katika Wizara, hivyo kwa moyo wa dhati napenda nimshukuru Profesa Sifuni Ernest Mchome, Katibu Mkuu na Ndugu Amon Mpanju, Naibu Katibu Mkuu, viongozi wakuu na watalaa mwa taasisi zote zilizo chini ya Wizara yangu kwa ushirikiano mkubwa walionipa katika kutekeleza majukumu yangu ya kila siku.

Vilevile naishukuru sana kama nilivyosema familia yangu kwa kuendelea kunifarji na kunitia moyo wakati wote wa utekelezaji wa majukumu mazito yanayoambatana na wadhifa huu wa Waziri wa Katika na Sheria. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango na bajeti ya Wizara kwa mwaka 2017/2018; na katika hawa wa kuwashukuru napenda leo kwa namna ya pekee kabisa nimshukuru mwalimu wangu wa darasa la kwanza na la pili Mwalimu Penina Mnyangwira aliyenifikisha hapa nilipofika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2017/2018 Wizara yangu itaendelea na juhudzi za kuimarisha utawala wa sheria na misingi ya haki za binadamu kwa kuhakikisha kuwa wananchi wanapata huduma bora na za uhakikika.

Katika kufanikisha azma hiyo Wizara imeainisha maeneo mahsus ya kipaumbele kwa mwaka kwa fedha ujao kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Katiba na Sheria:-

(i) Kukamilisha uhamishaji wa Makao Makuu ya Wizara kutoka Dar es Salaam kuja Dodoma.

(ii) Kuratibu masuala ya kisera katika Wizara na taasisi zake.

(iii) Kuratibu na kusimamia huduma na msaada wa kisheria nchini.

(iv) Kuimarisha usimamizi na ufuatiliaji wa masuala ya Katiba na Sheria.

(v) Kusimamia utekelezaji wa haki za binadamu Kitaifa, Kikanda na Kimataifa.

(vi) Kuwajengea uwezo watumishi kuendeleza ubunifu, maarifa na weledi ili kuleta tija na ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mahakama ya Tanzania:-

(i) Kuharakisha usikilizaji wa mashauri.

(ii) Kuimarisha utawala bora maadili na uwajibikaji.

(iii) Kuboresha mazingira ya kufanyakazi kwa kuongeza upatikanaji wa vitendea kazi muhimu.

(iv) Kujenga na kukarabati miundombinu katika ngazi mbalimbali.

(v) Kuongeza matumizi ya TEHAMA ili kurahisisha usikilizaji wa mashauri na shughuli za utawala ili kufikisha huduma kwa wananchi.

(vi) Kuimarisha uwezo katika ukaguzi na usimamizi wa shughuli za Kimahakama.

(vii) Kuendelea kuimarisha uwezo wa rasilimali watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali:-

(i) Kuimarisha mfumo wa uandishi na urekebu wa sheria.

(ii) Kusimamia shughuli za uendeshaji wa mashauri ya jinai madai Katiba na haki za binadamu.

(iii) Kuimarisha usimamizi wa masuala ya mikataba.

(iv) Kuongeza matumizi ya TEHAMA katika utoaji wa huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora:-

(i) Kukuza nakutetea haki za binadamu hususani haki za makundi yenye mahitaji maalum.

(ii) Kuongeza uelewa wa haki za binadamu, utawala bora na wajibu wa raia.

(iii) Kufanya uchunguzi wa malalamiko na kuyapatia ufumbuzi kwa njia ya upatanishi na usuluhishi.

(iv) Kushirikiana na wadau mbalimbali nchini Kikanda na Kimataifa kwenye masuala ya haki za binadamu na utawala bora.

(v) Kujenga uwezo wa watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Kurebisha Sheria Tanzania:-

(i) Kukamilisha utafiti kuhusu mfumo wa sheria za usimamizi haki jinai (*review of legal framework on criminal justice administration*).

(ii) Kufanya utafiti kuhusu sheria za mfumo wa ushahidi yaani (*review of legal framework on law of evidence*).

(iii) Kufanya utafiti kuhusu mfumo wa sheria za usuluhishi (*review of legal framework on arbitration*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Usimamizi wa Mahakama:-

(i) Kuboresha utoaji wa huduma za Mahakama kwa kuongeza idadi ya watumishi wa Mahakama wenye weledi na sifa stahiki.

(ii) Kuboresha mazingira ya kazi kwa kununua vitendea kazi pamoja na samani za ofisi.

(iii) Kuimarisha nidhamu ya maadili ya watumishi wa Mahakama kwa kufanya ukaguzi wa Kamati za Maadili za Mahakama.

(iv) Kuwajengea uwezo wajumbe pamoja na watumishi wa Tume kwa kuwawezesha kuhudhuria mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala wa Usajili na Ufilisi na Udhamini:-

(i) Kutekeleza mkakati wa kitaifa wa usajili wa matukio muhimu ya binadamu.

(ii) Kufanya mapitio ya sheria zinazohusu ujisili (*review of legal framework on solvency*).

(iii) Kuimarisha matumizi ya teknolojia katika kuboresha utoaji wa huduma.

(iv) Kuimarisha ukusanyaji na usimamizi ya maduhuli ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi ya Mafunzo ya Wanasheria kwa Vitendo:-

(i) Kudahili na kutoa mafunzo kwa wanafunzi 1,800 ili kuongeza idadi ya watalamu wa sheria nchini.

(ii) Kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa mawakili na wadau wengine; katika mambo mapya yanayojitokeza katika taaluma ya sharia (*continuing legal education*).

(iii) Kuendesha programu za mafunzo kwa Wasaidizi ya Sheria (*paralegals*).

(iv) Kuimarisha miundombinu ya taasisi.

Chuo cha Uongozi wa Mahakama – Lushoto:-

(i) Kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa Majaji na Mahakimu.

(ii) Kuimarisha na kuendelea kutoa mafunzo endelevu ya Kimahakama, pamoja na mafunzo kazini kwa watumishi wa Mahakama na watumishi wote wa sekta ya sheria kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kufanikisha utekelezaji wa vipaumbele hivi Wizara yangu inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 166,479,908,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo. Mchanganuo wa makadirio ya Bageti kwa mafungu saba ya Wizara na taasisi zake ni kama ifuatavyo; mishahara ya watumishi ni shilingi 76,141,279,000; matumizi mengineyo ni shilingi 66,801,799,000; miradi ya maendeleo shilingi 23,236,830,000; na jumla ni shilingi 166,479,908,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muhtasari wa matumizi; mchanganuo wa matumizi ya bajeti kwa kila fungu ni kama ifuatavyo:-

Fungu Namba 12 - Tume ya Utumishi wa Mahakama, matumizi ya mishahara ni shilingi 282,400,000; matumizi mengineyo milioni 820,507,000; matumizi ya maendeleo ya ndani haikutengewa, matumizi ya maendeleo kutoka nje pia haikutengewa katika kifungu hicho na jumla ni shilingi 1,102,911,000.

Fungu Namba 16 - Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, matumizi ya mishahara ni 3,863,792,000, matumizi mengineyo ni shilingi 3,418,731,000; matumizi ya maendeleo ya ndani na matumizi ya maendeleo ya nje hayakutengewa fedha katika kifungu hiki na jumla ni shilingi 7,282,523,000.

Fungu Namba 35 - Divisheni ya Mashtaka, matumizi ya mishahara ni shilingi 9,478,238,000; matumizi mengineyo ni shilingi 5,435,825,000; matumizi ya maendeleo ya ndani na matumizi ya maendeleo ya nje hayakutengewa fedha katika vifungu hivyo na jumla ni shilingi 14,914,063,000.

Fungu Namba 40 - Mfuko wa Mahakama, matumizi ya mishahara ni shilingi 54,524,408,000; matumizi mengineyo ni shilingi 52,434,610,000; matumizi ya maendeleo ya ndani ni shilingi 17,000,000,000, matumizi ya maendeleo ya nje ni shilingi 1,158,011,000 na jumla ni shilingi 125,117,029,000.

Fungu Namba 41 - Wizara ya Katiba na Sheria, matumizi ya mishahara ni shilingi 4,897,729,000; matumizi mengineyo ni shilingi 2,158,317,000; matumizi ya maendeleo ya ndani ni shilingi 1,000,000,000; matumizi ya maendeleo ya nje ni shilingi 1,806,020,000 na jumla ni shilingi 9,862,066,000.

Fungu Namba 55 - Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, matumizi ya mishahara ni shilingi 2,328,102,000; matumizi mengineyo ni shilingi 1,566,080,000; matumizi ya maendeleo ya ndani hayakutengewa fedha katika kifungu hiki, matumizi ya maendeleo ya nje ni shilingi 2,272,799,000 na jumla ni shilingi 6,116,981,000.

Fungu Namba 59 - Tume ya Kurekebisha Sheria, Matumizi ya mishahara ni shilingi 1,066,606,000, matumizi mengineyo ni shilingi 967,729,000, matumizi ya maendeleo ya ndani hayakutengewa fedha katika kifungu hiki na vivyo hivyo maendeleo ya nje na jumla ni shilingi 2,034,355,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makusanyo na maduhuli ya Serikali; katika mwaka wa fedha 2017/2018 Wizara yangu inatarajia kukusanya kiasi cha shilingi 24,087,507,200 ikiwa ni maduhuli ya Serikali kutokana na vyanzo mballimbali vya mapato vinavyosimamiwa kama ilivyoainishwa kwenye jedwali hapa chini.

Fungu Namba 16 ni shilingi 3,002,000; Fungu 35 ni shilingi 13,002,000; Fungu 40 ni shilingi 9,318,061,200; Fungu 41 ni shilingi 14,753,299,000 na Fungu 59 ni shilingi 150,000. Jumla ni shilingi 24,087,507,200.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchanganuo wa maombi ya fedha za bajeti ya kila Fungu imeainishwa kwenye vitabu vya kasma za mafungu husika ambavyo Wajumbe wa Bunge lako Tukufu wamegaiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.
(Makofii)

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:
Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(Hoja ilitolewa lamuliwe)

MWENYEKITI: Ahsante, hoja imetolewa na imeungwa mkono.

**HOTUBA YA WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA, MHESHIMIWA
PROF. PALAMAGAMBA JOHN AIDAN MWALUKO KABUDI
(MB), AKIWASILISHA BUNGENI MPANGO NA MAKADIRIO YA
BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018
KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

A. UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika**, kufuatia taarifa zilizowasilishwa leo katika Bunge lako tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria; na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako sasa likubali kupokea, kujadili na kuitisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

Shukrani na Pole

2. **Mheshimiwa Spika**, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniruzuku uhai na kunijalia afya njema kuweza kusimama mbele ya Bunge lako tukufu kuwasilisha Mpango na Makadirio ya Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka Fedha 2017/2018. Aidha, napenda kutoa shukrani nyingi kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, kwa heshima kubwa aliyonipa kwa kunitfea kuwa Mbunge na kushika wadhifa wa Waziri wa Katiba na Sheria. Kutokana na heshima hiyo, ninaahidi kuitumikia nafasi hii kwa hekima, uadilifu na uaminifu kwa kadri alivyonijalia Mwenyezi Mungu. Vivyo hivyo, ninaahidi kuwatumikia wananchi wote nikitambua kuwa wao ndio msingi wa mamlaka yote ya Serikali, kwa mujibu wa Katiba ya nchi.

3. **Mheshimiwa Spika**, kwa masikitiko makubwa nakupa pole wewe na Bunge lako tukufu kwa kuondokewa na Wabunge wenzetu waliotangulia mbele ya haki, ambao ni Mheshimiwa Hafidh Ally Tahir aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Dimani, CCM na Dkt. Elly Marko Macha aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum, CHADEMA. Pia, natoa pole kwako na

watanzania wote, ndugu, jamaa na marafiki kutokana na kifo cha Mheshimiwa Samwel John Sitta, aliyekuwa Spika wa Bunge la Kumi la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nitumie fursa hii kuwapa pole ndugu, jamaa na marafiki pamoja na wananchi walioguswa na misiba hii kwa namna moja au nyingine. Mwenye Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi, Amina.

Salamu za Pongezi

4. Mheshimiwa Spika, napenda nikupongeze wewe binafsi kwa uongozi wako mahiri wa kuliongoza Bunge letu na hivyo kudhihirisha uwezo na uzoefu ulionao katika kuwatumikia watanzania kupitia chombo hiki. Aidha, nitumie fursa hii kumpongeza Naibu Spika Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson Mwansasu na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kuendelea kutekeleza majukumu yao vema kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu.

5. Mheshimiwa Spika, pia nampongeza Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kassim M. Majaliwa (Mb), kwa hotuba yake nzuri ambayo imetoa mwelekeo wa kisera katika utekelezaji wa shughuli za Serikali kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha 2017/2018. Vilevile, nampongeza kwa uongozi wake thabiti katika kusimamia vema shughuli za Serikali ndani na nje ya Bunge lako Tukufu.

6. Mheshimiwa Spika, niruhusu sasa niwapongeze Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Mohamed Omari Mchengerwa, Mbunge wa Rufiji na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia, Mbunge wa Mtwara Vijijini kwa kuziongoza vema Kamati zao. Maoni na ushauri wao umekuwa ni msaada mkubwa kwa Wizara yangu katika kutekeleza majukumu yake ya kuwashudumia Watanzania. Napenda niwahakikishie kuwa Wizara yangu inayo imani kubwa katika uongozi wao na itaendelea kuwapatia ushirikiano unaostahili katika kipindi watakachokuwa katika nyadhifa hizo. Pia natoa shukrani zangu za dhati kwa kamati hizo kazi kubwa ya

kuchambua Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Mfuko wa Mahakama kwa mwaka wa fedha 2017/18. Hakika tunatambua na kuthamini mchango wa Kamati hizi katika kuhakikisha kuwa sekta ya sheria inabaki kuwa kiungo muhimu kwa maendeleo ya nchi yetu kiuchumi, kijamii, kisiasa, kimazingira na kiteknolojia.

7. Mheshimiwa Spika, niruhusu sasa niwapongeze wabunge wenzangu wote kwa hesima waliyopewa ya kuwa wabunge wa Bunge lako Tukufu. Kwa namna ya pekee natoa pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Abdallah Majura Bulembo (Mb), Mheshimiwa Anna Kilango Malecela (Mb), Mheshimiwa Juma Ali Juma (Mb), Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete (Mb) na Mheshimiwa Getrude Pangalile Rwakatare (Mb) kwa hesima kubwa waliyopewa ya kultumikia Taifa letu kupitia chombo hiki kitukufu. Binafsi, ninawatakitia kheri na Baraka za Mwenyezi Mungu katika kutekeleza majukumu yao ya Ubunge.

B. DIRA NA DHIMA

8. Mheshimiwa Spika, Dira ya Wizara ya Mambo ya Katiba na Sheria ni kuwa na Katiba na Sheria Wezeshi kwa Maendeleo ya Taifa. Madhumuni ya Dira hii nikuweka mazingira rafiki kisera na kisheria ya kuwezesha utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya Taifa, kudumisha hali ya amani, utulivu na utangamano wa kitaifa ambavyo vimeendelea kuwepo nchini. Aidha, Dhima ya Wizara ni Kuwa na Mfumo Madhubuti wa kikatiba na kisheria katika Kufanikisha Mipango ya Maendeleo ya Taifa. Dhima hii inahimiza kufanya kazi kwa weledi na ubunifu katika kuhakikisha kunakuwepo mazingira rafiki ya upatikanaji wa huduma muhimu za kisheria.

C. MUUNDO NA MAJUKUMU YA WIZARA

9. Mheshimiwa Spika, Wizara ya Katiba na Sheria inajumuisha Mahakama ya Tanzania, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania, Tume

ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Tume ya Utumishi wa Mahakama, Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini, Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo na Chuo cha Uongozi wa Mahakama-Lushoto. Kwa pamoja tumeendelea kutekeleza majukumu yetu ya kuwahudumia wananchi kwa kutoa huduma mbalimbali za kisheria na kuhakikisha kuwa wananchi wanaifikia na kupata haki kwa wakati wanapoitafuta.

10. Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inao wajibu wa kuhakikisha kuwa nchi inaongozwa kwa kuzingatia Katiba, sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa na vyombo halali na kwamba haki inaendelea kutawala katika jamii wakati wote. Hivyo, kwa kutambua wajibu huo Wizara yangu imeendelea kutekeleza majukumu yake kama yalivyo kwenye Hati ya mgawanyo wa majukumu kwa mawaziri (Instrument), iliyotolewa kupitia Tangazo la Serikali Na.144 la tarehe 22 Aprili, 2016, ambayo ni:

- i. kuweka sera kuhusu masuala ya sheria na utekelezaji wake;
- ii. kushughulikia masuala ya Katiba;
- iii. kusimamia haki na mfumo wa utoaji haki;
- iv. uandishi wa sheria;
- v. uendeshaji wa mashtaka;
- vi. Kushughulikia mashauri ya madai, usuluuhishi, mikataba na sheria za kimataifa;
- vii. kushughulikia masuala ya haki za binadamu na msaada wa kisheria;
- viii. kusimamia na kufanya utafiti wa maboresho ya sheria;
- ix. kushughulikia urejeshwaji wa wahalifu na

- kuendeleza ushirikiano na mataifa mbalimbali kwenye makosa ya jinai;
- x. kusajili matukio muhimu ya binadamu yanayohusu vizazi, vifo, ndoa, talaka na uasili wa watoto; pamoja na kusimamia masuala ya ufilisi na udhamini;
 - xi. kuboresha utendaji na maendeleo ya rasilimali watu katika Wizara; na
 - xii. kuratibu shughuli za taasisi, mipango na miradi ya maendeleo chini ya Wizara.

D. MAPITIO YA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2016/2017

11. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2016/2017 Wizara yangu ilipanga na kutekeleza majukumu yake kwa kubainisha maeneo mahsusini ya kipaumbele yafuatayo:

- i. Kuimarisha usimamizi na uratibu wa mfumo wa sheria;
- ii. Kuanzisha Divisheni ya Mahakama Kuu ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi;
- iii. Kuimarisha Mfumo wa Haki na Utoaji Haki
- iv. Kuimarisha usimamizi wa miradi ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya mahakama na taasisi nyingine zilizo chini ya Wizara;
- v. Kuimarisha matumizi ya mifumo ya kielektroniki ya kutunza kumbukumbu na nyaraka muhimu pamoja na kutolea huduma;
- vi. Kuimarisha shughuli za utafiti na uboreshaji wa sheria nchini;

- vii. Kuimarisha uandishi na urekebu wa sheria za nchi;
- viii. Kuboresha mazingira ya kufanyia kazi, maendeleo na ustawi wa watumishi;
- ix. Kuimarisha mfumo wa mafunzo ya uanasheria kwa vitendo kwa kuongeza udahili wa wanafunzi na kupanua wigo wa utoaji wa huduma;
- x. Kuimarisha upatikanaji wa msaada wa kisheria kwa watu wasio na uwezo;
- xi. Kuimarisha shughuli za usajili wa matukio muhimu ya binadamu.

12. Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia vipaumbele hivyo, Wizara iliandaa na kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Mpango na Bajeti na kupitishwa kwa utekelezaji. Kwa heshima na taadhima, naomba sasa uniruhusu kuwasilisha mbele ya Bunge hili taarifa kuhusu hatua mbalimbali zilizochukuliwa katika kutekeleza Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2016/17, mafanikio yaliyopatikana na changamoto mbalimbali ambazo Wizara ilikabiliana nazo, kama ifuatavyo:-

Sera na Masuala ya Sheria
Maandalizi ya Sera ya Taifa ya Sheria

13. Mheshimiwa Spika, Wizara iliendelea na juhudzi za kuandika sera mahsus kuhusu masuala ya sheria kwa kuandaa Rasimu ya Sera ya Taifa ya Sheria ambayo kwa sasa inajadiliwa na makundi mbalimbali ya wadau ili kutoa fursa kwa Wizara kukusanya maoni yatakayofanya Sera hiyo kukidhi mahitaji ya sasa ya sekta ya sheria na Taifa kwa ujumla. Ni matarajio yangu kwamba Serikali ikishapitisha Sera hii na kuanza kutumika itakuwa ni hatua muhimu katika kuimarisha usimamizi na uendelezaji wa mfumo wa sheria nchini kwa maendeleo ya Taifa.

Tathimini ya Hali ya Utekelezaji wa Sheria Nchini

14. Mheshimiwa Spika, Wizara ya Katiba na Sheria inayo dhamana ya kuimarisha na kusimamia mfumo wa sheria nchini. Katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2016/2017, Wizara ilifuatilia utekelezaji wa sheria mbalimbali kupitia wizara, idara, wakala na mamlaka nyingine za Serikali ili kutathmini hali ya utekelezaji wa sheria nchini. Kukamilika kwa zoezi hili kutaiwezesha Wizara kutoa mwongozo wa namna ya kuimarisha mfumo wa sheria nchini.

Sera na Makubaliano ya Kimataifa na Kikanda

15. Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu nchi yetu imekuwa mwanachama wa taasisi mbalimbali za kikanda na kimataifa kupitia Umoja wa Mataifa, Umoja wa Afrika, Jumuiya ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC), Jumuiya ya Afrika Mashariki na nyinginez. Kupitia taasisi hizo, Tanzania imeendelea kuridhia Sera, Malengo na Mipango ya Maendeleo inayopitishwa na taasisi husika ikiwemo (a) Malengo ya Maendeleo Endelevu [*Sustainable Developement Goals*], (b) Mpango wa Maendeleo wa Afrika na (c) Mpango Kazi wa Afrika wa Kugharamia Shughuli za Maendeleo [*Addis Ababa Action Agenda*]. Kwa kutambua wajibu ilionao katika kufanikisha makubaliano hayo, Wizara yangu imefanya uchambuzi wa maeneo muhimu na kuweka mikakati ya kuiwezesha kutekeleza vema wajibu huu wa kimataifa sanjari na mipango ya ndani ya sekta. Kutokana na uchambuzi huo Wizara imebainisha maeneo lengwa (*thematic areas*) manne ambayo kwa namna moja au nyingine yanaakisi malengo ya Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (FYDPII) na pia Mpango Mkakati wa Wizara. Maeneo hayo ni, upatikanaji haki kwa wote na utawala wa sheria; amani na ushirikishaji wananchi kwa maendeleo endelevu; usawa wa kijinsia; na haki za binadamu.

Haki na Mfumo wa Utoaji Haki

16. Mheshimiwa Spika, Katiba imeipa mamlaka Mahakama ya Tanzania kuwa ndicho chombo pekee cha utoaji haki

nchini. Katika kuhakikisha kuwa chombo hiki kinatekeleza majukumu yake ipasavyo na kwa ufanisi, sheria zimeweka mfumo rasmi wa utatuzi wa migogoro unaojumuisha mfumo wa upelelezi wa makosa ya jinai, uendeshaji wa mashtaka, usikilizaji wa mashauri pamoja na mifumo ya usuluhishi. Hivyo, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2016/17, Serikali ilichukua hatua madhubuti za kuimarisha mfumo wa utoaji haki nchini kwa kuanzisha Divisheni ya Mahakama Kuu ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi; kuharakisha usikilizaji wa mashauri; na ujenzi wa miundombinu muhimu kama ifuatavyo:-

Divisheni ya Mahakama Kuu ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi

17. Mheshimiwa Spika, katika kipindi hicho Wizara imetekeleza kwa vitendo azma ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, ya kupambana na rushwa na ufisadi nchini kwa nguvu zote kwa kuanzisha Divisheni ya Mahakama Kuu ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi. Divisheni imeanza kufanya kazi katika majengo yaliyoko kwenye Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo; na kwamba kila Kanda ya Mahakama Kuu ni Masjala Ndogo ya Divisheni hiyo. Hatua muhimu zilizochukuliwa ni pamoja na kufanya marekebisho ya sheria na kuandaa kanuni za uendeshaji wa Mahakama; kufanya ukarabati wa majengo, ununuzi wa vifaa, kuajiri na kutoa mafunzo kwa watumishi wa Divisheni. Hadi sasa Divisheni hiyo imeweza kusajili jumla ya maombi 25, kati ya hayo, 20 yamesajiliwa Dar es Salaam, 3 Mtwara, 1 Iringa na 1 Tabora. Aidha, kati ya maombi 25 yaliyosajiliwa maombi 13 yametolewa uamuzi na mengine yanaendelea kufanyiwa kazi.

Usikilizaji wa Mashauri Mahakamani

18. Mheshimiwa spika, mwaka 2016, Mahakama ya Tanzania ilianza na jumla ya mashauri 59,477 na kusajili mashauri mapya 276,147. Mashauri yaliyoamuliwa katika kipindi hicho yalikuwa 278,226, sawa na asilimia 83 ya wastani

wa uwezo wa kumaliza mashauri yote yaliyokuwepo. Mafanikio hayo yalitokana na Mahakama kuendelea kubuni na kutekeleza mikakati mbalimbali ikiwemo kufanya kazi kwa malengo na kupima utendaji kazi wa majaji na mahakimu. Pia, Mahakama ya Tanzania imeendelea kusisitiza matumizi ya njia mbadala za utatuzi wa migogoro na kuimarisha ushiriki wa wadau katika kubuni na kutekeleza mikakati ya kuharakisha usikilizaji wa mashauri. Maelezo ya ufanuzi kuhusu usikilizaji wa mashauri ni kama yalivyo kwenye **kiambatanisho Na: 1.**

Kesi za Uchaguzi Mkuu wa 2015

19. Mheshimiwa Spika, kufuatia matokeo ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015, yalifunguliwa jumla ya mashauri 53 yaliyohusu nafasi ya Ubunge na mashauri 196 ya nafasi za Udiwani. Hadi kufikia mwezi Machi, 2017 mashauri 52 ya Ubunge yallamuliwa, hivyo kubaki na shauri moja (1) na kwamba hivi sasa kuna rufaa mbili katika Mahakama ya Rufani kupinga uamuzi wa Mahakama Kuu. Aidha, mashauri yote ya udiwani yalisikilizwa na kuamuliwa katika kipindi kilichowekwa kwa mujibu wa Sheria, yaani, mwaka 1 kwa mashauri ya Ubunge na miezi sita kwa mashauri ya Udiwani. Haya ni mafanikio makubwa na ya kihistoria kuwahi kufikiwa kwa mashauri ya uchaguzi kusikilizwa na kutolewa uamuzi ndani ya muda uliowekwa kisheria. Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ilitoa mchango mkubwa kwa kusimamia uendeshaji wa mashauri hayo mahakamani ambapo katika mashauri yote, isipokuwa shauri moja, Serikali ilipata ushindi. Aidha, katika kuhakikisha kuwa tunaimarisha uwezo wa Serikali kushughulika kesi za uchaguzi, Mahakama ya Tanzania, kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo (UNDP), ilitengeneza vitabu vitatu, ambavyo ni kijitabu kinachoelezea Utaratibu na Mienendo Iliyotumika Katika Kuendesha Kesi za Uchaguzi; Ripoti Kuhusu Namna Mahakama Zilivyoshughulikia Kesi za Uchaguzi na Mafunzo Yatokanayo na Mkusanyiko wa Sheria na Kanuni za Uchaguzi. Vitabu hivi vilikabidhiwa kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwako wewe, Mheshimiwa Spika, tarehe 2 Februari, 2017 wakati wa maadhimisho ya Siku ya Sheria.

Miundombinu ya Mahakama

20. Mheshimiwa spika, Mahakama ya Tanzania imeendelea na utekelezaji wa mkakati wa kuboresha huduma za Mahakama ikiwa ni pamoja na kufanya ujenzi na ukarabati wa mahakama mbalimbali nchini. Hadi kufikia mwezi Machi, 2017, Mahakama ya Tanzania ilikamilisha ukarabati wa majengo ya Mahakama Kuu, Dar es Salaam na Tanga na kuendelea na ukarabati wa Mahakama Kuu, Kanda ya Mbeya, unaotarajiwa kukamilika hivi karibuni. Aidha, Mahakama ya Tanzania imekamilisha ujenzi wa jengo la Mahakama ya Hakimu Mkazi Pwani na Mahakama ya Wilaya Kibaha; na inaendelea na ujenzi wa Mahakama za Wilaya za Bagamoyo, Mkuranga, Kigamboni, Kinyerezi na Mahakama ya Mwanzo Kawe ambazo zipo katika hatua mbalimbali za ujenzi.

21 Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na changamoto ya miundombinu, Mahakama kwa kushirikiana na Chuo Kikuu Ardhi na Baraza la Taifa la Ujenzi ilifanya utafiti wa teknolojia ya gharama nafuu ya ujenzi wa majengo ambapo teknolojia ya Moladi imeonyesha unafuu wa gharama, kupunguza muda unaotumika kwenye ujenzi na ubora wa majengo. Kwa kutumia teknolojia hii, Serikali imeweza kuokoa takriban asilimia 50 ya gharama za ujenzi ambazo zingetumika kwa kutumia teknolojia ya kawaida. Chini ya utafiti huu, Mahakama sita za mfano zimejengwa ambazo ni Mahakama ya Hakimu Mkazi Pwani na Hakimu wa Wilaya Kibaha, Mahakama za Wilaya za Bagamoyo, Kigamboni, Mkuranga na Kinyerezi, pamoja na Mahakama ya Mwanzo Kawe. Ni dhahiri kuwa kutokana na uzoefu ulioupatikana katika mradi huu, Wizara itaweza kutumia teknolojia hiyo katika maeneo mengine ya nchi kwa gharama nafuu.

22. Mheshimiwa Spika, katika hatua nyingine Mahakama ya Tanzania imeanza kazi ya kukamilisha ujenzi wa Mahakama ya Mkoa wa Manyara na Mahakama za Mwanzo za Iguguno (Mkalama), Wasso (Ngorongoro), Magoma (Korogwe), Bereko (Kondoa), Karatu Mjini (Karatu), Mvomero (Mvomero), Old Korogwe (Korogwe) na Kilwa Masoko

(Kilwa), ambazo ujenzi wake ulisimama kwa muda mrefu kutokana na ukosefu wa fedha. Aidha, Mahakama ya Tanzania imeendelea kuimarisha shughuli za usimamizi na ukaguzi wa Mahakama kwa kununua na kusambaza jumla ya nakala 650 za vitabu vya mwongozo wa ukaguzi katika Mahakama mbalimbali nchini.

Uandishi wa Sheria

23. Mheshimiwa Spika, Wizara yangu iliendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuhakikisha kuwa sheria za nchi zinakuwa ni nyenzo ya kuharakisha maendeleo katika nyanja za kiuchumi, kijamii, kisiasa, kiutamaduni, kimazingira na kiteknolojia kuititia sera na mipango mbalimbali ya maendeleo. Hivyo, katika Mwaka wa Fedha wa 2016/17, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali iliratibu maandalizi ya miswada 12 ya sheria iliyowasilishwa na kujadiliwa Bungeni. Kutokana na miswada hiyo, sheria mbalimbali zilitungwa ikiwa ni pamoja na Sheria ya Haki ya Kupata Taarifa na Sheria ya Msaada wa Kisheria, ambazo ziko chini ya usimamizi wa Wizara yangu pamoja na Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali, Na. 3 ya Mwaka 2016, Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali, Na.4 ya mwaka 2016 na Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali, Na.1 ya Mwaka 2017.

Uendeshaji wa Mashtaka

24. Mheshimiwa Spika, Mkurugenzi wa Mashtaka aliendelea kuratibu shughuli za upelegelezi wa makosa ya jinai, kufungua na kuendesha mashauri mahakamani. Katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi, 2017, kulikuwa na jumla ya mashauri yajinai 31,723 yaliyoendeshwa katika mahakama mbalimbali nchini. Kati ya hayo, mashauri 14,732, sawa na asilimia 46, yalitolewa uamuzi na mahakama na mengine 16,991 yanaendelea kusikilizwa. Aidha, kulikuwa na mashauri matano yanayohusu urejeshaji wa mali zilizotokana na uhalifu yaliyokamilika kusikilizwa na fedha taslimu Shilingi 439,628,000 kurejeshwa Serikalini ikiwa ni pamoja na nyumba 8, magari 25, pikipiki 10, boti nane (8) na viwanja vinne (4). Aidha, jumla ya shilingi 1,110,893,995 zililipwa kama faini kutokana na mashauri hayo.

25. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2016 hadi Machi, 2017 kulikuwa na mashauri 463 ya ujangili. Kati ya hayo, mashauri 158 yalihitimishwa kwa washtakiwa kutiwa hatiani na kupewa adhabu za vifungo na kulipa faini ya Shilingi milioni 811 taslimu. Aidha, kulikuwa na mashauri 9,813 ya dawa za kulevyta yakiwemo mashauri 161 yanayohusu kiwango kikubwa cha dawa za kulevyta ambapo mashauri tisa kati ya hayo yalihitimishwa. Katika mashauri yaliyohitimishwa washtakiwa 13 walihukumiwa vifungo vyatia ya miaka 20 na maisha jela. Aidha, kilo 279 za dawa aina ya cocaine na heroine; na kilo 21 za mirungi zilitakatazwa kwa amri ya mahakama. Pia, Mkurugenzi wa Mashtaka alipokea jumla ya majalada 510 ya tuhuma za rushwa kutoka TAKUKURU yakiwemo majalada mapya 306 na 204 yaliyorejeshwa tena baada ya uchunguzi zaidi. Kati ya hayo, majalada 201 yaliandaliwa hati za mashtaka, majalada 136 yaliyorejeshwa TAKUKURU kwa hatua zaidi za uchunguzi; majalada 168 yanaendelea kufanyiwa uchambuzi wa kisheria na mengine matano yalifungwa.

Uendeshaji wa Mashauri ya Madai, Katiba na Haki za Binadamu

26. Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali iliendesha jumla ya mashauri 984 ya madai yaliyoihusisha Serikali katika Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufani, yakiwemo mashauri 883 ya zamani na mashauri 101 mapya. Kati ya hayo, mashauri 11 yalitolewa uamuzi na mashauri mengine 973 yanaendelea kusikilizwa. Serikali ilishinda katika mashauri tisa na kushindwa katika mashauri mawili. Kutokana na mafanikio hayo, Serikali iliweza kuokoa takriban shilingi Bilioni 23.75 sawa na asilimia 99.87 ya fedha zinazodaiwa katika mashauri yaliyoisha. Vilevile, kulikuwa na maombi 48 mapya na 277 ya zamani na hivyo kufanya maombi yote kuwa 325. Kati ya hayo, maombi 12 yamehitimishwa na maombi 313 yanaendelea kusikilizwa. Rufani za madai zilizokuwepo ni 59 ikiwemo rufani 1 mpya, na zote zinaendelea kusikilizwa.

27. Mheshimiwa Spika, kulikuwa na jumla ya mashauri

mapya 32 ya Kikatiba yalifunguliwa kwenye Mahakama Kuu ya Tanzania na kufanya jumla ya mashauri yaliyokuwepo kuwa 164 yakiwemo mashauri 132 ya zamani ambapo mashauri 19 yalihitimishwa na kubaki mashauri 145. Katika Mahakama ya Rufani kulikuwa na rufaa 7 ambazo bado zinaendelea. Aidha, katika Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu (African Court on Human and Peoples Rights) kulifunguliwa jumla ya mashauri 104, kati ya hayo mashauri 40 ni mapya na 64 ni ya zamani na yanaendelea kusikilizwa. Hali kadhalika, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu iliendesha jumla ya mashauri 6 katika Mahakama ya Haki ya Afrika Mashariki (East African Court of Justice). Kati ya hayo, Shauri moja lilimalizika na mengine mashauri 5 bado yanaendelea kusikilizwa.

Uhakiki wa Mikataba na Usimamizi wa Sheria za Kimataifa

28. Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, iliendelea kutoa ushauri wa kisheria kwenye Mikataba na Makubaliano mbalimbali ambapo katika kipindi cha Julai 2016 hadi Machi 2017 ilifanya upekuzi na uhakiki wa jumla ya mikataba 1,473 yenye thamani ya shilingi trillioni 12.6. Kazi hii ilihuisha mikataba ya ununuzi, ukarabati wa majengo, ujenzi wa barabara na hati za makubaliano (MOU) kutoka Wizara, Idara na Taasisi za Serikali na mamlaka za Serikali za Mitaa. Vilevile, katika ngazi ya kikanda na kimataifa, Ofisi hii ilishiriki katika mikutano 86 ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika na Umoja wa Mataifa iliyojadili masuala ya sheria na sera za sekta mbalimbali.

Haki za Binadamu na Msaada wa Kisheria

Usimamizi na Hifadhi ya Haki za Binadamu

29. Mheshimiwa Spika, Wizara iliendelea kuimarisha na kusimamia utekelezaji wa haki za binadamu kama zilivyoanishwa na kuhifadhiwa katika Katiba na Sheria za nchi. Katika kipindi cha Mwaka wa fedha 2016/17, Wizara iliandaa

Taarifa ya Nchi kuhusu utekelezaji wa haki za binadamu iliyowasilishwa kwenye Baraza la Haki za Binadamu la Umoja wa Mataifa, chini ya Mfumo wa Umoja wa Mataifa wa Mapitio kwa Kipindi Maalum (The Universal Periodic Review Mechanism). Taarifa hiyo ilijadiliwa kwenye vikao vya 25 na 33 vya Baraza la Haki za Binadamu vilivyofanyika Geneva, Uswisi kati ya Mei na Oktoba 2016. Kupitia Taarifa hiyo, Serikali ilipata fursa ya kufafanua mbele ya Jumuia ya Kimataifa kuhusu hali ya utekelezaji wa haki za binadamu nchini na kutoa msimamo wa nchi kuhusiana na mapendekezo mbalimbali yaliyotolewa na Baraza la Haki za Binadamu wakati wa kujadiliwa kwa Taarifa ya nchi yetu.

30. Mheshimiwa Spika, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ilifuatilia na kutoa ushauri kwa Serikali na taasisi zake kuhusu utekelezaji wa haki za binadamu na misingi ya utawala bora nchini. Hii ni pamoja na kufanya ufuatiliaji wa haki za binadamu kwa watu walio katika makundi yenye mahitaji maalum; haki za mahabusu na wafungwa; kufanya uchunguzi wa tuhuma za uvunjwaji wa haki za binadamu na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora; na kutoa elimu ya haki za binadamu na utawala bora kwa jamii. Katika kipindi hicho Tume ilitembelea jumla ya magereza 41 katika mikoa 15 ya Arusha, Kilimanjaro, Mbeya, Dar es salaam, Tanga, Mtwara, Lindi, Pwani, Manyara, Mara, Kigoma, Mwanza, Iringa, Singida na Dodoma. Pia, Tume ilikagua vituo vya polisi 59, mahabusu za watoto 5 na Shule ya Maadilisho ili kijiridhisha na utekelezaji wa haki za binadamu.

31. Mheshimiwa Spika, Tume ilipokea na kufanya uchunguzi wa malalamiko 7,101 yanayahusu ukiukwaji wa haki za binadamu na kuhitimisha uchunguzi katika malalamiko 1,443 ambapo malalamiko mengine 5,658 yanaendelea kuchunguzwa. Baadhi ya malalamiko yalihusu kubambikiziwa kesi; ucheleweshaji wa upeleva, uendeshaji wa mashauri mahakmani, utoaji wa nakala za hukumu na utekelezaji wa amri za mahakama. Pia, kulikuwepo malalamiko ya migogoro ya ardhi, rushwa katika vyombo vya utoaji haki na katika masuala ya mirathi. Aidha, Tume iliendelea na utekelezaji wa Mpango Kazi wa Taifa wa Haki

za Binadamu (NHRAP) kwa kutoa mafunzo kwa maafisa wa Serikali kutoka katika mikoa mbalimbali, asasi za kiraia, watumishi wa Mahakama pamoja na watumishi wa Tume, kwa lengo la kuwajenjea uwezo wa kusimamia na kukuza haki za binadamu katika maeneo yao ya kazi.

Huduma ya Msaada wa sharia

32. Mheshimiwa Spika, Kwa kutambua umuhimu wa msaada wa kisheria katika kuimarisha upatikanaji haki nchini hususan kwa watu wasio na uwezo wa kumudu gharama za uwakili, Wizara ilichukua hatua ya kuzitambua na kuzisajili asasi zisizo za kiserikali zinazojihusisha na utoaji wa msaada wa kisheria. Katika kipindi hicho, Wizara ilifanya utambuzi wa zaidi ya asasi 290 zinazotoa msaada wa kisheria nchini na kuwasimamia wasaidizi wa kisheria (paralegals) zaidi ya 5,000. Pia, ilichukua hatua za kuweka mwongozo wa kisheria ambapo Bunge lako Tukufu lilitunga Sheria ya Msaada wa Kisheria na hivyo kuweka mfumo rasmi wa kisheria wa kusimamia upatikanaji na utoaji wa msaada wa kisheria kwa wananchi wasio na uwezo wa kugharamia huduma za kisheria

Utafiti wa Kisheria

33. Mheshimiwa Spika, Wizara inatambua nafasi ya utafiti katika maendeleo ya sheria ili kuwa na mfumo wenye kuakisi mahitaji halisi ya nchi kwa maendeleo na ustawi wa watu. Hivyo, kwa kutambua hilo, Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania imekamilisha utafiti wa Mfumo wa sheria zinazohusu hifadhi ya taarifa binafsi (review of legal framework on personal data protection in Tanzania); Mfumo wa sheria kuhusu haki za walaji na watumiaji wa bidhaa (review of legal framework on consumers' protection); na Sheria zinazohusu masuala ya usajili wa matukio muhimu ya binadamu (review of the legal framework on civil registration and vital statistics). Maeleo ya kina kuhusu hali ya utafiti wa kisheria kwa mwaka wa fedha 2016/17 yanapatikana katika *kiambatisho Na. 2(a) & 2(b)*.

Urejeshwaji wa wahalifu na ushirikiano na mataifa kwenye makosa ya jinai

34. Mheshimiwa Spika, Tanzania imeendelea kutekeleza wajibu wake kimataifa wa kushirikiana katika kupambana na uhalifu wa kimataifa kwa kurejesha watuhumiwa wa uhalifu katika nchi walikofanya makosa. Katika kutekeleza wajibu huu, Tanzania ilipokea maombi ya kuwarejesha watuhumiwa wanne katika nchi wanakotuhumiwa kutenda uhalifu, maombi 3 yanaendelea kufanyiwa kazi na maombi mengine 2 yalikataliwa kwa kutokidhi matakwa ya kisheria. Pia, kwa mujibu wa Sheria ya Ushirikiano katika Masuala ya Jinai (Mutual Assistance in Criminal Matters Act) nchi yetu ilipokea jumla maombi 12 ya kukusanya ushahidi na vielelezo. Maombi 4 yалиshughulikiwa na mengine 8 yanaendelea kufanyiwa uchambuzi. Aidha, Tanzania ilipeleka nje ya nchi maombi 2 ya kukusanya ushahidi na vielelezo ambayo yanaendelea kushughulikiwa husika.

Usajili, Ufilisi na Udhamini

Usajili wa Matukio Muhimu ya Binadamu

35. Mheshimiwa Spika, Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA), kwa kipindi cha Julai 2016 mpaka Machi 2017 umesajili matukio muhimu kama ifuatavyo:-

- (i) Kusajili na kutoa vyeti kwa watoto 869,182 wa umri wa chini ya miaka mitano katika mikoa saba ya Iringa, Njombe, Mbeya, Songwe, Mwanza, Geita na Shinyanga;
- (ii) Usajili wa watoto walio shulen 28,554 katika shule za msingi zilizopo kwenye halmashauri za Manispaa ya Ilala, Temeke, Kinondoni na Iringa,
- (iii) Kampeni ya usajili katika wilaya za Nzega na Tunduru ambapo jumla ya watu 23,160 walisajiliwa na kupewa vyeti;

- (iv) Kufanya usajili wa kawaida wa vizazi 348,544; na
- (v) Matukio ya vifo 50,213; ndoa 21,057 na talaka 85.

Aidha, jumla ya leseni mpya 2,877 za kufungishia ndoa zilitolewa; na leseni 1,618 kuhuishwa. Pia, RITA umeendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu masuala ya usajili wa matukio muhimu ya binadamu kwa wananchi.

Miunganisho ya Wadhamini

36. Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kupitia RITA imesajili jumla ya miunganisho 164 ya wadhamini wa vyama vya siasa, Makanisa, Misikiti na Mali za vikundi vya kijamii na kuendelea kusimamila mali zisizokuwa na wenyewe pamoja na masuala ya mirathi kulingana na amri za mahakama. Aldha, mapitio yamefanywa katika Bodi za Wadhamini za taasisi zilizosajiliwa ili kufahamu uhai wake na jumla ya taasisi 181 zilifutiwa usajili wake. Pia jumla ya wosia 50 zimeandikwa na kuhifadhiwa na huduma ya ushauri wa masuala ya wosia na mirathi imetolewa kwa wananchi kupitia kampeni maalumu. Orodha kamili ya bodi za wadhamini zilizofutwa inapatikana kwenye **kiambatisho Na.3.**

Taasisi za Mafunzo, Mipango na Miradi ya Maendeleo

Chuo cha Uongozi wa Mahakama- Lushoto

37. Mheshimiwa Spika, Chuo cha Uongozi wa Mahakama – Lushoto katika kutekeleza jukumu la kutoa elimu endelevu kwa watumishi wa mahakama na sekta ya sheria, kimeendelea kutoa mafunzo ya Astashahada na Stashahada kwa watumishi wa mahakama na jamii nzima kwa ujumla. Katika mwaka wa fedha wa 2016/17 Chuo kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo (UN Women) na Chama cha Majaji Wanawake Tanzania (TAWJA) kiliandaa kitabu cha kuratibu, kuendesha na kufundishia wakufunzi wa masuala ya Haki za Binaadamu na Mapambano dhidi ya Ukatili kwa

Wanawake na Watoto na hadi sasa kitabu hicho kimetumika kuendesha mafunzo kwa majaji, wasajili, mahakimu, askari polisi, askari magereza pamoja na wahadhiri wa Chuo hicho.

38. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2016/17, Chuo kiliendesha mafunzo kwa watumishi wa mahakama zaidi ya 400 ikiwemo mafunzo maalumu kwa majaji 24 waliojengewa uwezo na weledi wa namna ya kuendesha mashauri ya makosa ya rushwa na uhujumu uchumi. Vilevile, kiliandaa na kuendesha mafunzo ya namna ya kufanya upelelezi na kuendesha ya namna ya kushughulikia mashauri ya ujangili kwa mahakimu 30, mawakili wa serikali 10, askari polisi watano na askari wa wanyama pori watano.

Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo

39. Mheshimiwa Spika, Taasisiimeendelea kuongeza uwezo wake wa kudahili wanafunzi katika makundi (cohorts) mbalimbali. Katika mwaka wa Fedha wa 2016/17 ilidahili jumla ya wanafunzi 1,680 katika makundi matatu, kundi la 22, 23 na 24. Kwa sasa, Taasisi ina jumla ya wanafunzi 2,234 ambao wamesajiliwa katika makundi manne (4) yaliyo katika hatua tofauti za mafunzo. Taasisi hii imeendelea kujimarisha katika masuala ya utafiti, kutoa huduma za udahili kwa njia za kielektroniki na kuendesha huduma za maktaba ya kisasa inayohifadhi zaidi ya nakala 7,000 za vitabu na machapisho ya aina mbalimbali.

Maendeleo ya Rasilimali Watu

40. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kusimamia watumishi wake ili kuhakikisha wanatekeleza wajibu wao kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu za utumishi wa umma. Wizara imechukua hatua za kinidhamu dhidi ya watumishi waliokiuka maadili ya kazi kwa baadhi yao kupewa onyo, kushushwa vyeo, na wengine kufukuzwa kazi. Aidha, Wizara iliajiri, kuthibitisha kazini na kupandisha vyeo kwa watumishi wote waliostahili. Ninatoa wito kwa watumishi wote kuzingatia nidhamu ya kazi na kutekeleza majukumu yao kwa juhudni, maarifa na weledi ili kufanikisha

malengo ya wizara ya kuwatumikia wananchi kwa kutoa huduma zilizo bora.

Mipango na Miradi ya Maendeleo

41. Mheshimiwa Spika, ni dhamira ya Wizara yangu kusogeza huduma za kisheria karibu na wananchi kwa kubuni na kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo na kwa kuimarisha ushirikiano na wadau wa maendeleo. Katika mwaka wa fedha wa 2016/17, Wizara inatekeleza miradi na programu mpya za maendeleo zikiwemo (a) Programu ya Maboresho ya Mahakama, (b) Mradi wa Kuimarisha Mfumo wa Upatikanaji Haki Nchini (Strengthening Access to Justice and Human Rights Protection in Tanzania) na (c) Programu ya Ulinzi na Upatikanaji wa Haki ya Mtoto. Maboresho ya mahakama ni programu ya miaka mitano inayoteklezwa na Serikali ya Tanzania kwa fedha kutoka Banki ya Dunia kwa madhumuni ya kuimarisha mfumo wa mahakama, upatikanaji na ubora wa huduma za mahakama nchini.

42. Mheshimiwa Spika, Programu inayohusu upatikanaji haki nchini ni sehemu ya Mpango wa Maendeleo wa Umoja wa Mataifa unaojulikana kama UNDAP II. Wizara kwa kushirikiana na UNDP imeandaa Andiko la Mradi na Mpango Kazi kwa Kipindi cha mwaka wa fedha 2017/18 ambapo kupitia programu ya UNDAP II, Tanzania itaendelea kutekeleza Mradi wa Usajili wa Watoto wa Umri Chini ya Miaka Mitano (U5BRI); Mradi wa Kudhibiti Vitendo vya Ukatili wa Kijinsia kwa Wanawake na Watoto; kukuza na hulinda haki za binadamu; pamoja na usimamizi wa mfumo wa utoaji haki nchini.

E. MAFANIKIO YALIYOPATIKANA

43. Mheshimiwa Spika, mafanikio yaliyopatikana kutohana na utekelezaji wa vipaumbele vya Wizara kwa mwaka 2016/2017 ni pamoja na, kuanzishwa kwa Divisheni ya Mahakama Kuu ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi; kukamilika kwa mfumo wa kisheria wa kusimamia na kuratibu utoaji wa msaada wa kisheria nchini; kutungwa kwa kwa sheria ya upatikanaji wa taarifa; kuendelea kusimamia mashauri yote ya jinai na madai; Kumalizika kwa mashauri

yote ya uchaguzi wa Ubunge na Udiwani kwa wakati kama ilivyo takwa la kisheria; kuweka mfumo wa usajili wa vizazi kwa watoto walio na umri chini ya miaka mitano katika mikoa saba ya Geita, Iringa Mbeya, Mwanza, Njombe, Shinyanga, na Songwe; Ujenzi na ukarabati wa majengo ya mahakama katika ngazi mbalimbali; Kufanya utafiti na kuhuisha sheria mbalimbali ili kuakisi mahitaji halisi kwa maendeleo na ustawi wa watu; Kuongezeka kwa matumizi ya TEHAMA katika utoaji wa huduma; na Ufuatiliaji wa hali za wafungwa na mahabusu magerezani uliopelekea kufanyika kwa maboresho ya huduma kwa wafungwa na mahabusu.

44. Mheshimiwa Spika, mafanikio engine ni pamoja na kukamilisha uhakiki wa watumishi wote wa Wizara; kuimarika kwa usimamizi wa rasillimali watu na huduma kwa watumishi ikiwa ni pamoja na kuboresha mazingira ya kazi; Kuendelea kusimamia maadili ya watumishi; Kukamilika kwa rasimu ya mkakati wa kitaifa wa usajili wa matukio muhimu ya binadamu na takwimu ambayo ipo katika hatua za maamuzi Serikalini; kukamilika kwa mfumo wa TEHAMA unaowezesha ubadilishanaji wa taarifa kati ya RITA, Tume ya Uchaguzi na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa; na kuendelea kutoa mafunzo ya uanasheria kwa vitendo. Nipende kusisitiza kuwa Wizara inatambua kwamba pamoja na mafanikio yaliyopatikana, yapo maeneo ambayo bado yanahitaji kufanyiwa kazi ili kufikia malengo tuliojijiwekea. Hivyo, Wizara yangu itahakikisha kuwa kazi mbalimbali zilizosalia zinakamilishwa sanjari na utekelezaji wa vipaumbele vya mwaka wa fedha 2017/18.

F. MTIRIRIKO WA MAPATO NA MADUHULI YA SERIKALI

45. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2016/17 Wizara ya Katiba na Sheria iliidhinishiwa jumla ya Shilingi 155,192,263,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, mishahara ni Shilingi 67,328,697,000 na matumizi mengineyo (OC) ni Shilingi

50,404,380,000. Fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo ni Shilingi 37,459,186,000 ambapo kati ya fedha hizo, Shilingi 13,919,000,000 ni fedha za ndani na Shilingi 23,540,186,000 ni fedha za nje.

46. Mheshimiwa Spika, Hadi kufikia mwezi Machi, 2017, Wizara ilipokea jumla ya Shilingi 80,503,233,855 sawa na asilimia 52 ya fedha zilizoidhinishwa. Kati ya hizo Shilingi 45,545,485,311 ni mishahara ya watumishi na Shilingi 31,434,746,899 ni kwa matumizi mengineyo, sawa na asilimia 62. Fedha za maendeleo ni Shilingi 3,523,001,645 sawa na asilimia 9 ya bajeti ya miradi, ambapo fedha za ndani ni Shilingi 246,882,000 na fedha za nje ni Shilingi 3,276,119,645. Aidha, katika mwaka wa fedha 2016/2017, Wizara ilipanga kukusanya jumla ya Shilingi 17,085,829,511 kama maduhuli ya Serikali kutoka vyanzo mbalimbali vinavyosimamiwa na Wizara. Kufikia mwezi Machi, 2017 Wizara ilikusanya jumla ya Shilingi 10,976,126,511 sawa na asilimia 64 ya makadirio yote.

G. CHANGAMOTO NA MIKAKATI ILIYOPO

47. Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2016/17, kumekuwepo na changamoto mbalimbali ambazo ni pamoja na upungufu wa rasilimali muhimu ikiwemo fedha, watu na vitendea kazi; uchakavu na uhaba wa miundombini ya mahakama; mahitaji ya TEHAMA katika usimamizi wa mashauri; uelewa mdogo wa jamii kuhusu haki na wajibu wa raia; kuwepo kwa uhalifu unaokutumia teknolojia za kisasa na kuhusisha nchi zaidi ya moja.

48. Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na changamoto hizo, Wizara yangu iliendelea kubuni na kutekeleza mikakati mbalimbali ya kukabiliana nazo katika kuhakikisha kuwa nchi inakuwa na mfumo imara kikatiba na kisheria ili kufanikisha mipango ya maendeleo ya Taifa. Mikakati hiyo ni pamoja na:

- (a) Kuendelea kushirikiana na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, katika

kuyapatia ufumbuzi matatizo yanayohusiana na upungufu wa watumishi, ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa vibali vya ajira, kujaza nafasi zilizoachwa wazi na kushughulikia maslahi ya watumishi;

- (b) Kutafuta vyanzo vipyta vya mapato ili kufanikisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo ukiwemo mradi wa e-Justice na Programu ya Maboresho ya Mfumo wa Mahakama;
- (c) Kuendelea kubana matumizi na kuelpukana na matumizi yasiyo ya lazima kufanyika kwa wakati uliopo;
- (d) Kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika utoajihuduma za kisheria na ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali;
- (e) Kuwajengea uwezo watumishi wa sekta ya sheria katika kukabiliana na aina mpya za halifu.
- (f) Kuboresha huduma za mafunzo ya uanasheria kwa vitendo;
- (g) Kutumia teknolojia ya gharama nafuu katika ujenzi wa miundombinu ya mahakama ili kukabiliana na ukubwa wa gharama za utekelezaji wa miradi ya maendeleo; na
- (h) Kuimarisha mfumo wa usimamizi, ufuatiliaji na tathmini ya kazi za Wizara.

49. Mheshimiwa Spika, mafaniko katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Katiba na Sheria yamewezekana kutokana na ushirikiano thabiti wa wadau wa maendeleo ambao wameendelea kutupatia katika utekelezaji wa

programu na miradi mbalimbali ya maendeleo. Kwa namna ya pekee, nichukuwe fursa hii kuwashukuru Benki ya Dunia (WB); Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo (UNDP); Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF); Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wanawake (UN Women); Shirika la Msaada wa Maendeleo la Kimataifa la Uingereza (DfID) na Taasisi ya Bloomberg Data for Health Initiative. Napenda kuwahakikisha wote kwamba, Wizara yangu inathamini sana michango wao na tutaendelea kutoa ushirikiano na kuhakikisha kwamba mipango na malengo ya Serikali kuhusu sekta ya sheria yanafikiwa.

50. Mheshimiwa Spika, nitakuwa mchoyo wa fadhila nisipotambua kazi kubwa iliyofanywa na viongozi wenzangu katika Wizara. Hivyo, kwa moyo wa dhati, napenda nimshukuru Prof. Sifuni E. Mchome, Katibu Mkuu na Bw. Amon A. Mpanju, Naibu Katibu Mkuu; viongozi wakuu na wataalam wa taasisi zote zilizo chini ya Wizara yangu kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa katika kutekeleza majukumu yangu ya kila siku. Vilevile, naishukuru sana familia yangu kwa kuendelea kunifariji na kunitia moyo wakati wote wa utekelezaji wa majukumu mazito yanayoambatana na wadhifa wa uwaziri wa Katiba na Sheria.

H. MPANGO NA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA 2017/18

51. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2017/18 Wizara yangu itaendelea na juhudzi za kuimarisha utawala wa sheria na misingi ya haki za binadamu kwa kuhakikisha kuwa wananchi wanapata huduma bora na za uhakika. Katika kufanikisha azma hiyo, Wizara imeainisha maeneo mahususi ya kipaumbele kwa mwaka wa fedha ujao, kama ifuatavyo:-

(a) Wizara ya Katiba na Sheria

- i. Kukamilisha uhamishaji wa Makao Makuu ya Wizara kutoka Dar es Salaam kwenda Dodoma;

- ii. Kuratibu masuala ya kisera katika Wizara na taasisi zake;
- iii. Kuratibu na kusimamia utoaji wa huduma ya msaada wa kisheria nchini;
- iv. Kuimarisha usimamizi na ufuutiliaji wa masuala ya Katiba na sheria;
- v. Kusimamia utekelezaji wa haki za binadamu kitaifa, kikanda na kimataifa; na
- vi. Kuwajenyea uwezo watumishi, kuendeleza ubunifu, maarifa na weledi ili kuleta tija na ufanisi.

(b) Mahakama ya Tanzania

- i. Kuharakisha usikilizaji wa mashauri;
- ii. Kuimarisha utawala bora, maadili na uwajibikaji;
- iii. Kuboresha mazingira ya kufanya kazi kwa kuongeza upatikanaji wa vitendea kazi muhimu;
- vii. Kujenga na kukarabati miundombinu katika ngazi mbalimbali;
- viii. Kuongeza matumizi ya TEHAMA ili kurahisisha usikilizaji wa mashauri na shughuli za utawala ili kufikisha huduma kwa wananchi;
- ix. Kuimarisha uwezo katika ukaguzi na usimamizi wa shughuli za kimahakama; na
- x. Kuendelea kuimarisha uwezo wa rasilimali watu.

(c) Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali

- i. Kuimarisha mfumo wa uandishi na urekebu wa sheria;
- ii. Kusimamia shughuli za uendeshaji wa mashauri ya jinai, madai, katiba na haki za binadamu;
- iii. Kuimarisha usimamizi wa masuala ya mikataba; na
- iv. Kuongeza matumizi ya TEHAMA katka utoaji wa huduma.

(d) Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora

- i. Kukuza na kutetea haki za binadamu hususan haki za makundi yenye mahitaji maalum;
- ii. Kuongeza uelewa wa haki za binadamu, utawala bora, na wajibu wa raia;
- iii. Kufanya uchunguzi wa malalamiko na kuyapatia ufumbuzi kwa njia ya upatanishi na usuluhishi;
- iv. Kushirikiana na wadau mbalimbali nchini, kikanda na kimataifa kwenye masuala ya haki za binadamu na utawala bora; na
- v. Kujenga Uwezo wa watumishi.

(e) Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania

- i. Kukamilisha utafiti kuhusu mfumo wa sheria za usimamizi wa haki jinai (Review of Legal

Framework on Criminal Justice Administration);

- ii. Kufanya utafiti kuhusu mfumo wa sheria za ushahidi (Review of Legal Framework on Law of Evidence); na
- iii. Kufanya utafiti kuhusu mfumo wa sheria za usuluhishi (Review of Legal Framework on Arbitration).

(f) Tume ya Utumishi wa Mahakama

- i. Kuboresha utoaji wa huduma za Mahakama kwa kuongeza idadi ya watumishi wa Mahakama wenye weledi na sifa stahiki;
- ii. Kuboresha mazingira ya kazi kwa kununua vitendea kazi pamoja na samani za ofisi;
- iii. Kuimarisha nidhamu na maadili ya watumishi wa Mahakama kwa kufanya ukaguzi wa Kamati za Maadili za Mahakama; na
- iv. Kuwajengea uwezo wajumbe pamoja na watumishi wa Tume kwa kuwawezesha kuhudhuria mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu.

(g) Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini

- i. Kutekeleza Mkakati wa Kitaifa wa Usajili wa Matukio Muhimu ya Binadamu.
- ii. Kufanya mapitio ya sheria zinazohusu ufilisi (review of legal framework on insolvency);
- iii. Kuimarisha matumizi ya teknolojia katika kuboresha utoaji wa huduma; na

- iv. Kuimarisha ukusanyaji na usimamizi wa maduhuli ya Serikali.

(h) Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo

- i. Kudahili na kutoa mafunzo kwa wanafunzi 1,800 ili kuongeza idadi ya wataalam wa sheria nchini;
- ii. Kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa mawakili na wadau wengine katika mambo mapya yanaoyojitokeza katika taaluma ya sheria (Continuing Legal Education),
- iii. Kuendesha programu za mafunzo kwa wasaidizi wa sheria (paralegals); na
- iv. Kuimarisha miundombinu ya taasisi.

(i) Chuo cha Uongozi wa Mahakama – Lushoto

- i. Kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa majaji na mahakimu; na
- ii. Kuimarisha na kuendelea kutoa mafunzo endelevu ya kimahakama pamoja na mafunzo kazini kwa watumishi wa mahakama na watumishi wote wa sekta ya sheria kwa ujumla.

52. Mheshimiwa Spika, ili kufanikisha utekelezaji wa vipaumbele hivi, Wizara yangu inaomba kuidhinishiwa jumla

ya Shilingi 166,479,908,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo. Mchanganuo wa makadirio ya bajeti kwa mafungu saba ya Wizara na taasisi zake ni kama ifuatayo:

Na.	Fungu la Matumizi	Bajeti 2017/18
	Mishahara yaWatumishi	- Sh. 76,441,279,000
	Matumizi Mengineyo	- Sh. 66,801,799,000
	Miradi ya Maendeleo	- Sh. 23,236,830,000
JUMLA		Sh. 166,479,908,000

53. Mheshimiwa Spika, kiasi hicho cha fedha kinaombwa kuititia mafungu ya bajeti yaliyo chini ya Wizara kama inavyoainishwa hapa chini.

Fungu 12	-	Tume ya Utumishi wa Mahakama	-	1,102,911,000
Fungu 16	-	Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali	-	7,282,523,000
Fungu 35	-	Divisheni ya Mashtaka	-	14,914,063,000
Fungu 40	-	Mfuko wa Mahakama	-	125,117,029,000
Fungu 41		Wzara ya Katiba na Sheria	-	9,862,066,000
Fungu 55	-	Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora	-	6,166,981,000
Fungu 59	-	Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania	-	2,034,335,000
JUMLA				166,479,908,000

(a) Muhtasari wa Matumizi

54. Mheshimiwa Spika, mchanganuo wa matumizi ya bajeti kwa kila Fungu ni kama ifuatavyo:-

(i) Fungu 12: Tume ya Utumishi wa Mahakama		
Matumizi ya Mishahara	-	Sh. 282,404,000
Matumizi Mengineyo	-	Sh. 820,507,000
Matumizi ya Maendeleo (Ndani)	-	Sh. 0
Matumizi ya Maendeleo (Nje)	-	Sh. 0
Jumla	-	Sh. 1,102,911,000

(ii) Fungu 35: Divisheni ya Mashtaka

Matumizi ya Mishahara	-	Sh. 3,863,792,000
Matumizi Mengineyo	-	Sh. 3,418,731,000
Matumizi ya Maendeleo (Ndani)	-	Sh. 0
Matumizi ya Maendeleo (Nje)	-	Sh. 0
Jumla	-	Sh. 7,282,523,000

(iii) Fungu 35: Divisheni ya Mashtaka

Matumizi ya Mishahara	-	Sh. 9,478,238,000
Matumizi Mengineyo	-	Sh. 5,435,825,000
Matumizi ya Maendeleo (Ndani)	-	0
Matumizi ya Maendeleo (Nje)	-	0
Jumla	-	14,914,063,000

(iv) Fungu 40: Mfuko wa Mahakama

Matumizi ya Mishahara	-	Sh. 54,524,408,000
Matumizi Mengineyo	-	Sh. 52,434,610,000
Matumizi ya Maendeleo (Ndani)	-	Sh. 17,000,000,000
Matumizi ya Maendeleo (Nje	-	Sh. 1,158,011,000
Jumla	-	Sh. 125,117,029,000

(vii) Fungu 59: Tume ya Kurekebisha Sheria

Matumizi ya Mishahara	-	Sh. 1,066,606,000
Matumizi Mengineyo	-	Sh. 967,729,000
Matumizi ya Maendeleo (Ndani)	-	Sh. 0
Matumizi ya Maendeleo (Nje)	-	Sh. 0
Jumla	-	Sh. 2,034,335,000

(b) *Makusanyo ya Maduhuli ya Serikali*

55. **Mheshimwa Mwenyekiti**, katika mwaka wa fedha 2017/2018 Wizara yangu inatarajia kukusanya kiasi cha Shilingi 24,087,507,200 ikiwa ni maduhuli ya Serikali kutokana na vyanzo mbalimbali vya mapato inavyovisimamia, kama inavyoainishwa kwenye jedwali hapa chini:-

Fungu 16	-	Sh. 3,002,000
Fungu 35	-	Sh. 13,002,000
Fungu 40	-	Sh. 9,318,061,200
Fungu 41	-	Sh. 14,753,292,000
Fungu 59	-	Sh. 150,000
JUMLA		Sh. 24,087,507,200

56. **Mheshimiwa Spika**, mchanganuo wa maombi ya fedha za bajeti ya kila Fungu umeainishwa kwenye vitabu vya KASMA za mafungu husika ambavyo wajumbe wa Bunge lako Tukufu wamegawiwa.

57. **Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.

MWENYEKITI: Tunakushukuru Waziri. Namuita sasa Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria, ambayo ndiyo imefanya kazi ya kuchambua utekelezaji wa bajeti ya sasa na maombi ya mwaka ujao wa fedha. Namuona Mwenyekiti mwenyewe Mheshimiwa Mchengerwa.

MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa hii ni mara yangu ya kwanza kusoma taarifa hii ya Kamati ya Kudumu ya Bunge, kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka huu wa fedha 2016/2017, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu makadirio ya mapato na matumizi, niruhusu kwanza nimshukuru sana Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kunijaalia uhai, afya njema na kunipa fursa ya kuwasilisha taarifa hii mbele ya Bunge lako Tukufu.

Pili, niendelee kuwapa pole wananchi wa Mkoa wa Pwani hususan Wilaya ya Rufiji, Mkuranga na Kibiti kwa taharuki ya ujambazi na nina imani kubwa sana na Serikali kwamba matatizo haya yatakwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mara nyiningine tena napenda kumpongeza aliyekuwa Mjumbe wa Kamati yangu hii ya Katiba na Sheria Profesa Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi, ambaye ameteuliwa na kupewa dhamana ya kuongoza Wizara hii muhimu ya Katiba na Sheria. Profesa Kabudi ni jungu la sheria, Kamati inamtakia kila la kheri katika kutekeleza majukumu yake mapya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo Januari, 2016, naomba kuwasilisha taarifa sasa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka wa fedha 2016/2017 pamoja na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Muheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa kifungu cha 6 (2) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge

Toleo Januari 2016, Kamati ya Katiba na Sheria ina jukumu la kusimamia Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na taasisi zake sita zifuatazo:-

- (i) Wizara ya Katiba na Sheria Fungu Na. 41;
- (ii) Mwanasheria Mkuu wa Serikali Fungu Na. 16;
- (iii) Mkurugenzi Mkuu wa Mashtaka Fungu Na. 35;
- (iv) Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora Fungu Na. 55;
- (v) Tume ya Kurekebisha Sheria Fungu Na. 59; na
- (vi) Tume ya Utumishi wa Mahakama Fungu Na. 12.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hii inatoa maelezo kuhusu maeneo makubwa matano yafuatayo:-

- (i) Ugaguzi wa Miradi ya Maendeleo kwa mujibu wa Kanuni ya 98 Kanuni ndogo ya kwanza ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo Januari, 2016.
- (ii) Utekelezaji wa mapendekezo na ushauri wa Kamati kwa mwaka wa fedha 2016/2017.
- (iii) Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti wa mwaka wa fedha 2016/2017.
- (iv) Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2017/2018, pamoja na Taasisi zilizo chini yake.
- (v) Maoni na ushauri wa Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ugaguzi wa miradi iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha 2016/2017; tarehe 22 Machi, 2017, Kamati ilipata fursa ya kutembelea Ofisi za Haki za Binadamu na Utawala Bora, Fungu Namba 55 zilizoko

Wete - Pemba na kupokea taarifa ya utekelezaji wa shughuli za Tume kwa upande wa Pemba. Mpaka kufikia Machi, 2017 gharama za upangishaji na ukarabati wa jengo ziliflikia shilingi milioni 40 ambazo zimekuwa zikitolewa kwa awamu, kuanzia mwaka wa fedha 2010 mpaka 2011. Baada ya kufanya ziara hiyo, Kamati imeridhishwa na ukarabati na hali halisi ya mazingira ya ofisi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Kamati kuridhishwa na hali halisi ya ukarabati na mazingira ya ofisi, kuna changamoto za kiutendaji kwa kuwa na watumishi wawili tu. Mmoja ni Afisa na mwingine ni Mlinzi ambao wapo katika ofisi hiyo toka ilipoanzishwa katika mwaka wa fedha 2010/2011. Hivyo ofisi hii inaendelea kuwa na changamoto nyingi za kiutendaji kutokana na upungufu wa watendaji. Changamoto hii kwa kiasi kikubwa imeathiri sana utekelezaji wa majukumu ya Tume kwa upande wa Pemba. Katika kutatua changamoto hiyo kiutendaji, Kamati imearifiwa kwamba kutokana na ongezeko la fedha katika Bajeti ya Tume katika mwaka wa fedha 2017/2018, watumishi wawili wataongezwa katika ofisi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maoni ya jumla kuhusu utekelezaji wa miradi ya maendeleo; Kamati hajjaridhishwa na kasi ya utoaji wa fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Karibu miradi yote iliyotengewa fedha imepokea sehemu tu ya fedha iliyoidhinishwa kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Vilevile Kamati inasikitishwa sana na hatua ya Serikali kutotoa fedha za ndani kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Miradi mingi ya maedeleo imekuwa inategemea fedha za nje kwa kiasi kikubwa. Mfano, Wizara ya Katiba na Sheria Fungu la 41 limepokea fedha za nje toka kwa ajili ya miradi Namba 6201 wa *e-Justice* kiasi cha shilingi bilioni moja na mradi namba 6517 *UNICEF Support to Multisectoral Program* ilipokea shilingi 396,472,613 zote zikiwa ni fedha za nje. Hapakuwa na fedha ya ndani yoyote iliyotolewa kwa ajili ya miradi hii yote. Hali hii pia imejitokeza kwenye Mirada mingi katika taasisi zilizo chini ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kukabiliana na changamoto za ukosefu wa fedha za ndani za kutosha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo, upo umuhimu kwa kila taasisi ya Serikali kubuni vyanzo vya mapato vitakavyosaidia kuongeza fedha za ndani ili kuepuka utegemezi wa fedha za nje. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 68 (2) Kanuni ya Kudumu ya Bunge iliyotolewa Januari, 2016, Kamati ilikutana Mjini Dodoma tarehe 31 Machi, 2017 mpaka tarehe 1 Aprili, 2017 kwa ajili ya uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa mpango wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2016/2017, pamoja na uchambuzi wa makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uchambuzi wa utekelezaji mpango wa bajeti wa Wizara hii, Kamati ilizingatia ulinganisho wa kiasi cha fedha zilizoidhiniwa na Bunge lako Tukufu Mei mwaka 2016 na kiwango ambacho kimepokelewa hadi kufikia Machi, 2017. Lengo la kufanya tathmini ya namna hii ni kufahamu mwelekeo wa mpango wa bajeti wa mapato na matumizi ya Serikali katika mwaka wa fedha 2016/2017 na kujua vipaumbele vya bajeti katika mwaka wa fedha unaofuata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2016/2017 Wizara ya Katiba na Sheria kwa ujumla iliidhinishiwa shilingi 191,450,901,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maedeleo, kati ya fedha hizo shilingi 65,949,643,300, kwa ajili ya mishahara na shilingi 108,562,097,961, kwa ajili ya matumizi mengineyo. Hadi kufikia mwezi Disemba mwaka 2016 Wizara ilipokea jumla ya shilingi 97,255,506,269, ikiwa ni asilimia 51 zilizoidhinishwa katika Bunge liliopita kama jedwali namba moja linaloonesha mlinganisho wa fedha iliyotengwa na kupokelewa katika mwaka wa fedha 2016/2017.

Mhesmiwa Mwenyekiti, Kamati inatoa wito kwa ofisi ya Hazina kutoa kiasi cha fedha kilichobaki ambacho kiliidhinishwa na Bunge lako Tukufu kwa Wizara hii ya Katiba

na Sheria katika kipindi kilichobaki kwa mwaka wa fedha wa 2016/2017 ili Wizara iweze kumaliza kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kama ilivyopangwa.

Mchanganuo wa fedha zilizoidhinishwa na zilizopokelewa katika mwaka wa fedha 2016/2017 hadi kufikia Machi, 2017 katika mafungu sita yaliyosimamiwa na Wizara hii, Fungu Namba 41, Fungu Namba 16, Fungu Namba 35, Fungu Namba 59, Fungu Namba 55 na Fungu Namba 12 umeainishwa kwenye jedwali kama ilivyoorodheshwa hapo chini jedwali namba mbili linaloonesha mlinganisho wa fedha iliyoidhinishwa na kupokelewa kwa mwaka wa fedha 2016/2017 hadi kufikia mwezi Machi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mlinganisho uliooneshwa katika jedwali namba mbili, inaonesha kwamba Fungu Namba 35 ndilo lillotengewa fedha nyangi zaidi ambayo ni shilingi 13,097, 619,000 kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Hata hivyo, hadi kufikia mwezi Machi, 2017 Fungu hili limepokea kiasi cha shilingi 7,955,545,061. Ukiangalia kiasi hicho cha fedha kilichotolewa ni pungufu ya asilimia 39 ya fedha ambazo ziliidhinishwa na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mlinganisho huo, Tume ya Utumishi wa Mahakama - Fungu Namba 12 liliidhinishiwa fedha kidogo zaidi kuliko mafungu mengine kwa kiasi cha shilingi 1,134,955,000, pamoja na kuidhinishiwa fedha hizo kidogo hadi kufikia mwezi Machi, 2017 fungu hili limepokea shilingi 609,858,475 tu. Ukiangalia kiasi hiki cha fedha kilichotolewa kinaashiria kwamba ni asilimia 53 tu ya fedha ambayo imetolewa na pungufu ya asilimia 47 ambayo ilitengwa na Bunge lako hili Tukufu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwenendo huu wa upokeaji wa fedha kwa ujumla unadhihirisha kuwa, fedha inayotolewa ni kidogo sana ukilinganisha na kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na Bunge lako Tukufu. Hivyo Taasisi hizi zinashindwa kutekeleza majukumu yake kwa wakati na ufanisi kutokana na ucheleweshwaji wa utoaji wa fedha kwa upande wa Hazina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa uchambuzi wa taarifa kuhusu ukusanyaji wa maduhuli kwa mwaka wa fedha 2016/2017; kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Taasisi zake ilitarajia kukusanya kiasi cha shilingi 17,085,879,511, kama maduhuli ya Serikali kutoka vyanzo mbalimbali yya mapato, hadi kufikia Disemba, 2016 Wizara ilikuwa imekusanya kiasi cha shilingi 10,943,491,845 sawa na asilimia 64 ya makusanyo yaliyotarajiwa kama ilivyochanganuliwa kwenye jedwali namba tatu. Makusanyo haya ni kutokana na ada mbalimbali za usajili wa matukio, ada za wanafunzi, uuzaji wa vitabu vya zabuni na huduma nyingine mbalimbali zilizotolewa na Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Katiba na Sheria Fungu Namba 41, imeongoza katika ukusanyaji wa maduhuli kwa kukusanya shillingi 5,599,313,845, ikifuatiwa na Idara ya Mahakama Fungu Namba 40 iliyokusanya shillingi 5,344,178,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafungu mengine yalikuwa na matarajio ya kukusanya maduhuli lakini hayakuwa kama yalivyopangwa. Hii ni changamoto ambayo Wizara, taasisi zote zenye vyanzo vya mapato zinazidi kuangalia kwa umakini kwani matarajio siyo mapato, hivyo kuna umuhimu wa kubuni vyanzo vingine vya ukusanyaji wa maduhuli ili kuongeza upatikanaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara hizi hasa kwa zile taasisi zilizokosa mapato kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapitio ya utekelezaji wa ushauri wa Kamati ni kuwa wakati wa uwasilishwaji wa makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Kamati ilitoa ushauri na mapendekezo 16 kuhusiana na Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na taasisi zake. Kamati imefurahishwa na utekelezaji wa maoni ya Kamati yaliyotolewa katika taarifa ya uchambuzi wa bajeti kwa Wizara hii Mei, 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo mahsusni ambalo

Kamati imeridhika nalo ni ongezeko kidogo kwenye bajeti na utekelezaji wa majukumu ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, ambayo imetengewa shilingi 1,566,080,000, katika mwaka ujao wa fedha 2017/2018 kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC) ikilinganishwa na mwaka wa fedha uliopita ambaao Tume hii iliidhinishiwa shilingi 994,500,014, tu kwa ajili ya matumizi mengineyo ambayo ilikuwa ni ndogo na haikulingana na uzito wa majukumu ya Tume kuhakikisha Haki ya Binadamu na Utawala Bora zinazingatiwa. Tofauti hii ni ya ongezeko la asilimia 57 ya bajeti inayoombwa kuidhinishwa kwa ajili ya Tume katika mwaka wa fedha unaokuja. Hata hivyo, fedha ilioidhinishwa haitoshelezi ikilinganishwa na majukumu yanayopaswa kutekelezwa na Tume hii katika nchi yetu. Kamati inaishauri Serikali kuendelea kuongeza fedha za kutosha kwa ajili ya Tume ili kutekeleza majukumu yake kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la mpango wa makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2017/2018; kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Wizara ya Katiba na Sheria imejiwekea malengo saba ya utekelezaji ili kuongeza ufanisi na ubora katika utoaji huduma za kisheria na masuala ya Katiba yakiwemo:-

Kwanza, ni kuendelea na uhamasishaji wa shughuli za Serikali kutoka Dar es Salaam kwenda Makao Makuu ya Nchi Dodoma.

Pili, ni kuimarisha mfumo wa Sheria na kuongeza uwezo wa Wizara katika maeneo maalum ya sheria pamoja na usimamizi wa utoaji haki.

Tatu, kuimarisha usimamizi na ufuatilaji wa masuala ya Katiba na Sheria na jambo la nne ni kuimarisha misingi ya haki za binadamu na kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inakubaliana na malengo ya Wizara kwa ujumla kwani yanalenga katika kuboresha utekelezaji wa majukumu yake na kuleta ufanisi zaidi katika suala zima la utoaji haki nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu makadirio ya mapato ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka wa fedha 2017/2018; kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Wizara inatarajia kukusanya kiasi cha shilingi 24,087,507,200, ikiwa ni maduhuli ya Serikali kama inavyoonekana katika jedwali namba nne ambalo linazungumzia matarajio ya maduhuli kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imebaini kuwa makadirio ya mapato hayaendani na hali halisi ya makusanyo, hivyo Kamati inashauri kuwa ni vizuri kuweka makadirio madogo yenye uhakika katika kukusanya kuliko kuweka makadirio makubwa ya fedha ambayo hayana matarajio makubwa katika kukusanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Haki za Binadamu na Utawa Bora - Fungu Namba 55, na Tume ya Utumishi wa Mahakama - Fungu Namba 12 hayana matarajio yoyote ya kukusanya maduhuli kwa sababu ya kutokuwa na vyanzo vya mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uchambuzi wa makadirio ya matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka wa fedha 2017/2018; katika mwaka wa fedha wa 2017/2018, Wizara pamoja taasisi zake inaomba kuidhinishiwa shilingi 159,331,822,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo ambayo ni upungufu wa asilimi 4.4 ikilinganishwa na bajeti ya mwaka wa fedha 2016/2017. Upungufu huu wa asilimia 4.4. unatokana na ukomo wa bajeti ya fedha za maendeleo kupungua kwa asilimia 55 ikilinganishwa na fedha za miradi ya maendeleo zilizoidhinishwa mwaka 2016/2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na taasisi zake kwa mwaka wa fedha wa 2017/2018 inaomba fedha kama ilivyooneshwa katika mchanganuo uliopo kwenye jedwali namba tano ambalo linaonesha uchambuzi wa makadirio ya matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka wa fedha 2017/2018 ambapo Wizara ya Katiba na Sheria - Fungu Namba 41 inaomba shilingi

9,862,066,000; Fungu Namba 16 - Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali inaomba shilingi 7,282,523,000 na Fungu Namba 35 - Divisheni ya Mashtaka inaomba shilingi 14,914,063,000 na Fungu Namba 12 - Tume ya Utumishi wa Mahakama inaomba shilingi 1,102,911,000; Fungu Namba 59 - Tume ya Kurekebisha Sheria inaomba shilingi 2,052,757,000 na Fungu Namba 55 - Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora inaomba shilingi 6,166,981,000. Jumla ya fedha zinazoombwa ni shilingi 41,381,301,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Divisheni ya Mashtaka - Fungu Namba 35 ina makadirio ya matumizi ya juu zaidi ikilinganishwa na mafungu mengine. Bajeti inayooombwa kwa ajili ya Fungu hili ni sawa na asilimia 37 ya bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2017/2018. Tume ya Utumishi wa Mahakama Fungu Namba 12 ina makadirio ya matumizi madogo zaldi ikilinganishwa na mafungu mengine ikiwa ni sawa na asilimia 3.2 ya bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na ushauri wa Kamati; kwa kuzingatia taarifa zilizowasilishwa mbele ya Kamati pamoja na majukumu ya Wizara ya Katiba na Sheria na taasisi zilizo chini yake, Kamati inatoa maoni na ushauri ufuatao ili kuboresha utendaji wa kazi na ufanisi katika kutekeleza majukumu ya Wizara hii:-

(i) Kamati inaipongeza Serikali kwa kuongeza bajeti ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora kwa fedha za matumizi mengineyo (*OC*) kutoka shilingi 994,000,514,000 katika mwaka wa fedha 2016/2017 hadi kufikia shilingi 1,566,080,000 katika mwaka wa fedha ujao 2017/2018. Ongezeko hili ni sawa na asilimia 57.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, Kamati inatoa rai kwa Wizara na taasisi zake kufanya rejea ya maagizo yaliyotolewa na Kamati katika taarifa ya mwaka wa fedha 2016/2017 na kuendelea kuyatekeleza katika kipindi cha robo ya mwisho wa mwaka huu unaoisha Juni, mwaka 2017.

(ii) Ofisi ya Hazina kutoa fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa Wizara husika kwa wakati ili kuiwezesha Wizara kutekeleza majukumu yake kama yalivyopangwa katika kila mwaka wa fedha.

(iii) Wizara kupitia Tume ya Kurekebisha Sheria kufanya mapitio ya maboresho yote ya msingi ya sheria zote zinazohitaji maboresho kutazama uwezekano wa kuhuisha mchakato wa upatikanaji wa Katiba Mpya kwa wakati muafaka. (*Makof*)

(iv) Wizara pamoja na taasisi zake kukamilisha kwa haraka utekelezaji wa mpango wa kuhamia Dodoma mapema iwezekanavyo ili kutekeleza uamuzi wa Serikali wa kuhamishia Makao Makuu ya nchi Dodoma.

(v) Kamati inatoa wito kwa Serikali kuleta Bungeni sheria mahsus ambayo itahalalisha utekelezaji wa maamuzi ya Serikali ya Awamu ya Tano ya kuufanya Mji wa Dodoma kuwa Makao Makuu ya nchi.

(vi) Tume ya Kurekebisha Sheria kuendelea kufanya mapitio ya sheria mbalimbali kwa lengo la kuzirekebisha na kuziboresha ili kuendana na mabadiliko mbalimbali tulitonayo sasa. Kamati inatoa rai kwa Tume kushirikiana na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ili kufanya mapitio ya Sheria ya Elimu kwa mwaka 1978 na kutazama uwezekano wa kuirekebisha ili kufanya elimu ya sekondari kuwa lazima na kuwawezesha vijana wanaomaliza elimu ya msingi kuendelea na elimu ya sekondari. Bila kusahau Tume pia kuweza kupitia Sheria ya Usalama Barabarani ambayo tunaona hatuelewi kuna kigugumizi gani, kwa nini sheria hii haitewti Bungeni kwa ajili ya marekebisho. Sheria hii imepitwa na wakati na ni sheria ya muda mrefu.

(vii) Serikali kuongeza ukomo wa bajeti kwa Wizara na taasisi zake katika mwaka ujao wa fedha ili ziweze kuanza utaratibu wa kujenga majengo ya ofisi zao katika Mji wa Kiserikali utakaojengwa Dodoma.

(viii) Wizara kuendelea kusimamia kwa ufanisi masuala yote ya haki za binadamu na upatikanaji wa haki nchini na kuhakikisha kwamba inachukua hatua za kutosha kupunguza wingi wa kesi mahakamani na wingi wa mahabusu katika rumande, jambo ambalo linavunja haki mbalimbali za watuhumiwa ambao wanakaa rumande kwa muda mrefu bila kesi zao zinazowahusu kusikilizwa na kumalizika kwa wakati. (*Makof*)

(ix) Serikali kuzingatia kwa umakini matakwa ya Ibara ya 13(6)(a) mpaka (e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 ambayo inatoa haki za msingi za kuhusiana na watuhumiwa wa makosa ya jinai ikijumuisha haki ya kupata dhamana, kusikilizwa kesi zao na kukata rufaa kwa wakati muafaka. Jambo hili ni la msingi sana kwa kuwa Ibara ya 13 iwapo ikikiukwa tunamaanisha kwamba zile *presumptions* zilizotolewa katika sheria zitakuwa zinakiukwa na watuhumiwa sasa watakuwa wametiwa hatiani kabla ya kusikilizwa kesi zao kama Ibara ya 13 inavyozungumza. (*Makof*)

(x) Wizara na Mhimili wa Mahakama kwa ujumla kuzingatia matakwa ya kisheria kuhusu uendeshaji wa kesi za jinai na hususani taratibu za utoaji wa dhamana kwa watuhumiwa kama zilivyowekwa katika kifungu cha 148 cha Sheria ya Mwenendo wa Kesi za Jinai iliyopitiwa kwa mwaka 2002 katika *Criminal Procedure Act*. Kamati inasisitiza kwamba dhamana ni haki ya mtuhumiwa na ni suala la Kikatiba hivyo taasisi za utoaji haki zinapaswa kuzingatia suala hili ili kutenda haki kwa watuhumiwa. Pia tunawakumbusha Mahakimu matumizi ya kifungu cha 222 mpaka 225 cha kesi ambazo zimekaa muda mrefu na ni jukumu lao Mahakimu kutenda haki kama ambavyo nimezungumza hapo. (*Makof*)

(xi) Serikali kuridhia na kutekeleza Mikataba mbalimbali ya Kimataifa iliyordhiwa na nchi yetu ili iweze kutekelezwa, kama vile mkataba wa Kimataifa wa mwaka 1984 unaopinga matumizi yote ya kikatili dhidi ya wanadamu (*Convention Against Torture*) sheria hii ya mwaka 1984.

(xii) Wakala wa Usajili na Ufilisi na Udhamini (*RITA*) kuendelea kufanya kazi kwa kuzingatia misingi ya sheria, taratibu na kanuni za uadilifu na weledi katika usajili wa Mabaraza ya Wadhamini wa vyama vya siasa au makundi mengine ya kijamii kwa kusimamia sheria, kanuni na taratibu zilizopo, hivyo kuepuka kuwa sehemu ya migogoro ya vyama hivyo. (*Makofi*)

(xiii) Wizara kuanzisha na kukamilisha mchakato wa upatikanaji wa Kanuni za Sheria za Utoaji wa Msaada wa Kisheria (*The Legal Aid Act*) iliyopitishwa na Bunge lako hili Tukufu katika Mkutano wa Sita wa Bunge uliofanyika mwezi Februari mwaka 2017. Hapa ninaipongeza Kamati ya Katiba na Sheria kwa ku-*pioneer* uundwaji wa sheria hii ambayo itakwenda kuwasaidia Wabunge wote ndani ya Bunge lako Tukufu katika maeneo yetu huko tunakotoka. (*Makofi*)

(xiv) Tume ya Utumishi wa Mahakama kusimamia kwa umakini mkubwa maslahi ya Mahakimu wote na hasa upandishwaji wa vyeo na nyongeza ya mishahara kwa Mahakimu waliopo kwenye Mahakama za mwanzo. Kamati inafahamu kwamba wapo Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo ambao hawajapandishwa vyeo kwa zaidi ya miaka kumi sasa. Ni vema pia Waziri wa Katiba na Sheria akaangalia marekebisho ya Sheria ya *Magistrate Court Act*, Marekebisho Namba Moja ya mwaka 2013 ambayo inakinzana na Waraka Namba Moja wa mwaka 2010, waraka wa Katibu Mkuu Utumishi ambao unazungumzia watumishi wa Mahakama hususan katika suala zima la upandishwaji wa vyeo, Mahakimu wana zaidi ya miaka 10 hawajapandishwa vyeo, hususan Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo. (*Makofi*)

(xv) Kamati inatoa wito kwa watendaji wa Mahakama wote kufanya kazi kwa weledi na kuzingatia sheria, taratibu na mipaka ya kazi zao na kutoingilia majukumu ya msingi ya Mahakama katika utoaji na usimamiaji wa haki. (*Makofi*)

(xvi) Wizara na Mhimili wa Mahakama, Fungu Namba

40 kuendelea kuboresha mfumo wa utoaji haki nchini na kuendesha kesi kwa kutumia njia ya mfumo wa kisasa wa mawasiliano (*E-Justice*). Kamati inawapongeza wadau wote wa maendeleo kama Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (*UNDP*) na Shirika la Watoto la Umoja wa Mataifa (*UNICEF*) ambao wamekuwa mstari wa mbele katika kufadhili miradi mbalimbali ya maendeleo iliyo chini ya Wizara ya Katiba na Sheria ikiwemo mradi huu wa *E-Justice*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho napenda kumshukuru Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge lako Tukufu kwa busara na umakini wa namna ambavyo mnaendesha Bunge letu hili Tukufu. Kwa namna ya kipekee kabisa napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe aliyekuwa Waziri wa Katiba na Sheria ambaye kwa zaidi ya mwaka mmoja alifanya kazi kwa weledi na kutoa ushirikiano mkubwa kwa Kamati wakati wa utekelezaji wa majukumu yake, hasa katika wakati wa uchambuzi wa Sheria ya Huduma ya Utoaji wa Msaada wa Kisheria wa mwaka 2016. Niipongeze pia Kamati, kama nilivyo sema, kwa ku-*pioneersheria* hii ambayo inakwenda kuwasaidia Wabunge wetu wote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nitumie nafasi hii pia kumshukuru Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Profesa Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi (Mbunge), Katibu Mkuu Profesa Sifuni Ernest Mchome, Naibu Katibu Mku Ndugu Amon Mpanju na Watendaji wote wa Wizara ya Katiba na Sheria kwa ushirikiano wao mkubwa walioutoa wakati Kamati ilipojadili makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka wa fedha 2017/2018. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee nawashukuru Wajumbe wa Kamati kwa kazi nzuri waliyoifanya wakati wa kujadili na kuchambua makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka wa fedha 2017/2018. Uzalendo, uchapakazi pamoja na ushirikiano mkubwa walionipa umesaidia kufanikisha kukamilika kwa taarifa hii kwa wakati, ningependa majina haya niyasome

lakini kwa kuwa Kanuni haziruhusu, naomba majina yao yote yaingie katika *Hansard*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia niseme Kamati hii ndiyo Kamati bora kuliko Kamati zote za Bunge lako hili Tukufu, kwa kuwa Kamati hii imefanya marekebisho sheria nydingi na imevunja rekodi ya Bunge hili Tukufu. (*Makofii/ Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile napenda kuwashukuru kwa dhati watumishi wote wa Ofisi ya Bunge, chini ya uongozi makini kabisa wa Dkt. Thomas Kashililah, Katibu wa Bunge kwa kusaidia kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee namshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge, Ndugu Athumanli Hussein, Mkurugenzi Msaidizi, Ndugu Angelina Sanga na Makatibu wa Kamati Ndugu Stella Bwimbo na kijana wetu ndugu Dunford Mpelumbe kwa kazi nzuri kabisa wanayoifanya pamoja na Msaidizi wa Kamati Ndugu Rachel Masima, Makatibu Muhtasi wa Idara ya Kamati za Bunge, Ndugu Chiku Ramadhani, Ndugu Grace Wambura, Ndugu Irene Makongoro kwa kuratibu vema kazi za Kamati na kuhakikisha kuwa taarifa hii inakamilika kwa wakati uliopangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo sasa naomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka wa fedha 2017/2018 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti wa Katiba na Sheria kwa wasilisho lako.

**TAARIFA YA KAMATI YA KATIBA NA SHERIA KUHUSU
UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA KATIBA NA
SHERIA KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017 PAMOJA NA
MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA
MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018 -
KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

1.0 UTANGULIZI

Mheshimwa Spika, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu mwangi wa rehema kwa kunijalia uhai, afya njema na kunipa fursa ya kuwasilisha Taarifa hii mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine tena, napenda kumpongeza aliyekuwa Mjumbe wa Kamati hii, Prof. Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi (Mb), ambaye ameteuliwa na kupewa dhamana ya kuongoza Wizara hili muhimu ya Katiba na Sheria. Kamati inamtakia kila la heri katika kutekeleza majukumu yake mapya.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kifungu cha 6 (2) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, Kamati ya Katiba na Sheria ina jukumu la kusimamia Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Taasisi zake sita (6) zifuatazo:

- i. Wizara ya Katiba na Sheria (**Fungu 41**)
- ii. Mwanasheria Mkuu wa Serikali (**Fungu 16**)
- iii. Mkurugenzi Mkuu wa Mashtaka (**Fungu 35**)
- iv. Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (**Fungu 55**)
- v. Tume ya Kurekebisha Sheria (**Fungu 59**)

vi. Tume ya Utumishi wa Mahakama (**Fungu 12**)

Mheshimiwa Spika, Taarifa hii inatoa maelezo kuhusu maeneo makubwa matano yafuatayo:

- (i) Uguzi wa Miradi ya Maendeleo kwa mujibu wa Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016;
- (ii) Utekelezaji wa mapendekezo na ushauri wa Kamati kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017;
- (iii) Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017;
- (iv) Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 pamoja na Taasisi zilizo chini yake; na
- (v) Maoni na Ushauri wa Kamati.

2.0 UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017

Mheshimiwa Spika, tarehe 22 Machi, 2017 Kamati ilipata fursa ya kutembelea Ofisi ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (**Fungu 55**) zilizoko Wete - Pemba na kupokea Taarifa ya Utekelezaji wa Shughuli za Tume kwa upande wa Pemba.

Mheshimiwa Spika, mpaka kufikia Machi, 2017 gharama za upangishaji na ukarabati wa jengo hili zilifika Shilingi Milioni Arobaini (**40,000,000.00**) ambazo zimekua zikitolewa kwa awamu kuanzia Mwaka wa Fedha 2010/2011. Baada ya kufanya ziara hiyo, Kamati imeridhishwa na ukarabati na hali halisi ya mazingira ya Ofisi hiyo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Kamati kuridhishwa na hali halisi ya ukarabati na mazingira ya Ofisi hii, kuna changamoto ya kiutendaji kwa kuwa na Watumishi Wawili (2) tu, Mmoja (1) ni Afisa na mwingine ni Mlinzi ambao wapo katika Ofisi

hiyo toka ilipoanzishwa katika Mwaka wa Fedha 2010/2011. Hivyo Ofisi hii inaendelea kuwa na changamoto nydingi za kiutendaji kutokana na upungufu wa Watendaji. Changamoto hii kwa kiasi kikubwa imeathiri sana utekelezaji wa majukumu ya Tume kwa upande wa Pemba.

Mheshimiwa Spika, katika kutatua changamoto hiyo ya kiutendaji, Kamati imearifiwa kwamba, kutokana na ongezeko la fedha katika bajeti ya Tume katika Mwaka wa Fedha 2017/2018, Watumishi Wawili (2) wataongezwa katika Ofisi hiyo.

2.1 MAONI YA JUMLA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017

Mheshimiwa Spika, Kamati hajjaridhishwa na kasi ya utoaji wa fedha zinazoidhinishwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Karibu miradi yote iliyotengewa fedha imepokea sehemu tu ya fedha iliyoidhinishwa katika Mwaka wa Fedha 2016/2017. Vilevile Kamati inasikitishwa na hatua ya Serikali kutotoa fedha za ndani kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Miradi mingi ya maendeleo imekuwa inategemea fedha za nje kwa kiasi kikubwa. Mfano, Wizara ya Katiba na Sheria (**Fungu 41**) ilipokea fedha za nje tu kwa ajili ya Mradi namba 6201 (E-Justice) kiasi cha Shilingi Bilioni Moja (**1,000,000.000.00**) na Mradi namba 6517 (Unicef Multi-Sectoral Support Program) ilipokea Shilingi Milioni Mia Tatu Tisini na Sita, Laki Nne Sabini na Mbili Elfu, Mia Sita Kumi na Tatu (**396,472,613.00**) zote zikiwa ni fedha za nje. Hapakuwa na fedha yoyote ya ndani iliyotolewa kwa ajili ya Miradi hii yote. Hali hii pia imejitokeza kwenye miradi mingine katika Taasisi zilizo chini ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na changamoto ya ukosefu wa fedha za ndani za kutosha kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo, uko umuhimu kwa kila Taasisi ya Serikali kubuni vyanzo vya mapato vitakavyosaidia kuongeza fedha za ndani ili kuepuka utegemezi wa fedha za nje.

3.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MPANGO WA BAJETI NA UZINGATIAJI WA MAONI YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 98 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, Kamati ilikutana Mjini Dodoma Tarehe 31 Machi na 01 Aprili, 2017 kwa ajili ya uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 pamoja na uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Spika, katika uchambuzi wa Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Wizara hii, Kamati ilizingatia mlinganisho wa kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na Bunge Mwezi Mei 2016 na kiwango ambacho klimepokelewa hadi kufikia Machi 2017.

Mheshimiwa Spika, lengo la kufanya tathmini ya namna hii ni kufahamu mwelekeo wa Mpango na Bajeti ya Mapato na Matumizi ya Serikali katika Mwaka wa Fedha 2016/2017 na kujua vipaumbele vya kibajeti katika Mwaka wa Fedha unaofuata.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2016/2017 Wizara ya Katiba na Sheria kwa ujumla, ilidhiinishiwa Shilingi Bilioni Mia Moja Tisini na Moja, Milioni Mia Nne Hamsini, Laki Tisa na Moja (**191,450,900,001.00**) kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo Shilingi Bilioni Sitini na Tano, Milioni Mia Tisa Arobaini na Tisa, Laki Sita Arobaini na Tatu Elfu na Mia Tatu (**65,949,643,300.00**) ni kwa ajili ya Mishahara na Shilingi Bilioni Mia Moja na Nane, Milioni Mia Tano Sitini na Mbili, Tisini na Saba Elfu, Mia Tisa Sitini na Moja (**108,562,097,961.00**) ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Hadi kufikia Mwezi Disemba 2016, Wizara ilipokea jumla ya Shilingi Bilioni Tisini na Saba, Milioni Mia Mbili Hamsini na Tano, Laki Tano na Sita Elfu, Mia Mbili Thelathini na Tisa (**97,255,506,239.00**) sawa na asilimia 51 ya fedha zilizoidhinishwa kama inavyoonyeshwa kwenye jedwali hapa chini.

Jedwali Namba 1: Mlinganisho wa Fedha iliyotengwa na kupokelewa katika Mwaka wa Fedha 2016/2017 Chini ya Fungu 41 Hadi kufikia Disemba 2016.

Fungu	Fedha Iliyoidhinishwa Sh.	Fedha Iliyopatikana Sh.	Tofauti Sh.	Asilimia Sh.
41	91,450,900,001.00	Sh.97,255,506,239.00	Sh.94,195,393,762	51

Mheshimiwa Spika, Kamati inatoa wito kwa Ofisi ya Hazina kutoa kiasi cha fedha kilichobaki ambacho kiliidhinishwa na Bunge kwa Wizara ya Katiba na Sheria katika kipindi hiki kilichobaki cha Mwaka wa Fedha 2016/2017 ili Wizara iweze kumaliza utekeleza majukumu yake kwa Ufanisi kama ilivyopanga.

Mheshimiwa Spika, mchanganuo wa fedha zilizoidhinishwa na zilizopokelewa katika Mwaka wa Fedha 2016/2017 hadi kufikia Machi 2017 katika Mafungu Sita yanayosimamiwa na Wizara hii, yaani Fungu 41, 16, 35, 59,55 na 12 umeainishwa kwenye jedwali hapa chini kwa kila Fungu.

Fungu	Taasisi	Fedha Zilizoidhinishwa	Fedha Zilizopokelewa	Asilimia ya kiasi kilichopokelewa
41	Wizara ya Katiba na Sheria	Sh.9,141,681,000.00	Sh.3883,679,000.00	42
16	Mwanasheria Mkuu wa Serikali	Sh.6,997,324,000.00	Sh.5,306,378,890.89	76
35	Mkurugenzi wa Mashtaka	Sh.13,097,619,000.00	Sh.7,955,545,061.32	61
12	Tume ya Utumishi wa Mahakama	Sh. 1,134,955,000.00	Sh. 609,858,475.00	53.7
59	Tume ya Kurekebisha Sheria	Sh. 1,658,192,000.00	Sh.1,021,696,624.65	61
55	Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora	Sh. 3,741,929,226.22	Sh.2,074,860,878.22	55.44

Jedwali Namba 2: Mlinganisho wa Fedha Iliyoidhinishwa na Kupokelewa kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 Hadi Kufikia Machi 2017

Mheshimiwa Spika, katika mlinganisho ulioonyeshwa kwenye jedwali namba 2 hapo juu, Fungu 35 (Divisheni ya Mashitaka) ndio liliotengewa fedha nyngi zaidi ambazo ni Shilingi Bilioni Kumi na Tatu, Milioni Tisini na Saba, Laki Sita Kumi na Tisa Elfu (**13,097,619,000.00**) kwa Mwaka 2016/2017. Hata hivyo hadi kufikia Mwezi Machi, 2017 fungu hili limepokea Shilingi Bilioni Saba, Milioni Mia Tisa Hamsini na Tano, Laki Tano Arobaini na Tano Elfu Sitini na Moja (**7,955,545,061.00**).

Mheshimiwa Spika, katika mlinganisho huo, Tume ya Utumishi wa Mahakama (**Fungu 12**), liliidhinishiwa fedha kidogo zaidi kuliko mafungu mengine, kwa kiasi cha Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Moja Thelathini na Nne, Laki Tisa Hamsini na Tano Elfu (**1,134,955,000.00**). Pamoja na kuidhinishiwa fedha hizo kidogo, hadi kufikia Mwezi Machi, 2017 fungu hili limepokea Shilingi Milioni Mia Sita na Tisa, Laki Nane Hamsini na Nane Elfu, Mia Nne Sabini na Tano (**609,858,475.00**).

Mheshimiwa Spika, mwenendo huu wa upokeaji fedha kwa ujumla, unadhihirisha kuwa, fedha inayopokelewa ni ndogo sana ukilinganisha na kiasi kinachoidhinishwa na Bunge lako Tukufu. Hivyo Taasisi hizi zinashindwa kutekeleza majukumu yake kwa wakati na ufanisi kutokana na ucheleweshaji wa utoaji wa fedha kwa upande wa Hazina.

3.1 UCHAMBUZI WA TAARIFA KUHUSU UKUSANYAJI MADUHULI KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017

Mheshimiwa Spika, kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Taasisi zake, ilitarajia kukusanya kiasi cha Shilingi Bilioni Kumi na Saba, Milioni Themanini na Tano, Laki Nane Ishirini na Tisa Elfu, Mia Tano Kumi na Moja (**17,085,829,511.00**) kama maduhuli ya Serikali kutoka vyanzo mbalimbali vya mapato. Hadi kufikia Mwezi Disemba, 2016, Wizara ilikuwa imekusanya kiasi cha Shilingi Bilioni Kumi, Milioni Mia Tisa Arobaini na Tatu, Laki Nne Tisini na Moja Elfu, Mia Nane Arobaini na Tano (**10,943,491,845.00**) sawa na asilimia 64 ya makusanyo yaliyotarajiwa kama ilivyochanganiuliwa kwenye jedwali hapa chini

Jedwali Namba 3: Mlinganisho wa Makadirio, Makusanyo na Asilimia Kwa Mafungu yaliyo Chini ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 Hadi Kufikia Disemba 2016

Mheshimiwa Spika, makusanyo haya ni kutohana na ada mbalimbali za Usajili wa Matukio, Ada za Wanafunzi, Uuzaji wa Vitabu vya Zabuni na Huduma nyingine mbalimbali zinazotolewa na Wizara.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Katiba na Sheria (**Fungu 41**) imeongoza katika ukusanyaji wa Maduhuli kwa kukusanya Shillingi Bilioni Tano, Milioni Mia Tano Tisini na Tisa, Laki Tatu Kumi na Tatu Elfu, Mia Nane Arobaini na Tano (**5,599,313,845.00**) ikifuatiwa na Idara ya Mahakama (**Fungu 40**) iliokusanya Shilingi Bilioni Tano, Milioni Mia Tatu Arobaini na Nne, Laki Moja Sabini na Nane Elfu (**5,344,178,000.00**).

Mheshimiwa Spika, mafungu mengine yalikuwa na matarajio ya kukusanya Maduhuli lakini matarajio hayakuwa kama yalivyopangwa. Hii ni changamoto ambayo Wizara na Taasisi zote zenye vyanzo vya mapato zinabidi kuiangalia kwa umakini kwani matarajio sio mapato. Hivyo kuna umuhimu wa kubuni vyanzo vingine vya ukusanyaji wa Maduhuli ili kuongeza upatikanaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara hasa kwa zile Taasisi zilizokosa mapato kabisa.

3.2 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA USHAURI WA KAMATI

Mheshimiwa Spika, wakati wa uwasilishaji wa Makadirio ya

Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017, Kamati ilitoa ushauri na mapendekozo Kumi na Sita (16) kuhusiana na Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Taasisi zake.

Mheshimiwa Spika, Kamati imefurahishwa na utekelezaji wa maoni ya Kamati yaliyotolewa katika Taarifa yake ya Uchambuzi wa Bajeti kwa Wizara hii Mwezi Mei, 2016. Jambo mahsus ambalo Kamati imeridhika nalo, ni ongezeko kidogo kwenye Bajeti ya utekelezaji wa majukumu ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, ambayo imetengewa Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Tano Sitini na Sita, Themanini Elfu (**1,566,080,000.00**) katika Mwaka ujao wa fedha (2017/2018) kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC), ikilinganishwa na Mwaka wa Fedha uliopita ambapo Tume hii illidhinishiwa Shilingi Milioni Mia Tisa Tisini na Nne, Laki Tano Kumi na Nne Elfu (**994,514,000.00**) tu kwa ajili ya Matumizi Mengineyo ambayo ilikuwa ni ndogo na haikulingana na uzito wa majukumu yake katika kuhakikisha Haki za Binadamu na Utawala Bora zinazingatiwa. Tofauti hii ni ongezeko la asilimia 57 ya Bajeti inayoombwaa kuidhinishwa kwa ajili ya Tume katika Mwaka wa Fedha unaokuja. Hata hivyo fedha iliyoidhinishwa haitoshelezi ikilinganishwa na majukumu yanayopaswa kutekelezwa na Tume katika Nchi nzima. Kamati inaishauri Serikali kuendelea kuongeza fedha za kutosha kwa Tume hii ili itekeleze majukumu yake kikamilifu.

4.0 MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

Mheshimiwa Spika, kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 Wizara ya Katiba na Sheria, imejiwekea malengo saba (7) ya kutekeleza ili kuongeza ufanisi na ubora katika kutoa huduma za Kisheria na masuala ya Katiba yakiwemo:

- i) Kuendelea na uhamasishaji wa shughuli za Serikali kutoka Dar es Salaam kwenda Makao Makuu ya Nchi, Dodoma;
- ii) Kuimarisha mfumo wa Sheria na kuongeza uwezo wa Wizara katika maeneo maalum ya Sheria, usimamizi na utoaji haki;

iii) Kuimarisha usimamizi na ufuutilaji wa masuala ya Kikatiba na Sheria;

iv) Kuimarisha misingi ya haki za Binadamu na Kisheria;

Mheshimiwa Spika, Kamati inakubaliana na malengo ya Wizara kwa ujumla kwani yanalenga katika kuboresha utekelezaji wa majukumu yake na kuleta ufanisi zaidi katika suala zima la utoaji haki nchini.

4.1 MAKADIRIO YA MAPATO YA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

Mheshimiwa Spika, kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018, Wizara inatarajia kukusanya kiasi cha Shilingi Bilioni Ishirini na Nne, Milioni Themanini na Saba, Laki Tano na Saba Elfu, Mia Mbili (**24,087,507,200.00**) ikiwa ni Maduhuli ya Serikali, kama inavyoonekana kwenye jedwali hapa chini:

Jedwali Namba 4: Matarajio ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa Makadirio ya Mapato hayaendani na hali halisi ya makusanyo. Hivyo Kamati inashauri kuwa, ni vizuri kuweka makadirio madogo yenye uhakika katika kukusanya kuliko kuweka makadirio makubwa ya fedha ambayo hayana matarajio makubwa katika ukusanyaji.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (**Fungu 55**) na Tume ya Utumishi wa Mahakama (**Fungu 12**) hayana matarajlo yoyote ya kukusanya maduhuli kwa sababu ya kutokuwa na vyanzo nya mapato.

4.2 UCHAMBUZI WA MAKADIRIO YA MATUMIZI YA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2017/2018, Wizara pamoja na Taasisi zake inaomba kuidhinishiwa **Shilingi Bilioni Mia Moja Hamsini na Tisa, Milioni Mia Tatu Thelathini na Moja, Laki Nane Ishirini na Mbili Elfu, (159,331,822,000.00)** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo ambayo ni upungufu wa asilimia **4.4** ikilinganishwa na Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2016/2017. Upungufu huu wa asilimia **4.4** unatokana na ukomo wa Bajeti ya fedha za maendeleo kupungua kwa wastani wa asilimia 55 ikilinganishwa na fedha ya Miradi ya maendeleo iliyoidhinishwa Mwaka 2016/2017.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Taasisi zake, kwa Mwaka 2017/2018 inaomba fedha kama ilivoonyeshwa katika mchanganuo uliopo kwenye jedwali hapa chini.

Jedwali Namba 5: Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi kwa Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018

Fungu	Taasisi	Kiasi
41	Wizara ya Katiba na Sheria	9,862,066,000.00
16	Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali	7,282,523,000.00
35	Divisheni ya Mashitaka	14,914,063,000.00
12	Tume ya Utumishi wa Mahakama	1,102,911,000.00
59	Tume ya Kurekebisha sheria	2,052,757,000.00
55	Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora	6,166,981,000.00
JUMLA		41,381 ,301,000.00

Mheshimiwa Spika, Divisheni ya Mashitaka (**Fungu 35**) lina makadirio ya matumizi ya juu zaidi ikilinganishwa na mafungu mengine. Bajeti inayoombwaa kwa ajili ya Fungu hili ni sawa na asilimia **37%** ya Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa 2017/2018.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Utumishi wa Mahakama (**Fungu 12**) lina Makadirio ya Matumizi madogo zaidi ikilinganishwa na mafungu mengine ikiwa ni sawa na asilimia 3.2% ya Bajeti ya Wizara kwa Mwaka 2017/2018.

5.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia Taarifa zilizowasilishwa mbele ya Kamati pamoja na majukumu ya Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zilizo chini yake, Kamati inatoa maoni na ushauri ufuataao ili kuboresha utendaji kazi na ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii.

i) Kamati inaipongeza Serikali kwa kuungeza bajeti ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora kwa Fedha ya Matumizi Mengineyo (OC) kutoka **Shilingi Milioni Mia Tisa Tisini na Nne, Laki Tano Kumi na Nne Elfu (994,514,000.00)** katika Mwaka wa Fedha 2016/2017 mpaka **Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Tano Sitini na Sita, Themanini Elfu (1,566,080,000.00)** katika Mwaka wa Fedha ujao (2017/2018). Ongezeko hili ni sawa na asilimia **57**. Hata hivyo, Kamati inatoa rai kwa Wizara na Taasisi zake kufanya rejea ya maagizo yalivytotolewa na Kamati katika Taarifa ya Mwaka wa Fedha 2016/2017 na kuendelea kuyatekeleza katika kipindi cha robo ya mwisho ya mwaka huu wa Fedha unaoishia Mwezi Juni, 2017;

ii) Ofisi ya Hazina kutoa fedha zinazoidhinishwa na Bunge kwa Wizara husika kwa wakati ili kuiwezesha Wizara kutekeleza majukumu yake kama yalivyopangwa katika kila Mwaka wa Fedha;

- iii) Wizara kupitia Tume ya Kurekebisha Sheria kufanya mapitio na maboresho yote ya msingi ya Sheria zote zinazohitaji maboresho na kutazama uwezekano wa kuhuisha Mchakato wa Upatikanaji wa Katiba Mpya kwa wakati muafaka;
- iv) Wizara pamoja na Taasisi zake kukamilisha kwa haraka utekelezaji wa Mpango wa kuhamia Dodoma mapema iwezekanavyo ili kutekeleza uamuzi wa Serikali wa kuhamishia Makao Makuu ya Nchi Dodoma;
- v) Kamati inatoa wito kwa Serikali kuleta Bungeni Sheria mahsus ambayo itahalalisha utekelezaji wa maamuzi ya Serikali ya awamu ya Tano ya kuufanya Mji wa Dodoma kuwa Makao Makuu ya Nchi;
- vi) Tume ya Kurekebisha Sheria kuendelea kufanya mapitio ya Sheria mbalimbali kwa lengo la kuzirekebisha na kuziboresha ili kuendana na mabadiliko mbalimbali tuliyonayo sasa. Kamati inatoa rai kwa Tume hii kushirikiana na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ili kufanya mapitio ya Sheria ya Elimu ya Mwaka 1978 na kutazama uwezekano wa kuirekebisha ili kufanya Elimu ya Sekondari kuwa ya lazima na kuwawezesha vijana wanaomaliza Elimu ya Msingi kuendelea na Elimu ya Sekondari;
- vii) Serikali kuongeza ukomo wa Bajeti kwa Wizara na Taasisi zake katika mwaka ujao wa fedha ili ziweze kuanza utaratibu wa kujenga majengo ya Ofisi zao katika mji wa Kiserikali utakaojengwa Dodoma;
- viii) Wizara kuendelea kusimamia kwa ufanisi masuala yote ya haki za Binadamu na upatikanaji haki nchini na kuhakikisha kwamba inachukua hatua za kutosha kupunguza wingi wa kesi Mahakamani na wingi wa mahabusu katika rumande, jambo ambalo linavunja haki mbalimbali za watuhumiwa ambao wanakaa rumande kwa muda mrefu bila kesi zinazowahusu kusikilizwa na kumalizika kwa wakati;
- ix) Serikali kuzingatia kwa umakini matakwa ya lbara ya 13(6) (a-e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya

Mwaka 19777 ambayo inatoa haki za msingi za kuhusiana na watuhumiwa wa makosa ya Jinai ikijumuisha haki yakupata dhamana, kusikilizwa kwa kesi zao na kukata rufaa kwa wakati muafaka;

x) Wizara na Mhimili wa Mahakama kwa ujumla, kuzingatia matakwa ya kisheria kuhusu uendeshaji wa kesi za jinai na hususani taratibu za utoaji wa dhamana kwa watuhumiwa kama zilivyowekwa na kifungu cha 148 cha Sheria ya Mwenendo wa Kesi za Jinai iliyopitiwa Mwaka 2002 (*Criminal Procedure Act*). Kamati inasitisiza kwamba dhamana ni haki ya Mtuhumiwa na ni suala la Kikatiba. Hivyo Taasisi za utoaji haki zinapaswa kuzingatia suala hili ili kutenda haki kwa watuhumiwa;

xi) Serikali kuridhia na kutekeleza Mikataba mbalimbali ya Kimataifa iliyordhiwa na Nchi yetu ili iweze kutekelezwa kama vile Mkataba wa Kimataifa wa Mwaka 1984 unaopinga matendo yote ya kikatili dhidi ya mwanadamu (*Convention Against Torture*, 1984);

xii) Wakala wa Usajili,Ufilisi na Udhamini (RITA) kuendelea kufanya kazi kwa kuzingatia misingi ya Sheria, Taratibu, Kanuni, uadilifu na weledi katika usajili wa mabaraza ya wadhamini wa vyama vya siasa au makundi mengine ya kijamii kwa kusimamia Sheria, Kanuni na Taratibu zilizopo, hivyo kuepuka kuwa sehemu ya migogoro ya vyama hivyo;

xiii) Wizara kuanzisha na kukamilisha mchakato wa upatikanaji wa Kanuni za Sheria ya Utoaji wa Msaada wa Kisheria (*The Legal Aid Act*) iliyopitishwa na Bunge katika Mkutano wa Sita wa Bunge uliofanyika Mwezi Februari, 2017;

xiv) Tume ya Utumishi wa Mahakama kusimamia kwa umakini mkubwa maslahi ya Mahakimu wote na hasa upandishaji wa vyeo na nyongeza ya mishahara kwa mahakimu walioko kwenye Mahakama za Mwanzo. Kamati inafahamu kwamba wapo mahakimu wa Mahakama za Mwanzo ambao hawajapandishwa vyeo kwa miaka zaidi ya Saba (7) kinyume kabisa na taratibu za kazi na ajira kwa Watumishi wa Umma;

xv) Kamati inatoa wito kwa Watendaji wa Mahakama wa Wilaya kufanya kazi kwa weledi na kwa kuzingatia Sheria,Taratibu na Mipaka ya Kazi zao na kutokuingilia majukumu ya msingi ya Mahakama katika kutoa na Kusimamia Haki;

xvi) Wizara na Mhimili wa Mahakama (**Fungu 40**) kuendelea kuboresha mfumo wa utoaji haki nchini na uendeshaji wa kesi kwa kutumia njia na mifumo ya Kisasa ya Mawasiliano (E-Justice). Kamati inawapongeza wadau wote wa Maendeleo kama Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) na Shirika la Watoto la Umoja wa Mataifa (UNICEF) ambayo yamekuwa mstari wa mbele katika kufadhili Miradi mbalimbali ya Maendeleo iliyo chini ya Wizara ya Katiba na Sheria ukiwamo mradi huu wa E-Justice.

6.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, mwisho napenda kukushukuru wewe binafsi, Mheshimiwa Spika kwa kunipa nafasi hii muhimu kuwasilisha maoni ya Kamati yangu. Aidha, hatuna budi kukupongeza wewe binafsi Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa kuliongoza Bunge letu Tukufu kwa busara, umakini na umahiri mkubwa.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee, napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Dr. Harrison G.Mwakyembe aliyekuwa Waziri wa Katiba na Sheria, ambaye kwa zaidi ya mwaka mmoja alifanya kazi kwa weledi na kutoa ushirikiano mkubwa kwa Kamati wakati wa utekelezaji wa majukumu yake, hasa katika wakati wa uchambuzi wa Sheria ya Huduma za Utoaji wa Msaada wa Kisheria ya Mwaka 2016.

Mheshimiwa Spika, napenda nitumie nafasi hii pia kumshukuru Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria Prof. Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi (Mb), Katibu Mkuu Prof. Sifuni Ernest Mchome, Naibu Katibu Mkuu Ndugu Amon Mpanju na Watendaji wote wa Wizara ya Katiba na Sheria kwa ushirikiano mkubwa walijoutoa wakati Kamati ilipojadili Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Spika, kipekee nawashukuru Wajumbe wa Kamati kwa kazi nzuri waliyoifanya wakati wa kujadili na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018. Uzalendo, uchapakazi pamoja na ushirikiano mkubwa walionipa umesaidia kufanikisha kukamilika kwa Taarifa hii kwa wakati. Kwa ruhusa yako naomba majina yao yaingizwe kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge kama yalivyo yaani Hansard.

- (i) Mhe. Mohamed Omary Mchengerwa, Mb, **Mwenyekiti**
- (ii) Mhe. Najma Mutraza Giga, Mb, **Makamu Mwenyekiti**
- (iii) Mhe. Ajali Rashid Akbar, Mb, Mjumbe
- (iv) Mhe. Ally Saleh Ally, Mb, Mjumbe
- (v) Mhe. Anna Joram Gidarya, Mb, Mjumbe
- (vi) Mhe. Asha Abdallah Juma, Mb, Mjumbe
- (vii) Mhe. Dkt Mathayo David Mathayo, Mb, Mjumbe
- (viii) Mhe. Gibson Blasius Meiseyeki, Mb, Mjumbe
- (ix) Mhe. Joram Ismael Hongoli, Mb, Mjumbe
- (x) Mhe. Joseph Kizito Mhagama, Mb, Mjumbe
- (xi) Mhe. Juma Hamadi Kombo, Mb, Mjumbe
- (xii) Mhe. Makame Mashaka Foum, Mb, Mjumbe
- (xiii) Mhe. Mboni Mohamed Mhita, Mb, Mjumbe
- (xiv) Mhe. Nassor Suleiman Omar, Mb, Mjumbe
- (xv) Mhe. Omary Ahmed Badwel, Mb, Mjumbe
- (xvi) Mhe. Rashid Abdallah Shangazi, Mb, Mjumbe
- (xvii) Mhe. Riziki Shahari Mngwali, Mb, Mjumbe
- (xviii) Mhe. Saumu Heri Sakala, Mb, Mjumbe
- (xix) Mhe. Seif Ungando Ally, Mb, Mjumbe
- (xx) Mhe. Selemani Jumanne Zedi, Mb, Mjumbe
- (xxi) Mhe. Suleiman Masoud Nchambi, Mb, Mjumbe
- (xxii) Mhe. Taska Restituta Mbogo, Mb, Mjumbe
- (xxiii) Mhe. Twahir Awesu Mohamed, Mb, Mjumbe
- (xxiv) Mhe. Wanou Hafidhi Ameir, Mb, Mjumbe
- (xxv) Ussi Pondeza, Mb, Mjumbe

Mheshimiwa Spika, vilevile napenda kuwashukuru kwa dhati, Watumishi wa Ofisi ya Bunge, chini ya Uongozi wa Dkt. Thomas D. Kashililah, Katibu wa Bunge, kwa kusaldia na kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Kipekee, namshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndugu

Athumani Hussein, Mkurugenzi Msaidizi, Ndugu Angelina Sanga na Makatibu wa Kamati Ndugu Stella Bwimbo na Ndugu Dunford Mpelumbe pamoja na Msaidizi wa Kamati, Ndugu Raheli Masima, Makatibu Muhtasi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndugu Chiku Ramadhan, Ndg. Grace Wambura na Ndg. Irene Makongoro kwa kuratibu vyema kazi za Kamati na kuhakikisha kuwa Taarifa hii inakamilika kwa wakati uliopangwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sasa naomba Bunge lako Tukufu, likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 kama yaliyyowasilishwa na Mto Hoja.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono Hoja.

Mohamed Omary Mchengerwa, Mb.

MWENYEKITI,

KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA

25 Aprili, 2017

MWENYEKITI: Tunaendelea, sasa namuita Mwenyezekiti wa Kamati ya Bajeti mwakilishi wake Mheshimiwa Subira Mgaliu.

MHE. SUBIRA K. MGALU (K.n.y MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI): Mheshimiwa Mwenyezekiti, awali naomba uniruhusu na mimi nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha afya njema kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu na kuwasilisha maoni ya Kamati.

Pia nichukue fursa hii kuwapa pole wananchi wenzangu wa Mkoa wa Pwani hususan Wilaya za Mkuranga, Kibiti na Rufiji kutokana na madhila mbalimbali yaliyojitezea, lakini niishukuru sana Serikali kwa kufanya kila jitihada kurejesha hali ya usalama katika maeneo hayo na naomba wananchi wenzangu tuendelee kutoa ushirikiano kwa vyombo vyaa usalama ili kuweza wahalifu na kuwafikisha

kwenye vyombo vya sheria. Kwa mujibu wa Kanuni ya 99 ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bajeti kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Mfuko wa Mahakama kwa mwaka wa 2016/2017 na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilikutana na Waziri wa Fedha na Mipango, Waziri wa Katiba na Sheria pamoja na Mtendaji Mkuu wa Mahakama na kujadiliana na kufanya mashauriano kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Mfuko wa Mahakama kwa mwaka wa fedha 2016/2017 na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2017/2018. Mashauriano haya yamefanyika kwa mujibu wa kifungu cha 75 cha Sheria ya Bajeti Na. 11 mwaka 2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa majukumu ya Mfuko wa Mahakama kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Kwa mujibu wa Katiba jukumu kubwa la Mahakama ni kusimamia utoaji wa haki katika kutekelza hili Mahakama imefanikiwa kutekeleza yafuatayo:-

- (a) Mahakama imefanikiwa kuanzisha Division Maalum ya Mahakama Kuu inayoshughulikia makosa ya rushwa na uhujumu uchumi.
- (b) Watumishi 539 wamepata mafunzo ya muda mfupi ya ndani ya nchi baadhi yao Waheshimiwa Majaji 57 Wasajili watatu, Naibu Wasajili tisa na Mahakimu 144.
- (c) Imekarabati Mahakama Kuu ya Dar es Salaam, Tanga na ukarabati wa Makahama Kuu ya Mbeya upo katika hatua za mwisho.
- (d) Imesambaza nakala mbalimbali za vitabu vya mwongozo wa usimamizi na ukaguzi wa shughuli za Mahakama ili kuwezesha Mahakama nchini kutoa huduma bora ziasi kwa wananchi.
- (e) Imeendelea kukamilisha miradi yake ya maendeleo

ikiwemo ujenzi na ukarabati wa majengo ya Mahakama kwa gharama nafuu katika maeneo ya Kibaha, Bagamoyo, Kigamboni, Mkuranga, Kawe na Kinyerezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na utekelezaji wa majukumu haya bado Mfuko wa Mahakama unakabiliwa na changamoto mbalimbali kama vile; moja, utolewaji wa fedha usiondana na mpango kazi wa Mfuko wa Mahakama, pili, uhaba wa watumishi wenyewe sifa zinazotakiwa kwenye kada mbalimbali na tatu, bajeti ndogo ya Mfuko wa Mahakama isiyolingana na mahitaji halisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka wa fedha 2016/2017; katika mwaka wa fedha 2016/2017 Mfuko wa Mahakama Fungu 40 uliidhinishiwa jumla kiasi cha shilingi 131,627,043,504, kati ya fedha hizo shilingi 50,345,775 ni kwa ajili ya mishahara, shilingi 34,519,534 kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi 46,761,734,504, kwa ajili ya mpango wa maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Julai hadi Februari, 2017 jumla ya shilingi 55,427,630,446.56 zilitolewa na Wizara ya Fedha kwa Fungu 40 kwa ajili ya mishahara na matumizi mengineyo, hii ikiwa ni sawa na asilimia 42 ya bajeti iliyotengwa kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Aidha, kwa upande wa fedha za maendeleo jumla ya shilingi 829,593,993 zilitolewa, hii ikiwa ni sawa na asilimia mbili ya bajeti iliyotengwa kwa mwaka 2016/2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kupokea fedha hizo bado kumeonakana kuna changamoto kubwa ya kutotolewa fedha kwa wakati kwa Fungu husika na hivyo kuathiri utekelezaji wa baadhi ya majukumu ya Mfuko wa Mahakama. Aidha, Kamati ya Bajeti ilifanya mashauriano na Serikali na kukubaliana kiasi cha fedha kilichobakia kwenye Fungu hili kitolewe kabla ya tarehe 30 Juni, 2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Mfuko wa Mahakama kwa mwaka wa fedha 2016/2017; kwa mwaka wa fedha 2016/2017 fedha

zilizokasimiwa kwenye Mfuko wa Mahakama zimetengwa katika maeneo mbalimbai kwa ajili ya kuhakikisha Mahakama inatekeleza majukumu yake ya Kikatiba. Baadhi ya majukumu ambayo yamepangwa kutekelezwa katika bajeti ya mwaka 2017/2018 ni kama yafuatayo:-

- (a) Kuendelea kutoa huduma ya haki sawa kwa wote na kwa wakati.
- (b) Kuimarisha uongozi, utawala bora na uwajibikaji kwa Mahakama pamoja na kuongeza upatikanaji wa haraka wa huduma za Mahakama wa Wananchi.
- (c) Kuimarisha ufanisi wa kazi za Mahakama kwa kutumia TEHAMA
- (d) Kuongeza mahusiano baina ya wadau wanje na ndani ya Mahakama.
- (e) Kujenga taswira mpya ya Mahakama yenye mtazamo chanya

Mheshumiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2017/2018. Mfuko wa Mahakama umepanga kukusanya maduhuli ya kiasi cha shilingi 9,318,061,200 ikilinganishwa na makadirio ya shilingi 6,504,132,435 ya mwaka 2016/2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2017/2018 Mfuko wa Mahakama umetengewa jumla ya shilingi 125,117,029,000 baada ya Serikali kushauriana na Kamati ya Bajeti na kuongeza fedha za matumizi mengineyo kwa mfuko wa kiasi cha shilingi bilioni Sita na Kamati ya Bajeti inaipongeza Serikali. Kati ya fedha hizo zilizotengwa, shilingi 56,477,636,000 ni kwa ajili ya mishahara, shilingi 50,481,382,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi 18,150,011.000 ni kwa ajili ya maendeleo ambapo kati ya hizo shilingi bilioni 17 ni fedha za ndani na shilingi 1,154,011,000 ni fedha za nje. Mchanganuo wa namna ya fedha za matumizi ya kawaida na maendeleo zitakavyotumika zimeainishwa katika jedwali naomba isomeke kwenye *Hansard*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na ushauri wa Kamati; kwa kuwa tathmini ya utekelezaj wa bajeti ya mfuko wa Mahakama kwa mwaka wa fedha 2016/2017 inaonesha kuwa hadi kufikia Machi, 2017 Mfuko huu unakabiliwa na changamoto ya kutokupokea fedha kwa wakati pamoja na kupokea fedha pungufu tofauti na ilivyoombwa na hivyo kuathiri utekelezaji wa majukumu ya Mfuko huu hasa kwa upande wa miradi ya maendeleo. Hivyo basi, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba kwa mwaka wa fedha 2017/2018 Mfuko wa Mahakama unapatiwa fedha kwa wakati na kwa mujibu wa maelekezo ya Sheria ya Bajeti ya mwaka 2015 kama zilivyoidhinishwa na Bunge.

Kwa kuwa Mfuko wa Mahakama unakabiliwa na uhaba wa watumishi wenye sifa zinazostahili katika kada mbalimbali, hivyo basi Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha inaongeza idadi ya watumishi wanaohitajika kwenye kada mbalimbali kwa awamu ili kusaidia utekelezaji wa majukumu ya Mfuko huu.

Kwa kuwa mtiririko wa fedha kwenye Mfuko wa Mahakama umekuwa hauzingatii mpango kazi wa mfuko husika, hivyo basi Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha inazingatia maelekezo ya kifungu cha 48 cha Sheria ya Bajeti Namba 11 ya mwaka 2015 kinachoitaka Hazina kutoa fedha kwenda Mfuko wa Mahakama kwa kila robo mwaka. Pia Serikali ihakikishe ukomo unaotolewa unazingatia hali halisi ya mahitaji ya Mahakama. (*Makof*)

Kwa kuwa bajeti iliyotolewa kwa mwaka 2016/2017 haikidhi mahitaji ya msingi ya Mfuko wa Mahakama hadi kupelekea Mfuko huu kukabiliwa na madeni mbalimbali yanayohusu posho za Wazee wa Baraza, malipo ya pango za nyumba wanazoishi Majaji, Ofisi za kuendeshea Mahakama pamoja na madai mbalimbali ya watumishi, hivyo basi Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha inamalizia kupeleka kwenye Mfuko wa Mahakama bakaa ya matumizi mengineyo ya kiasi cha shilingi bilioni 20 katika bajeti ya mwaka 2016/2017 ili Mfuko huu uweze kulipa baadhi ya madeni hayo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho; naomba nihitimishe kwa kumshukuru Spika, Mheshimiwa Job Yustino Ndugai na Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kuongoza vyema Bunge letu na pia kwa kuongoza vyema mashauriano kati ya Kamati ya Bajeti na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Dkt. Philipo Mpango, Waziri wa Fedha na Mipango na Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango kwa ushirikiano wao kwa Kamati. Aidha, Kamati inamshukuru na kumpongeza Profesa Palamagamba Kabudi, Waziri wa Katiba na Sheria na Mtendaji Mkuu wa Mahakama kwa kushirikiana na Kamati wakati wa majadiliano. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwashukuru wajumbe wa Kamati kwa umakini wao katika kujadili na kutoa maoni na mapendekezo mbalimbali kuhusu bajeti ya Mfuko wa Makama. Ukurasa wa 15 umewatambua wajumbe hawa na naomba *Hansard* inukuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas D. Kashilllah kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo pamoja na Sekretarieti ya Kamati ya Bajeti kwa kuipa ushauri wa kitaalam Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo haya, naliomba Bunge lako Tukufu sasa lijadili na kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya Mfuko wa Mahakama - Fungu 40 kwa mwaka wa fedha 2017/2018 kama yalivyowasilishwa na Waziri wa Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Tunakushukuru kwa wasilisho lako zuri. (*Makofii*)

**MAONI YA KAMATI KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA
MFUKO WA MAHAKAMA KWA MWAKA WA FEDHA 2016/17
PAMOJA NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA
MWAKA WA FEDHA 2017/18 KAMA
ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

1.0 UTANGULIZI.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bajeti, kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Mahakama kwa Mwaka wa Fedha 2016/17 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/18.

Mheshimiwa Spika, kamati ilikutana na Waziri wa Fedha na Mipango, Waziri wa Katiba na Sheria pamoja na Mtendaji Mkuu wa Mahakama na kujadiliana na kufanya mashauriano kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Mahakama kwa Mwaka wa Fedha 2016/17 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/18. Mashauriano haya yamefanyika kwa mujibu wa kifungu cha 75 cha Sheria ya Bajeti Na. 11 ya Mwaka 2015.

**2.0 UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA MFUKO WA
MAHAKAMA KWA MWAKA 2016/17**

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Katiba, jukumu kubwa la Mahakama ni kusimamia utoaji wa haki. Katika kutekeleza hili Mahakama imefanikiwa kutekeleza yafuatayo:-

a) Mahakama imefanikiwa kuanzisha divisheni Maalum ya Mahakama Kuu inayoshughulikia makosa ya rushwa na uhujumu uchumi;

b) Watumishi 539 wamepata mafunzo ya muda mfupi ya ndani ya nchi, baadhi yao ni Waheshimiwa Majaji 57, Wasajili 3, Naibu Wasajili 9 na Mahakimu 144;

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

- c) Imekarabati Mahakama Kuu Dar es Salaam, Tanga na Ukarabati wa Mahakama kuu ya Mbeya upo katika hatua za mwisho;
- d) Imesambaza nakala mbalimbali za Vitabu vya mwongozo wa usimamizi na ukaguzi wa shughuli za Mahakama ili kuwezesha Mahakama nchini kutoa huduma bora zaidi kwa wananchi;
- e) Imeendelea kukamilisha miradi yake ya maendeleo ikiwemo ujenzi na ukarabati wa majengo ya Mahakama kwa gharama nafuu katika maeneo ya Kibaha, Bagamoyo, Kigamboni, Mkuranga, Kawe na Kinyerezi;

Mheshimiwa Spika, pamoja na utekelezaji wa majukumu haya, bado Mfuko wa Mahakama unakabiliwa na changamoto mbalimbali kama vile:-

- I. Utilewaji wa fedha na usioendana na Mpango Kazi wa Mfuko wa Mahakama;
- II. Uhaba wa watumishi wenyewe sifa zinazotakiwa kwenya kada mbalimbali;
- III. Bajeti ndogo ya Mfuko wa Mahakama isiyolingana na mahitaji halisi.

3.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2016/2017

Mheshimiwa Spika, Katika mwaka wa fedha 2016/17 Mfuko wa Mahakama – **Fungu 40** uliidhinishiwa jumla ya kiasi cha **Sh.131,627,043,504** Kati ya fedha hizo **Sh.50,345,775,000** ni kwa ajili ya Mishahara (PE), **Sh.34,519,534,000** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC), na **Sh.46,761,734,504** kwa ajili ya Mpango wa Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwezi Julai 2016 hadi Februari 2017 jumla ya **shilingi 55,427,630,446.56** zilitolewa na Wizara ya Fedha kwa **Fungu 40** kwa ajili ya

mishahara na matumizi mengineyo, hii ikiwa sawa na **asilimia 42** ya fedha zilizotengwa kwa mwaka 2016/17. Aidha, kwa upande wa fedha za maendeleo jumla ya **shilingi 829,593,993** zilitolewa hii ikiwa sawa na **asilimia 2** ya bajeti iliyotengwa kwa mwaka 2016/17 (**shilingi 46,561,734,000**).

Mheshimiwa Spika, Hata hivyo pamoja na kupokea fedha hizi bado kumeonekana kuna changamoto kubwa ya kutokutolewa fedha kwa wakati kwa fungu husika na hivyo kuathiri utekelezaji wa baadhi ya majukumu ya Mfuko wa Mahakama. Aidha, Kamati ya Bajeti ilifanya mashauriano na Serikali na kukubaliana kiasi cha fedha kilichobakia kwenye fungu hili kitolewe kabla ya tarehe 30 Juni 2017.

4.0 MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA MFUKO WA MAHAKAMA KWA MWAKA WA FEDHA 2017/18.

Mheshimiwa Spika, Katika mwaka wa Fedha 2017/18, fedha zilizokasimiwa kwenye Mfuko wa Mahakama zimetengwa katika maeneo mbalimbali kwa ajili ya kuhakikisha Mahakama inatekeleza majukumu yake ya Kikatiba. Baadhi ya majukumu ambayo yamepangwa kutekelezwa katika bajeti ya mwaka 2017/18 ni kama yafuatayo:

- a) kuendelea kutoa hukumu ya haki sawa kwa wote na kwa wakati;
- b) kuimarisha uongozi, utawala bora na uwajibikaji kwa Mahakama pamoja na kuongeza upatikanaji wa haraka wa huduma za Mahakama kwa wananchi;
- c) kuimarisha ufanisi katika kazi za Mahakama kwa kutumia TEHAMA;
- d) Kuongeza mahusiano baina ya wadau wa nje na ndani ya Mahakama;
- e) kujenga taswira mpya ya Mahakama yenye mtazamo chanya;

4.1 Maduhuli

Mheshimiwa Spika, Katika mwaka wa fedha 2017/18 Mfuko wa Mahakama umepanga kukusanya maduhuli ya kiasi cha **Sh. 9,318,061,200** ikilinganishwa na makadirio ya shilingi **6,504,132,435** mwaka 2016/17.

4.2 Matumizi ya Kawaida na Maendeleo

Mheshimiwa Spika, Katika mwaka wa fedha 2017/18 Mfuko wa Mahakama umetengewa jumla ya **Sh.125,117,029,000**; baada ya Serikali kushauriana na Kamati ya Bajeti na kuongezea fedha za matumizi mengineyo (OC) kwa mfuko huu kiasi cha **shilingi 6,000,000,000**.

Mheshimiwa Spika, Kati ya fedha hizo zilizotengwa; **Sh.56,477,636,000** ni kwa ajili ya Mishahara, **Sh.50,481,382,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Mengineyo (OC) na **Sh.18,158,011,000** ni kwa ajili ya maendeleo ambapo kati ya kiasi hicho **Sh.17,000,000,000** ni fedha za ndani na **Sh.1,158,011,000** ni fedha za nje. Mchanganuo wa namna fedha za Matumizi ya Kawaida na maendeleo zitakavyotumika zimeanishwa kwenye jedwali lifuatalo.

JEDWALI: Mchanganuo wa Makisio ya Bajeti kwa mwaka 2017/18

NA.	MAELEZO	BAJETI YA MWAKA 2016/2017	MAKISIO YA MWAKA 2017/2018
1.	Mishahara	50,345,775,000	56,477,636,000
2	Matumizi Mengineyo (OC)	34,519,534,000	50,481,382,000
3	Matumizi Maendeleo Ya	46,761,734,504	18,158,011,000
	Fedha za Ndani	24,000,000,000	17,000,000,000
	Fedha za Nje	22,761,734,504	1,158,011,000
4	Jumla ya Matumizi ya Kawaida na Maendeleo	131,627,043,504	125,117,029,000

5.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

5.1 **Kwa kuwa**, Tathmini ya utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Mahakama kwa mwaka wa fedha 2016/2017 inaonyesha kuwa hadi kufikia mwezi Machi 2017; mfuko huu unakabiliwa na changamoto ya kutopokea fedha kwa wakati pamoja na kupokea fedha pungufu tofauti na ilivyoombwa na hivyo kuathiri utekelezaji wa majukumu ya Mfuko huu hasa kwa upande wa miradi ya maendeleo'

Hivyo basi, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba kwa mwaka wa fedha wa 2017/2018 Mfuko wa Mahakama unapatiwa fedha kwa wakati na kwa mujibu wa maelekezo ya Sheria ya Bajeti (2015) kama zilivyoidhinishwa na Bunge.

5.2 **Kwa kuwa**, Mfuko wa Mahakama unakabiliwa na uhaba wa watumishi wenye sifa zinazotakiwa katika kada mbalimbali,

Hivyo basi, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha inaongeza idadi ya watumishi wanaohitajika kwenye kada mbalimbali kwa awamu ili kusaidia kutekeleza majukumu ya Mfuko huu;

5.3 **Kwa kuwa**, mtiririko wa utoaji fedha kwenye Mfuko wa Mahakama umekuwa hauzingatii Mpango Kazi wa Mfuko husika,

Hivyo basi, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha inazingatia maelekezo ya kifungu cha 48 cha Sheria ya Bajeti Na. 11 ya mwaka 2015 kinachoitaka Hazina kutoa fedha kwenda Mfuko wa Mahakama kwa kila robo mwaka. Pia, Serikali ihakikishe ukomo unaotolewa unazingatia hali halisi ya mahitaji ya Mahakama,

5.4 **Kwa kuwa**, bajeti iliyotolewa kwa mwaka 2016/17 haikidhi mahitaji ya msingi ya Mfuko wa Mahakama hadi kupelekea Mfuko huu kukabiliwa na madeni mbalimbali yanayohusu posho ya wazee wa baraza, malipo ya pango

la nyumba za kuishi Majaji, ofisi za kuendesha Mahakama pamoja na madai mbalimbali ya watumishi,

Hivyo basi, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha inamalizia kupeleka kwenye Mfuko wa Mahakama baka ya matumizi mengineyo kiasi cha **shilingi bilioni 20** katika bajeti ya mwaka 2016/17 ili Mfuko huu uweze kulipa baadhi ya madeni hayo.

6.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, naomba nihitimishe kwa kukushukuru wewe Mheshimiwa Spika na Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson (Mb), Naibu Spika kwa kuongoza vema mashauriano kati ya Kamati ya Bajeti na Serikali. Namshukuru Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango (Mb), Waziri wa Fedha na Mipangona Mheshimiwa Dkt Ashatu Kijajil (Mb), Naibu Waziri wa Fedha na Mipango kwa ushirikiano wao kwa Kamati. Aidha, Kamati inamshukuru pia Mheshimiwa Proff. Palamagamba Kabudi , (Mb), Waziri wa Katiba na Sheria na Mtendaji Mkuu wa Mahakama kwa kushirikiana na Kamati wakati wa majadiliano.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru wajumbe wa Kamati hii kwa umakini wao katika kujadili na kutoa maoni na mapendekezo mbalimbali kuhusu Bajeti ya Mfuko wa Mahakama. Naomba kuwatambua wajumbe hao kama ifuatavyo;

- 1) Mhe. Hawa Abdulrahman Ghasia, Mb – Mwenyekiti
- 2) Mhe. Josephat Sinkamba Kandege, Mb - M/Mwenyekiti
- 3) Mhe. Hamida Mohamedi Abdallah, Mb
- 4) Mhe. David Ernest Silinde, Mb
- 5) Mhe. Mbaraka Kitwana Dau, Mb
- 6) Mhe. Mendrad Lutengano Kigola, Mb
- 7) Mhe. Maria Ndilla Kangoye, Mb
- 8) Mhe. Susan Peter Maselle, Mb
- 9) Mhe. Agustino Manyanda Masele, Mb
- 10) Mhe. Freeman Aikael Mbewe, Mb
- 11) Mhe. Flatei Gregory Massay, Mb

- 12) Mhe. Makame Kassim Makame, Mb
- 13) Mhe. Janet Zebedayo Mbene, Mb
- 14) Mhe. Cecil David Mwambe, Mb
- 15) Mhe. Susana Chogisasi Mgonukulima, Mb
- 16) Mhe. Subira Khamis Mgali, Mb
- 17) Mhe. Juma Hamad Omar, Mb
- 18) Mhe. Ali Hassan Omari, Mb
- 19) Mhe. Martha Jachi Umbulla, Mb
- 20) Mhe. Jerome Bwanausi, Mb
- 21) Mhe. Jitu Vrajjal Soni, Mb
- 22) Mhe. Abdallah M. Bulembo, Mb
- 23) Mhe. Andrew John Chenge, Mb
- 24) Mhe. Mussa A. Zungu, Mb
- 25) Mhe. Japhet Ngalilonga Hasunga, Mb
- 26) Mhe. Dalali Peter Kafumu, Mb
- 27) Mhe. Albert Obama Ntabaliba, Mb

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii, pia kumshukuru Katibu wa Bunge Dkt Thomas Kashililah kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo, pamoja na Sekretarieti ya Kamati ya Bajeti kwa kuipa ushauri wa kitaalamu Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo naliomba Bunge lako tukufu sasa lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mfuko wa Mahakama – Fungu 40, kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 kama yalivyowasilishwa na Waziri wa Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja hii.

Subira Khamis Mgali, Mb

Kny: MWENYEKITI

KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI

25 APRILI, 2017

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, sasa namwita Msemaji wa Kambi ya Upinzani awasilishe taarifa, Mheshimiwa Tundu Lissu. (*Makof*)

MHE. TUNDU A.M. LISSU – MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako Tukufu, naomba kuwasilisha maoni ya Kambi kuhusu Mpango na Makadirio ya mapato...

KUHUSU UTARATIBU

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU): Kuhusu Utaratibu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Tundu Lissu, hebu keti kitako, naona kuna Kuhusu Utaratibu.

MHE. TUNDU A.M. LISSU – MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA: *Okay.*

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU): Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu, nakwenda na ile Kanuni ya 68(1) lakini inakwenda kuzungumzia Kanuni ya 64(1) na vifungu vyake vidogo. Kwanza nitasoma Kanuni ya 64(2) ambayo inasema:-

"Mbunge yoyote anayeamini kuwa Mbunge mwingine amevunja au amekiuka masharti ya fasili ya (1) ya Kanuni hii, atasimama mahali pake na kumwambia Mheshimiwa Spika "Kuhusu utaratibu".

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuniruhusu nizungumze maneno ya utaratibu. Nimekuwa nikipitia hotuba ya Kambi ya Upinzani...

WABUNGE FULANI: Umeitoa wapi?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU): Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeipitia hotuba ya Kambi ya Upinzani na naomba kusema kwamba, namheshimu sana Mheshimiwa Tundu Lissu kwa weledi mkubwa alionao na kwa kazi ambazo amekuwa akizifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kupitia hotuba hiyo, nataka kuzungumza maneno ya utaratibu ambayo yanajitokeza kwenye Kanuni ya 64(1). Jambo la kwanza la kiutaratibu ambalo nimeligundua kwenye hotuba hii, yapo maeneo mengi tu kwenye hiyo hotuba ambayo kwa kiasi kikubwa yanahusiana na mienendo ya kesi ambazo ziko mahakamani na hii ni kinyume na Kanuni ya 64(1)(c). (*Makofî*)

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU): Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile katika hotuba hii yapo mambo ambayo yanazungumzia mwenendo wa Rais ambayo ni kinyume na Kanuni 64(1)(e). (*Makofî*)

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU): Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ndani ya hotuba hii yamezungumziwa mambo ambayo yanahusika na mwenendo wa watu ambao wanashughulikia masuala ya kutoa haki ambapo ni kinyume na Kanuni 64(1)(e). (*Makofî*)

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU): Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo pia maeneo ambayo yanazungumzia mambo ambayo tulikwishayafanya maamuzi humu ndani.

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU): Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo hayo yalishawasilishwa wakati wa hotuba pia ya Kiongozi ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni na tulishayaondoa kwa mujibu ya Kanuni 64(1)(c). (*Makof*)

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu hoja yenye we imekiukwa Kanuni hizo ambazo nilizisema, naomba unipe utaratibu ni kwa nini hoja hii isirudishwe Mezani kwako na maeneo ambayo yanakiuka Kanuni hizi yaweze kuondolewa na ndipo hoja hii iweze kuwasilishwa ndani ya Bunge hili. (*Makof*)

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, naomba utulivu. Nimeombwa suala la utaratibu, amelielezea Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu kwa sahihi kabisa. Kikanuni ndivyo hivyo zilivyokaa.

Waheshimiwa Wabunge, sasa kuhusiana na tukio, mimi mwenyewe hapa nina tatizo moja, naona ndiyo naletewa sasa...

WABUNGE FULANI: Ndiyo. (*Makof*)

MWENYEKITI: Sasa uamuzi wangu kuhusu utaratibu, maeneo hayo ambayo Mheshimiwa Waziri Nchi ameyasema

...

WABUNGE FULANI: Ameyapata wapi?

MWENYEKITI: Yeye ameyapata...

WABUNGE FULANI: Wapi?

MWENYEKITI: Hiyo sio hoja, tusibishane na Kiti.

MBUNGE FULANI: Ni hoja.

MWENYEKITI: Kitu kimoja ambacho nimeambiwa na nilikuwa naulizia kwa nini sijaletewa hotuba hapa, nimepewa maelezo na Meza kwamba Kambi Rasmi ya Upinzani walichelewesha kupeleka kwenye uchapishaji, hilo ni la huko.

MBUNGE FULANI: Yeye ameipata wapi?

MWENYEKITI: Hata hivyo, ili twende vizuri sasa, maana taarifa hii lazima iwasilishwe hatua ya kwanza lakini kama yapo maeneo ambayo tayari yameshatolewa maamuzi kwamba yasirudiwe hatuwezi kuyarudia. (*Makofi*)

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)

MWENYEKITI: Ninachomtaka Mheshimiwa Waziri yeye anayajua maeneo hayo atuambie ibara...

MBUNGE FULANI: Siyo atuambie awasilishe kwanza.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, sasa mnaongoza Bunge ninyi?

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)

MWENYEKITI: Mniachie basi nitoe...

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, mbona linawasumbua sana suala hili?

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: *(Hakutumia kipaza sauti)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Msigwa, nakuheshimu sana, tafadhali.

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)

MWENYEKITI: Mkiendelea hivi, mnajua nina madaraka ya kuweza kutumia, sitaki kufika huko.

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)

MWENYEKITI: Sasa naongeza muda usiozidi dakika 30 ili turuhusu shughuli hii ikamilike. *(Makof)*

MBUNGE FULANI: Hapo sawa.

MWENYEKITI: Ninachotaka sasa Serikali wanisaidie zile *paraghaphs* ambazo zina tatizo utasema ...

MBUNGE FULANI: Asome zijulikane.

MWENYEKITI: Lakini Mheshimiwa Tundu Lissu uwasilishe hotuba yako.

MHE. TUNDU A.M. LISSU – MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA: *Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuwa nasoma kwa siku mbili zilizopita maandiko ya Walimu wangu, Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe (the Parliament and Electoral Process) na mwalimu wangu mwingine leo ni Waziri Katiba na Sheria, Profesa Pala Kabudi (the state and party). Kwa hiki kinachoendelea katika Bunge hili linaloitwa la vyama vingi yanathibitisha kitu kimoja, hili litakuwa Bunge la hovyo kuliko Bunge la wakati wa chama kimoja. Kama Bunge litaruhusu Serikali iwe inaanua namna ya kukosolewa hili halitakuwa Bunge. (Makof) [Maneno haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]*

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU: Taarifa.

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)

MHE. TUNDU A.M. LISSU – MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA: *Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba niendelee.*

WABUNGE FULANI: Wewe endelea.

MHE. TUNDU A.M. LISSU – MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni mara yangu ya saba kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu ...

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU: Taarifa.

MHE. TUNDU A.M. LISSU – MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA: ...na kutoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Tundu Lissu, wewe ni mwanasheria mzuri tu na una uzoefu...

MHE. TUNDU A.M. LISSU – MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA: Nafahamu.

MWENYEKITI: Huwezi ukatusomea taarifa hapa ambayo ni tofauti na hiyo ambayo umetuandikia, haiwezekani! Kwa hiyo, maneno yako *so called* utangulizi, naagiza yafutwe kwenye *Hansardsasa* hivi. (*Makofii*)

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)

MWENYEKITI: Wewe nenda *straight* kwenye taarifa yenu kama mlivyoandika, niliyonayo hapa hayana maneno hayo uliyoyasema sasa hivi.

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)

MBUNGE FULANI: Afute.

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)

MHE. TUNDU A.M. LISSU – MSEMADI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni mara yangu ya saba kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu na kutoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako Tukufu kuhusu Wizara ya Mambo ya Katiba na Sheria. Tangu mwaka 2010 hadi mwezi uliopita, Wizara hii imeongoza kwa kuwa na mabadiliko mengi ya Mawaziri kuliko Wizara nyingine yoyote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, itakumbukwa kwanza Wizara hii mwaka 2010 ilianza na Waziri Mheshimiwa Celina Ompeshi Kombani, Mheshimiwa Mathias Mendrad Chikawe, Mwalimu wangu Dkt. Asha-Rose Mtengeti Migiro, Mwalimu wangu wa pili Dkt. Harrison George Mwakyembe na sasa kaka yangu na Mwalimu wangu wa tatu wa sheria, Mheshimiwa Profesa Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ushahidi huu, tangu niwe Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako Tukufu, tumekuwa na Mawaziri tofauti wa Mambo ya Katiba na Sheria kwa takribani kila baada ya mwaka mmoja na miezi mitatu. Kwa vyovyyote vile inavyoweza kuelezeza hii ni *rate of turn over* kubwa sana katika uongozi wa Wizara yoyote ile. Kama nilivyosema mwanzoni katika kipindi hicho hakuna Wizara nyingine yoyote katika Serikali hii ambayo imekuwa na mabadiliko ya mara kwa mara ya namna hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako Tukufu mabadiliko haya ya mara kwa mara ya Mawaziri ya Mambo ya Katiba na Sheria yanaashiria kitu kimoja kikubwa. Mawaziri husika walishindwa ama kwa sababu zao binafsi, ama kwa sababu za mfumo wetu wa kisiasa na kikatiba kuiongoza nchi yetu katika kutatua matatizo makubwa ya kisiasa na kikatiba ambayo yameikabili nchi yetu kwa miongo kadhaa. Tumeyazungumza matatizo haya kwa kipindi chote ambacho nimekuwa Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani wa Bunge lako Tukufu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Profesa Kabudi anaweza kuwa mgeni katika Bunge lako Tukufu na katika Wizara ya Mambo ya Katiba na Sheria. Hata hivyo, Mheshimiwa Profesa Kabudi sio mgeni hata kidogo katika uelewa wa matatizo makubwa ya kisiasa na kikatiba ya nchi yetu. Mwaka 1984 Profesa Kabudi akiwa mwanafunzi wa Shahada ya Uzamili ya Sheria ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam aliandika *thesis* yake kuhusu Muungano wa Tanganyika na Zanzibar (*the International Law Examination of the Union between Tanganyika and Zanzibar*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika *thesis* yake, Mheshimiwa Profesa Kabudi alikuwa mtu wa kwanza kuweka hadharani ushahidi wa nyaraka wa chanzo cha kuchafuka kwa hali ya hewa ya kisiasa Zanzibar mwaka 1983/1984 kulikopelekeea kung'olewa madarakani kwa Rais wa pili wa Zanzibar Alhaj Aboud Jumbe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaalam wa Mheshimiwa Profesa Kabudi haukuishia kwenye uelewa wake wa masuala ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar. Mwaka 1985 Profesa Kabudi na Dkt. Agrey Mlimuka walikuwa wasomi wa kwanza kabisa kuelewa na kuelezea historia ya jinsi chama kimoja kwanza TANU na badaye CCM kilivyotumika kulimbikiza madaraka makubwa kikatiba na kisheria kwa Serikali na ndani ya Serikali kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, makala yao *The State and the Party* (Dola na Chama) katika *The State and Working People in Tanzania* kitabu kilichohaririwa na Profesa Issa Shivji na kuchapishwa mwaka 1985 lilikuwa andiko la kwanza la kisomi kuelezea dhana ya chama dola katika mfumo wetu wa kisiasa na kikatiba na jinsi chama dola hicho kilivyovunja nguvu ya Bunge kama chombo kikuu cha maamuzi katika nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya utaalam na uelewa wake mkubwa wa masuala muhimu ya kikatiba na kisheria ya nchi yetu, mwaka 2012 Mheshimiwa Profesa Kabudi

aliteuliwa na Rais Jakaya Mrisho Kikwete kuwa mjumbe wa Tume ya Mabadiliko ya Katiba maarufu kama Tume ya Warioba. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama inavyofahamika, Tume hiyo ndiyo ilikusanya maoni ya Watanzania kuandaa ripoti na rasimu ya Katiba mpya kwa ajili ya nchi yetu na kuiwasilisha mbele ya Bunge Maalum mnamo mwezi Februari 2014. Kama mwanafunzi wake na mmoja wa wale ambao tumefuatilia maisha ya kitaaluma ya Mheshimiwa Profesa Kabudi kwa karibu, naweza kusema bila wasiwasi wala shaka yoyote kwamba ripoti ya Tume ya Warioba na Rasimu ya Katiba Mpya ina alama za vidole vya kitaaluma vya Mheshimiwa Profesa Kabudi kuliko pengine vya mjumbe mwingine yejote wa Tume hiyo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kusema hivyo hakuna maana ya kudharau michango ya Wajumbe wengine wote wa Tume ya Warioba bali ni kutambua mchango mkubwa wa Waziri wa sasa wa Mambo ya Katiba na Sheria katika mchakato huo wa kihistoria katika nchi yetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu zote hizi, wakati ni halali kabisa kumpongeza Profesa Kabudi kwa kuteuliwa katika nafasi yake hii mpya, ni vizuri kumkumbusha juu ya majukumu makubwa na mazito ambao nafasi yake hii inamlazimisha kuyabeba. Ni vizuri zaidi kumkumbusha kwamba mazingira ya utekelezaji wa majukumu hayo yanamlazimisha kuchagua kati ya kusimamia maslahi ya kweli na ya kudumu ya nchi yetu ambayo yanajonesha katika maandiko yake ya kitaaluma na katika ripoti ya Tume ya Mabadiliko ya Katiba na maslahi ya muda ya kisiasa ambayo mara nydingi hayana maisha marefu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutaanza na suala la Katiba Mpya. Katika taarifa yake kwa Kamati ya Kudumu ya Katiba na Sheria ya mwezi uliopita, Mheshimiwa Profesa Kabudi amezungumzia suala la Katiba Mpya kwa aya moja tu yenye

kichwa cha habari 'mambo ya Katiba' na nimeona kwenye hotuba yake ameifuta kabisa hiyo habari ya Katiba Mpya. (*Makof/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Mheshimiwa Waziri, Serikali ya Awamu ya Tano inatambua umuhimu wa nchi kuwa na Katiba Mpya. Hata hivyo, ikumbukwe kuwa mara baada ya Serikali ya Awamu ya Tano kuingia madarakani ilianza kazi kwa kuunda Serikali na kufanya mabadiliko ya kina ya miundo na mifumo ya kiutendaji. Kwa sasa baada ya kazi hiyo kukamilika Serikali inapitia sheria zinazohusika na mchakato wa mabadiliko ya Katiba kwa madhumuni ya kubaini utaratibu mzuri wa kuendelea na mchakato huo kutoka pale ulipoishia. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hiyo imeainisha mambo saba ambayo Mheshimiwa Waziri ameyaita maeneo mahsusini ya kipaumbele. Kati ya hayo, hakuna jambo hata moja linalohusu Katiba Mpya ambayo hata hajatajwa kabisa. Aidha, katika mchanganuo wa matumizi ya bajeti kwa kila fungu hakuna fungu hata moja linalohusu Katiba Mpya. Vilevile katika vitabu vya randama kwa mafungu yote sita yaliyo chini ya Wizara ya Mambo ya Katiba na Sheria hakuna kasma hata moja ambayo imetengwa kwa ajili ya Katiba Mpya. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maneno mengine mchakato wa Katiba Mpya ambayo Mheshimiwa Waziri anataka tuamini kwamba haujauawa na Serikali ya Awamu ya Tano haujatengewa hata senti moja katika bajeti inayopendekezwa kwa Bunge lako Tukufu mwaka huu. Huu ni mwendelezo wa bajeti ya mwaka jana ambayo nayo haikutenga hata senti moja kwa ajili ya mchakato wa Katiba Mpya. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maoni yangu juu ya bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka 2015/2016, nilielezea kwa kirefu jinsi ambavyo Katiba Mpya imekwama. Tarehe 26 Aprili, 2014 yaani *the Golden Jubilee* ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ambayo Rais Dkt. Jakaya Kikwete

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

aliwaahidi Watanzania kuwa ndiyo tarehe ya nchi yetu kuwa na Katiba Mpya ilifika na ikapita bila nchi yetu kuwa na Katiba mpya. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 30 Aprili, 2015 ambayo Rais Kikwete aliwaahidi wananchi kuwa ndiyo ingekuwa siku ya kufanyika kwa kura ya maoni kuhusu Katiba inayopendekezwa, ahadi ambayo ilirudiwarudiwa na kila kiongozi wa CCM na Serikali yake ndani na nje ya Bunge hili Tukufu ilifika na kupita bila kura ya maoni kufanyika. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo na kwa kipindi kilichobakia cha utawala wa Rais Kikwete, viongozi wa CCM na Serikali waliendelea kusisitiza ijapo kwa sauti za kinyonge kwamba kura hiyo ya maoni ingefanyika katika tarehe ambayo hata hivyo hawakuwa tayari kuitaja tena. Haikufanyika hadi wakati Rais Kikwete anaondoka madarakani na Rais Magufuli anaingia madarakani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana nilisema katika maoni yangu ya mwaka juzi kwamba kwenye *signature issue ya utawala wake yaani Katiba Mpya huyu ni Rais aliyeshindwa na hii ni Serikali iliyoshindwa.* (*Makof*) **[Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais John Pombe Magufuli alisema...

KUHUSU UTARATIBU

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Kuhusu Utaratibu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa AG.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 64(2), kuhusu utaratibu, hayo maneno yanayosemwa, moja, Serikali haijashindwa wala Rais hajashindwa...

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)

WABUNGE FULANI: Si una muda wa kujibu?

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Hapana!

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Hakuna hiyo kwa sababu hata maneno yalivyoandikwa huwezi kuainisha ni Serikali ipi na Serikali ni ileile ya Chama cha Mapinduzi. (*Makofii*)

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)

MBUNGE FULANI: Katiba iko wapi, mnayo?

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Katiba hatujapiga kura...

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, maneno yalivyowekwa yamekaa vibaya haya, hayaweki mpaka lakini hata hayaweki kuweka mpaka kwa sababu ni mwendelezo wa Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Naomba maneno haya yaondoke yanakiuka Kanuni ya 64.

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Tundu Lissu...

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, naomba utulivu. Mheshimiwa Tundu Lissu, kwa haya maneno yanayosema kwenye *signature issue* ya utawala wake mpaka neno iliyoshindwa, naomba uyaondoe, uendelee tu na mtiririko wako ili twende vizuri. Kwa hiyo na *Hansard* na yenyeewe yawe *expunged* maneno haya yasiwepo. Endelea na hotuba yako.

MHE. TUNDU A.M. LISSU – MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo ni maneno ambayo yapo kwenye *Hansard* kwa miaka mitatu iliyopita, nimeyatoa kwenye *Hansard*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais Dkt. John Pombe Magufuli ameshatangaza hadharani kwamba Katiba Mpya siyo kipaumbele cha Serikali yake. Rais amedai kwamba wakati wa kampeni za Uchaguzi Mkuu wa 2015 yeye hakutoa ahadi yoyote kwa Watanzania kwamba atawaleta Katiba Mpya akichaguliwa kuwa Rais. Kwa hiyo, kwa msimamo huo wa Rais Magufuli, mchakato wa Katiba Mpya ambao hadi ulipoishia kwa kuitishwa kwa Katiba Inayopendekezwa ulikwisha kugharimu jumla ya shilingi bilioni 121.463, umekwishakufa na kuzikwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Profesa Kabudi ni mtu mwelewa sana wa siasa za kikatiba za Tanzania. Kwa uelewa wake mkubwa wa masuala haya, Mheshimiwa Profesa Kabudi anafahamu vyema kivuli kirefu cha urais wa kifalme ambao ndio imekuwa *the organizing principle* ya katiba na siasa za Tanzania tangu mwaka 1962 ilipotungwa Katiba ya Jamhuri. Kwa uelewa wake huo, Mheshimiwa Profesa Kabudi anafahamu au anatakiwa kufahamu kwamba kwa katiba na sheria za Tanzania na kwa mila na desturi za kisiasa na kikatiba Rais akishasema hawezikubishiwa na Waziri wake. Ni suala la kama wasemavyo Wakatoliki *Roma locuta, causa finita* yaani Roma ikishasema ndiyo mwisho wa mashauri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu hiyo Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako Tukufu inataka kujua kutoka kwa Mheshimiwa Waziri Serikali ya Awamu ya Tano inatambuaje umuhimu wa nchi yetu kuwa na Katiba Mpya wakati Rais Magufuli amekwishesha Katiba Mpya sio kipaumbele cha Serikali yake. Je, kama kweli Serikali hii ina mpango wa kuundeleza mchakato wa Katiba kutoka pale ulipoishia ni kwa nini Serikali hii haijatenga hata senti moja kwenye bajeti hii kwa ajili ya jambo hili muhimu? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila majibu ya kweli ya maswali haya, Waziri Mheshimiwa Kabudi atakuwa ameangukia kwenye shimo lile lile waliloangukia watangulizi wake wanne la kushindwa kutekeleza matakwa na matarajio ya Watanzania ya kupata Katiba Mpya na ya kidemokrasia itakayokidhi mahitaji ya kizazi hiki na vizazi vijavyo. Sio ajabu maisha yake kama Waziri wa Mambo ya Katiba na Sheria yakawa mafupi kama ilivyokuwa kwa watangulizi wake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nizungumzie mahakama...

MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MHE. TUNDU A.M. LISSU – MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mahakama ya Tanzania haina kiongozi kamili yaani Jaji Mkuu...

MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MHE. TUNDU A.M. LISSU – MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA: Hii ni kwa sababu tangu Jaji Mkuu Mohamed Chande Othman astaafu tarehe 1 Januari, 2017, Rais John Pombe Magufuli hajateua Jaji Mkuu mpya kuchukua nafasi iliyoachwa wazi na Jaji Mkuu Chande Othman. (*Makofii*)

KUHUSU UTARATIBU

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU): Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

MWENYEKIDI: Mheshimiwa Lissu subiri kidogo, Mheshimiwa Waziri wa Nchi.

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tulikuwa tunamwomba sana Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani atupeleke kwa mujibu wa kitabu chake cha ...

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)

MHE. TUNDU A.M. LISSU – MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA: Ukurasa wa 29.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU): Mheshimiwa Mwenyekiti, atupeleke kwa mujibu wa kitabu chake...

MHE. TUNDU A.M. LISSU – MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA: Ukurasa wa 29.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU): Mheshimiwa Mwenyekiti ...

MWENYEKITI: Nimekuelewa Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Tundu Lissu kwa sababu hawa viongozi wana hii hotuba...

MHE. TUNDU A.M. LISSU – MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA: Ndiyo.

MWENYEKITI: Wewe unapofanya *summary* useme kwamba naenda sasa ukurasa wa ...

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)

MHE. TUNDU A.M. LISSU – MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA: Sawasawa.

MWENYEKITI: Itawasaidia ili wawe pamoja na wewe.
(Makofii)

MHE. TUNDU A.M. LISSU – MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU): Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kiutaratibu...

MWENYEKITI: Ngoja kidogo Mheshimiwa Lissu, Mheshimiwa Waziri wa Nchi.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waheshimiwa Wabunge tuelewane, Mheshimiwa Tundu Lissu nakuelewa. Mheshimiwa Tundu Lissu unatupeleka ukiwa umeacha maeneo mengine...

MHE. TUNDU A.M. LISSU – MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA: Nitarudi.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU): Na unaenda kutupeleka kwenye *page*...

MHE. TUNDU A.M. LISSU – MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA: Nitarudi.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba suala la utaratibu na utaratibu wangu ni kwamba...

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU): Mheshimiwa Mwenyekiti, pale ambapo anatakiwa kuanza sasa ni masuala ya haki za binadamu. (*Makofi*)

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU): Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hatatusomea eneo hili la haki za binadamu ina maana kwamba ...

MHE. TUNDU A.M. LISSU – MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA: Sijasema hivyo.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU): Utaratibu wangu...

MHE. TUNDU A.M. LISSU – MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA: Sijasema hivyo.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU): Basi naomba ...

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU): Mheshimiwa Mwenyekiti, vinginevyo basi utuambie utaratibu wa kusoma hii...

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)

MHE. JOHN J. MNYIKA: Ni wajibu wako kufuatilia?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU): Kwa hiyo, kama tunaanza ...

MHE. JOHN J. MNYIKA: Ni wajibu wako kufuatilia anasoma wapi.

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)

MWENYEKITI: Waheshimiwa hebu kaeni chini. Nakuomba Mheshimiwa Gekul kaa chini. Hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi ni kwamba mtiririko wako usipokuwa wa wazi utawachanganya watu.

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)

MWENYEKITI: Ndijo maana nikasema kwa sababu lazima ufanye *summary*...

MHE. JOHN J. MNYIKA: *(Hakutumia kipaza sauti)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mnyika mimi siyo mtu wa kujaribiwa, nakuomba sana. *(Makof)*

MHE. JOHN J. MNYIKA: Anayoyasoma yamo humu humu.

MWENYEKITI: Mimi ndijo naongoza shughuli humu.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Sawa, lakini anayoyasoma yamo humu humu.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Hata Mheshimiwa January jana alifanya hivyo hivyo.

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)

MWENYEKITI: Sasa Mheshimiwa Tundu Lissu hebu soma hotuba yako kwa mtiririko ambao tunataka kuuona. *(Makof)*

MHE. JOHN J. MNYIKA: Ni wajibu wao kufuatilia.

WABUNGE FULANI: Unapendelea.

MHE. TUNDU A.M. LISSU – MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa 29, wa Kaimu Jaji Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mahakama ya Tanzania haina kiongozi wake kamili yaani Jaji Mkuu. Hii ni kwa sababu tangu Jaji Mkuu Mohamed Chande Othman astaaafu tarehe 1 Januari, 2017, Rais John Pombe Magufuli hajateua Jaji Mkuu mpya kuchukua nafasi iliyoachwa wazi na Jaji Mkuu Chande Othman. Badala yake Rais Magufuli amemteua Jaji wa Rufaa Profesa Ibrahim Hamis Juma kuwa Kaimu Jaji Mkuu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 118(4) ya Katiba yetu Rais anaruhusiwa kuteua Kaimu Jaji Mkuu iwapo itatokea kitu cha Jaji Mkuu kitakuwa wazi au kwa Jaji Mkuu kuwa hayupo Tanzania au Jaji Mkuu atashindwa kutekeleza kazi yake kwa sababu yoyote na Rais ataona kuwa kwa muda wa tukio lolote kati ya hayo matatu inafaa kumteua Kaimu Jaji Mkuu. Kaimu Jaji Mkuu aliyeulewa kwa utaratibu huu atatekeleza kazi za Jaji Mkuu mpaka atakapoteuliwa Jaji Mkuu mwengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwapo kwa Ibara ya 118(4), Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako Tukufu inaamini kwamba *Rais Magufuli anavunja Katiba ya nchi* yetu kwa kushindwa kuteua Jaji Mkuu kamili takribani miezi mitano tangu kustaafu. (*Makofii*) **[Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

KUHUSU UTARATIBU

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE WALEMAVU): Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Tundu Lissu, nenda ukakae tu, Kuhusu Utaratibu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU): Mheshimiwa Mwenyekiti, nilishayasema haya mambo toka mwanzo na ndio maana nilisema Kanuni ya 64(1) na maeneo niliyoyataja yameendelea kuvunjwa kwa kutumia hotuba hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipokuwa nasema hotuba hii isomwe kwa mtiririko maana yangu ilikuwa twende eneo moja na lingine ili la kubaki libaki na la kuondoka liweze kuondoka.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Msigwa na jirani yako kaeni chini, kaa chini.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU): Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nirudi kwenye hili la kikatiba. Ibara ya 118(3) na (4) imeeleza ni wakati gani Mheshimiwa Rais atateua Kaimu Jaji lakini Ibara hizo wala hazioneishi...

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

MBUNGE FULANI: Atajibu, anapoteza muda.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU): Ni kwa muda gani...

MHE. TUNDU A.M. LISSU – MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA: Huu ni utaratibu gani?

MBUNGE FULANI: Anapoteza muda.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Kuhusu Utaratibu.

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

MWENYEKITI: Mheshimiwa huwezi ukaomba utaratibu juu ya utaratibu.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Kwa sababu anachokisema kinavunja utaratibu. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Kaa chini wewe.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Anachokisema kinavunja utaratibu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mnyika kaa chini.

MBUNGE FULANI: Mtoe nje.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU): Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge tusiwadanganye Watanzania...

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)

MHE. JOHN J. MNYIKA: Wewe unajibu kama nani?

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU): Mheshimiwa Mwenyekiti ...

MWENYEKITI: Jielekeze sasa kwenye hiyo ninayoitafuta mimi.

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU): Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kusema ni kwamba maneno yanayosema Mheshimiwa Rais anavunja Katiba yaondoke kwa sababu...

MHE. JOHN J. MNYIKA: Yaondoke kwa sababu gani?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU): Kwa sababu ibara ndogo ya (5) inasema, Kaimu Jaji Mkuu atatekeleza kazi za Jaji Mkuu mpaka atakapoteuliwa Jaji Mkuu mwingine. Kipengele hiki hakisemi ni muda gani?

WABUNGE FULANI: Wewe.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU): Ni mpaka pale atakapoteuliwa Jaji Mkuu mwingine. Kwa hiyo, Rais amevunjaje Katiba hapo? (*Makofii*)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Jenista, Waziri wa Nchi. Tafsiri hiyo ya Katiba kuhusiana na Jaji Mkuu kipindi ambacho anakaimu uliyoyasema ndio sahihi. (*Makofii*)

Sasa kitu ambacho Mheshimiwa Tundu Lissu amekosea ni pale aliposema Rais anavunja Katiba ya nchi. (*Makofii*)

WABUNGE FULANI: Kweli.

MWENYEKITI: Sasa hizo *sweeping statements* mimi sitaziruhusu humu...

(*Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio*)

MWENYEKITI: *No, no. Masuala hayo kama una-feel very strongly kwamba there is ukiukwaji wa Katiba, ninyi wanasheria mnajua cha kufanya. Humu Bungeni msituletee taarifa ambazo zinapotosha wananchi.* (*Makofii*)

(*Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio*)

MWENYEKITI: Naagiza maneno yale ambayo yanasema, *Rais kwa kufanya hivyo anakiuka Katiba...*

MBUNGE FULANI: Ni kweli.

MWENYEKITI: Yaondolewe kwenye *Hansard*. Endelea sasa Mheshimiwa. (*Makofii*)

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)

MWENYEKITI: Mheshimiwa nitakutoa nje sasa hivi, nakuheshimu sana.

MHE. TUNDU A.M. LISSU – MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 118(4) ya Katiba haikutungwa kwa lengo la kumwezesha Rais kuteua Kaimu Jaji Mkuu bila kikomo cha muda. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyo kwa sheria zote, Ibara ya 118(4) ina sababu yake maalum. Ibara hiyo imewekwa kwa makusudi ya kuhakikisha kwamba kwa muda wote kunakuwa na kiongozi wa Mahakama ya Rufani ya Tanzania pamoja na kiongozi wa Mahakama ya Tanzania wakati Jaji Mkuu kamili anasubiria kuteuliwa. Kaimu Jaji Mkuu ni sawa na kile kinachoitwa na wanasheria *an interlocutory position*. Kaimu Jaji Mkuu ni nafasi ya muda inayoshikiliwa na mtu mwenye sifa za kuwa Jaji Mkuu kabla nafasi hiyo haijajazwa na Jaji Mkuu kamili. Swali halali linalohitaji majibu ni, je, Kaimu Jaji Mkuu anastahili kuwepo madarakani kwa muda gani? Hili ni suala la tafsiri ya Katiba linalohitaji kujibiwa na Mahakama. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, miezi mitano ni muda mrefu mno wa kuwa na Kaimu Jaji Mkuu. Hii ni kwa sababu katika historia yetu yote tangu uhuru haijawahi kutokea Rais wa nchi yetu akashindwa kuteua Jaji Mkuu kamili kujaza nafasi iliyo wazi ya Jaji Mkuu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge lako Tukufu kama mojawapo ya mihimili mikuu ya dola Tanzania lina kiongozi wake mkuu muda wote, Spika au Naibu Spika. Serikali kama mihimili mwingine mkuu ina kiongozi wake mkuu muda wote, Rais au Makamu wa Rais. Kwa Mahakama ya Tanzania

mhimili mkuu wa tatu wa dola ya Tanzania kutokuwa na kiongozi wake kamili miezi mitano baada ya kustaaifu kwa Jaji Mkuu Chande Othman kunatoa taswira potofu kwamba mahakama ina hadhi hafifu au ya chini ikilinganishwa na mihimili mingine mikuu ya dola ya Tanzania.

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)

MHE. TUNDU A.M. LISSU – MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA: Kitendo hiki vilevile kinatoa taswira potofu kwamba mionganoni mwa Majaji wote wa Rufaa au wa Mahakama Kuu...

MWENYEKITI: Naku-*interrupt* sasa, Mheshimiwa AG.

MBUNGE FULANI: Mlinde muda wake.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, hadhi ya mahakama na mihimili yote mitatu ya dola imewekwa kikatiba, haiwezi kuwa kwa sababu huyu hajateuliwa. Kwa mujibu wa Sheria ya Tafsiri ya Sheria, *The Interpretation of Laws Act, Cap 1* inasema...

MBUNGE FULANI: Si utajibu bwana.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mwongozo.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, inasema kwamba anayekaimu...

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Atakuwa na mamlaka sawa na mwenye cheo mwenyewe na kwa sababu yapo kwenye Katiba...

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)

MHE. JOHN J. MNYIKA: Kuhusu utaratibu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mwanasheria Mkoo wa Serikali, nimekuelewa. Nasema hivi kwa suala hili ambalo linahusu tafsiri naamini mtoha hoja Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria atakapokuja kujibu kuna maeneo ambayo yanahitaji yanyooshwe. Nategemea hilo Profesa mtalifanya kwa ukamilifu. *AG* kwa sababu ya muda, tusiliendeleza, *it is okay. (Makof)*

MHE. TUNDU A.M. LISSU – MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kitendo hiki vilevile kinatoa taswira potofu kwamba pengine Kaimu Jaji Mkoo wa sasa hatoshelezi nafasi hiyo au kwamba mionganii mwa Majaji wote wa Rufaa au wa Mahakama Kuu ya Tanzania au Mawakili na Wanasheria wengine wa nchi hii pamoja na wale wa nchi za Jumuiya ya Madola hakuna hata mmoja wao mwenye uwezo au sifa za kuwa Jaji Mkoo wa Tanzania. *(Makof)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako Tukufu inamtaka Mheshimiwa Waziri amshauri Rais Magufuli kwa heshima zote anazostahili amthibitishe Kaimu Jaji Mkoo Profesa Juma katika nafasi hiyo au vinginevyo atue mwanasheria mwininge ye yeyote anayemuona anafaa na ana sifa za kuwa Jaji Mkoo kamili wa Tanzania. Hali ilivyo sasa inawatia aibu wanasheria wote wa Tanzania na inaitia aibu nchi yetu katika Jumuiya ya Kimataifa. *(Makof)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kurudi kwenye ukurasa wa kumi, haki za binadamu. Katika taarifa yake kwa Kamati Mheshimiwa Profesa Kabudi alidai kwamba Wizara inaendelea kuimarisha na kusimamia uzingatiwaji wa misingi ya haki za binadamu kama ilivyoainishwa na kuhifadhiwa katika katiba na sheria za nchi. Madai haya hayaelezi hali halisi ya haki za binadamu katika nchi yetu. Ukweli ni kwamba kauli ya Mheshimiwa Profesa Kabudi inapotosha ukweli juu ya haki za binadamu katika nchi yetu. *(Makof)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, badala ya kupungua matukio ya ukiukwaji wa haki za binadamu unaofanywa na hasa vyombo vya ulinzi na usalama...

KUHUSU UTARATIBU

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU): Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

MHE. TUNDU A.M. LISSU – MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA: Ambayo Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako Tukufu...

MWENYEKITI: Kuhusu Utaratibu, Mheshimiwa Tundu Lissu kuna suala la utaratibu hapa.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU): Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni suala la utaratibu. Kanuni ya 64(1)(c) inazungumzia mambo ambayo yalikwishakufanyiwa maamuzi hayatakiwi kurejewa tena. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo analotaka kulisoma Mheshimiwa Tundu Lissu sasa.

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU): Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa uwasilishaji wa hotuba ya Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni, jambo hili na yale yanayofuata tuliyaoondo na Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni aliyaoondo kwa maneno yake. Ukipuafilia *Hansard* mambo haya yalishaondolewa kwa maamuzi ya Bunge. Ni suala la utaratibu mambo haya hayatakiwi kuendelea kubaki leo. (*Makofi*)

MHE. JOHN J. MNYIKA: Siyo jambo sahihi.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Tunaomba utusikilize na sisi.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Kuhusu Utaratibu kabla hujatoa uamuvi.

MBUNGE FULANI: Unasikiliza upande mmoja?

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge...

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)

MWENYEKITI: Hivi utalazimisha, kwanza sijakutambua.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla hujatoa uamuvi ungetusikiliza nini...

MWENYEKITI: Sijakuruhusu kuongea, kaa kwanza, twende vizuri. Mheshimiwa Tundu Lissu nenda ukaketi.

MBUNGE FULANI: Muwe mnatenda haki.

MWENYEKITI: Hebu sema sasa, unaongelea *point of order*, unaongelea nini?

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kuhusu utaratibu kwamba hayo anayoyasema kwanza hakukuwa na uamuvi wowote wa Bunge juu ya mambo anayoyasema. Pili, mambo anayosema yaliondolewa yaliondolewa kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu, hayahusu hii Wizara ya Katiba na Sheria. Hapa ambapo yanazungumzwa sasa ndio mahali pake. Kwa hiyo, Serikali isikilize iweze kutoa majibu juu ya mambo haya. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Kanuni ni kanuni tu, hatuwezi kujidai kwamba hatuzifahamu. Narudia uamuvi wa Kiti uliotolewa wakati wa majadiliano kuhusu hoja ya Waziri Mkuu kwenye eneo hili na ambalo Kiongozi wa Kambi Rasmi Bungeni

alikubali kuyaondoa ambayo yanahuusu haki za binadamu na tukienda kuangalia *Hansard* ipo, tusibishane.

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)

MHE. JOHN J. MNYIKA: Anazungumzia haki za binadamu na ana wajibu wa kujibiwa.

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, uamuzi ukishachukuliwa na Bunge wewe kama unataka kubadilisha

...

MHE. JOHN J. MNYIKA: Hapana, sio sahihi.

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, yale ya Waziri aliyojasema kwenye hotuba ndiyo maana nimeyaruhusu lakini hayo unayoshuka nayo ambayo ndiyo moja ya hoja...

MHE. JOHN J. MNYIKA: Yapi sasa?

MWENYEKITI: Nasema hayo hayapo.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Yapi sasa?

MBUNGE FULANI: Muachenii asome.

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, nimelinda sana muda wa Mheshimiwa Tundu Lissu, namuongezea dakika mbili tu halafu nasitisha shughuli za Bunge.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Hapana, muda wake ulindwe.

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)

MHE. TUNDU A.M. LISSU – MSEMADI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti...

MWENYEKITI: Usiendeleze malumbano.

MHE. TUNDU A.M. LISSU – MSEMADI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, wenyewe hatia huwa ni waoga. Wenyewe hatia na wenyewe madhambi ni waoga, ahsante sana. (*Makofii/Vigelegele*)

WABUNGE FULANI: Rais, Rais, Rais. (*Makofii/Vigelegele*)

WABUNGE FULANI: Waoga.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, nawasihi sana kwa lugha zetu hizi.

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)

MWENYEKITI: Nawasihi sana kwa lugha zetu hizi ambazo siyo za Kibunge. Hiyo ndiyo taarifa ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni. Mimi naamini kuititia mtoa hoja kuna maeneo mengi katika hotuba hii ambayo yanahitaji kunyooshwa.

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)

MWENYEKITI: Haiwezekani tukapotosha wananchi. (*Makofii*)

MHE. JOHN J. MNYIKA: Kama unataka yanyooshwe yazungumzwe basi.

MWENYEKITI: Sasa hiyo sio kazi yangu.

WABUNGE FULANI: Nyie waoga.

MWENYEKITI: Hiyo siyo kazi yangu mimi kama Kiti, lakini naamini wakati muafaka ninyi mtakapoanza kuchangia mpaka tutakapofika hatua ya kuhitimisha hoja hii kuititia mtoa hoja, kuna maeneo mengi yatanyooshwa tu.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Yazungumzwe sasa ili yanyooshwe.

MWENYEKITI: Na yatanyooshwa tu na ni lazima yanyooshwe. (*Makofii*)

**MAONI YA MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI
BUNGENI, WIZARA YA KATIBA NA SHERIA, MHESHIMIWA
TUNDU A.M. LISSU (MB.) KUHUSU MPANGO NA
MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA
FEDHA YA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA**
KWA MWAKA 2017/2018 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

(Kanuni ya 99(9) ya *Kanuni za Kudumu za Bunge, 2016*)

UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika,

Hii ni mara yangu ya saba kusimama mbele ya Bunge lako tukufu na kutoa Maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako tukufu kuhusu Wizara ya Mambo ya Katiba na Sheria. Tangu mwaka 2010 hadi mwezi uliopita, Wizara hii imeongoza kwa kuwa na mabadiliko mengi ya mawaziri kuliko Wizara nyingine yoyote. Kama utakavyokumbuka, Mheshimiwa Spika, mara baada ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2010, mtu wa kwanza kuteuliwa Waziri wa Mambo ya Katiba na Sheria alikuwa marehemu Mheshimiwa Celina Ompeshi Kombani. Hakumaliza mwaka mmoja, kwani nafasi yake ilikabidhiwa kwa mwanasheria Mathew Meindrard Chikawe.

Mheshimiwa Chikawe alidumu kwenye nafasi hiyo kwa takriban miaka mitatu. Ilipofika mwezi Disemba 2014, Waziri Chikawe aliondolewa na nafasi hiyo ikakasimishwa kwa mwalimu wangu wa sheria, Mheshimiwa Dkt. Asha-Rose

Mtengeti-Migiro. Huyu alidumu kama Waziri wa Mambo ya Katiba na Sheria hadi mwezi Disemba, 2015, wakati nafasi yake ilipokasimishwa kwa mwalimu wangu mwagine wa sheria, Mheshimiwa Dkt. Harrison George Mwakyembe. Sasa, baada ya mwaka na miezi mitatu, nafasi ya Waziri wa Mambo ya Katiba na Sheria imekabidhiwa kwa kaka yangu na mwalimu wangu wa tatu wa sheria, Mheshimiwa Prof. Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi.

Kwa ushahidi huu, Mheshimiwa Spika, tangu niwe Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako tukufu, tumekuwa na Waziri tofauti wa Mambo ya Katiba na Sheria kwa takriban kila baada ya mwaka mmoja na miezi mitatu. Kwa vyovypole vili inavyoweza kuelezeza, hii ni *rate of turnover* kubwa sana katika uongozi wa Wizara yoyote ile. Na kama nilivyosema mwanzoni, katika kipindi hicho, hakuna Wizara nyiningine yoyote katika Serikali hii ya CCM ambayo imekuwa na mabadiliko ya mara kwa mara namna hii.

Mheshimiwa Spika,

Kwa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako tukufu, mabadiliko haya ya mara kwa mara ya Mawaziri wa Mambo ya Katiba na Sheria yanaashiria kitu kimoja kikubwa: Mawaziri husika walishindwa, ama kwa sababu zao binafsi ama kwa sababu za mfumo wetu wa kisiasa na kikatiba, kuiongoza nchi yetu katika kutatua matatizo makubwa ya kisiasa na kikatiba ambayo yameikabili nchi yetu kwa miongo kadhaa. Tumeyazungumza matatizo haya kwa kipindi chote ambacho nimekuwa Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako tukufu.

Mheshimiwa Spika,

Mheshimiwa Prof. Kabudi anaweza kuwa mgeni katika Bunge lako tukufu na katika Wizara ya Mambo ya Katiba na Sheria. Hata hivyo, Mheshimiwa Prof. Kabudi sio mgeni hata kidogo katika uelewa wa matatizo makubwa ya kisiasa na ya kikatiba ya nchi yetu. Mwaka 1984, Mheshimiwa Prof. Kabudi akiwa mwanafunzi wa Shahada ya Uzamili ya Sheria ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, aliandika *Thesis* yake kuhusu Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, *The International Law Examination of the Union Between Tanganyika and Zanzibar*.

Katika *Thesis* yake, Prof. Kabudi alikuwa mtu wa kwanza kuweka hadharani ushahidi wa nyaraka wa chanzo cha 'kuchafuka kwa hali ya hewa ya kisasa Zanzibar' mwaka 1983-84, kulikopelekea kung'olewa madarakani kwa Rais wa Pili wa Zanzibar, Alhaj Aboud Jumbe Mwinyi.

Mheshimiwa Spika,

Utaalamu wa Mheshimiwa Prof. Kabudi haukuishia kwenye uelewa wake wa masuala ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar. Mwaka 1985, Prof. Kabudi na Dkt. Aggrey K.L.J. Mlimuka walikuwa wasomi wa mwanzo kabisa kuelewa na kuelezea historia ya jinsi chama kimoja, kwanza TANU na baadae CCM, kilivyotumika kulimbikiza madaraka makubwa kikatiba na kisheria kwa Serikali na, ndani ya Serikali, kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano.

Makala yao, '*The State and the Party*', yaani '*Dola na Chama*', katika *The State and the Working People In Tanzania*, kitabu kilichohaririwa na Prof. Issa G. Shivji na kuchapishwa mwaka 1985, ilikuwa andiko la kwanza la kisomi kuelezea dhana ya 'chama-dola' katika mfumo wetu wa kisasa na kikatiba, na jinsi chama-dola hicho kilivyovunja nguvu ya Bunge kama chombo kikuu cha maamuzi katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika,

Kwa sababu ya utaalamu na uelewa wake mkubwa wa masuala muhimu ya kikatiba na kisheria ya nchi yetu, mwaka 2012 Mheshimiwa Prof. Kabudi aliteuliwa na Rais Jakaya Kikwete kuwa mjambe wa Tume ya Mabadiliko ya Katiba, maarufu kama Tume ya Warioba. Kama inavyofahamika, Tume hiyo ndiyo iliyokusanya maoni ya waTanzania, kuandaa Ripoti na Rasimu ya Katiba Mpya kwa ajili ya nchi yetu na kuiwasilisha mbele ya Bunge Maalum mnamo mwezi Aprili, 2014.

Kama mwanafunzi wake na mmoja wa wale ambao tumefuatilia maisha ya kitaaluma ya Mheshimiwa Prof. Palamagamba Kabudi kwa karibu, ninaweza kusema bila wasi wasi wala shaka yoyote kwamba Ripoti ya Tume ya Warioba na Rasimu ya Katiba Mpya ina alama za vidole vya kitaaluma vya Prof. Kabudi kuliko, pengine, vya mjambe

mwagine yeote wa Tume hiyo. Na kusema hivyo hakuna maana ya kudharau michango ya Wajumbe wengine wote wa Tume ya Warioba, bali ni kutambua mchango mkubwa wa Waziri wa sasa wa Mambo ya Katiba na Sheria katika mchakato huo wa kihistoria katika nchi yetu.

Kwa sababu zote hizi, wakati ni halali kabisa kumpongeza Mheshimiwa Prof. Kabudi kwa kuteuliwa katika nafasi yake hii mpya, ni vizuri kumkumbusha juu ya majukumu makubwa na mazito ambayo nafasi yake hii inamlazimisha kuyabeba. Na ni vizuri zaidi kumkumbusha kwamba mazingira ya utekelezaji wa majukumu hayo yanamlazimisha kuchagua kati ya kusimamia maslahi ya kweli na ya kudumu ya nchi yetu – ambayo yanajionyesha katika maandiko yake ya kitaaluma na katika Ripoti ya Tume ya Mabadiliko ya Katiba – na maslahi ya muda ya kisiasa ambayo mara nydingi hayana na maisha marefu. Tutaanza na suala la Katiba Mpya.

YA KATIBA MPYA

Mheshimiwa Spika,

Katika Taarifa yake kwa Kamati ya Kudumu ya Katiba na Sheria ya mwezi uliopita, Mheshimiwa Prof. Kabudi amezungumzia suala la Katiba Mpya kwa aya moja tu yenye kichwa cha habari ‘Mambo ya Katiba.’ Kwa mujibu wa Mheshimiwa Waziri, “*Serikali ya Awamu ya Tano inatambua umuhimu wa nchi kuwa na Katiba Mpya. Hata hivyo, ikumbukwe kuwa mara baada ya Serikali ya Awamu ya Tano kuingia madarakani ilianza kazi kwa kuunda Serikali na kufanya mapitio ya kina ya miundo na mifumo ya kiutendaji. Kwa sasa, baada ya kazi hiyo kukamilika Serikali inapitia sheria zinazohusika na mchakato wa mabadiliko ya Katiba kwa madhumuni ya kubaini utaratibu mzuri wa kuendelea na mchakato huo kutoka pale ulipoishia.*”¹

¹*Taarifa ya Mhe. Prof. Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi (MB), Waziri wa Mambo ya Katiba na Sheria, Akiwasilisha Mpango na Makadirio ya Bajeti ya Wizara kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/2018, Dodoma, Machi, 2017, uk. 8*

Mheshimiwa Spika,

Taarifa hiyo imeainisha mambo saba ambayo Mheshimiwa Waziri ameyaita 'maeneo mahususi ya kipaumbele.' Kati ya hayo, hakuna jambo hata moja linalohusu Katiba Mpya, ambayo hata haijatajwa kabisa. Aidha, katika 'mchanganuo wa matumizi ya bajeti kwa kila Fungu', hakuna Fungu hata moja linalohusu Katiba Mpya. Vile vile, katika vitabu vya Randama kwa Mafungu yote sita yaliyo chini ya Wizara ya Mambo ya Katiba na Sheria, hakuna kasma hata moja ambayo imetengwa kwa ajili ya Katiba Mpya.

Kwa maneno mengine, Mheshimiwa Spika, mchakato wa Katiba Mpya, ambayo Mheshimiwa Waziri anataka tuamini kwamba haujauawa na Serikali ya Awamu ya Tano, haujatengewa hata senti moja katika bajeti inayopendekezwa kwa Bunge lako tukufu mwaka huu. Na huu ni mwendelezo wa bajeti ya mwaka jana ambayo nayo haikutenga hata senti moja kwa ajili ya mchakato wa Katiba Mpya.

Mheshimiwa Spika,

Katika Maoni yangu juu ya bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka 2015/2016, nilielezea kwa kirefu jinsi ambavyo 'Katiba Mpya imekwama.' Tarehe 26 Aprili, 2014, yaani *The Golden Jubilee* ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, ambayo Rais Jakaya Kikwete aliwaahidi wa Tanzania kuwa ndiyo tarehe ya nchi yetu kuwa na Katiba Mpya, ilifika na ikapita bila ya nchi yetu kuwa na Katiba Mpya.

Tarehe 30 Aprili, 2015, ambayo Rais Kikwete aliwaahidi wananchi kuwa ndiyo ingekuwa siku ya kufanyika kwa kura ya maoni kuhusu Katiba Inayopendekezwa - ahadi ambayo ilirudiwa rudiwa na kila kiongozi wa CCM na Serikali yake ndani na nje ya Bunge hili tukufu – ilifika na kupita bila kura ya maoni kufanyika.

Baada ya hapo, na kwa kipindi kilichobakia cha utawala wa Rais Kikwete, viongozi wa CCM na Serikali waliendelea kusisitiza, ijapo kwa sauti za kinyonge, kwamba kura hiyo ya maoni ingefanyika katika tarehe ambayo, hata hivyo,

hawakuwa tayari kuitaja tena. Haikufanyika hadi wakati Rais Kikwete anaondoka madarakani na Rais Magufuli anaingia madarakani. Ndio maana nilisema, katika Maoni yangu ya mwaka juzi, kwamba

(Maneno ya mwisho ya aya hapo juu yalifutwa na Bunge)

Mheshimiwa Spika,

Rais John Pombe Magufuli ameshatangaza hadharani kwamba Katiba Mpya sio kipaumbele cha Serikali yake. Rais amedai kwamba wakati wa kampeni za Uchaguzi Mkuu wa 2015, ye ye hakutoa ahadi yoyote kwa waTanzania kwamba atawaleta Katiba Mpya akichaguliwa kuwa Rais. Kwa hiyo, kwa msimamo huo wa Rais Magufuli, mchakato wa Katiba Mpya ambao, hadi ulipoishia kwa kupitishwa kwa Katiba Inayopendekezwa, ulikwisha kugharimu jumla ya shilingi billioni 121.463, umekwishakufa na kuzikwa.

Mheshimiwa Prof. Kabudi ni mtu mwelewa sana wa siasa za kikatiba za Tanzania. Kwa uelewa wake mkubwa wa masuala haya, Prof. Kabudi anafahamu vema kivuli kirefu cha 'Urais wa Kifalme', ambayo ndiyo imekuwa '*the organizing principle*' ya katiba na siasa za Tanzania tangu mwaka 1962 ilipotungwa Katiba ya Jamhuri. Kwa uelewa wake huo, Mheshimiwa Prof. Kabudi anafahamu, au anatakiwa kufahamu, kwamba, kwa Katiba na Sheria za Tanzania, na kwa mila na desturi zake za kislasa na kikatiba, Rais akishasema hawezi kubishiwa na Waziri wake. Ni suala la – kama wasemavyo Wakatoliki - *Roma locuta, causa finita*, yaani Roma ikishasema, ndio mwisho wa mashauri!

Kwa sababu hiyo, Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako tukufu inataka kujua kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, Serikali ya Awamu ya Tano inatambuaje umuhimu wa nchi yetu kuwa na Katiba Mpya wakati Rais Magufuli amekwishesema Katiba Mpya sio kipaumbele cha Serikali yake? Na, je, kama kweli Serikali hii ina mpango wa kuuendeleza mchakato wa Katiba Mpya kutoka pale ulipoishia, ni kwa nini Serikali hii hajatenga hata senti moja kwenye bajeti hii kwa ajili ya jambo hili muhimu?

Bila majibu ya kweli kwa maswali haya, Waziri Kabudi atakuwa ameangukia kwenye shimo lile lile walimoangukia watangulizi wake wanne: kushindwa kutekeleza matakwa na matarajio ya waTanzania ya kupata Katiba Mpya na ya kidemokrasia itakayokidhi mahitaji ya kizazi hiki na vizazi vijavyo. Na sio ajabu, maisha yake kama Waziri wa Mambo ya Katiba na Sheria, yakawa mafupi kama ilivyokuwa kwa watangulizi wake.

A HAKI ZA BINADAMU

Mheshimiwa Spika,

Katika Taarifa yake kwa Kamati, Mheshimiwa Prof. Kabudi alidai kwamba *"Wizara iliendelea kuimarisha na kusimamia uzingatiwaji wa misingi ya haki za binadamu kama ilivyoainishwa na kuhifadhiwa katika Katiba na sheria za nchi...."* Madai haya hayaelezi hali halisi ya haki za binadamu katika nchi yetu. Ukweli ni kwamba kauli ya Mheshimiwa Prof. Kabudi inapotosha ukweli juu ya haki za binadamu katika nchi yetu.

*(Aya zinazofuata baada ya aya ya hapo juu
zilifutwa na Bunge)*

UENDESHAJI WA MASHTAKA YA JINAI

Mheshimiwa Spika,

Mamlaka ya uendeshaji wa mashtaka ya jinai imekasimiwa kwa Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwa mujibu wa ibara ya 59B(2) ya Katiba. Aidha, kwa mujibu wa ibara ya 59B(4), katika kutekeleza mamlaka yake, "Mkurugenzi wa Mashtaka atakuwa huru, hataingiliwa na mtu ye yeyote au na mamlaka ye yeyote na atazingatia ... nia ya kutenda haki, kuzuia matumizi mabaya ya taratibu za utoaji haki na maslahi ya umma." Kanuni hii kuu imetamkwa pia na kifungu cha 8 cha *Sheria ya Utumishi wa Mashtaka ya Taifa, Na. 27 ya 2008 (National Prosecutions Service Act, 2008)* ambayo pia imefafanua na kutilia nguvu mamlaka haya ya kikatiba.

Kwa mujibu wa Sheria hii, Mkurugenzi wa Mashtaka ana mamlaka sio tu ya kudhibiti mashtaka yote ya jinai bali pia kuratibu shughuli za upelelezi wa makosa ya jinai [kifungu cha 16(1)]. Aidha, kwa mujibu wa kifungu cha 17(1) na (3), Mkurugenzi ana uwezo wa kutoa maelekezo ya maandishi kwa ofisa ye yeyote wa umma ili apatiwe taarifa yoyote inayohusu upelelezi au uendeshaji wa mashtaka ya jinai na ofisa huyo anatakiwa kutii maelekezo hayo.

Mheshimiwa Spika,

Ili kumwezesha Mkurugenzi wa Mashtaka kutekeleza wajibu wake wa kikatiba kwa uhuru kamili na bila woga au upendeleo, Mkurugenzi wa Mashtaka amewekewa kinga ya ajira yake. Kwa mujibu wa kifungu cha 19(1) na (2) cha *Sheria ya Utumishi wa Mashtaka ya Taifa*, sifa, masharti na mafao ya ajira ya Mkurugenzi wa Mashtaka yatakuwa sawa _ay a_e ya ajira ya Jaji wa Mahakama Kuu.

Aidha, kwa mujibu wa kifungu cha 19(3), Mkurugenzi wa Mashtaka hawezi kuondolewa kwenye madaraka yake isipokuwa kwa kushindwa kutimiza wajibu wake kwa sababu ya ugonjwa au kwa kukiuka Kanuni za Maadili ya Kitaaluma ya Maafisa wa Sheria, Mawakili wa Serikali na Wanasheria Walioko kwenye Utumishi wa Umma chini ya *Sheria ya Utekelezaji wa Mamlaka ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Sura ya 268 ya Sheria za Tanzania*.

Hii ndio kusema kwamba, kwa mujibu wa Sheria Na. 27 ya 2008, utaratibu wa kumwondoaa Mkurugenzi wa Mashtaka kwenye ajira yake hauna tofauti na utaratibu wa kumwondoaa Jaji wa Mahakama Kuu kwenye ajira yake.

Mheshimiwa Spika,

Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaamini kwamba utaratibu huu wa kikatiba na kisheria umempa Mkurugenzi wa Mashtaka nyenzo za kutosha kisheria za kupambana na uhalifu mkubwa hapa nchini na vile vile kuzuia matumizi mabaya ya mfumo wa uendeshaji na utoaji haki na hasa hasa ya mfumo wa mashtaka ya jinai. Licha ya kuwa na mamlaka na kinga hizi za kisheria, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka imeshindwa kutekeleza wajibu wake ipasavyo.

Hii inathibitishwa na kitendo cha kutowachukulia hatua za kijinai Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam Paul Makonda alias David Bashite kwa vitendo nya kijinai alivyofanya katika uvamizi wake wa Clouds Media Group. Inathibitishwa pia na kitendo cha kushindwa kuwachukulia wale wote waliteka wa Tanzania na kuwatesa kama ambavyo tumeelezea humu kwa kirefu; na wale waliomtishia Mheshimiwa Nape Nnauye silaha hadharani mbele ya waandishi habari. Na hii inathibitishwa na kushindwa kwake kuchukua hatua za kijinai dhidi ya wale wote waliokula njama za kumfungulia mashtaka ya uongo na kumfunga Mheshimiwa Lijualikali.

Mheshimiwa Spika,

Katika mazingira haya, Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako tukufu inataka Mheshimiwa Waziri alieleze Bunge lako tukufu, kama bado Mkurugenzi wa Mashtaka anastahili kuendelea kushikilia nafasi hiyo muhimu wakati ni wazi hana uwezo wala nia ya kutekeleza majukumu yake ya kikatiba na kisheria.

YA KAIMU JAJI MKUU

Mheshimiwa Spika,

Mahakama ya Tanzania haina kiongozi wake kamili, yaani Jaji Mkuu. Hii ni kwa sababu, tangu Jaji Mkuu Mohamed Chande Othman astaafu tarehe Mosi Januari ya mwaka huu, Rais John Pombe Magufuli hajateua Jaji Mkuu mpya kuchukua nafasi iliyoachwa wazi na Jaji Mkuu Chande Othman. Badala yake, Rais Magufuli amemteua Jaji wa Rufaa Prof. Ibrahim Hamisi Juma kuwa Kaimu Jaji Mkuu.

Mheshimiwa Spika,

Ibara ya 118(4) ya Katiba yetu, Rais anaruhusiwa kuteua Kaimu JAji Mkuu iwapo itatokea kiti cha Jaji Mkuu kitakuwa wazi; au Jaji Mkuu hayupo Tanzania; na au Jaji Mkuu atashindwa kutekeleza kazi yake kwa sababu yoyote, na Rais ataona kuwa kwa muda wa tukio lolote kati ya hayo matatu inafaa kumteua Kaimu Jaji Mkuu. Kaimu Jaji Mkuu aliyeulewa kwa

utaratibu huu "... atatekeleza kazi za Jaji Mkuu mpaka atakapoteuliwa Jaji Mkuu mwingine...."³

Mheshimiwa Spika,

Pamoja na kuwapo kwa ibara ya 118(4), Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako tukufu inaanini kwamba Rais Magufuli anavunja Katiba ya nchi yetu kwa kushindwa kuteua Jaji Mkuu kamili takroban miezi mitano tangu kustaafu kwa Jaji Mkuu Chande Othman. Hii ni kwa sababu, ibara ya 118(4) haikutungwa kwa lengo la kumwezesha Rais kuteua Kaimu Jaji Mkuu bila kikomo cha muda.

Kama ilivyo kwa sheria zote, ibara ya 118(4) ina sababu yake maalum. Ibara hiyo imewekwa kwa makusudi ya kuhakikisha kwamba kwa muda wote kunakuwa na kiongozi wa Mahakama ya Rufani ya Tanzania pamoja na kiongozi wa Mahakama ya Tanzania, wakati Jaji Mkuu kamili anasubiriwa kuteuliwa. Kaimu Jaji Mkuu ni sawa ni kile kinachoitwa na wanasheria 'interlocutory position.' Kaimu Jaji Mkuu ni nafasi ya muda inayoshikiliwa na mtu mwenye sifa za kuwa Jaji Mkuu kabla nafasi hiyo hajijazwa na Jaji Mkuu kamili.

Swali halali linahitaji majibu ni, je, Kaimu Jaji Mkuu anastahili kuwapo madarakani kwa muda gani? Hili ni suala la tafsiri ya Katiba linalohitaji kujibowi na Mahakama. Kwa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, miezi mitano ni muda mrefu mno wa kuwa na Kaimu Jaji Mkuu. Hii ni kwa sababu, katika historia yetu yote tangu uhuru, hajjawahi kutokea Rais wa nchi yetu akashindwa kuteua Jaji Mkuu kamili kujaza nafasi iliyo wazi ya Jaji Mkuu.

Mheshimiwa Spika,

Bunge lako tukufu, kama mmojawapo wa mihimili mikuu ya dola ya Tanzania, lina kiongozi wake mkuu muda wote: Spika au Naibu Spika. Serikali, kama mhimili mwingine mkuu, ina kiongozi wake mkuu muda wote: Rais au Makamu wa Rais. Kwa Mahakama ya Tanzania, mhimili mkuu wa tatu wa dola ya Tanzania, kutokuwa na kiongozi wake kamili miezi mitano baada ya kustaafu kwa Jaji Mkuu Chande Othman, kunatoa

³Ibara ya 118(5) ya Katiba

taswira potofu kwamba Mahakama ina hadhi hafifu au ya chini ikilinganishwa na mihimili mingine mikuu ya dola ya Tanzania.

Kitendo hiki vile vile kinatoa taswira potofu kwamba pengine Kaimu Jaji Mkuu wa sasa hatoshelezi nafasi hiyo; au kwamba mionganoni mwa Majaji wote wa Rufaa au wa Mahakama Kuu ya Tanzania au mawakili na wanasheria wengine wa nchi hii pamoa na wale wa nchi za Jumuia ya Madola hakuna hata mmoja wao mwenye uwezo au sifa za kuwa Jaji Mkuu wa Tanzania.

Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako tukufu inamtaka Mheshimiwa Waziri amshauri Rais Magufuli, kwa heshima zote anazostahili, amthibitishe Kaimu Jaji Mkuu Prof. Juma katika nafasi hiyo au, vinginevyo, atuee mwanasheria mwengine anayemwona ana sifa za kuwa Jaji Mkuu kamili wa Tanzania. Hali ilivyo hivi sasa inawatia aibu wanasheria wote wa Tanzania na inaitia aibu nchi yetu katika jumuia ya kimataifa.

Mheshimiwa Spika,

Naomba nimalizie maoni yangu haya kwa kusema yafuatayo. Watanzania hawastahili Serikali ya aina hii. Kama alivyosema Baba wa Taifa katika kitabu chake *Uongozi Wetu na Hatima ya Tanzania*: " *Hatulazimiki kuendelea na uongozi mbovu wa Chama na Serikali. Wala tukiendelea na hali hii, bila kubadili uongozi wa Chama na Serikali, sina hakika kama tutafika huko salama. Masuala muhimu ya nchi yetu hayatashughulikiwa.... Na masuala mengine muhimu ... yataachwa yajitatu yenye. Nasema katika hali kama hiyo sina hakika kama tutafika salama; na tukifika salama tukiwa na uongozi huu huu wa Chama na Serikali mbele kutakuwa ni giza tupu. Majuto ni mjukuu, huja baadaye.*"

Tundu Antiphas Mughwai Lissu
MSEMAJI & WAZIRI KIVULI, SHERIA NA KATIBA
KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI
25/04/17

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

MWENYEKITI: Sasa baada ya kusema hayo, nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni.

(Saa 7.24 Mchana Bunge lilitishwa hadi saa 11.00 Jioni)

(Saa 11.00 Jioni Bunge lilitrudia)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge, ili kuweka mambo sawa kwa madhumuni ya kumbukumbu za kudumu za Bunge letu. Nilitoa uamuzi kwamba katika hotuba iliyotolewa na Kambi ya Upinzani maeneo yote ambayo mapema wakati wa hotuba ya Waziri Mkuu yalikuwa yameondolewa na yamerudiwa tena katika hotuba hii yasiwepo. Kwa kuwa hata mwasilishaji wa taarifa ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni wakati anahitimisha hoja yake hakusema kwamba hotuba yake yote iingie kwenye *Hansard*, maelekezo yangu ni kwamba maeneo yote ambayo yana ukakasi ambayo yanatokana na uamuzi huo hayataingia kwenye *Hansard* pamoja na yale alioanza nayo ya utangulizi ambayo nilisema moja kwa moja hayataingia. *(Makof)*

Baada ya kusema hayo, sasa tuendelee na hatua muhimu ya ninyi kuijadili hoja hii. Naombeni tuongee kwa staha tu, unafahamu ninyi kama viongozi wa nchi hii, unawenza ukajenga hoja yako ujumbe ukafika kwa lugha ya staha tu bila hata kumtukana mtu au kufanya nini. Hilo ndilo ombi langu kwenu Wabunge. Nashukuru sana.

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuomba mwongozo wako na kwa lugha hizohizo za staha na za utaratibu sana ndiyo najielekeza huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikumbukwe kwamba leo wakati wa mchana hapa Mbunge alitoa hoja juu ya suala zima la kumchangia mrembo ambaye atatuwakilisha katika

shughuli huko anakokwenda. Hata hivyo, ikumbukwe kwamba Wabunge wengi kabla ya kutuhoji tulioonesha hisia zetu tena kali kwamba sisi hatutaki tukatwe fedha hizi. Tumekwenda katika maelezo mbalimbali ya kukisihi Kiti, kukipembejea Kiti, kukiomba Kiti kwa lugha za staha sana, kwa wingi wa upande mwininge Kiti kikasema jambo hili limepita fedha hizi zitakatwa. (*Makofij*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako kama mtu jambo hili limeingia ndani ya imani yake na halitaki na hasa kipindi hiki ambacho hata Mheshimiwa Khatib alisema kwa nini tulazimishwe? Naomba mwongozo wako, hatupendi tuvutane katika mambo mengine maana tukienda hivi itakuwa hatufiki tunakokwenda. Wewe mwenyewe umesema hapa tutumie lugha nzuri, lugha za staha, lugha za kufahamiana kwa hili tutakuwa hatufahamiani lazima nikwambie kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako jambo hili uliondoe kabisa mtu kuchangia iwe ni hiari. Naomba Mwongozo wako wa ziada. (*Makofij*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Masoud wewe ni mzoefu wa Kanuni, Bunge limehojiwa likaamua. Mimi naomba tuheshimu uamuzi huo.

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)

MWENYEKITI: Mnisikilize basi, mnisikilize kwanza.

WABUNGE FULANI: Sawa.

MWENYEKITI: Kwamba uamuzi wa Bunge wa wengi utabaki kama ulivyo. Mbunge mmojammoja kwa vile tunajua utaratibu unaofuata baada ya hapo uende ukamuone Katibu wa Bunge ukaelezee ya kwako maana tusiingize humu suala la imani ya dini kwa suala ambalo tunajua tukifika huko tutaanza kutoka kila mmoja na njia yake humu. Kwa hiyo, nasema uamuzi unabaki palepale

lakini kama unadhani kwamba ni hiari ya moyo pamoja na uamuzi huo basi wewe fika kwa Ofisi ya Katibu wa Bunge ukaelezee tatizo ulilonalo. Huo ndiyo uamuzi wangu. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge, uwiano wa wachangiaji wote mnaujua kwa kambi na majina yako hapa, tusingiziane muda wenyewe ndiyo huo. Naanza na hawa wawili ambao wamekubaliana kugawana dakika zao tanotano, maana nafasi zilizopo hapa ni CHADEMA Mbunge mmoja, CUF Mbunge mmoja, CCM Wabunge wanne, ndiyo uwiano huu kwa mjadala huu. Kwa hiyo, nasema hawa ambao wamegawana dakika zao kumi naanza nao nimalizane nao. Mheshimiwa Sabreena, dakika tano atafuatiwa na Mheshimiwa Kubenea dakika tano.

MHE. SABREENA H. SUNGURA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa dakika chache nilizopata, lakini namwomba Mwenyezi Mungu niweze kuzitendea vyema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu napenda kujielekeza kwenye suala zima la usafirishaji wa binadamu ambao ni Watanzania kwenda nchi za nje kufanya kazi na wengi wao wamekuwa wakiuawa na *clips* zinatumwa hapa nchini, zinazagaal kwenye mitandao ya kijamii, sisi kama Wabunge tunaona, Serikali imekaa kimya haisemi jambo lolote. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hii ni hatari kwa sababu hawa wanaofanya biashara hii ya kusafirisha binadamu kwa maana ya *human trafficking* na kuwapeleka huko wanakwenda kuuawa kinyama, kwa nini Serikali haifanyi msako maalum wa kuhakikisha inawakamata? Vijana wetu tena vijana wa kike wanakwenda huko wanafanyiwa unyama lakini Serikali imekaa kimya. Tunataka tamko leo litoke, ni hatua gani zimechukuliwa kubainisha watu wanaosafirisha wasichana wa Kitanzania bila ridhaa ama kwa ridhaa lakini kwa udanganyifu. Wanakwenda kwa wazazi wanawahonga dola 200, 300 wanawaambia kijana

wako anakwenda huko atafanya kazi nzuri *supermarket*, wapi, akifika kule anadhalilika anauawa, Serikali inasemaji juu ya hili? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo napenda kulizungumzia ni *conflict of laws*. Nchi yetu ina tabaka za watu mbalimbali, kuna mila na desturi mbalimbali. Sheria zetu zimeingia kwenye mgongano, tuna Sheria ya Mirathi lakini pia tuna Sheria ya Ndoa, tunayo *Islamic Restatement Act* lakini pia tunayo Sheria ya Kimila ambayo ni *Customary Declaration Order* ya mwaka 1963.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi sheria zinakinzana, kuna sheria ambayo inamtambua mtoto ni kuanzia umri wa miaka 21 lakini kuna sheria inayosema mtoto mwisho wake itakuwa ni miaka 18, lakini kuna sheria za Kiislamu zinazosema mtoto mwisho wake ni pale anapobalehe. Sasa linapokuja suala la mtoto aolewe ama aozeshwe kwenye umri gani ama aoe kwenye umri gani kuna mwingiliano wa mila, desturi, dini na sheria. Je, mambo haya tunakwenda nayo vipi? Ni lazima mijadala ya kina ifanyike ili kuhakikisha kwamba pande zote zinabaki bila dukuduku. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi siungi mkono ndoa za utotoni, naunga mkono wanaopendekeza watoto waolewe kuanzia umri wa miaka 18. Hata hivyo, kuna watoto ambao na wenye wanaingia kwenye mapenzi kabla ya umri suala ambalo linapelekea ubebaji wa mimba. Sasa mtoto yule alivyopata mimba kwenye umri wa miaka 13, 14 ni mzazi gani atakayekubali kuona mtoto wake mwenye umri huo mdogo anakaa nyumbani na anazalishwa, hapohapo sheria zetu haziwaruhusu watoto hao kuendelea na shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tukubaliane, kama tutaaamua mtoto aanzie umri wa miaka 18 aweze kuo na kuolewa, je, mtoto anayepata ujauzito kabla ya miaka hiyo *status yake* itakuwaje? Kama tutakubaliana miaka 18 basi kuwe kuna *exception*, kama atapewa ujauzito kabla ya hapo aruhusiwe kuozeshwa kwa sababu kuna watu ambao mila zao kukaa na binti nyumbani mama yake mzazi

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

anapata ujauzito na mtoto anapata ujauzito ni matusi. Naomba hili lifanyiwe kazi kwa namna ya kipekee. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kuzungumzia suala moja, tunayo Sheria ya *Probate and Administration of Estate Act* ya Tanzania ambayo inaunda *Waqt Commission*. Wenzetu wa Zanzibar tayari wana *Waqt Commission* na watu ambao wanataka mali zao zigawanywe kwa mtindo huo wanakwenda kwenye *Waqt Commission* wanapeleka mapendekezo yao na yanafanyiwa kazi. Kwa upande wetu wa Tanzania Bara tume hii ipo kwenye sheria lakini haijawahi kuundwa toka uhuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka majibu kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, ni lini Serikali itaunda *Waqt Commission* kwa upande wa Tanzania Bara ili wale ambao wanajisikia kupeleka mali zao pale ambazo zitakuja kusaldla vizazi vinyavyokuja basi waweze kuzingatiwa na waweze kufanya hivyo kwa mujibu wa sheria. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, umuhimu wa hili ni nini? BAKWATA imekuwa na malalamiko mengi sana, watu wengi hapa nchini hawana imani na BAKWATA hususan Waislam wengi hawana imani na BAKWATA. BAKWATA wanauza mali za Waislam, BAKWATA wanaingia kwenye migogoro wamewauzia akina Yussuf Manji mali za Waislam, kesi, vita, ngumi kila siku. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini sasa msitengeneze hii *Waqt Commission* ambayo itatoa sasa mali hizi ambazo zinawekwa kwenye mikono ya watu ambao kwa kiasi fulani hawaaminiki ziweze kuwa kwenye mfumo wa Serikali ili...

TAARIFA

MHE. ALHAJ ABDALLAH M. BULEMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Sabreena, taarifa, kaa kidogo. Taarifa Mheshimiwa Alhaji Bulembo.

MHE. ALHAJ ABDALLAH M. BULEMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa, msemaji anasema Waislam hawana imani na BAKWATA ana ushahidi gani? Ni Waislam wapi, ni Msikiti gani, tunaomba ushahidi uwepo Mezani. BAKWATA ni taasisi iliyosajiliwa, BAKWATA ni taasisi ambayo ina Waislam wanaoamini, naomba aweke ushahidi Mezani asigonganishe dini kwa imani yake yeye. (*Makofii*)

MBUNGE FULANI: Kweli.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Sabreena taarifa hiyo umepewa.

MHE. SABREENA H. SUNGURA: Mheshimiwa Mwenyekiti, namsikitikia sana Mbunge mwenzangu aliyesimama, kama ni Mtanzania ambaye anafuatilia vyombo vya habari na anafuatilia habari za kila siku katika nchi hii hawezi kuhoji BAKWATA kwamba haikubaliki na kundi kubwa la Waislam Tanzania. Kwa hiyo, hilo ni jibu ambalo linamtosha kama halijatosha aje nitampa *research* na mifano ya kesi ambazo BAKWATA wameuza mali za Waislam, kitu ambacho kinapelekea vita nchi hii. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Unaikubali au unaikata?

MHE. SABREENA H. SUNGURA: Kwa hiyo, napendekeza kabisa kwamba *Waqt Commission* iundwe kama ilivyo Zanzibar ili hawa waporaji ambao wamejificha kwa mgongo wa BAKWATA suala hilo liweze kwisha na lipatiwe muafaka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kugusia suala zima la migogoro ya kazi katika chombo chetu cha *Commission of Mediation and Arbitration*. Chombo kile tumekianzisha ili kiweze kupunguza mrundikano wa kesi za *labour* hususan katika mahakama zetu kuu. Hata hivyo, nasikitika kusema kwamba, majengo yake hayatoshi ku-*accommodate* wateja wanaokwenda pale. Ukienda pale unakuta makundi ya watu yamekaa kwenye vyumba vidogovidogo, kelele, hata wale wanaosikiliza mashauri

hawawezi kuelewana, joto, giza, mrundikano wa watu, mpaka watu wengine wanafanya kupangiwa ...

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Kubenea.

MHE. SAED A. KUBNEA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nakushukuru kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa wakati anazungumza Bungeni akijibu swalil la Kiongozi wa Upinzani, alisema Serikali yetu hii tuiamini sana ifanye uchunguzi wa mambo haya ya utekaji na utesaji na sisi humu ndani ukiulliza nani haiamini hii Serikali hayupo atakayetokea. Kwa sababu Serikali hii ni yetu sote ndiyo maana tuko hapa tunaisimamia Serikali, tuko hapa tunaishauri Serikali, lakini Serikali inayotaka kuaminika ni lazima iwe wazi. Hivi kwa mfano mtu aliyetaka kumpiga risasi Mheshimiwa Nape hajulikani, Serikali haimjui, kama inamjua basi ijitenge naye, kama haimjui iseme, lakini tunavyojuua Serikali inamjua. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna makosa ya kijinai yametendwa katika nchi hii na watendaji wa Serikali. Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam ameingia kwenye chumba cha habari akitumia silaha, kwa mujibu wa sheria zilizopo ule ni unyang'anyi, wizi wa nguvu. Amekwenda kupora CD za chumba cha habari...

MBUNGE FULANI: Una ushahidi?

MBUNGE FULANI: Ndiyo.

MHE. SAED A. KUBNEA: Kamera zimeonesha, Tume ya Mheshimiwa Nape Nnauye imeripoti. Ripoti ya Tume ya Mheshimiwa Nnauye imeundwa na waandishi wa habari na imekuwa *submitted* kwa Mheshimiwa Waziri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu anayetenda jinai, *DPP* yuko pale, moja ya majukumu yake ni kuendesha kesi za jinai mahakamani, lakini pia kuangalia ni nani anayetenda jinai kuagiza *DC/wafanye uchunguzi*, hiyo ndiyo kazi ya *DPP*. Sasa *DPP* yupo amenyamaza, polisi wapo wamenyamaza. Mtu anatumia jina ambalo sio lake, ametenda makosa mengine yenye adhabu ya zaidi ya miaka 30 gerezani. Watu wamekwenda mpaka Kolomije, wamekwenda nyumbani kwao kijijini kwake wamezungumza na mama yake, vyombo vya habari vimefika huko, Waziri Mkuu anasema tuiamini Serikali, tunaiamini kweli lakini Serikali lazima iwe wazi iache *double standards. (Makof)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna watumishi wa umma kwenye nchi hii wamefukuzwa kazi wengine wameshtakiwa wamefungwa lakini mtu mmoja anaitwa Paul Makonda jina lake Daudi Bashite anaachwa kwa sababu gani, *who is Makonda?* Mtu anaingia kwenye chumba cha habari akiwa na silaha za moto na polisi, *who is Makonda?* Halafu Serikali inasema iaminike, waandishi wa habari wanafanya kazi kwenye mazingira magumu halafu Waziri wa Habari ananyamaza, inasikitisha. Waziri wa Habari ananyamaza, ameona waandishi wa habari wananyanyasika kwenye nchi hii anatetea uhalifu halafu anasema tuamini Serikali, tunaaminije? *(Makof)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna makosa zaidi ya nane wanasheria wanasema. Rais wa Chama cha Wanasheria yuko humu ndani, *TLS* haichukui hatua dhidi ya Makonda, Tume ya Haki za Binadamu haichukui hatua dhidi ya Makonda halafu mnasema Serikali tuiamini. Bunge limenyamaza linapigwa pini, linapigwa kufuli lisimzungumzie Makonda, jamani, halafu mnasema tuamini Serikali, Serikali inaaminikaje ikiwa imejifunika kwenye blanketi. Kutoa silaha hadharani ni kosa la jinai. Leo Kamishna Siro amesema ni kosa la jinai, Mheshimiwa Nape ametolewa silaha hadharani. Juzi watu wametoa silaha hadharani, aliyetoa silaha Mheshimiwa Nape anamjua, dunia inamjua, vyombo vya habari vinamjua, waandishi wa habari ndio waliozuia... *(Makof)*

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante.

MHE. SAED A. KUBNEA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Kambi ya Upinzani, nashukuru sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Tunaendelea na msemaji wetu wa Chama cha Wananchi *CUF*, ni Mheshimiwa Riziki Shahari Mngwali.

MHE. RIZIKI S. MNGWALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, Muumba wa mbingu na ardhi ambaye kwa matakwa yake mwenyewe ametuchagua sisi kuwa mionganii mwa waja wake ambao amewatunuku uhai na uzima na akili timamu na akawajalia pia kufanya kile ambacho wamejipangia wenyewe kukifanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa imani ya dini yangu, katika mambo ambayo tunaambiwa tuyafanye kwa wingi sana ni kukumbushana kwa sababu katika kukumbusha hutoa msaada kwa wale wenye kuamini. Nami nalifanya hilo nikiamini kabisa kwa dhati ya moyo wangu kwamba nyumba hii imejaa wenye kuamini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kitabu ambacho kwa dini yangu nikiamini, Kitabu cha *Quran*, kuna aya ya 54 iko katika Sura ya 36 na sura hii kwa jina lake mahsusii inaitwa "Surat Yaseen" na kwa hadhi yake hii sura ndiyo inaitwa ndiyo moyo wa *Quran*. Katika hiyo aya ya 54 inasema:-

"langalieni ile siku ya hukumu ambapo haitadhulumiwa nafsi chochote na wala haitolipwa isipokuwa yale ambayo imeyatenda". (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niliseme hili kama tahadhari kwetu sisi sote, iko siku ambayo hakuna chochote

ambacho tutaulizwa isipokuwa kile ambacho tumekitenda hapa. Kwa imani ya dini yangu, maisha ya kila siku, mahusiano yetu, kusoma kwetu, kuwa Wabunge kwetu yote haya yataulizwa siku hiyo na hayo ndiyo katika hayo ambayo tunayatenda. Kwa hiyo, naomba nitoe hiyo tahadhari na nimwombe Mwenyezi Mungu ashuhudie kwamba nimewakumbusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kuchangia kwa kusema kwamba naunga mkono hoja hotuba hii ya Waziri Kivuli wa Kambi ya Upinzani lakini pia mengi yaliyomo kwenye taarifa ya Kamati ya Katiba na Sheria hususani yale ambayo yameelezwa ukurasa wa 18 na 19 kuhusu msisitizo wa kuangalia masuala mazima ya haki za binadamu hasa yakiendana na namna ambavyo vyombo vya kutoa sheria ikiwemo Mahakama vinavyotakiwa vitende haki. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sitaki kuhoji Mahakama zinafanyaje kazi lakini nataka kuhoji sera za nchi hii, sheria na taratibu kuhusu masuala ya haki za binadamu. Mheshimiwa Waziri amesema hili na Kamati imesema na Waziri Kivuli amesema namna gani kesi zinacheleweshwa, namna gani mahabusu na wafungwa wanateseka katika nchi hii lakini tumenyamaza kimya au hatuchukui hatua inavyostahiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Mashekhe ambao wanaoza mahabusu kwa miaka minne sasa ambapo suala lao linapigwa danadana hilo sijui kama siyo suala la haki za binadamu au siyo katika zile kesi ambazo taarifa zote hizi zimesema lazima masuala ya upelelezi yakamilishwe katika wakati ambao ni *reasonable*. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana Mheshimiwa Waziri huyu ambaye yuko leo na hoja yake Mezani lakini jana alikuwa anatupa utaalam kama Profesa wa Sheria, alipokuwa anazungumzia Sheria ya Ndoa alisema kwamba, kuna kitu kinaitwa *legal anthropology*. Ombi langu ni kwamba hii *legal anthropology* sipati maneno sahihi lakini ninachotaka

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

kusema ni kwamba isiangalie tu masuala ya *abstract*, zile *values* ambazo huzioni, lakini pia iangalie masuala ambayo ni *real and tangible*, yale unayoyaona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili, inapokuja suala la dini, viongozi ni katika *values* hizo. Sasa tunapoona viongozi wetu wa dini wanadhalilika, wananyanyasika kwa miaka nenda, rudi, mjue mnatukwaza kiimani na mnateteresha hivyo vitu ambavyo mnasema *legal anthropology* inaviangalia kwa umakini sana. Kaka yangu Mheshimiwa Profesa Kabudi utanisamehe huko mwishoni kama nitashika shilingi ya mshahara wako. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Profesa Kabudi kama ambavyo Waziri Kivuli amesema hapa kwenye ukurasa wa nne kwamba hakuna shaka yoyote kwamba Ripoti ya Tume ya Warioba na Rasimu ya Katiba Mpya ina alama za vidole vyta kitaalam vyta Profesa Kabudi, ni kweli. Ninachoongeza tu ni kwamba alikuwa ana wasaidizi wake kama *proof-readers* wake, wanawake wawili, mmoja napenda nimitaje Mheshimiwa Kibibi Mwinyi Hassan, mwingine kwa leo nahifadhi jina lake, walifanya kazi ile kwa kukesha, tukatoka na *document* zile na mimi nilibahatiika kuwa katika Tume ya Warioba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ripoti ile haikuzumngumzia tu pendekezo la Katiba Mpya lakini kuna masuala kadhaa ya kijamii, kisheria, kitaratibu ambayo Tume ya Warioba iliandaa kwa *volumes* na zikakabidhiwa Serikalini. Laiti mchakato ule ungefikishwa mwisho haya mambo yote hapa tunayozongwazongwa nayo sasa hivi yasingekuwepo. Taratibu zingekaa sawa, Katiba Mpya ingepatikana masuala yote haya tunayosema huyu asitajwe, huyu asifanywe hivi yalishajadiliwa na wananchi kwa kina kabisa mpaka suala la viroba na zile suruali ambazo vijana wetu wanavaa, wananchi walilisema. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kama tungeupeleka mchakato mpaka mwisho wake yale yote yasingekuwa *issues* sasa hivi, lakini imekuwa hivyo kwa sababu

suala la Katiba Mpya limekuwa kizungumkuti, sasa sijui nikisema limepigwa kaputi nalo nitaambiwa msamiati siyo, lakini ni katika lahaja tu na nadhani Waziri anayehusika na utamaduni alisimamie hili. Lugha yetu ya Taifa ni Kiswahili, tutumie utajiri wa lugha hii, tutumie lahaja ambazo zinaleta ladha masikioni, lugha ina ladha yake masikioni. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala hilo la Katiba Mpya masuala ya maadili ya kijamii, mila na desturi zetu, tunu hizi za Taifa ikiwemo lugha yetu, uongozi na mihimili hasa mihimili hii mitatu *versus* masuala ya vyama vyaya siasa yamefanyiwa kazi vizuri kabisa. Wananchi walisema hatutaki kumuona Spika ambaye ni *m-NEC*, hatutaki kumwona Rais ambaye ni Mwenyekiti wa Chama cha Siasa na walitaja kwa vitu *specific* lakini hatukulifanya kazi sasa hivi tunahangaishana hapa kila kinachosemwa kinaambiwa sicho, kila kinachoandikwa kinaambiwa kifutwe, lakini kile kisu cha jana kile kwa bahati mbaya kimebaki humu na kinaendelea kutesa watu, mimi sijui kisu gani. (*Makofii/ Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshuhudia humu asubuhi haki ya msingi kabisa ikitetereshwa ambayo ni haki ya kujieleza. Hivi Mbunge, Waziri Kivuli anapozongwazongwa, anapokatazwa kueleza kile ambacho yeye ana imani nacho inashangaza. Mimi nitashangaa sana ikiwa Mawaziri Vivuli wa Kambi hii watarudia yale hotuba za Mawaziri wa upande ule itakuwa kituko! Yule Waziri akisema tumefanya kila kitu na Waziri Kivuli naye aseme Serikali ile imefanya kila kitu, itakuwa kiini macho gani hicho? Hebu tupewe haki hii ambayo tunaizungumzia hapa, haki za binadamu, utawala wa sheria uachwe utekelezwe katika nchi hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kaka yangu Mheshimiwa Profesa Kabudi amevishwa viatu au sijui amevishwa kilemba hiki ambacho inabidi akifanyie kazi sawasawa. Namshauri asisite kushauri mamlaka husika kuhusu utawala wa sheria unavyotakiwa kufanya kazi kwa sababu sasa hivi tumefikishwa mahali ambapo hatujui twende kwa sheria au kwa matamko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria inasema, vyama vyaa siasa vipewe ruzuku vifanye kazi, vifanye shughuli za kisiasa ikiwemo mikutano ya hadhara. Matamko yanasema, hakuna kufanya kazi za siasa, hakuna mikutano ya hadhara mpaka tarehe fulani, kipi ni kipi? Hii haifai na haikubaliki katika nchi ambayo tunasema tunafuata utawala wa sheria, tuna demokrasia ya vyama vingi lakini zaidi tunasema kila siku tuombeane dua, tuombeane Mungu, hatuwezi ... (*Makofii*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea na wachangiaji wafuatao; Mheshimiwa Almas Athuman Maige atafuatiwa na Mheshimiwa Kiteto Zawadi Koshuma na Mheshimiwa Ester Michael Mmasi ajiandae.

MHE. ALMAS A. MAIGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa ya kuchangia Wizara hii ya Sheria na Katiba. Kabla ya kuanza kuchangia, naomba ku-*declare interest* kwamba mimi taaluma yangu ni ya ulinzi na usalama katika sekta binafsi lakini vilevile nina kampuni kubwa ya ulinzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipeleka kwa Katibu wa Bunge Muswada Binafsi kama ilivyo katika Kanuni yetu ya 81(1)(2) na (3), Toleo la 2016. Baada ya kupeleka Muswada wangu binafsi katika Ofisi ya Katibu wa Bunge alinijibu rasmi kwamba Muswada ule ulikuwa ni mzuri na Serikali iliuchukua Muswada huo kwa nia ya kuuleta tena Bungeni baada ya kutimiza kanuni za kuleta Muswada Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makampuni binafsi ya ulinzi yalianza mawili tu mwaka 1980 lakini leo yapo makampuni karibu 850, yameajiri askari walinzi wengi zaidi ya mara tano au mara sita ya Jeshi la Polisi. Makampuni haya yanafanya kazi nzuri sana ya kulinda raia na mali zao lakini hayana miongozo, kanuni, sheria na wala hayana mamlaka binafsi ya kuongoza makampuni haya kama ilivyo kule nje yalikotokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilifungua milango ya sekta ya ulinzi binafsi hapa nchini na ikafungia nje sheria za kuyaongoza makampuni haya. Suala hili limekuwa ni tatizo kwani makampuni haya yana silaha, yanavaa sare kama za jeshi, yanacheza gwaride, yanafuata kanuni za kijeshi na yameajiri wataalam kutoka nje ya nchi wenye taaluma kubwa ya kijeshi. Hatuwezi kuyazuia tena makampuni haya hapa nchini yasifanye kazi kwa sababu kila kwenye uwekezaji mkubwa makampuni haya yapo na yanafanya kazi nzuri sana, tunachoweza kufanya ni kuyadhibiti makampuni haya binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makampuni haya hayawezi kudhibitiwa bila sheria. Ni lazima Sheria inayoitwa *Private Security Industry Act or Bill* iletwe Bungeni ipitishwe. Huko yalikotokea makampuni haya kote, wenzetu Kenya, Uganda, Afrika Kusini, Uingereza, Marekani, Ulaya ziko sheria na mamlaka ya sekta ya ulinzi binafsi. Sheria ile niliyoleta mimi kama Muswada Binafsi ilizingatia kuanzishwa kwa mamlaka ya sekta binafsi ya ulinzi. Nia ile na sababu hiyo hajafutika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa, ajaribu kulieleza Bunge lako kama maslahi na madhumuni ya kuwepo sheria sasa yamefutika au mchakato wake umefikia wapi ili tujue tuweze kudhibiti makampuni haya ya ulinzi binafsi yaweze kulipa kodi na vilevile yanaajiri watu kinyume na kanuni. Kule kwenye Mahakama ya Kazi, robo tatu ya kesi zote ni za makampuni ya ulinzi, inakuwa kama ile Mahakama ya Kazi imeandalisha kwa sababu ya makampuni ya ulinzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile makampuni haya yanatumia sheria ya kiraia, Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini ya mwaka 2004. Sheria hii ni ya kiraia na imepigwa marufuku majeshini kote. Hairuhusiwi kutumika Polisi, JWTZ, Magereza wala *Immigration*. Sheria hii kutumika katika sekta ya ulinzi binafsi inaenda kinyume na inashindwa kuyadhibiti makampuni hayo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria hii inaruhusu migomo. Hebu tufikirie ikatokea siku makampuni ya ulinzi yamegoma au wafanyakazi wa kampuni za ulinzi wamegoma, wakaacha malindo wazi na wana silaha mikononi, itakuwaje? Naomba Waziri atakapokuja hapa aeleze Bunge lako hili amefika wapi na Sheria hiyo niliyoipendekeza ya Sekta ya Ulinzi Binafsi yaani *Private Security Industry Act or Bill* pamoja na pendekezo la kuanzishwa *Private Security Industry Authority*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo niende kwenye Idara ya Mahakama. Waziri wa Sheria hapa mwanzoni alisema kwamba wangependa kila Kata iwe na Mahakama. Kule kwetu Tabora Kaskazini (Uyui) kuna Mahakama ya Mwanzo ina kila kitu, Mahakama ipo, ina mabenchi, jengo zuri la Mahakama, nyumba nane za wafanyakazi wa Mahakama lakini imetelekezwa, huu ni mwaka wa 10 haifanyi kazi. Watu wameiba milango na madirisha yaliyojengwa kwa thamani kubwa na mpaka sasa sijui sababu ni nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu nimekuwa Mbunge, wananchi wananiuliza imetokea nini Mahakama ikatelekezwa na kuna kesi nyingi. Juzi juzi kumetokea kesi ya mauaji kule Tabora, Uyui ndiyo inaongoza kwa kesi mbaya za mauaji, wizi na kadhalika lakini Mahakama ya Mwanzo imefungwa. Nimeona katika hotuba yake Mheshimiwa Waziri anaongelea kujenga Mahakama za Mwanzo katika maeneo mbalimbali, lakini Mahakama ya Mwanzo katika Kata ya Upuge, Wilaya ya Uyui, Mkoa wa Tabora imesimama na haifanyi kazi na majengo yanabomolewa tu wananchi wanachukua kama shamba la bibi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba atakapokuja Mheshimiwa Waziri kuhitimisha hoja yake ya bajeti, anieleze kimetokea nini mpaka Mahakama ya Mwanzo inayotakiwa sana kutelekezwa. Pia anieleze majengo yale yafanyeweje sasa, maana watu wanaingia na kuiba milango kama haina mwenyewe. Mimi ningeshukuru Mahakama ile ingeanzishwa

tena kwa sababu kesi za kutosha zipo, lakini kama kuna sababu iliyofanya Mahakama ile ifungwe naomba nielezwe ili nikawaambie wananchi wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuniruhusu kwa heshima kubwa, nakushukuru sana na niwaachie wenzangu wachangie. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Maige Almas. Mheshimiwa Kiteto Zawadi Koshuma na Mheshimiwa Ester Michael Mmasi ajandae.

MHE. KITETO Z. KOSHUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Mnamo tarehe 5 Mei, 2016 nilisimama katika Bunge lako Tukufu kuwatetea watoto ambao wanaolewa wakiwa na umri chini ya mika 15. Nami naomba niahidi kwamba nitaendelea na ari hii hii ya kuwatetea watoto wa kike ambao wamekuwa wakipoteza ndoto zao wakiolewa katika umri mdogo sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na utangulizi huo, Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 inaonekana ni sheria ambayo inambagua mtoto wa kike ambapo katika kifungu kile cha 13 na 17, kinamtaka mtoto wa kike kuolewa akiwa na umri wa miaka 15 wakati mtoto wa kiume anaoa akiwa na umri wa miaka 18. Ukiangalia katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ibara ya 13 nitanukuu, inasema:-

"(1) Watu wote ni sawa mbele ya sheria na wanayo haki bila ya ubaguzi wowote kulindwa na kupata haki sawa mbele ya sheria".

(2) Ni marufuku kwa sheria yoyote iliyotungwa na mamlaka yoyote katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuweka sharti lolote ambalo lina ubaguzi wa dhahiri au kwa taathira yake."

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Sheria hii ya Ndoa ya mwaka 1971 utaona ni kwa namna gani inakinzana na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa

kumbagua mtoto wa kike ambaye anatakiwa kuolewa na umri wa miaka 15 ilihali mtoto wa kiume anatakiwa kuo akiwa na umri wa miaka 18 na kuendelea. Ni jukumu letu sasa sisi kama wanawake na wawakilishi wa watoto wa kike na wanawake wote Tanzania nzima lakini tukishirikiana na Waheshimiwa Wabunge wote bila kujali rika na kujali jinsia kuwatetea watoto wa kike ili na wao pia waweze kutimiza ndoto zao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaona madhara ya ndoa yakiwemo ya kiafya. Watoto wengi wa kike wanapokuwa wanaolewa na umri mdogo wa miaka 15, kiafya watoto hawa wanakuwa hawajapevuka katika maumbile yao na hivyo basi kitu hiki kinasababisha watoto hawa wanapopata ujauzito, hizo tunaziita ni mimba za utotoni kwa sababu zile ni mlimba ambazo bado yule mtoto hajapevuka maumbile yake na madhara makubwa ambayo yanatokea ni vifo vya akinamama. Naamini kabisa Serikali haitapenda kuona vifo vya wanawake vikiendelea kutokea ambavyo vinasababishwa na sheria hii ya ndoa za utotoni. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia madhara mengine ya ndoa za utotoni ni vifo vya watoto wachanga ambao wanazaliwa na akinamama ambao bado hawajapevuka. Kitu kingine, wasichana wanakosa elimu na kuna msemo unaosema kwamba unapompa elimu mtoto wa kike umesaidia jamii nzima, hili linaonekana wazi kabisa. Wapo Waheshimiwa sasa hivi humu ndani wakiamua watoe shuhuda zao kwa kweli kila mtu atastaajabu. Basi ni jukumu letu sisi Waheshimiwa Wabunge kuiomba au kuishawishi Serikali iweze kutusaidia kurekebisha Sheria hii ya Ndoa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na madhara ambayo yanawakuta wasichana, kwa sababu wasichana ndiyo waathirika wakubwa, wanapoolerwa na umri mdogo, kwa nini tunasema Sheria ya Ndoa ibadilishwe. Mchakato wa kuomba Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 ifanyiwe

marekebisho haukuanza leo. Hivyo naamini kwamba Bunge hili halitakuwa la kwanza kuishawishi Serikali kuleta mabadiliko ya Sheria ya Ndoa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchakato huu ulianza mwaka 1984 ambapo Umoja wa Wanawake Tanzania waliishauri Serikali kupitia Tume ya Kurekebisha Sheria kwamba Serikali irekebishe Sheria hii ya Ndoa kwa sababu walizunguka Tanzania nzima na wakaona kwamba watoto wengi wa kike wanapata hasara kubwa sana wanapoolerwa na umri mdogo. Kwa hiyo, utaona kwamba mchakato huu haukuanza leo ulianza siku nyingi sana mwaka 1984 wakati sheria imeundwa mwaka 1971, mchakato huu ulianza mapema sana. Wanawake Tanzania waliona ni kwa namna gani watoto wa kike wanaathirika katika kuolewa na umri mdogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchakato huu pia mwaka 1994 Tume ya Mabadiliko ya Sheria baada ya kupokea maoni mbalimbali kutoka kwenye *NGO's* mbalimbali walileta pia mapendekezo yao. Kama ningepata nafasi ya kukuletea hapo mezani na wewe pia ukayapitia mapendekezo ya Tume hii ambayo ilishauri kwamba Serikali ifanyie marekebisho Sheria hii ya Ndoa. Pamoja na changamoto zote ambazo zinaonekana za kimila na za dini lakini bado Tume hii ilishauri Serikali kufanya marekebisho Sheria hiyo ya Ndoa ili kuwanusuru watoto wa kike. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakin pia tumeingia mikataba mbalimbali ya kimataifa ukiwepo Mkataba wa Haki za Watoto, Mkataba wa Kutokomeza Aina Zozote zile za Ubaguzi hapa Nchini Tanzania na kwingineko. Pia *Sustainable Development Goals* inazingatia sana kutokomeza ndoa za utotoni ifikapo mwaka 2030. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, juzi juzi tu hapa ilitoka hukumu dada mmoja anayeitwa Rabeca Gyumi alipeleka mapendekezo yake Mahakamani kuhusiana na kubadilishwa kwa Sheria hii ya Ndoa. Kama tunavyofahamu Mahakama ndiyo sehemu pekee ambayo wanaweza

kutusaidia kutafsiri sheria na hapa ninayo nakala ya hukumu. Katika hukumu hii iliyotolewa na Mahakama inapendekeza Serikali kupitia Mwanasheria Mkuu wa Serikali kubadilisha Sheria hii ya Ndoa kile kifungu cha 13 na 17 ambacho kinapendekeza umri wa mtoto wa kike kuolewa kuwa miaka 15 na wa kiume kuo akiwa na miaka 18. Kwa hiyo, hukumu imetoka ikieleza au ikiitaka Serikali kubadilisha vifungu hivyo vya Sheria ya Ndoa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa leo sina mengi sana ya kuongea lakini naomba nihitimishe kwa kusema kwamba, sisi Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tukikaa kimya bila kuwasemea watoto wa kike kwa kweli watu wengi huko nje watabaki wanatushangaa. Nasema hivi kwa sababu nimekuwa nikifuatilia sana kwenye TV, wanawake wanalia na kutoa machozi tena wanabaki wanauliza, wako wapi wanawake wa Tanzania waweze kututetea watoto wetu wasiolewe katika umri mdogo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ndoa hizi wanaaoathirika sana ni watoto wetu wa kike. Japokuwa kuna juhudzi za Serikali ambazo kwa kweli zimeonekana na siwezi kukataa kwamba juhudzi za Serikali hazijaonekana. Tunaona marekebisho ya Sheria ya Elimu ya mwaka 2016 ambayo inataka watoto wasiolewe chini ya umri wa miaka 15 au wakiwa wako shulenii. Hata hivyo, ukiangalia sheria hii inawabagua wale ambaa wapo nje ya mfumo wa elimu. Kwa hiyo, ni ombi langu kwa Serikali kutusaidia tu kutekeleza hii hukumu ambayo imekwisha kutoka au la sivo naomba wanapokuja kuhitimisha hoja yao...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

MHE. KITETO Z. KOSHUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea, Mheshimiwa Ester Michael Mmasi na wa mwisho atakuwa Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa.

MHE. ESTER M. MMASI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nikushukuru kwa kunipa fursa hii adimu nami niweze kuchangia kwenye Bunge lako hili Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kabla sijaenda mbali, napenda sana kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutupa si tu Waziri lakini pia ametupa *encyclopedia* ya sheria katika Bunge hili. Si *encyclopedia* ametupa guru wa masuala ya sheria katika muktadha huu. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais, kwa kweli ametutendea haki sisi Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nichangie masuala ya ajira kwa vijana kwa mlengo wa sheria. Kwa kuanza naomba nichangie Sheria ya Madini ya mwaka 2010 ni kwa namna gani inasigma fursa ya ajira kwa vijana wetu lakini si hivyo tu ni kwa namna gani sheria hii imetumika katika kupora rasilimali ya Tanzania na kusafirisha na hata wazawa tumebacki kuwa watazamaji katika muktadha huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukianza na Sheria hii ya Madini ya mwaka 2010, ukiangalia Kanuni ya 16(1) inaruhusu mgeni kusafirisha madini nje ya nchi. Tukienda kifungu cha 16 tunaona kabisa hata kwenye maonyesho ya kibiashara, mgeni anaruhusiwa kununua madini na kusafirisha nje ya nchi. Si hivyo tu, tunaambiwa kwamba mgeni ambaye amekuja kwa *visa* siku tatu nchini Tanzania anaruhusiwa kusafirisha madini kwa kadri awezavyo lakini tu kama *at-comply* kwenye *requirement* na miongozo ya kisheria. Namba moja atalipa mrhaba unaotakiwa kwa kusafirisha madini hayo lakini pia Kamishna wa Madini atakapokuwa ametoa kibali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini si hilo tu, inasikitisha sana kuona kwamba mchimbaji mdogo ambaye ni *brokers licensed holders* ananyimwa kibali cha kusafirisha madini nje ya nchi. Hii hatutokubali hata siku moja, sisi ambao tunaamini vijana wetu vitovu vyao vilivyoziwa katika ardhi ya Tanzania,

kijana ambaye anajua kuongea lugha ya Kiingereza ananyimwa fursa ya kufanya biashara nje ya nchi kwa kigezo ambacho hatukielewi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye Sheria ya Madini kifungu cha 18 unaona adhabu iliyotolewa, unaambiwa kwamba mtu atakapokuwa amefanya biashara akakiuka haya yote katika muktadha wa sheria, adhabu ni miaka mitatu jela au shilingi milioni 10 tu, hii tunakataa. Tunakataa kwa sababu hata kwenye llani ya Chama cha Mapinduzi tumeagizwa tutetee haya. Nitasoma ni kwa namna gani llani ya Chama cha Mapinduzi imesimama kuona kwamba imefika mwisho tuzuie biashara ya utoroshaji wa madini. Hili tulili-swear kwa wananchi wetu, naomba nirejee. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma llani ya Chama cha Mapinduzi, ukurasa wa 34, kipengele 'K' kinasema:-

*"Katika kipindi cha 2015 hadi 2020, Chama cha Mapinduzi kitaiielekeza Serikali yake kutekeleza mambo yafuatayo: Kubuni na kutekeleza mikakati mabsusi itakayowezesha kupunguza au kukomesha kabisa vitendo vya utoroshaji wa madini kwenda nje ya nchi na biashara haramu ya madini nchini". Hii ni llani ya Chama cha Mapinduzi. (*Makof*)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nasema kwamba imefika mwisho, tunachotaka kuona ni kwamba viwanda vya uchenjuaji wa madini vinajengwa nchini Tanzania. Kwenye sheria hii kwenye kifungu cha 52 wameweka obligations za mwekezaji lakini hatujaona kipengele kinachomlazimisha mwekezaji kuweka plants katika nchi ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili nalitetea kwa nguvu zote kwa sababu naamini kiwanda cha uchenjuaji wa madini kitakapojengwa Tanzania, kwanza tutatengeneza ajira kwa vijana wetu lakini pili tutaongeza thamani ya madini na tatu mimi kama mwana Kilimanjaro, ninyi ni mashahidi tulipoenda

juzi kwenye msiba Kilimanjaro, mliona Kilimanjaro hatuna ardhi. Mkoa wa Kilimanjaro ardhi iliyobaki ni kwa ajili ya makaburi ya bibi na babu zetu, hatuna pa kulima. Mimi ninapotetea viwanda hivi vya uchenjuaji vijengwe ni kwa sababu vijana wangu watapata ajira kwenye migodi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona nchi ya Botswana ilivyopiga hatua. Miaka 40 wananchi wa pale wamebaki kuwa watazamaji kwenye masuala haya ya uwekezaji wa madini lakini baada ya kubadilisha sheria na kusema kwamba viwanda vya uchenjuaji vijengwe katika nchi ya Botswana ndipo ambapo nchi hiyo imeweza kuchangia asilimia 50 ya pato la ndani katika bajeti yake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi vijana wa Chama cha Mapinduzi, sisi Wabunge wa Chama cha Mapinduzi, tunasema kwamba tuna kila sababu viwanda hivi vijengwe. Tofauti na Mheshimiwa Kaka yangu wa Siha pale, Mheshimiwa Dkt. Mollel, nilishangaa sana tarehe 20 mwezi huu hapa Bungeni aliona hakuna mantiki lakini amesahau vijana hawa wa Kilimanjaro hawana pa kulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitasema hata kama Mwanri hayupo, nitatetea vijana wa Kilimanjaro, nitatetea Siha, Hai, Moshi Vijijini, Moshi Mjini, Same na Mwanga, nitasema bila kuogopa, msilogope vijana wangu mimi nipo. Nitasema nitapaza sauti kwa ajili yenu Kilimanjaro. (*Makofii*)

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)

MHE. ESTER M. MMASI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nayasema haya lakini pia tukumbuke dada yangu Mheshimiwa Angella Kairuki hata tungepitisha vifungu vyake mamia na maelfu, hana *absorption capacity* ya kutengeneza ajira hizi ni sisi tumsaidie. Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria mimi na wewe ni mashahidi tulienda kufungua mabweni ya Chuo Kikuu pale lakini uliona juhudzi za Mheshimiwa Rais, alitoka nje ya mikataba, alitoka nje ya

utaratibu akaona kwamba tutengeneze ajira kwa kufanya *TBA* waweze kufanya kazi, vijana na akinamama waajiriwe ili tuweze kusonga mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumwambia Mheshimiwa Waziri tunadaiwa, llani hii tuliahidi watu, nasema kwamba ifike mahali tujenge viwanda. Nitasoma llani ya Chama cha Mapinduzi maana imeniagiza niseme, ukurasa wa 34 kwenye kipengele cha 10 tumeambiwa pamoja na majukumu haya Chama cha Mapinduzi kitafanya yafuatayo:-

"Kitasimamia na kuhamasisha uwekezaji katika shughuli za uongezaji thamani madini ili kukuza mchango wa sekta hiyo katika pato la Taifa".

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasadiki hili na nitalisema siyo leo tu, kesho na kesho kutwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika musuala haya ya ajira ukienda ukasoma *Public Procurement Act* ya Kenya utaona ni kwa namna gani kijana anathaminika katika nchi ile. Katika sheria ile ya Kenya inasema asilimia 30 ya *public procurement activities* zinafanywa na vijana na kunakuwa na dawati maalum katika Ofisi ya Rais. Mheshimiwa Waziri naomba utusaidie, ulipokuwa Kitengo cha Sheria kama *Dean wafanyakazi* wako walikuwa na imani sana na wewe, ulikuwa mkali lakini ulikuwa tayari kutetea maslahi ya Tanzania. Nakuomba Mheshimiwa Waziri usiishie kufundisha pale Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, tunadaiwa ajira, llani hii imetuagiza tutengeneze ajira. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi kwa sababu gani? Hata Bertha Soka, Mkurugenzi wa *PPRA* alikuwa hapa Dodoma, kuna siku...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

MHE. ESTER M. MMASI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Haya tunaendelea na Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa.

MHE. MOHAMED O. MCHENERWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wana Rufiji wote duniani, nasimama hapa nami kuwasilisha ya kwangu lakini kwa kuzingatia maelekezo yaliyowahi kutolewa katika kitabu chake Paul Flynn, mmoja wa Wabunge wazoefu nchini Uingereza kinachozungumzia *how to be an MP*. Pia Profesa Phillip Collin naye katika kitabu chake aliwahi kuzungumzia mambo ya msingi kabisa ambayo Mbunge anapaswa kuyafanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kumshauri dada yangu Mheshimiwa Sabreena atambue kwamba BAKWATA sasa ina uongozi ulio imara na wachapakazi sana. (*Makofii*)

MBUNGE FULANI: Aaah.

MHE. MOHAMED O. MCHENERWA: Shekhe Mkuu wa sasa, Shekhe Zuberi ni mchapakazi sana na mambo haya ya dini tusiyalete kwenye Bunge hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu mmoja anaitwa K. Sachiarith mmoja kati ya wa washindi wa *Global Award*, katika Mkutano wa 136 wa Bunge wa Dunia uliofanyika kule Bangladesh, aliwahi kuzungumza maneno ambayo napenda niyazungumze katika Bunge lako hili Tukufu. Ndugu Sachiarith aliwahi kusema kwamba kama akinamama wangewezeshwa miaka 50 iliyopita basi dunia tungekuwa na Taifa jema sana (*if women were empowered in the last fifty years we could have a better world*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, aliendelea kwa kusisitiza kwamba iwapo vijana wangezaliwa na akinamama waliowezeshwa miaka 50 iliyopita basi tungekuwa na vijana wazalendo wa Taifa, waadilifu na tungekuwa na Taifa lenye nguvu sana, Tanzania ingekuwa ni Taifa lenye nguvu sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona niseme maneno haya kwa sababu tunaona kabisa kwamba vijana waadilifu utawakuta upande huu tuliokaa wengi. Hapa nataka nimtofautishe ndugu yangu Bwana Tundu Lissu ni mionganoni mwa *ignorant pan-politician*. Nimeona niseme hivi kwa sababu Tundu Lissu hana uzalendo wa Taifa hili, anaendekeza harakati, yeche na mwanaharakati lakini si mwanasiasia. Kwa hiyo, tunawaomba Watanzania kumuepuka na kuepukana naye kwani dhamira yake ni kuligawa Taifa hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jukumu la Bunge kwa mujibu wa Ibara ya 63 na 64 ni kutunga sheria na kuvisimamia Serikali.

TAARIFA

MHE. KHATIB SAID HAJI: Taarifa Mwenyekiti.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mchengerwa.

MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, wanasheria wote duniani wanatambua kwamba nchi hii inaendeshwa na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mchengerwa taarifa. Mheshimiwa Khatib endelea.

MHE. KHATIB SAID HAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpe taarifa Mheshimiwa Mchengerwa...

MBUNGE FULANI: Kanuni ya ngapi?

MHE. KHATIB SAID HAJI: Kanuni waijua wewe. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, amemwambia Mheshimiwa Sabreena kwamba BAKWATA ya sasa hivi ina uongozi unaoaminika. Nataka nimpe taarifa Mheshimiwa Mchengerwa, BAKWATA ya Tanzania (Baraza Kuu la Waislamu wa Tanzania) ambapo pia mimi ni Mwislam, haijawahi,

haitawahi kuwa na uongozi unaoaminika. BAKWATA ni chombo kinachotumika kuwakandamiza Waislam wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mchengerwa unaikubali au kuikataa taarifa hiyo?

MHE. MOHAMED O. MCCHENGERWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba unitunzie muda na ikiwezekana leo uniongezee dakika ishirini nina mambo mengi ya kuzungumza.

WABUNGE FULANI: Aaah.

MHE. MOHAMED O. MCCHENGERWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hii naikataa kwa sababu Shekhe Zuberi ni Shekhe ambaye anatambua elimu ya dunia pamoja na ya akhera. Ni mtu muadilifu na mchapakazi sana na ameweza kui-transform BAKWATA kuwa ni chombo kizuri sana kwa Waislam. Niwaombe Waislam wote kuendelea kuiamini BAKWATA. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanasheria wote duniani wanatambua kwamba nchi inaongozwa na katiba, sheria, kanuni na taratibu. Vilevile inaongozwa na taratibu za Chama Tawala ambacho ndicho kimeiweka Serikali madarakani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona niseme hili kwa sababu upo upotoshaji mkubwa uliozungumzwa na Tundu Lindu kuhusu Rais kwamba haitaki Katiba Mpya. Naomba nikumbushe llani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015 ambayo katika ukurasa wake wa nne (4) inazungumzia mambo yatakayoteklezwa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Katika Sura ya Saba ya llani ya Uchaguzi wa Chama cha Mapinduzi pamoja na maneno mengine ukurasa 163 katika aya ya 144 inazungumzia mambo yafuatayo ambayo naomba niyanukuu hapa.

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

"Mchakato wa kutunga Katiba Mpya umeendeshwa na umefikia hatua ya Katiba Inayopendekezwa iliyopitishwa na Bunge Maalum la Katiba ambayo itapigiwa kura ya maoni".

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni llani ya Chama cha Mapinduzi ambayo nchi hii inaongozwa kwa mujibu wa taratibu kama ambavyo nimezisema.

MHE. ANTONY C. KOMU: Taarifa Mheshimiwa Mwenyekiti.

MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nirejee hapo...

TAARIFA

MHE. ANTONY C. KOMU: Taarifa Mheshimiwa Mwenyekiti.

MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA: Katika Ibara ya 118...

MBUNGE FULANI: Uzalendo siyo uwoga.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge mnanielewa mimi kuhusu mambo ya taarifa, lakini leo endelea taarifa.

MHE. ANTONY C. KOMU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwa Kanuni 68(7) naomba nimpe Mheshimiwa Mchengerwa taarifa kwamba Mheshimiwa Tundu Lissu yupo sahihi kusema kwamba Rais hataki Katiba Mpya.

WABUNGE FULANI: Ndiyo.

MHE. ANTONY C. KOMU: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu Rais alivyotimiza mwaka mmoja...

MBUNGE FULANI: Taarifa.

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)

MHE. ANTONY C. KOMU: Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais alipotimiza mwaka mmoja aliiitisha vyombo vya habari akazungumza na wahariri

MBUNGE FULANI: Taarifa.

MHE. ANTONY C. KOMU: Na aliulizwa swali kuhusu Katiba Mpya akasema hajawahi kusema mahali popote katika kampeni zake.

MBUNGE FULANI: Taarifa.

MHE. ANTONY C. KOMU: Kwa hiyo, Katiba Mpya sio ajenda yake na ajenda peke yake aliyonayo yeye ni kunyoosha nchi.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MHE. ANTONY C. KOMU: Kwa hiyo Tundu Lissu yupo sahihi.

MBUNGE FULANI: Taarifa.

MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nitunzie muda.

MWENYEKITI: Muda wako unalindwa lakini unaikubali au unaikataa taarifa hiyo?

MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hii naikataa kutoka kwa *layman* huyu na naomba nimsaidie kwamba nchi inaongozwa na katiba, sheria na kanuni na taratibu ambazo Chama Tawala ndicho kilichosimamisha dola madarakani. Chama cha Mapinduzi kilikuwa na llani ya Uchaguzi ambayo wananchi walio wengi waliona na kuisoma wenzetu walikuwa na tovuti ambayo ilikuwa ni vigumu kwa wananchi wa vijiji kuionna na kuisoma na kuikubali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 118 ya Katiba ambayo Tundu Lissu amepotosha hapa jamii kwa kusema kwamba Mheshimiwa Rais amevunja Katiba kwa kutomchagua Jaji Mkuu wa Tanzania. Ibara ya 118 haimlazimisha Rais kuchagua Jaji Mkuu wa Tanzania. Ibara ya 118 iko wazi kabisa. Mheshimiwa Tundu Lissu anaifahamu sheria na anajua Ibara hii imezungumza vizuri lakini anachofanya ni kupotosha Watanzania na kuleta tataruki katika nchi yetu hii ya Tanzania. (*Makofi*)

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)

MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, yamezungumzwa masuala mengi kuhusu demokrasia na utawala bora. Chama cha Mapinduzi kinaongozwa na Ilani na ukurasa wa 146 umezungumzia demokrasia na utawala bora. Nataka niseme hapa kwamba chama hiki kina demokrasia ya kutosha na unapomwona nyani anamtukana mwenzie ni vyema akaijangalia nyumanzi kwake. Chama hiki kimekuwa na Wenyevitii kadhaa kila baada ya miaka kumi wenzetu wamekuwa na Mwenyekiti amekaa madarakani zaidi ya miaka 20. Hauwezi kuzungumzia demokrasi wakati nyumbani kwako kunaungua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hii mwaka 1961 ilikuwa na Rais wa kwanza alikuwa Mzanaki, Mheshimiwa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Baada ya Mwalimu Nyerere wananchi walimchagua Rais wa Awamu ya Pili, Mzee wetu Mheshimiwa Ally Hassan Mwinyi, alikuwa Mzaramo wa kutoka Zanzibar.

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)

MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 1995 baada ya kuitishwa mfumo wa vyama vingi 1992 tulimchagua Mheshimiwa Benjamin Mkapa, huyu alikuwa Mmakonde kutoka kule Kusini. Mwaka 2005 tulimchagua Mheshimiwa Dokta Jakaya Mrisho Kikwete huyu alikuwa Mkwere kutoka pale Pwani. Taifa letu leo hii

tunashuhudia kuwa na Rais Msukuma kutoka Kanda ya Ziwa. Hii ni demokrasia ya hali ya juu ambayo wenzetu hawana. (*Makofii*)

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)

MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vyema nyani akawa anaona kundule kuliko kutukana wenzio wakati wewe mwenye una matatizo. (*Makofii/ Kicheko*)

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa

MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nijielekeze katika kuishauri Serikali yangu njema ya Chama cha Mapinduzi. (*Makofii/ Kicheko*)

MBUNGE FULANI: Taarifa.

MHE. KASUKU S. BILAGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa

MHE. KASUKU S. BILAGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa kwamba maneno anayoyatumia Mbunge...

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, naomba utulivu Bungeni.

MHE. KASUKU S. BILAGO: Haya maneno ya nyani haoni kundule sio maneno ya Kibunge ayafute.

MBUNGE FULANI: Jana mmelalamikia ngariba nyie.

MWENYEKITI: Taarifa unaikubali au unaikata Mheshimiwa.

MBUNGE FULANI: Kundule na ngariba.

MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni mtoto wa Pwani na neno hilo ni la kawaida tu kule kwetu Pwani. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika miaka ya 90...

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka ya 90 katika moja ya mikutano yake Mheshimiwa Mwalimu Julius Nyerere...

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)

MWENYEKITI: Hebu subiri kidogo Mheshimiwa Mchengerwa.

Waheshimiwa Wabunge, upande wangu wa kushoto, mnisikilize, mimi siamini kwamba Bungeni humu kuna fisi. Haiwezekani watu wazima mnatoa milio ya wanyama wale, tafadhalii tuvumilliane. (*Makofi/Kicheko*)

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA. Tumpe maji marefu awanyooshe mafisi hao.

MWENYEKITI: Kiswahili yawezekana wengine tuna matatizo nacho lakini *as long as* Mheshimiwa Mbunge hajatumia lugha ya kutukana au ya kuudhi twende mbele.

MBUNGE FULANI: Ngariba je?

MWENYEKITI: Ngariba ni Kiswahili kinafahamika.

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mchengerwa hebu hitimisha hoja yako dakika zako tumelinda.

MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka ile ya 90....

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

WABUNGE FULANI: Ahaaa.

MWENYEKITI: Haya kaa Mheshimiwa.

MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka ile ya 90....

MBUNGE FULANI: Kaa wewe.

MWENYEKITI: Kanuni gani bwana?

MHE. MWITA M. WAITARA: Kanuni ya 68(1).

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niulize kuhusu utaratibu na natumia Kanuni ya 64(1)(a), (b) na (g). Kanuni ya 64(1)(a) inasema mchangaiji hatatao ndani ya Bunge taarifa ambazo hazina ukweli. Mheshimiwa Mchengerwa ambaye anaendelea kuchangia sasa anasema Mheshimiwa Tundu Lissu hana uzalendo. Tunaomba athibitishe kwenye Bunge hili ametumia vigezo gani kumpima Mheshimiwa Tundu Lissu hana uzalendo katika nchi hii?

WABUNGE FULANI: Alete huyo.

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba athibitishe vinginevyo afute maneno yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili wakati anachangia anaendelea kupotosha, anajadili jambo ambalo halipo kwenye mjadala sasa. Hatuzungumzii uongozi wa vyama vyaya siasa, hatujauliza CCM wanachagua namna gani wala habari ya CHADEMA wala CUF. Hapa mjadala

uliopo mezani ni hoja ya mapato na makadirio ya Wizara ya Mambo ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu mchangaji anaendelea kutoa maneno ya kuudhi sana kadri anavyoendelea kuchangia. Kwa hiyo, naomba Meza yako ituongoze kuhusu utaratibu hapa Bungeni.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, nimesema lugha inayotakiwa Bungeni ni lugha ya kibunge wala hakuna mabishano hilo na ndijo maana nilisema kama ametumia neno hilo ambalo halikubaliki, nimesema ngariba sio neno ambalo, ni Kiswahili tu...

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)

MWENYEKITI: Msibishane na mimi nasema huo ndio utaratibu wetu tutumie lugha ya kibunge. La pili...

MBUNGE FULANI: Tuvumiliane.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waitara sidhani kama Mheshimiwa anayechangia kwamba hajielekezi kwenye hoja ilio mbele yetu kwa sababu Wizara ya Katiba na Sheria imebeba mambo mengi yakiwemo ya utawala bora na demokrasia. Kwa hiyo, hilo lisikusumbue hata kidogo. *(Makof)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la uzalendo unampimaje mtu? Unampima mtu kwa kauli zake na vitendo vyake. *(Makof)*

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, sisi tumeletwa na Watanzania hawa, wana matumaini makubwa sana kwamba Bunge hili linaweza likatoa maamuzi na mwongozo kwa faida wa mustakabali wa nchii hii. Sasa tukienda namna hii tunaanza kutoa taswira tofauti na matarajio ya wananchi. Mheshimiwa Mchengerwa nakuomba umalizie. *(Makof)*

MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nianzie hapo kwenye uzalendo, miaka ya 90 Mwalimu Nyerere aliwahi kumthibitisha Kawawa katika moja ya mikutano yake pale Mnazi mmoja kusema kwamba Kawawa ni muadilifu sana na alikuwa tayari kutoa machozi kuthibitisha kwamba Kawawa alikuwa ni muadilifu. Nami ndani ya Bunge lako Tukufu naomba kuthibitisha kwamba iwapo siku moja Wabunge walio wengi wakasema kwamba mambo mazuri anayofanya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa nchi hii si uzalendo, basi nitaliomba Bunge lako hili Tukufu kufuta hili neno uzalendo katika *dictionaryya Kiswahili*. Kwa sababu mambo makubwa anayoyafanya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli ni uzalendo wa hali ya juu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijielekeze kwa maneno mawilli matatu ambayo nilmeyaacha pemberi. Mheshimiwa Waziri nikuombe sana wakati unahitimisha hoja yako hapa...

MBUNGE FULANI: Uteuzi umekwisha. (*Kicheko*)

MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA: Nikukumbushe jambo moja, kwanza, tuiangalie kada ya Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo ambao wamekuwa wakipata mishahara midogo. Zipo taarifa wako Mahakimu zaidi ya 118 ambao hawajapandishwa vyeo na hao ni Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pili, kwa hali ya uchumi tuliyonayo ni vyema tukawaangalia Mahakimu pamoja na Wanasheria wa Serikali ili kuwawezesha fedha kidogo kwa ajili ...

(*Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio*)

MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa napenda niseme kwamba Taifa hili linategemea Bunge na uzalendo wetu ndio utakaoliweka Bunge hili katika...

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)

MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niunge mkono hoja na nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kila jambo alilolifanya katika Bunge hili. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana.

MBUNGE FULANI: Uteuzi hamna, uteuzi umekwisha.

MBUNGE FULANI: Tukuteue wewe.

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. MUSSA B. MBAROUK: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema. Naanza kwa kuchangia Wizara hii ambayo inahusiana na Katiba na Sheria ambavyo vyote ndio msingi wa haki. Mfano; katika kitabu cha Hotuba ukurasa wa 36 kipengele cha Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora:-

- (i) Kukuza na kutetea haki za binadamu hususan makundi yenye mahitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maneno haya yameandikwa lakini hayafanyiwi kazi na ushahidi kuna mahabusu na wafungwa wengi ambao wamefungwa bila kupatiwa haki za kisheria kwa kutetewa na wanasheria wa Serikali, kutojua haki zao lakini pia kwa kesi za kubambikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo akinamama wajawazito wanaojifungulia Magerezani na pia wapo wanaotiwa hatiani wakiwa na watoto wachanga ambao bado wananyonya maziwa ya mama zao na hawawezi kuishi bila ya mama zao, wanakuwa wafungwa bila hatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu; Serikali itafute adhabu mbadala kuwaepusha watoto kuwa wafungwa bila hatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Katiba na Sheria nimeishangaa kwa kutoweka katika Bajeti yake Fungu la Fedha kwa ajili ya kuendeleza mjadala wa Katiba mpya ambayo ndio haja ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali kupitia Wizara ya Katiba na Sheria itenye fedha kwa ajili ya mwendelezo wa mjadala wa Katiba mpya ili kuondoa kiu ya Katiba mpya kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mahakimu kukaa katika Vituo vyao kwa muda mrefu wanazoeleka na wanazoea na kuwa wepesi kuweza kupokea rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mahakimu waongezewe mishahara ili kuwaepusha katika suala zima la kupokea rushwa.

MHE. DKT. HAJI H. MPONDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kuunga mkono Hoja. Wilaya ya Malinyi ni mionganini mwa wilaya mpya na zilizoko katika mazingira magumu (pembezoni). Hivyo, wahitaji kupewa kipaumbele na jicho la kipekee. Wilaya ya Malinyi haina Mahakama ya Wilaya hivyo, hutegemea Wilaya jirani (mama) Ulanga. Tumepeleka maombi ya kuanzisha au kujengewa majengo ya Mahakama ya Wilaya ya Malinyi. Tunaomba Serikali kulipa kipaumbele ombi hili la ujenzi wa Mahakama ya Wilaya kwa kuwa huduma hiyo inapatikana mbali sana kilomita 200 hadi 300 toka Wilayani Malinyi kwenda Ulanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Malinyi ina Mahakama za Mwanzo mbili tu kuhudumia wilaya nzima yenye ukubwa wa kilomita za mraba 10,576 na idadi ya watu karibu 250,000. Hivyo tunaomba tuongezewe Mahakama za Mwanzo. Aidha, Mahakimu waliopo wa Mahakama za Mwanzo wamekuwepo muda mrefu katika vituo vyao vya kazi; hivyo kuathiri sana utendaji/ufanisi wa majukumu yao ya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara iweke na kumwezesha Hakimu wa Wilaya ya Ulanga ambaye pia anahudumia Wilaya ya Malinyi kuja kusikiliza mashtaka (kesi) katika Wilaya ya Malinyi ili kupusha au kupunguza usumbu kwa watuhumiwa kwani wanapata adha kubwa sana kwenda na kurudi Mahenge (Ulanga). Ahsante.

MHE. KASUKU S. BILAGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ukosefu wa Mahakama ya Wilaya ya Kakonko; Wilaya ni mpya ina Mahakama za Mwanzo tatu, ambazo hata moja hakuna hakimu (aliyekuwepo yuko masomoni) kama Wilaya tuna kiwanja cha kujenga Mahakama ya Wilaya. Ombi naomba kujengewa Mahakama; na mbili naomba Mahakama ya Mwanzo Kakonko ipewe Hakimu ili kupunguza umbali kwa wananchi kufuata huduma hiyo wilaya jirani ya Kibondo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Burundi kukamatwa ovyo na kufungwa bila kosa lolote. Polisi wanakuwa wakiwakamata warundi wanaokuja kufanya biashara Kokonko (Jimbo la Buyungu) kwa kukutwa sokoni kuwa ni wahamiaji haramu. Matokeo yake hata wanaokuja kulima vijiji vya jirani Burundi na kurudi jioni kwao nao hukamatwa na kufungwa vifungo bila kujadili ni nchi ya Afrika Mashariki. Wapo warundi wapatao 254 wamefungwa gereza la Nyamisinyi- Kibondo kwa makosa kama hayo. Kimsingi Burundi na raia wake pamoja na sisi tunaopakana nao hatufaidi kuwa kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo, Warundi waruhusiwe kuja Wilayani Kakonko kulima na kurudi kwao (uwekwe utaratibu). Warundi wanaokuja kufanya biashara wasikamatwe na kufungwa. Sheria ya kukamatwa ovyo iangaliwe upya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, polisi kubambikiza kesi wananchi, kesi nyangi ni za kubambikiza tu na hivyo kujaza wafungwa gerezani wasio na hatia. Polisi Kakonko

wamekuwa wakiwabambikiza kesi wananchi, sheria zilizopitwa na wakati zifanyiwe marekebisho hapo Bungeni. Mfano Sheria ya Ndoa ya 1971.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mashauri kuchelewa kupelekwa mahakamani. Kumekuwa na tatizo la mashauri kutopelekwa Mahakamani mapema hivyo kuwekwa polisi zaidi ya saa 24.

MHE. TWAHIR AWESU MOHAMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia na kuwezesha kupata fursa hii muhimu ya kutoa mchango wangu huu katika hoja hii iliypopo mbele yenu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haki za binadamu, tumekuwa na tabia kwa Serikali yetu hii tukufu kuweka maneno kwenye makarasi mazuri yenye kuonesha kwamba nchi inafuata taratibu nzuri za kisheria suala zima la utoaji na utekelezaji wa haki za binadamu wakati haki hiyo haipo na haipatikani badala yake Serikali na vyombo vyake vya dola vinatumia nguvu kupita uwezo kwa kuwakandamiza na kuwanyanyasa raia zake kuwekwa magerezani na kuwapa vifungo kwa makosa ya kuwabambikiza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na watuhumiwa wa makosa ya ugaidi zaidi ya miaka minne sasa Watanzania wenzetu wamo wanateseka na kufanyiwa vitendo vya kinyama na kiudhalilishaji wako mbali na familia zao. Kesi hadi leo inaelezwa ushahidi haujakkamilika, naiomba Serikali kwanza itambue hapa duniani tunapita, iache kutesa raia zake, basi kama wanahatia ni vyema wakahukumiwa, wakapewa adhabu kulingana na ukubwa wa makosa yao na kama makosa hayakukidhi wakaachiwa huru wakarudi na kuishi na familia zao ambazo hivi sasa zinateseka sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la katiba mpya, suala hili sasa si suala rahisi tena kutekeleza ni dhahiri Serikali halimo kabisa katika mpango wake wa utekelezaji wake, pamoja na Watanzania kuhitaji sana suala hili. Ni vyema kwa Serikali kuzingatia na kusikiliza maoni na matakwa ya wananchi

wake kuepusha nchi yetu kuingia katika kutoelewana kitu ambacho kinaweza kuleta mgawanyiko mkubwa, utakaopelekea Taifa kusambaratika na kugombana wenyewe kwa wenyewe. Naiomba Serikali ikae na ilifikirie jambo hili kwa umakini mkubwa ili thamani ya kazi na michango waliyotoa Watanzania ionekane umuhimu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MHE. ELIAS J. KWANDIKWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa tumehamia Makao Makuu ya Halmashauri ya Ushetu, Makao Makuu katika Kijiji cha Nyamilangano (Jimbo la Ushetu) na kwa kuwa Mahakama inayohudumia eneo hili yako mbali na kwa kuwa tunayo Ofisi ya *OCD* – Ushetu tuliyopewa hivi karibuni na ni muhimu mashauri mbalimbali yanaelekezwa umbali mrefu kupata huduma za Kimahakama na kwa kuwa Halmashauri ya Ushetu iko tayari kutoa eneo kwa ajili ya ujenzi wa Mahakama tunaomba Serikali itujengee Mahakama ya Mwanzo eneo hili la Kijiji cha Nyamilangano (Makao Makuu ya Halmashauri ya Wilaya Ushetu) ili wananchi wapate huduma ya haki zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kukupongeza kwa hotuba yako nzuri. Pia naunga mkono kwa asilimia mia moja pamoja na kuunga mkono hoja hii naomba kuchangia maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, upungufu wa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo. Mahakimu wa Mahakama ya Mwanzo ni wachache sana hapa nchini. Wilaya yangu ya Mpwapwa ina Kata 33 lakini *PCM* wapo wanne tu na hawana usafiri, angalau *PCM*wote nchini wangepata pikipiki au magari madogo ya kuwasaidia kutembelea Mahakama za mbali kuliko ilivyo sasa *PCM* wengi wanapanda mabasi ambapo ni hatari hasa *PCM* akiwa na mafaili ya kesi anaweza kuporwa ndani ya basi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo wajengewe nyumba za kuishi badala ya kuishi mitaani ambapo ni hatari kwa maisha yao, bahati mbaya anaweza kupanga na mtu mwenye kesi katika Mahakama yake. Maslahi ya *PCM* ni duni sana waongezwe mishahara ili kumudu mazingira wanayoishi au kuboresha maisha yao kuliko hali ilivyo sasa. Wilaya ya Mpwapwa tulijengewa jengo la Mahakama ya Wilaya lakini *Rest House* ya Mheshimiwa Jaji haikujengwa mpaka sasa. Je, itajengwa lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kila Tarafa zijengwe Mahakama za Mwanzo nne ili kuwasogezea wananchi huduma ya Mahakama karibu kuliko hali ilivyo sasa wananchi hutembea kilomita zaidi ya 100 kufuata huduma hiyo. Chuo cha Mahakama Lushoto waongeze wanafunzi ili kuongeza idadi ya *PCM* hapa nchini.

MHE. OSCAR R. MUKASA: Mheshimiwa Mwenyekiti, *coverage* ya *civil registration* ni ndogo sana hapa nchini, inawezekana ni chini ya asilimia kumi. Kwa nini msitumie watendaji wa Kata na Vijiji kama mawakala wa *RITA* kwa kuwapa gawio kwa kila kizazi, kifo na ndoa wanavyoorodhesha na kutumia taasisi za utafiti kwa kuhakiki ubora.

MHE. ALLAN J. KIULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kuipongeza Wizara ya Katiba na Sheria kwa kazi nzuri inayofanywa. Pamoja na kuwepo changamoto ya umuhimu wa kuboresha baadhi ya sheria ambazo ama zimepitwa na wakati au zinahitaji kuweka mkazo/udhibiti katika baadhi ya maeneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesoma hotuba hii kikamilifu na kubaini kuwa ahadi iliyotolewa Bungeni na Waziri mtangulizi kuhusu Wilaya mpya ya Mkalama kutokuwa na Mahakama ya Wilaya ilihali wananchi wakiifuata haki Wilaya ya Iramba Magharibi. Wakati jibu likitolewa katika swali la msingi liloulizwa na Mbunge wa Iramba Mashariki Mheshimiwa Allan Kiula iliahidiwa kuwa bajeti ya Wizara ya

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

mwaka wa fedha 2017/2018 itaweka/itatenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa Mahakama ya Wilaya ya Mkalama lakini sijaona utekelezaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Wizara itenye fedha katika bajeti hii ili kuwasaidia wananchi wa Mkalama ambao wamewekwa wakihangaika kupata haki katika Wilaya nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na naunga mkono hoja.

MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga hoja mkono. Aidha, naomba kuchangia katika maeneo mawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ucheleweshaji wa kesi hususan za jinai Mahakamani ni tatizo kubwa sana ambalo linahusisha Wizara nyingine kuu za Mambo ya Ndani. Makosa ya mauaji ni moja ya makosa ambayo watuhumiwa wake wanakaa muda mrefu mahabusu. Nashauri Serikali iangalie upya utaratibu wa *High Court Session* ili kesi hizo zisichukue muda mrefu kama inavyochukua wakati huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mahabusu pia ambao wanahukumiwa kifo utekelezaji wake haufanyiki vizuri. Suala hilo likaangaliwe mawakili wa Serikali maslahi yao yaangaliwe upya. Mishahara na marupurupu yao ni midogo sana ukilinganisha na kazi zinavyofanyika.

MHE. MBARAKA K. DAU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Sheria na Katiba Palamagamba Kabudi. Nianze na hali za Mahakama zetu nchini hususan Mahakama za Mwanzo. Hali za majengo, watumishi na vitendea kazi ni mbaya sana. Katika Wilaya ya Mafia tuna Mahakama ya Mwanzo moja tu na imechakaa na haina watumishi wa kutosha. Wananchi wa Mafia wanalazimika kusafiri masafa marefu kwenda kufuata huduma za Mahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kuiomba Serikali ituongezee Mahakama za Mwanzo angalau mbili katika maeneo ya Utende na Vunjanazi sambamba na kuimarisha vitendea kazi na kuongeza watumishi wa Mahakama ya Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haki ya dhamana kuu mahabusu kwenye rumande zetu kuna mahabusu wengi wanashikiliwa katika mahabusu zetu wakati wapo wenye kukidhi vigezo vya kumchukulia dhamana. Namwomba Mheshimiwa Waziri wakati wa kuhitimisha hoja alitolee ufanuzi hili jambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upo umuhimu wa Serikali kuongeza bajeti ya Wizara hii ili kuhakikisha suala la utoaji wa haki nchini linafanyika kwa weledi wa hali ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na naomba kuunga mkono hoja.

MHE. ABDALLAH A. MTOLEA: Mheshimiwa Mwenyekiti, katiba mpya, Wizara haina muda tena wa kusubiri kuanza kumalizia mchakato wa kupata katiba mpya. Kama bajeti hii ya 2017/2018 haitatenga pesa kwa ajili ya jambo hili, maana yake Watanzania wasitegemee tena kupata katiba mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, marekebisho ya sheria, Serikali ilete Muswada Bungeni kwa ajili ya kubadilisha sheria ya mabadiliko ya katiba ya 2011 na ile ya kura ya maoni ya 3013 ili iendane na hali ya sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zuio la shughuli za kisiasa, Serikali itengue zuio lake la kuwakataza wanasiasa kufanya mikutano ya kisiasa kwani kwa kufanya hivyo inavunja sheria ya vyama vya siasa. Ni haki ya msingi ya vyama vya siasa kufanya mikutano ya kisiasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majengo chakavu, Wizara itafute vyanzo vyake vingine ili ipate fedha za kujenga na

kukarabati majengo ya mahakama hasa Mahakama ya Mwanzo.

MHE. LUCY F. OWENYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata nafasi ya kuchangia. Ucheleweshwaji wa kusikiliza kesi za mahabusu. Baada ya kesi zilizopo katika uchunguzi chini ya *DPP* zinachukua muda mrefu sana na wakati watuhumiwa wengine hawana hatia lakini wanaweza kuwa gerezani kwa zaidi ya miezi sita. Je, kesi hizi hazina kikomo cha uchunguzi? Inakuwa kama wanakomoa na kudhalilisha wengine na huu ni ukiukwaji wa haki za binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya Mfuko wa Mahakama, bado mfuko huu wa fedha zinazoainishwa hazifiki kwa wakati na hata wakizipata zinakuja zimechelewa na pungufu ambayo inakuwa ni vigumu kutekeleza miradi ya maendeleo hii inajionesha mpaka Machi 2017, fedha hazikutumwa kwa wakati. Chombo hiki ni muhimu sana nashauri fedha zipelekwe kwa wakati ikiwa ni pamoja na kuhakikisha wapo watumishi wa kutosha, kuhakikisha posho za wazee wa mabaraza zinalipwa, wazee hawa wanaacha shughuli zao wengine inabidi watumie nauli zao, hivyo, wana haki ya kupata stahili zao kwa wakati.

MHE. ZACHARIA P. ISSAAY: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuishauri Serikali kuptitia upya sheria mbalimbali, naomba Serikali itafute utaratibu wa kila Tarafa nchini kuwa na Mahakama za Mwanzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu wa kupata wazee wa Mahakama uboreshwe. Hivi sasa wazee wengi wa Mahakama wanakaa muda mrefu bila kuteuliwa kwa kuzingatia jinsia na kutoka Kata au Tarafa kulingana na idadi yao, hata hivyo uteuzi haushirikishi Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mabaraza ya Ardhi baadhi yake yamejihuisha na rushwa kiasi kwamba wapokea huduma toka Mabaraza mbalimbali nchini yanakosa imani.

Kwa sasa kuna haja ya ufanuzi wa Wizara kuhusu masuala mbalimbali ya wananchi kufahamu utaratibu wa kupata haki zao mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa Wakuu wa Wilaya ndiyo Wenye viti wa Kamati ya Maadili ya Mahakama. Kuna haja ya kuwa na ratiba ya vikao vya Kamati hiyo muhimu kwa ustawi wa Mahakama nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku ya Maadhimisho ya Mahakama nchini itumike kuwa siku ya wapokea huduma kutoa mawazo yao kuhusu huduma hiyo ili Watendaji wa Mahakama waweze kujijua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo wa malipo ya Wazee wa Mahakama utazamwe ili kuleta tija, kwa sasa wazee wengi wanalamikiwa kujihusisha na rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwe na kipindi cha kuwahabarisha umma kuhusu huduma ya Wasaidizi wa Kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali isaidie kutoa fedha za ujenzi wa jengo la Mahakama ya Wilaya ya Mbulu na Jengo la nyumba ya Hakimu wa Wilaya. Kwa sasa majengo yaliyoko ni chakavu sana, hayafai kwa matumizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa Wilaya ya Mbulu yenyewe Kata thelathini na tano ina Mahakama moja ya Wilaya na Mahakama za Mwanza tatu lakini Mahakama za Mwanza haina Mahakimu wa kutosha na kesi nyingi hucheleva sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naomba Waziri mwenye dhamana afanye ziara Wilayani Mbulu na kuona changamoto ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante

MHE. GIMBI D. MASABA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kuwasilisha mchango wangu wa maandishi kuhusu Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria. Ningependa kuzungumzia kuhusu suala la uwazi katika mchakato wa utoaji haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu ni nchi mwanachama wa *OGP Open Government Partnership* ambapo mojawapo ya misingi muhimu ni Serikali za nchi husika kutekeleza majukumu yao kwa uwazi wa hali ya juu ili wananchi wajue Serikali zao zinavyofanya kazi. Hata hivyo kwa Tanzania hali ni tofauti kwa kuwa uhuru wa habari umeminywa kwa kiwango cha juu kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na usiri mkubwa sana katika mchakato wa utoaji haki Mahakamani. Vyombo vyaa habari vinazuiwa kuingia Mahakamani kuona mwenendo wa kesi, jambo ambalo limesababisha kushamiri kwa vitendo vyaa rushwa na wanyonge kudhulumiwa haki zao kutokana na usiri uliogubika Mhimili wa Mahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika nchi jirani ya Kenya, kesi zote zenye maslahi kwa Taifa huwa zinarushwa moja kwa moja kwenye Televisheni na wananchi wanaona mwenendo wa mchakato wa utoaji haki. Kesi za uchaguzi na katiba katika nchi ya Kenya zilirushwa moja kwa moja na *Citizen TV*. Aidha, kuhusu kesi ya *BREXIT* ya Uingereza juu ya nani kati ya Bunge na Serikali ya Uingereza anatakiwa kuanzisha mchakato wa kujitoa katika umoja wa Ulaya ilirushwa /ive moja kwa moja na *BBC* na dunia nzima ilishuhudia na kuona mwenendo wa utoaji haki. Kwa kutumia mifano ya Kenya na Uingereza, nadhani Tanzania sasa inatakiwa kwenda *level* nyingine kwa kuruhusu uwazi zaidi katika mchakato wa utoaji haki Mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na vyombo vyaa habari kuruhusiwa kuingia katika vyumba vyaa Mahakama ili kuripoti mwenendo wa mchakato wa utoaji haki, vyombo hivyo pia viruhusiwe kuwatemeblea wafungwa Magerezani ili wafungwa wapate haki ya kueleza fikra na mtazamo wao

kuhusu maisha yao Magerezani. Kwa kufanya hivyo, tutakuwa tumepeiga hatua kubwa ya kudumisha uwazi katika utendaji wa Mahakama, lakini pia tutakuwa tumepeiga hatua kubwa katika kujali haki za wafungwa ambazo ni mionganoni mwa haki za binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MHE. JOHN J. NYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Katiba na Sheria ina wajibu wa kuiwezesha nchi kuwa na mfumo mbalimbali wa Kikatiba na Kisheria katika kufanikisha Mipango ya Maendeleo ya Taifa. Pamoja na wajibu huu muhimu hotuba nzima ya Waziri haijazungumzia kabisa kuhusu mchakato wa Katiba mpya. Aidha, katika vitabu vyatengwa fedha zozote/kiasi chochote kwa ajili ya kuendeleza mchakato wa Katiba mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali inadhihirisha kwamba Serikali ya Rais Dkt. John Magufuli lazima dhamira ya kuendeleza kwa wakati mchakato wa mabadiliko ya katiba. Hivyo ni vyema Serikali ikatoa kauli hii Bungeni ni kwa nini haijatenga fedha kwa ajili ya mchakato huu muhimu kwa maslahi ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika aya ya 20, 21, 22, Waziri wa Katiba na Sheria amezungumzia kuhusu utekelezaji wa mkakati wa kuboresha huduma za Mahakama ikiwa ni pamoja na kufanya ujenzi na ukarabati wa Mahakama mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika orodha hiyo imetajwa Wilaya mpya ya Kigamboni, hata hivyo Wilaya mpya ya Ubungo haijatajwa hivyo, Serikali itoe kauli ni kwa nini Wilaya mpya ya Ubungo haijajumuishwa na lini Mahakama ya Wilaya ya Ubungo itajengwa. Aidha, Mahakama hiyo ni vyema ikajengwa katika Jimbo la Kibamba yalipo Makao Makuu ya Wilaya mpya ya Ubungo kama ilivyopendekezwa kwa nyakati mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya kurekebisha Sheria ina wajibu na mpango muhimu ya maboresho ambayo yamependekezwa muda mrefu ni pamoja na matumizi ya lugha ya Kiswahili katika mfumo mzima wa Mahakama na utungaji sheria nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora imeeleza kuwa imefanya uchaguzi kuhusu mabadiliko yaliyowasilishwa katika THUB.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiwa Mbunge wa Ubungo niliwasilisha malalamiko na madai ya kutaka, uchunguzi kuhusu ukiukwaji wa haki za binadamu na misingi yake ya utawala bora juu ya mgogoro wa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu matatizo ya maji katika Kata ya Goba naomba kupatiwa majibu juu ya hatua ambazo Tume imechukua na kupatiwa nakala ya ripoti ya Tume kuhusu uchunguzi huo. Aidha pamoja na uwekezaji mkubwa wa Serikali juu ya miradi ya Ruvu juu na Ruvu chini tume ielewé kwamba Goba bado imeachwa kama kisiwa kwa kuwa haina mtaro wa mabomba.

MHE. OMARI M. KIGUA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kuipongeza Serikali na Waziri husika kwa hotuba nzuri inayohusu makadirio na matumizi kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi zimekuwa mahali muhimu kwa ajili ya kutoa haki katika nchi yetu. Hata hivyo, nimesikitika sana kuona kuwa katika bajeti ya mwaka wa fedha 2016/2017 Wizara ilitaja Wilaya 17 zitakazojengwa Mahakama ya Wilaya na moja ya Wilaya hizo ni Kilindi. Naomba kupata majibu ya kuridhisha kwa nini Wilaya ya Kilindi si miongoni mwa Wilaya zilizopo katika ujenzi kwa mwaka huu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni takribani miaka 30 sasa wakazi wa Wilaya ya Kilindi wamekuwa wakipata huduma za Mahakama za Wilaya katika Wilaya jirani ya Handeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upo umbali mrefu sana kutoka Kilindi na Handeni hususani kwa Kata za Pagwi, Kikunde, Tunguli kata hizo zipo karibu kabisa na Wilaya ya Gairo. Utaona kwa kiasi wananchi wa kilindi wanahitaji Mahakama hii kwani kupata Mahakama ni sehemu ya haki za msingi kwa wananchi wa Kilindi. Halmashauri inalo eneo kwa ajili ya ujenzi wa Mahakama. Niombe sasa Wizara ione umuhimu wa kuwapatia wananchi Mahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uhaba wa Mahakama za Mwanzo; Mahakama za Mwanzo pia zimekuwa ni chombo muhimu sana katika kutoa haki kwa wananchi wetu, lakini maeneo mengi hayana Mahakama za Mwanzo na hata kama zipo basi zimechakaa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano katika Jimbo langu la Kilindi yote tarafa nne, kata 21 na vijiji 102 tunazo Mahakama za Mwanzo zisizozidi tano, hali hii ni mbaya sana. Ningombaa kauli ya Wizara na Waziri mwenye dhamana ya Mahakama hizi ni lini watu wa Kilindi watapata Mahakama za Mwanzo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa na Mahakama za Mwanzo Kata za Kimbe, Mgora, Kwekiku, lakini Mahakama hizi zote majengo yake yote yamekuwa magofu na hakuna Mahakimu, je, lini Mahakama hizi zitajengwa upya? Niombe Waziri alichukue jambo hili kwa uzito mkubwa unaostahiki

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na kumpongeza Waziri Profesa Kabudi na watendaji wote wa Wizara kwa kutuletea bajeti yao ili tuweze kuijadili. Kuna mambo ambayo nataka kuyapatia ufanuzi wake na kushauri pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ucheleweshaji wa kesi za ubakaji; Mkoa wetu wa Iringa ni kat i ya mikoa inayokabiliwa na idadi kubwa sana ya kesi ya ubakaji na ulawiti. Inasikitisha sana Bunge lililopita nililetwa swali langu hapa Bungeni na

niliweza kutoa takwimu ya mwaka 2016 kesi 217 lakini zilizoweza kufikishwa Mahakamani ni kesi 27 tu lakini kila mwaka katika mkoa wetu matukio ya ubakaji yanazidi kuongezeka. Napenda kujuu mkakati wa Serikali kuhusiana na jambo hili ni kwa nini kusiwepo na Mahakama Maalum ya kushughulikia kesi hizi. Matukio haya yamekuwa yakiwaathiri watoto wetu kiakili pamoja na mama zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ucheleweshaji wa mabadiliko ya sheria zilizopitwa na wakati; baadhi ya sheria zetu hapa nchini zimekuwa ni za muda mrefu sana na zimepitwa na wakati na kusababisha baadhi ya sheria zetu hapa nchini kutoendana na mabadiliko na kasi ya maendeleo ya Taifa na kuonekana kuwa zimepitwa na wakati. Mara nydingi sana sisi Wabunge tumekuwa tukileta hoja zetu hapa Bungeni lakini bado hatupatiwi majibu ya kuridhisha. Kwa mfano, 12 Aprilli, 2017 nililetwa swali kuhusiana na Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 lakini bado majibu yake hayaridhishi. Je, ni lini sasa Serikali italeta hoja ya kufanya marekebisho ya kuboresha baadhi ya sheria zilizopitwa na wakati?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufinyu wa bajeti, Wizara hii ni muhimu sana na imekuwa na malalamiko mengi kwa wananchi kutomaliza kesi zao au kuchukua muda mrefu sana. Pia miradi mingi kutoamilika kwa wakati pamoja na bajeti yao kuwa kidogo sana lakini pia pesa yao imekuwa ikicheleweshwa sana na kusababisha miradi kutoamilika kwa wakati hivyo kusababisha miradi hiyo kutumia pesa nydingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. FLATEI G. MASSAY: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naunga mkono Hoja ya Serikali au Wizara ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo malalamiko katika eneo hili la Mahakama. Hatuna Mahakama katika eneo la Haydom ambapo pana watu zaidi ya hamsini elfu na wapo

pembezoni na Halmashauri ya Mji wa Mbulu ni kilomita 86 toka Makao Makuu ya Wilaya ambapo ipo Mahakama ya Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunacho Kituo cha Polisi Haydom ambapo tunaomba tujengewe Mahakama hata ya Mwanzo. Tumekwisha tengen kwanza cha kujenga Mahakama. Kituo cha Polisi kinafanya kazi ya kukamata wabadhirifu na kuwasafirisha Mbulu zaidi ya kilomita 86 hivyo kuipa Serikali gharama kubwa sana ya kupeleka mahabusu/watuhumiwa zaidi ya kilometra nillizozitaja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tujengewe Mahakama Haydom maana wakati mwingine Polisi hutumia mabasi kusafirisha watuhumiwa na wakati mwingine kutoroka na kupotea. Hivyo naomba sana.

MHE. JUMA OTHMAN HIJA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kukushukuru wewe kwa kunipatia fursa hii ya kutoa mchango kwa njia ya maandishi. Napenda kumpongeza Waziri wa Katiba na Sheria ye ye pamoja na wataalam wake kwa kuandaa hotuba hii yenye kuonesha ubora na utaalam mkubwa. Katika kuchangia hotuba hii, napenda kuchangia maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, urejeshwaji wa wahalifu na ushirikiano na Mataifa kwenye makosa ya jinai, hili ni jambo zuri ambalo linaongeza ushirikiano na mahusiano mazuri kwa Mataifa ya nje. Uhali ni jambo baya ambalo linahitaji kupigwa vita kwa nguvu zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu katika suala hili, Serikali iwe makini katika utekelezaji wake. Inapotokelezea ulazima wa kuwapeleka wananchi wetu (wahalifu) ni vyema tukaangalia usalama wa nchi tunayotaka kuwapeleka. Kwa mfano; juzi imetokezea wahalifu wa biashara ya unga ambao wanafika kupelekwa Marekani lakini hivi sasa katika nchi ya Marekani kuna vita ya maneno kati ya Marekani na Korea ya Kaskazini.

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hii inatisha na ni vyema tukachukulia tahadhari kubwa. Korea ya Kaskazini wametishia na wanaendeleza vitisho la kuipiga Marekani kwa silaha za *nuclear*, hii ni hatari kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maendeleo ya rasilimali watu, rasilimali watu ni jambo jema katika sehemu zote za maendeleo. Ushauri wangu katika jambo hili ni kwamba, Serikali ni vyema ikawatayarisha kwa kuwasomesha na kuwapatia elimu juu ya masuala ya kisheria ili kuendeleza ufanisi katika Wizara hii nyeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. MGENI JADI KADIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema na kuniwezesha kuchangia hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiukwaji wa haki za binadamu, kwanza kuna jambo la kusikitisha kuhusu vijana wanaokwenda kufanya kazi za ndani katika nchi ya Uarabuni-Dubai. Vijana hawa wanateswa, wanajisiwa, wanaauliwa lakini hawana watetezi. Je, ni kwa nini Balozi zetu wanakaa kimya na kwa nini hawafuatilii matokeo haya? Huu ni ukiukwaji wa haki za kibinadamu kwa hiyo Serikali yetu ya Tanzania ifuatilie tatizo hili ni kubwa, Watanzania wetu wanapotea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Masheikh wetu wa upande wa Zanzibar walishikwa huku Bara sasa ni miaka minne wako mahabusu mpaka leo upelelezi haujapatikana, basi sasa waachiliwe huru wakaishi na familia zao kwa sababu jambo hili linaonekana ni la kisiasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mahakama ya Kadhi, Mahakama ya Kadhi ni chombo cha Kisheria kwa dini ya Kiislam. Chombo hiki ndicho kinachosimamia mirathi na ndoa. Ni kwa nini nchi hii ina Waislamu wengi na inazuia chombo hiki?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi nyngi duniani zinazo Mahakama ya Kadhi kama vile Kenya, Uganda, Zanzibar na kadhalika. Je, ni lini chombo hiki kitafanya kazi hapa Tanzania bara kwa faida ya Waislam wa nchi hii? Naomba Waziri atakapofanya majumuisho nipate ufanuzi tafadhalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mchango huu, naomba kuwasilisha.

MHE. SUSAN L. KIWANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuunga mkono Hotuba ya Kambi ya Upinzani Bungeni. Naomba Serikali ione haja ya kuwaokoa Watanzania wanaoishi Wilaya ya Kilombero, Jimbo la Mlimba ambako jimbo zima pamoja na kuwa na miundombinu mibovu lakini hakuna huduma ya uhakika ya Mahakama. Hivyo kupelekea watu wengi kukaa mahabusu kwa kukosa usafiri ama mashahidi kushindwa kufika mahakamani kutoa ushahidi, zaidi ya kilometra 260 hadi Mahakama ya Wilaya iliyopo Ifakara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu, naomba Mheshimiwa Waziri atembelee Jimbo la Mlimba; pili, tupatiwe mahakama Jimbo la Mlimba; na tatu Mahakimu waajiriwe ili haki zipatikane.

MHE. MARY D. MURO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia kama ifuatavyo:-

Nishauri Serikali kuweka bayana mambo ya kisheria na kuyatendea haki mfano haki ya kujieleza, haki ya kupata habari, haki ya kuishi, ni vizuri Serikali ikatendea haki maeneo hayo ili taifa liwe na Amani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali itambue kuwa amani haiwezi kuwepo bila haki ambayo inatokana na utawala wa Sheria. Sheria za Ndoa na mirathi zipo lakini wananchi wa kawaida hawana elimu ya sheria. Pia nashauri Serikali kufanya juhudhi ili kutoa elimu ya sheria kama ilivyo kwa matangazo mengine ya UKIMWI na madawa ya kulevya.

Nashauri Serikali kutembelea mahakama zetu zilivyo na wafanyakazi wanaoishi na kufanya kazi katika wakati mgumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nishauri kuhusu upelekaji wa wafungwa kutoka mahabusu imekuwa shida, hivyo Serikali iangalie kwa nini kutohana na ukosefu wa usafiri, kesi zao huahirishwa mara kwa mara hivyo kusababisha mahabusu kutumikia vifungo vyao kabla ya hukumu. Mfano halisi mtuhumiwa anakaa mahabusu miaka minne kabla ya hukumu, hivyo Serikali inaingia hasara ya kulisha mahabusu. Pia kupunguza nguvu kazi ya Taifa kwa kuwaweka gerezani. Nashauri Serikali iongeze fedha kwa mahakama ili kuongeza utendaji.

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mheshimiwa Mwenyekiti, usikilizaji wa mashauri mahakamani; pamoja na Serikali kueleza 80% ya mashauri yameweza kusikilizwa, kasi hii bado inahitaji kuwekewa nguvu zaidi ili kuendelea kupunguza mrundikano wa kesi zilizopo mahakamani. Serikali lazima itie nguvu na mkazo katika Mahakama za Mwanzo na Mahakama za Wilaya kwani huko ndiko kwenye mrundikano wa kesi nyingi, jambo ambalo linawafanya wananchi wenyе kesi mbalimbali kuendelea kutumia muda mwingi mahakamani. Hata hivyo, haki inayocheleweshwa ni sawa na haki iliyonyimwa. Nashauri Serikali iendelee kujipanga kuhakikisha mrundikano wa kesi katika mahakama za chini zinakwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo; pamoja na umuhimu wa Taasisi hii ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo, ipo haja ya kuongeza chuo hiki katika kanda nyingine za nchi hii. Ni ukweli kuwa nchi hii ni kubwa na wanafunzi wanaohitaji kupata mafunzo haya ni wengi. Hivyo basi, ni muhimu kwa Serikali kuongeza vituo vya mafunzo hayo kwa angalau Kanda ya Kaskazini, Kanda ya Kati, Kusini na Magharibi. Kwa kuongeza vituo hivyo itasaidia wanafunzi kumudu gharama za mafunzo na hivyo kuongeza wanafunzi zaidi.

MHE. LUCIA M. MLOWE: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika nchi yetu kuna hali ya kutisha kwa sababu ya utekwaji wa watu (wananchi) lakini Serikali imenyamaza kimya, mfano kutekwa kwa Ben Saanane. Naiomba Serikali ishughulikie suala hili na hasa kumleta Ben Saanane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria zetu za jinai zimesisitiza kwamba utekaji nyara kwa lengo la kuua au kuumiza mtu ni kosa kubwa la jinai. Chini ya Kifungu cha 248 cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu, kwa mfano;

"Mtu ye yote ambaye anamteka nyara au kumtorosha mtu ye yote ili mtu huyo auawe, au aweze kutupwa ili kuwekwa katika hatari ya kuuawa, atakuwa anatenda kosa na anawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miaka kumi"

Kwa mujibu wa kifungu cha 250 cha sheria hiyo, kuteka nyara kwa lengo la kumuumiza mtekwa nyara ni kosa la jinai vilevile na adhabu yake ni kifungo jela kwa muda wa miaka kumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kuwazuia watu wasiwe na uhuru wa mawazo ni kukiuka Katiba ya nchi lbara ya 18(a) inayosema:-

"Kila mtu-

(a) Anao uhuru wa kuwa na maoni na kueleza fikra zake"

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwepo na kamatakamata ya baadhi ya Wabunge na wananchi wengine kwa sababu ya kueleza au kutoa mawazo yao ya kuikosoa Serikali. Naishauri Serikali kusikiliza mawazo hayo na kuyatendea kazi kwani ni kwa njia ya kukosolewa Serikali inaweza kuboresha utendaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ndoa za utotoni, naiomba Serikali kurekebisha Sheria ya Ndoa ili kuwatendea haki watoto wa kike.

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuzuia mikutano ya hadhara, hapa naona Serikali inakiuka Katiba ya Jamhuri ya Muungano Ibara ya 20(1) inayosema:

"Kila mtu anao uhuru wa kukutana na watu wengine kwa hiari yake na kwa amani, kuchanganyika, kushirikiana na watu wengine, na kwa ajili hiyo kutoa mawazo yake hadharani na kuanzisha na kujunga na vyama au mashirika yaliyoanzishwa kwa madhumuni ya kuhifadhi au kuendeleza imani au maslahi yake au maslahi mengineyo."

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali iruhusu mikutano ya vyama vyta siasa kwani hii ni kulingana na Katiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MHE. JOSEPH L. HAULE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana nami niweze kuchangia kidogo kwenye Wizara hii nyeti ya Sheria na Katiba. Kumekuwa na malalamiko na kilio cha muda mrefu sana cha wafanyakazi walioachishwa kazi *Kilombero Sugar Companymwaka* 2,000. Wafanyakazi hao karibu 3,000 walipoachishwa kazi hawakulipwa stahiki zao na wamekuwa wakidai stahiki zao hizo kwa muda mrefu sana, wengine wameshatangulia mbele za haki na wengine bado wapo hai. Wafanyakazi hao walipoona hawatendewi haki walikwenda Mahakamani na kukawa na Jalada la Kesi Namba 50/2000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafanyakazi hao wamekwenda mara kadhaa Wizara ya Katiba na Sheria wakiomba wapewe nakala ya hukumu ya jalada lao la kesi Namba 50/2000 bila mafanikio. Pia, waliandika barua kwa Waziri wa Wizara ya Katiba na Sheria tarehe 24 Machi, 2016 na nakala kupelekwa kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu ambaye mnamo tarehe 25 Julai, 2016 (Kumb. Na. PM/P/1/569/82), Katibu wa Waziri Mkuu alijibu kuwa ameipata na ataisisitiza Wizara ya Katiba na Sheria ishughulikie kikamilifu kwa mujibu wa Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnamo mwaka 2014 Mahakama Kuu iliwapatia tamko la kuvumilia na kwamba, walikuwa wakilifanya kazi, mpaka sasa hakuna majibu. Ndipo walipoamua kulipeleka Wizara ya Katiba na Sheria mwezi Julai, 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, kwa niaba ya wafanyakazi walioachishwa kazi *Kilombero Sugar Company* 2000, namwomba Waziri atakapokuja kwenye majumuisho yake aje atupe majibu kwamba, ni lini sasa wananchi hao watapata haki yao ya kupata nakala ya hukumu ya kesi Namba 50/2000. Ni matumaini yangu mtawasaidia kilio cha wanyonge hawa, ili wapate haki yao ya kulipwa mafao yao wanayostahili ambayo wamekuwa wakiyapigania kwa muda mrefu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

MHE. YAHAYA O. MASSARE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naanza kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri na pili, naunga mkono hoja. Napenda kujielekeza katika ujenzi wa Mahakama ya Mwanzo hasa katika halmashauri mpya kama ilivyo Halmashauri yangu ya Itigi. Pia, kuna upungufu mkubwa wa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo na hata watumishi katika mahakama hizi. Nashauri Wizara yake iajiri Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo na hasa vijiji, kama ilivyo Jimbo langu la Manyoni Magharibi. Halmashauri za Wilaya zina hadhi sawa na wilaya ya kiserikali, hivyo zipewe hadhi ya kuwa na Mahakama za Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri alitazame Jimbo langu la Manyoni Magharibi kwa jicho la kipekee katika ujenzi wa Mahakama za Mwanzo kwani, zilizopo ni chakavu na hazina hadhi, kama ilivyo Wizara yako ilivyo na heshima kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na narudia tena naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. VEDASTUS M. MANYINYI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri nakupongeza kwa hotuba yako nzuri, nami naunga mkono hoja. Pamoja na pongezi hizo napenda kupata ufanuzi mdogo, mwaka jana Jaji Mkuu alipokwenda Musoma pamoja na shida mbalimbali na hoja zilizotolewa mbele ya Jaji, moja ilikuwa posho za Wazee wa Baraza kulipwa 5,000/= kwa kesi, vilevile kucheleweshwa malipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jaji Mkuu aliwaahidi wale Wazee wa Baraza kulipwa 10,000/= badala ya 5,000/=. Mpaka sasa wale Wazee wa Baraza wanalipwa 5,000/= na cha ajabu toka mwaka jana mwezi Septemba hawajalipwa hadi leo. Mheshimiwa Waziri, ikumbukwe kwamba, wazee hawa wanakwenda Mahakamani tangu asubuhi hadi mchana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufanuzi na majibu ya maslahi ya wazee hawa. Ahsante na naomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, sasa nitamwita Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa muda wa dakika ishirini watagawana na mtoa hoja ili mtoa hoja atumie dakika arobaini. Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kunipatia fursa hii ili nami niweze kuchangia. Kubwa nakushukuru kwa jinsi ulivyoongoza Bunge lako Tukufu asubuhi kwenye sala ama dua. Wabunge tuna tabia tunapofika hapa asubuhi shughuli zetu kabla hazijaanza tunaanza na sala au dua. Unapotafakari maneno mazuri yaliyopo kwenye ile sala hakika huwezi kuamini kwamba baada ya muda mfupi tu ule tunaweza kusahau *commitment* yetu kwa Mungu tukaanza ku-behave kama watu ambao hatukutambua mamlaka ya Mungu tunayemwomba kila siku. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa fursa ya kuchangia hapa na aendelee

kutukuzwa sana. Pia nimshukuru Waziri na kumpongeza Mheshimiwa Profesa Kabudi kwa hotoba hii nzuri ya bajeti yake ambayo naiunga mkono. Kusema kweli imezungumza mambo ya msingi ambayo yanalihusu Taifa hili. Kwa sababu hiyo, naungana nawe Mwenyekiti kwa ushauri wako ulioutoa mbele ya Bunge lako Tukufu muda mfupi uliopita kwamba hotuba hii imesheheneza mambo ya msingi kwa mustakabali wa Taifa hili. Laiti Wabunge tungeelekeza michango yetu kwenye mambo mazuri yanayosimamiwa na Wizara ya Katiba basi tungeweza kuishauri Serikali vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kitu ambacho napenda kusema hapa kwamba Bunge kama Bunge tunapaswa tutambue wajibu wetu. Wakati fulani huwa nakaa hapa nasikiliza sana kwa makini, lakini hatuwezi kuligeuza Bunge hili kuwa sehemu ya burudani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mambo ya msingi yanazungumzwa kwa mustakabali wa Taifa hili halafu baadhi yetu tunageuza Bunge hili kuwa sehemu ya burudani na watu wengine wanaleta sauti za wanyama kama ulivyosema fisi, wakati fulani najiuliza mimi kama Mshauri wa Sheria wa Serikali hii hivi tutumie Sheria ya Afya ya Akili? Maana tunayo Sheria ya Afya ya Akili ambayo tunaweza kuitumia kuangalia kama baadhi yetu akili zetu ziko sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mtu ambaye akili yake iko sawa na anashiriki mjadala kuna namna ya kushughulika na mjadala, mjadala ama ni kwa kuzungumza au kwa maandishi lakini siyo kwa kuzomea au kwa kupiga kelele. Unapofika hatua hiyo katika mjadala sisi ambao tumeshiriki sana kwenye mjadala, mimi nilikuwa Mwenyekiti *debating clubshulen*, ujue huyu mtu ameishiwa hoja za msingi na kwenye hotuba kama hii hamkupaswa kuishiwa hoja za msingi yapo mambo mengi ambayo yalipaswa yazingatiwe.

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimishiwa Mwenyekiti, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

pamoja na mambo mengine inataja mihimili mitatu ya dola na mgawanyo wake katika Ibara ya 4; Bunge linatunga sheria, Mahakama inatafsiri sheria na kutoa haki na Serikali inasimamia utekelezaji wa sheria. Sasa humu ndani yamezungumzwa mambo ambayo mengine yameingilia kwenye mihimili mingine kwa mfano yale mambo ambayo yako Mahakamani, hayo hayapaswi kuletwa hapa Bungeni. Moja, yamezungumzwa hapa mambo ya kesi ambazo ziko Mahakamani.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Zipi?

MBUNGE FULANI: Usimjibu Msigwa.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Huyu Msemaji wa Kambi ya Upinzani yeye mwenyewe ana kesi nne Mahakamani analeta hoja hapa kuhusu mambo ya Mahakamani. (*Makofii*)

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Godbless Lema ana kesi mbili Mahakamani. Hawa ambao wanashaktiwa kwa sababu ya kukiuka Sheria ya Makosa ya Mitandao wana kesi Mahakamani. Kwa hiyo, mambo yote haya ambayo yako Mahakamani tuyaachie mhimili wa Mahakama iyashughulikie. Bunge haliwezi kugeuka kuwa ndiyo mtunga sheria, Jaji na Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kuna tuhuma, Bunge linapotunga sheria hapa maana yake zifanyiwe kazi. Bunge hili lilitunga Sheria ya *Cyber Crimes Act, Electronic Transactions Act* na sheria chungu nzima, kama wapo watu ambao wamekiuka zile sheria, Serikali iliopewa jukumu la kusimamia utekelezaji wa sheria lazima ichukue hatua ipasavyo. Watu hawa wanaposhtakiwa Serikali isichukuliwe kwamba ni dikteta au inanyanyasa, ndiyo wajibu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kushauri, katika hotuba hizi zote na michango yote hii yale mambo ambayo

yako Mahakamani Kiti chako kisiyatilie maanani na wananchi wayapuuze kwa sababu upo mhimili mahsus i kwa ajili hiyo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Subira Sungura amezungumza juu ya utata wa umri wa mtoto wa kike kuolewa. Hili pia limezungumzwa na Mheshimiwa Kiteto Koshuma, ni hoja za msingi sana lakini Serikali imekuwa ikichukua hatua. Jana Waziri wa Katiba na Sheria alizungumza na atazungumza lakini suala hili jinsi liliivyo Serikali imeshachukua hatua. Moja, kuna kesi Mahakamani. Kwa hiyo, kwa vile kuna kesi iko Mahakamani Kanuni zetu na Katiba vinakataza tusiyazungumze haya humu ndani jamani. Tuna *prejudice* Mahakama. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katiba hii Ibara ya 30(2)(d) inasema kwamba:-

"Kulinda sifa, haki na uhuru wa watu wengine au maisha binafsi ya watu wanaohusika katika mashauri mahakamani; kuzuia kutoa habari za siri; kutunza heshima, mamlaka na uhuru wa mahakama".

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, pamoja na michango yao mizuri kuhusu huu utata wa umri wa kuolewa kwa sababu kuna kesi Mahakamani, naomba kulishauri Bunge lako Tukufu Wabunge wavute subira, tuiachie fursa Mahakama, Mahakama itaamua, tuishie tu pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mimba za utotoni pia Serikali imeshachukua hatua. Kwanza, kuna Sheria ya Kanuni ya Adhabu ambayo inapiga marufuku mtu kujamiana na mtoto wa kike ambaye yuko chini ya umri wa miaka 18. Ukifanya kitendo hicho basi unakuwa umetenda kosa la kubaka na adhabu yake ni miaka 30 na kama yuko chini ya miaka 12 ni kifungo cha maisha.

MBUNGE FULANI: Uwiiii.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tumerekebisha Sheria ya Elimu kama alivyosema Mheshimiwa Koshuma, mwaka 2016 hapa, tukaweka kwenye kifungu cha 60A kwamba ikawa ni marufuku mtu kuoa au kuolewa na mwanafunzi au kuozesha au kwa namna yoyote kumfanya mwanafunzi aache kusoma, ni kosa la jinai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi ya hapo, tuliwapa jukumu wakuu wa shule kwamba kila robo wawe wanatoa taarifa za *incidences case* za ndoa, za utoro kwa Afisa Elimu wa Wilaya. Kwa hiyo, Serikali kama Serikali imechukua hatua za kisheria. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, licha ya hilo, Serikali pia imechukua hatua za kisera, moja, imejenga sekondari za Kata kila sehemu; sekondari nyingine zipo mpaka vijijini. Pia ikaifanya elimu hii ya msingi mpaka sekondari kuwa bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ukingo ule uliowekwa unamwezesha huyu mtoto asome. Ni wakati gani anapata umri wa kuolewa? Polisi hawezি kuwa kila wakati, lakini Sheria ya Mtoto (*The Law of the Child, 2009*) kifungu cha (8) na (9) kinatoa jukumu kwa mzazi kuhakikisha kwamba mtoto wake anapata elimu. (*Makof*)

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waitara kaa chini.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa kuwa Serikali imeweka sera hizi za elimu bure, imejenga shule, imetunga sheria, ombi langu kwa wazazi sisi, tuipe Serikali ushirikiano ili tuisimamie hii sheria na watoto wetu wapate elimu. Kwa hiyo, wazazi tuna jukumu hilo la msingi sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Sabreena Sungura amezungumzia juu ya Serikali... (*Kicheko/Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza masuala ya kidini, Waheshimiwa Wabunge hatuwezi kutumia Bunge hili kuleta mtafaruku wa kijamii kwa kutumia Bunge hili kuwafanya watu ambao ni ndugu wasielewane. Unapozungumza, unailaumu BAKWATA hapa, sasa unatambua taasisi gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katiba yetu Ibara ya 19 inasema, masuala ya kidini na ya imani hayawezi kuingiliwa na Serikali. Eeh, hatuwezi kwenda huko. Katiba iko wazi, kama kuna mgogoro uende kwa Kabidhi Wasii Mkuu, ndivyo sheria zinavyosema. Hamwezi kutumia Bunge hili kupanda mbegu za chuki kwa wananchi wa Tanzania. *We cannot allow this. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninashangaa hata mnayoyaleta humu ndani, nawe Mheshimiwa Kubenea, unajua vitu vinazungumzwa hapa, ngoja nianze kuwashauri. Hili la Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam lazima tuheshimu Sheria na Katiba tulizozitunga.

WABUNGE FULANI: Aaaaah!

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo sheria hapa, inaitwa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma. Sheria hii inatoa fursa kwa sisi viongozi wa umma tunaokiuka kushitakiwa kule. Meya wa Ubungo amefungua kesi dhidi ya huyo *RC*, iko pale. Kwa hiyo, tusiwe na haraka. Mnayoiharakisha, mnaiharibu.

WABUNGE FULANI: Aaaaah!

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mnataka Mheshimiwa Rais achukue hatua gani dhidi ya huyu mtu wakati tayari iko kwenye mamlaka nydingine inashughulikiwa? Ile Tume ikiona kuna mambo ya jinai, itapendekeza, kwa sababu ina mamlaka mle ya kupeleka *PCCB*, kupeleka polisi. Eeh, msiwahishe hivi vitu. Mnajua mkiingilia hizi kesi Mahakamani, mnaziharibu. Sisi tunaoendesha kesi, kuna kitu kinaitwa *mis-trial*; na mimi naende kule tunasema bwana umeshahukumiwa, hiyo kesi

unaiharibu. Kwa hiyo, isije ikawa ni mikakati ya kuharibu hizi kesi. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, vuteni subira. Utawala wa Sheria mnaoutaka ni lazima mzingatie hamwezi kuwa mnaisema Serikali tu, na ninyi hamtaki kuizingatia hiyo kitu. Kwa hiyo, *RC* anayo mamlaka yake ya uteuzi na sasa hivi sjuij ametuhumiwa amevunja, amepelekwa kwenye hiyo Sekretariati. *Let us be patient*, hatuwezi kuwa tunahukumu tu hivi hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, aaah, Mheshimiwa Shahari amezungumza hili la mashehe. Hili suala liko mahakamani na ni ushauri wangu tu ni kwamba tuliache Mahakama ichukue hatua. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wetu sisi tutajitahidi kuharakisha uendeshaji wa kesi hii, ama upelelezi ukamilike mapema hatima yake ijulikane, lakini hili siyo jambo la kuzungumzia humu ndani, unajua masuala ya kuzungumzia kesi zilizopo Mahakamani, mnaziharibu halafu mnaingilia uhuru wa Mahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ya Mheshimiwa Maige na Muswada binafsi tuliupokea ule Muswada unashughulikiwa na Serikali. Kwa wakati muafaka atashirikishwa, kwa hiyo naomba Mheshimiwa Maige uwe na subira. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Ester Mmasi ametushauri vizuri sana Serikali. Ushauri wa Mheshimiwa Mmasi ni mzuri sana, kuna kila sababu ya sisi Serikali kuchukua mambo mazuri anayoyatoa pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ambacho naweza kuahidi, moja, tunachoweza kufanya, Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini atazungumza wakati wa Bajeti yake, kuna umuhimu wa kuirekebisha ile sheria ili nako tuweke fursa *local content* kwa maana ambayo itazingatia ajira, fursa nyingine, *goods and services* na kadhalika; na hapa Watanzania anaowazungumza watapata hizo fursa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siwezi kwenda kwa undani, lakini ninachoweza kusema ni kwamba ni ushauri mzuri, Serikali itautafakari na muda muafaka Waheshimiwa Wabunge mtaona matokeo yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli niseme tu kwamba Mheshimiwa Mchengerwa ambaye pia ni Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria amelisaidia sana Bunge hili. Kwa hiyo, sisi kwa upande wetu tumeunga mkono mchango wake katika hili na tuseme tu kwamba kama Wabunge wote mkiwa mnatoa michango ya aina hii ingetusaidia sana. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba, haya mambo ya kuzungumza viongozi wa mahakama yakome. Kambi yenu ya Upinzani na hasa Msemaji wenu wa Upinzani ana tabia sana ya kuwasema Majaji Wakuu. (*Makofi*)

WABUNGE FULANI: Ndiyo.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tumekuwa hapa kwenye Bunge, kila akiwemo Jaji Mkuu, alikuwa anamshambulia sana Jaji Mohamed Chande amekuja huyu, naye anamshambulia tu. Sasa uliwha kuona anaingia humu ndani? Kwa hiyo, acheni. Wananchi, muwapuuze hawa watu. Huyo anayekaimu ana mamlaka sawa na Jaji mwenyewe *In full*. Ndivyo tafsiri ya sheria inavyosema na wananchi waendelee kuwa na imani na mahakama yao. Hakuna kitu chochote kinachovurugwa. Kama ni mashauri waende mahakamani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine la ushauri, tuzingatie sana sheria. Haiwezekani Serikali ambayo imepewa jukumu la kusimamia utekelezaji wa Sheria, inapochukua hatua za kusimamia zile sheria mliozitunga ninyi wenyewe, mnasema hii ni Serikali ya kidikiteta, haiwezekani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, unavunja sheria, unashitakiwa. Huwezi kushitakiwa halafu ukasema ni dikiteta. Mwalimu Nyerere alisema hivi, Serikali ni sheria. Hakuna kitu

kinaitwa Serikali bila sheria na sheria zikishatungwa ni lazima zifuatwe. Ndiyo msingi wa utawala wa sheria mnaousema Mheshimiwa Shahari na ndiyo msingi wa lbara ya 26 ya Katiba ya nchi yetu inayotaka kila mtu kuzingatia Katiba na sheria za nchi hii. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hapa hakuna cha dikteta. Nchi hii inaongozwa kwa demokrasia na taasisi zake zote za kidola likiwemo Bunge, Mahakama na *Executive*, vinafanya kazi kwa ufanisi; na Ma-Rais walioko madarakani, wameingia madarakani kidemokrasia kwa Uchaguzi Mkuu. Eeh, Mheshimiwa Rais Magufuli na Mheshimiwa Rais Shein, wala hapa hakuna cha Udikteta. (*Makof*)

(*Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio*)

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ile ya kubadilisha Mawaziri na yenewe ni kitu cha kawaida. Mheshimiwa Rais amepewa mamlaka ya kuteua Mawaziri wake na hatukuweka sheria ya ukomo kwamba huyu ata-serve kwa muda fulani na akimbadilisha anampeleka Wizara fulani. Msianze kuwatisha viongozi. (*Makof*)

Mazingira hayo mnayo jenga kwenye jamii ya watu kwamba kuna hofu imetanda, mwache. Kwa sababu huko nyuma mliwahi kusema kwamba mtaifanya Serikali isitawalike, haiwezekani. Mliwahi kusema mtafanya nchi isitawalike, haiwezekani. Wakati ule mllichukua vitendo, sasa mnaleta hoja kwamba hofu hofu, wakati mambo yanaendelea hapa. Shughuli zote za kijamii, kiuchumi, kisiasa zinaendelea kama kawaida, halafu mnasema eti kwamba kuna hofu. Haya lazima tuyapuuze. (*Makof/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia kushauri, haya mambo yote ambayo yametajwa hapa kwamba kesi sijui na vitu gani, haiwezekani ninyi mnashabikia wengine washitakiwe, ninyi mkshtakiwa mnasema sijui tunaonewa. *That cannot be the case.* Kesi nytingine mnayosema walifikishwa mahakamani wakaachiwa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa
muda wa Mzungumzaji)*

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa mchango wako mzuri, umetuelimisha, tunakushukuru sana. (*Makofi*)

Tunaendelea, sasa namwita mtoa hoja ahitimishe hoja yake, Mheshimiwa Profesa Kabudi, Waziri wa Katiba na Sheria na muda wako ni dakika zisizozidi 40.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kutoa hotuba yangu leo asubuhi na kuwawezesha Waheshimiwa Wabunge kuchangia hotuba ya Wizara yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee, nachukua fursa hii kukushukuru wewe binafsi, kwanza kwa mchango wako mkubwa kwangu katika taaluma ya sheria. Mimi na Dkt. Harrison George Mwakyembe baada ya kuhitimu Shahada ya Sheria wakati wa mafunzo ya sheria, tukiwa *State Attorney grade III* Mheshimiwa Chenge ulikuwa Mkurugenzi wa Mambo ya Kimataifa na ultusaidia sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru pia, kwa miaka mitano niliyoazimwa katika Ofisi ya Makamu wa Rais kushughulikia mambo ya mazingira, ambapo tulifika tukatunga Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004, wewe ulikuwa msaada kwangu sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka, naomba niliseme ndani ya Bunge hili, kazi ya Muswada ule haikuwa rahisi, ilinizulia watu wengi na maadui wengi, wengine walioona husuda ya fedha niliyolipwa; na wengine ambaao hawakuelewa kwa nini sheria ile itungwe. Kwenye kikao kimoja unakumbuka nilitolewa kwa hali iliyokuwa

haikunifurahisha. Hata hivyo, wewe uliniambia jambo moja na leo nataka niliseme; "*In public service, learn to swallow your pride. In public service learn to suppress your eagle.*" Kweli mambo hayo sasa naona umuhimu wake ndani ya jengo hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa George Masaju, Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ushirikiano alionipa katika kutekeleza majukumu yangu na kwa kuungana na mimi katika kujibu baadhi ya hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mara nyingine, naishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge la Katiba, Sheria na Utawala pamoja na Kamati ya Bajeti kwa maoni na ushauri wao ambao wameipatia Wizara na Taasisi zake katika kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizihakikishie Kamati na Waheshimiwa Wabunge wote kuwa tumepokea maoni, hoja na ushauri mliotupa katika mjadala wa Bajeti yetu na tunaahidi kufanya kazi masuala yote yaliyojitekeza katika mjadala huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Kambi ya Upinzani, nashukuru pia kwa maoni yenu yaliyotolewa na kukubaliwa na Bunge hili kutoka kwa Msemaji wa Kambi ya Upinzani wa mambo ya Katiba na Sheria; ni mdogo wangu, kaka yake Mheshimiwa Tundu Lissu, Ndugu Alute Mughwai na mimi tumesoma pamoja Milambo. Kwa sababu hayupo, sipendi kuleta mambo ya mila hapa ndani, lakini wale wote tunaotoka Singida mnajua mila yetu na heshima kwa watu, eeh, kwa neno lililokataliwa jana, waliotangulia kwa ngariba kabla ya wewe. (*Makofi/Kicheko*)

Mhesimiwa Mwenyekiti, niseme hili, nimeshangaa sana kuwa watu katika jengo hili kubagazana. Waheshimiwa Wabunge kama ni kawaida, ni kawaida mbaya. Hatuwezi kubagazana. Jengo hili siyo la kubagazana; na tunabagazana kwa sababu kwa bahati mbaya tumepoteza

pia uelewa mzuri wa lugha ya Kiswahili. Tunazungumza Kiswahili kikavu kama alivyosema Mheshimiwa, Riziki Shahari Mngwali, tumepteza uelewa wa Kiswahili wa kutumia lugha ya kumfanya mtu mpuuzi ajue ni mpuuzi bila kumwambia mpuuzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ukimsikia muingereza anakwambia *your stupid*, siyo muingereza. Muingereza mstaarabu ndani ya Bunge, atakwambia *I am sorry, your level of appreciation of issues is diminishing, which means you are stupid!* Yes. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ugeni una faida wa kusema mambo ambayo hayakfurahishi. Nimefundisha wanasheria, na mimi nimefundishwa. Mwanasheria yejote *worth being called a lawyer, he must have sense of respect and more so, as officer of the court to the judiciary.* Ndiyo maana naanza kuelewa kwa nini nchi nyininge Bajeti ya Mahakama hailetwi Bungeni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mionganoni mwa vitu ambavyo vinanisumbua na nilisema siku ya hotuba ya Mheshimiwa Mboge na ninamheshimu sana kwa *maturity* yake, niliomba *tusii-drag judiciary in our mucky politics. It is abominable! It is flabbergasting!* Tusii-drag Mahakama katika mazungumzo yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nitaanza na suala la uteuzi wa Majaji, ikiwa ni pamoja na Jaji Mkuu na naomba mnisikilize; na kama hamniheshimu kwa umri wangu, *I am above 60, mniheshimu kwa utu wangu.* (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua nafasi ya Rais inagombewa, anachaguliwa...

MBUNGE FULANI: Kama Wabunge. (*Makofi*)

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nafasi ambayo ndiye mkuu wa nchi, naomba mnisikilize.

MWENYEKITI: Waheshimiwa pale, Mheshimiwa Msigwa, nawaombeni sana jamani. Nawaombeni sana.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nafasi ya Rais tunayempigia kura, Rais wa Tanzania, Rais wa *South Africa* hapigiwi kura, anachaguliwa na Wabunge kama alivyo Waziri Mkuu. Ndiyo maana *South Africa* chama ni juu. Rais Zuma, chama kinaweza kikamwondoa leo, ndiyo kama kilivyomwondoa Mbeki. Hapigiwi kura. Lakini Rais wa Jamhuri ya Muungano Tanzania, anapigiwa kura. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Spika wa Bunge, anapigiwa kura. Mtu pekee wa mhimili ambaye hapigiwi kura, anateuliwa, ni Jaji Mkuu. Mnajua kwa nini?

WABUNGE FULANI: Hatujui.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Ni msingi wa kuhakikisha mtu huyu anayeteuliwa kushika nafasi hiyo, aachwe bila laumu ya mpumbavu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme hivi, katika uteuzi wa Jaji, nafasi ya Jaji katika hilli, kwanza siyo kweli kwamba hapajawahi kuwa na Kaimu Jaji Mkuu kwa kipindi. Mara baada ya Jaji wa mwisho wa Tanzania, muingereza Windham kumaliza muda wake, Tanzania 1965, Mwalimu hakuona sababu ya kuwa tena na Jaji Mzungu. Ndipo jitihada zilanza za kutafuta Jaji mwafrika na huyo Jaji alipatikana kutoka nchi ya *Trinidad and Tobago* Telford Philip Georgies. Illichukua muda kwa sababu Majaji walikuwa wanasita kuja kwa sababu ya elimu ya watoto wao. Ni mwafrika, tena alikuwa mweusi kuliko wewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mionganoni mwa vitu nawasifu waafrika, wamekaa kule miaka 500, wengine ni weusi kuliko sisi; na ni Waafrika kuliko sisi kwa sababu wameishi ugenini. Ndipo nafasi ile ilikaa kwa kipindi kirefu ikisubiri Jaji Telford Philip Georgies afike nchini aapishwe. *These are facts. (Makof!)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, alichaguliwa mwingine akaimu kwa sababu daima nafasi ya Jaji Mkuu haiwezi kuwa wazi hata kwa dakika moja. Ndiyo maana hata Jaji Mkuu akisafiri, akiteuliwa mwingine kukaimu, anaapishwa. Hakuna Kaimu Jaji Mkuu ambaye haapishwi, hata kama atakuwa Kaimu Jaji Mkuu kwa siku mbili, ataapishwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ukiangalia Katiba, iko wazi kabisa, inamruhusu Rais kuteua Kaimu Jaji Mkuu na haiweki mipaka. Haiweki, haiweki. Ukienda kwenye Katiba mpaka mwaka 2000 wakati Mwenyekiti akiwa *Attorney General* kabla ya hii 2005 kufanya marekebisho kupunguza maneno, niwasomee tafsiri ya Jaji Mkuu ilikuwa inasemaje. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jaji Mkuu maana yake ni Jaji Mkuu wa Mahakama ya Rufani aliyetajwa katika Ibara 115(1) ambayo sasa ni 118 ya Ibara hii, ambaye ameteuliwa kwa mujibu wa masharti ya Ibara ndogo ya pili ya Ibara hiyo ya 118 au iwapo Jaji Mkuu hayupo au anashindwa kutekeleza kazi zake kwa sababu yoyote, Kaimu Jaji Mkuu aliyeulewa kwa mujibu wa masharti ya Ibara 118(4) ya Katiba hii na Kaimu Jaji Mkuu naye hayupo au anashindwa kutekeleza kazi yake, Jaji Mkuu, Jaji wa Mahakama ya Rufani aliyeo kazini kwa wakati huo na ambaye yuko kwenye daraja la juu zaidi la madaraka kuitia Majaji wote wa Mahakama waliopo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiisoma ya sasa inaeleza wazi kabisa Jaji Mkuu ni nani, maana yake ni Jaji Mkuu anayetajwa kuteuliwa na ambaye majukumu yake yameelekezwa katika Ibara ya 118 ya Katiba. Ukiisoma hiyo ni pamoja na Kaimu Jaji Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake nini? Watu wengine wote wanaoteuliwa kukaimu, hawaapishwi. Ni Jaji Mkuu tu. Kaimu Jaji Mkuu anaapishwa, peke yake. Maana yake, kitendo cha kumwapisha kinampa mamlaka na ulinzi kamili wa cheo hicho. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uteuzi wa Jaji Mkuu, mimi nalisihu Bunge liheshimu Mamlaka ya Uteuzi. Rais anayo mamlaka kamili ya uteuzi na Rais anavyo vigezo vingi vya uteuzi na Rais msidhani ni mtu anayetembea, ni taasisi. Hivyo, kwa sababu ni taasisi, haina macho mawili tu, ina zaidi ya macho mawili, tuiache ifanye kazi yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwasihisana Waheshimiwa Wabunge, tuache Kaimu Jaji Mkuu afanye kazi yake. Tusimfikishe mahali tukamtweza. Kwa sisi wanasheria, tuheshimu sana mhimili huo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo napenda nilzungumzie ni kuhusu Rais. Ndiyo maana dada yangu Mheshimiwa Riziki Shahari Mngwali ametoa, ni kweli alichokisema. Kwenye Tume ya Mabadiliko ya Katiba tulikuwa na Kamati tatu; Kamati ya Maadili na Hakiza Binadamu chini ya Mzee Ussi, Mwenyekiti; Kamati ya Muungano, chini ya Mzee Butiku, Mwenyekiti na Kamati ya Mihimili, mimi nikiwa Mwenyekiti. Watu walionisaidia sana, nikiri ni Kibibi Mwinyi Hassan kutoka Unguja, Zanzibar na Mheshimiwa Riziki Shahari Mngwali kutoka Tanzania Bara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa kuzunguka kule tulikuta nafasi ya Rais watu hawailewi. Nimekuja na maoni hapa na mengine nimeyaacha. Watu hawailewi nafasi ya Rais, yaani kama kuna nafasi ilikuwa inazungumzwa mpaka tunashtuka, ni nafasi ya Rais, mpaka tukajiliza hawa Watanzania kwa nini nafasi hii hawailewi? Tukabaini, tunachanganya mambo mengi katika nafasi ya Rais. Ndiyo maana tukasema, ni vyema tukapambanua tuelewe nafasi ya Rais na Rais ni nani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais anazo nafasi tatu; moja, ni Mkuu wa Nchi (*Head of State*); pili, ni Kiongozi wa Serikali na tatu ni Amiri Jeshi Mkuu. Sasa yako madaraka ya nafasi ya Rais kama Mkuu wa Nchi na kama Amiri Jeshi Mkuu yanayompa hadhi tofauti ambayo haistahili kubezwa na ndiyo maana Bunge kwa Kanuni limezuia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, Rais ni taswira ya nchi. Kwa nafasi yake ya Mkuu wa Nchi Rais ni taswira ya nchi. Malkia wa Uingereza kwa nafasi yake ya ukuu wa nchi, ni taswira ya nchi (*Head of State*). Kwa maana hiyo, ye ye ndio alama ya umoja, ye ye ndio alama ya uhuru wa nchi na mamlaka yake. Kumuonesha kwamba ye ye ni alama ya uhuru wa nchi, ndio maana Rais peke yake ana fuatana na mtu ambaye tumezoea kumwita mpambwe, ambaye amevaa mavazi ya kijeshi. Maana yake ni kwamba anawaonyesha kwamba huyu ndiye alama ya Serikali yenu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu hiyo Rais ana dhamana ya kukuza na kuhifadhi umoja wa kitaifa, ana dhamana hiyo. Sasa ukiangalia madaraka ya Mkuu wa Nchi, yale huwezi kuyapunguza; lakini ukiangalia mamlaka yake ya Amiri Jeshi Mkuu, huwezi kuyapunguza na ukiangalia mamlaka yake kama Mkuu wa Serikali, kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania majukumu ya Rais kama Mkuu wa Serikali, akiwa Mkuu wa Serikali, hayo unaweza kuyapunguza. Unaweza kuyasimamia, unaweza kuyadhibiti. (*Makofii*)

Mdogo wangu Tundu Lissu asubuhi ame eleza zile makala ya mimi na Mlimuka na ya Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe tulioandika wakati wa mfumo wa chama kimoja, tena tukielekea mabadiliko makubwa ya Katiba ya mwaka 1985. Niseme hivi, mwaka 1985 hii Katiba, Mzee Chenge yuko hapa, kwa maudhui hii siyo Katiba ya mwaka 1977, ni Katiba ya mwaka 1985. Iliandikwa yote upya. Kwa nini ilitwa Katiba ya mwaka 1977, ni kwa sababu *The Constituent Assembly* haikuwa convened. (*Kicheko*)

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)

MWENYEKITI: Waheshimiwa tuheshimiane tu!

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa sababu *Constituent Assembly* haikuwa convened na kwa nini Mwalimu haku-convene *Constituent Assembly*? Mimi na Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe...

MBUNGE FULANI: Tulieni mfundishwe! (*Kicheko/Makofi*)

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni kwa sababu wapo watu wanaoamini *the Constituent Assembly is only convened once. Only convened once.* Ndiyo maana nilipokuwa amidi, Kiswahili cha dini ni amidi. Nilipokuwa amidi wa Shule Kuu ya Sheria, nimeanzisha course mpya ya *Legal History* na nimeifundisha mwenyewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nilianza *course* ya *Legal History*? Ni kwa sababu niligundua vijana wetu wengi wanaidhani Tanzania ni hii ilivyo leo. Hii ilivyo leo haikuwa hivi. Kabla ya mabadiliko yale, Bunge hili Wabunge wengi humu ndani walikuwa ni wa kuteuliwa na siyo wa kuchaguliwa, ndiyo! Tena nina fahari sana ya kuwa Mbunge wa Kuteuliwa, ndiyo. (*Kicheko/Makofi*)

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Bora wewe umeteuliwa kwa akili.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nitawaambia kuwa sisi wasomi hakuna *Doctorate unayoiheshimu kama Honorary (Honoris Causa)*, ndiyo. Unapokuwa *Doctor Honoris Causa*, tena ukiwa multi...

MBUNGE FULANI: Hebu ingia kwenye kampeni kama...

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Shauri yako, sikukutuma. (*Kicheko/Makofi*)

Wewe umejituma mwenyewe. Kwa hiyo, wakati huo Waziri Mkuu yuko hapa hakuwa Mbunge wa kuchaguliwa, walikuwa ni Wabunge wa kuteuliwa. Ndiyo. (*Makofi*)

MBUNGE FULANI: Wape sumu hao.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati huo, Bunge lilikuwa ni Kamati ya

Halmashauri Kuu ya Chama. Sasa mtu asijejua historia atabeza mafanikio yaliyofikiwa. (*Makofi*)

MBUNGE FULANI: Tango pori eeh.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Ndiyo maana Wangazija wana msemo, ukitaka kujua mafanikio ya mtu usiangalie kimo alichofika, angalia shimo alikotokea. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme mara baada ya kile kitabu kutoka, ndugu yangu Mheshimiwa Dkt. Harrison George Mwakyembe yupo, wako Mabalazi waliodhani Mwalimu angetutia kizuizini, yuko hapa. Leo ninyi mnaongea Sheria ya Kizuizini hayupo! Tuliongea wakati yupo. *Don't dare me, don't dare me. We spoke when the law was law and when the President was President.* (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ndiyo maana Katiba hii kwa mapendekezo ya wakati huo Mwalimu anaondoka ilikubaliwa kabisa, lazima madaraka ya Rais yapunguzwe. Someni mapendekezo ya Halmashauri Kuu ya Taifa ya mwaka 1983/1984 na yalipunguzwaje? Moja ya kuyapunguza ilikuwa ni kuanzisha cheo cha Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Uwaziri Mkuu wetu huu, siyo kama wa Uingereza, huu ni kama wa Ufaransa. Kwa sababu ni kama wa Ufaransa ambapo Mzee Joseph Sinde Warioba alitumwa kwenda kujifunza, Mzee Msekwa alitumwa India na Canada, Waziri Mkuu wetu huyu mjisoma Katiba anatokana na chama chenye Wabunge wengi na anapigiwa kura ndani ya Bunge. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, aina hii ya Katiba yetu ambayo una Mkuu wa Nchi ambaye amechauguliwa na wananchi moja kwa moja, siyo kama wa Afrika Kusini na una Waziri Mkuu anayetokana na chama chenye Wabunge wengi au anayeungwa mkono na wengi, kinaweza kukupa aina ya *government* inayoitwa kwa Kifaransa *kohavision*.

MBUNGE FULANI: Eeh!

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna hiyo, madaraka ya Rais yakawa yamepunguzwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili kubwa liliolofanyika mwaka huo, ilikuwa ni kuweka ukomo wa Rais. Mwalimu alitawala kama Rais miaka 23, anaondoka madarakani sisi ilikuwa ndiyo nchi ya kwanza Barani Afrika kuweka ukomo wa Rais kuwa ni vipindi vivili nya miaka mitano mitano. Eeh, kule Cameroon, Rais Ahidjo; Wafaransa walipomchoka Rais Ahidjo, wakamwambia anaumwa; alipoondoka akagundua haumwi, hawezি kurudi. Rais Séder Senghor wa Senegal alikuwa ndiye Rais wa pili kung'atuka na yeye kuweka *term limit*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu muhimu ndani ya Katiba hii, ilikuwa ni kuweka sura ya haki za binadamu. Hazikuwepo wakati huo, hazikuwepo. Ndizo hizo leo, Ibara ya 12 mpaka ya 29, hazikuwemo. Hayo ndiyo maendeleo na mapito ambayo nchi hii imeyapitia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mabadiliko ya mwaka 2005 kuhusu haki za binadamu, yaliyondoa *clawback clauses* zote. Tena yalikwenda mbali, hayakuondoa tu *clawback clauses*, yaliondoa hata *enabling clauses*.

MBUNGE FULANI: Muda unaisha.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Acha uishe. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninachotaka kusema katika mambo ya Katiba, eeh, *lecture room*, kwa sababu Waswahili wana msemo, mwana wa muhunzi asiposana hufukuta. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ndugu zangu, tumefika hapa tulipofika kwa sababu nchi hii imejaliwa

kuchukua maamuzi kwa wakati, lakini maamuzi hayo ni lazima yajenge umoja wa Taifa, maamuzi hayo ni lazima yajenge mshikamano, ni lazima yajenge utu, ni lazima yalenge ustawi wa watu. Ndiyo maana katika Katiba hii kama kuna Ibara naisoma kila siku, ni Ibara ya nane. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *at the bottom line* wananchi ndio source ya mamlaka yote, sio sisi. Kwa hali hiyo, nashauri sana tutunze heshima ya Rais akiwa Mkuu wa Nchi, tutunze heshima ya Rais akiwa Amiri Jeshi, lakini inapokuja kwenye nafasi ya ukoo wa Serikali, isimamiwe na ishauriwe. Hapa ndani ni kupitia kwa Waziri Mkuu na Baraza la Mawaziri liliromo humu ndani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja mbalimbali zimetolewa, jumla ya Waheshimiwa Wabunge 24 wamechangia hotuba yetu ambapo Wabunge 17 wamechangia kwa maandishi na Wabunge saba wamechangia kwa kuzungumza. Mionganini mwa mambo ambayo yamezungumzwa, yako ambayo yamegusa vyombo na mambo mbalimbali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza na hoja zilizotolewa kuhusu Mahakama; hoja kubwa iliyotolewa na Mahakama ni kuhusu ujenzi wa majengo ya Mahakama. Ujenzi wa majengo ya Mahakama Kuu, za Wilaya na za Mwanzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kueleza kwa ujumla kwamba moja ya changamoto kubwa zinazoikabili Mahakama ya Tanzania ni uhaba na uchakavu wa miundombinu. Mathalani katika ngazo ya Mahakama za Wilaya, tuna majengo katika Wilaya 30 na Wilaya nyingine huduma zinatolewa katika majengo ya kuazima kutoka taasisi nyingine za Serikali. Aidha, tuna Wilaya 23 zinapata huduma za Mahakama katika Wilaya za jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kwa upande wa Mahakama za Mwanzo kuna Mahakama 960 tu kati ya Mahakama 3,963 zilizopo nchini. Sasa katika kukabiliana na changamoto hii, Wizara kwa kushirikiana na Mahakama

imeanza kutekeleza mpango wa ujenzi katika ngazi zote za Mahakama. Kwa hiyo, kupitia mpango huo, katika kipindi cha miaka mitano tumpanga kuhakikisha kwamba mikoa yote itakuwa na majengo ya Mahakama, ndani ya miaka mitano. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika hiyo miaka mitano, imepangwa kujenga Mahakama za Wilaya 109 na Mahakama za Mwanzo 150 katika maeneo mbalimbali nchini. Kwa hiyo, kwa msingi huo ni matarajio yetu kuwa hadi mwaka 2021 Wilaya zote nchini ziwe na majengo ya Mahakama, huo ndiyo mpango. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika mpango huo yapo maeneo ambayo tunaomba msaada, moja likiwa Jimbo la Mheshimiwa John Mnyika, tusaidiwe kupata viwanja, mahali ambapo tunaweza tukajenga Mahakama na pia Wilaya nydingine. Nimetaja yako Mheshimiwa Mnyika kwa sababu nimeona umeleta mchango wako kwa maandishi na nimeu-note. Sasa tukishapata viwanja hivyo, itatusaidia sisi kuweza kujenga Mahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo limeelezwa na michango ya Waheshimiwa Wabunge wengi ni kuhusu Mahakimu wa Mahakama ya Mwanzo kukaa muda mrefu katika kituo kimoja. Sasa hili limechangiwa na gharama za uhamisho na vituo vya kuhamishwa kwa watumishi wote wa Mahakama ambao ni pamoja na Mahakimu wa Mwanzo. Gharama ya zoezi hili inakwenda takriban shilingi billioni 2.3.

Kwa hiyo, Wizara yangu kwa kuthamini kwamba ni vyema Mahakimu au Mahakama za Mwanzo wakawa wanapata uhamisho, kwa sababu kukaa mahali pamoja muda mrefu na wewe unakuwa sehemu ya ile jamii.

Kwa hiyo, tunashirikiana Wizara na Mahakama kuhakikisha kwamba tunaongea na Hazina ili kulifanya suala la upatikanaji wa fedha za uhamisho wa watumishi wakiwemo Mahakimu waliokaa kituo kimoja kwa muda mrefu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo limezungumzwa kuhusu Mahakama ni juhudzi za kuondoa mlundikano wa mashauri katika ngazi zote za Mahakama. Sasa Mahakama ya Tanzania pia imeweka muda maalum wa mashauri kuwa mahakamani. Kwa Mahakama za Hakimu Mkazi na Mahakama za Wilaya, shauri linatakiwa kukaa mahakamani kwa muda wa miezi 12. Mahakama za Mwanzo, shauri linatakiwa kukaa muda wa miezi sita tu. Kwa Mahakama za Mwanzo hazina mashauri yanayozidi miezi sita. Sasa kama ambavyo tumeeleza katika hotuba yetu na maelezo ya Mahakama, Mahakama ya Tanzania imejjiwekea mpango wa kuondoa mlundikano wa mashauri katika ngazi zote za Mahakama, iwe ni Mahakama ya Hakimu Mkazi au ya Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia katika Mahakama ya Hakimu Mkazi na Mahakama ya Wilaya zina mashauri 2,912 yanayoangukia kwenye mlundikano. Mashauri hayo yako katika Programu Maalum ya Uondoaji wa Mlundikano wa Mashauri inayoendelea nchi nzima. Nachukua fursa hii tena kuipongeza Mahakama kwa kazi kubwa waliyoifanya katika kuhakikisha kwamba kesi zote za uchaguzi wa Wabunge na Madiwani zinamalizika ndani ya muda uliopangwa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili ni la kihistoria na ni vyema tukaipongeza Mahakama, kwa sababu ni mara ya kwanza kesi za kupinga matokeo ya uchaguzi zimemalizika katika kipindi kifupi. Huko nyuma tunafahamu, mpaka kipindi cha Bunge kilikwisha kesi bado zinaendelea Mahakamani. Kwa hiyo, ni imani yangu kwangu kwamba rasilimali fedha ikiongezekwa, uhamisho wa Mahakimu utafanyika, ajira zaidi zitapatikana na majengo ya Mahakama zaidi yatajengwa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo napenda kulizungumzia ingawa Mwanasheria Mkuu wa Serikali amelizungumzia na mimi pia napenda nilizungumzie. Suala lolote linamlohusu Mtanzania ye yeyote au mtu ye yeyote kufunguliwa mashtaka na kupelekwa Mahakamani au

kuwekwa mahabusu au rumande, siyo suala ambalo mtu ye yote angelifurahia. Tungependa uhalifu usiwepo, tungependa wahalifu wasiwepo, lakini hulka ya binadamu, tunatenda makosa. Makosa yakitendeka kwa mujibu wa sheria, lazima mtu aitwe, ahojiwe, kesi ifunguliwe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimeanza na hilo, niliseme wazi. Serikali haifurahii kuona watu wako ndani. Ingetokea muujiza leo pakawa hakuna uhalifu na Magereza yakafungwa, lingekuwa ni jambo la furaha kubwa sana, lakini huo ni utashi na mapenzi ambayo ni vigumu kuyatekeleza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kama alivyosema Mwanasheria Mkuu wa Serikali, moja ya mambo ambayo yamezungumzwa sana humu ndani, ni suala la kesi inayohusu Mashehe wa Zanzibar ambao wameshitakiwa chini ya Sheria ya Kuzuia Ugaidi (*Prevention of Terrorism Act*) ambayo inatumika Tanzania Bara na Zanzibar. Sasa maadam suala hili liko mahakamani, kama alivyosema Mwanasheria Mkuu wa Serikali, sisi kazi yetu kubwa tuharakishe uchunguzi na kesi ikamilike mahakamani. Sasa uchunguzi unategemea mambo mengi ambayo pia siyo vyema kuanza kuyazungumza ndani ya Bunge hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyosema Mwanasheria Mkuu wa Serikali kufanya hivyo tutakuwa badala ya kuksaidia kesi hii, labda tukaivuruga zaidi. Kwa hiyo, naomba tuendelee kuviachia vyombo vinavyofanya shughuli hiyo pamoja na Mahakama na wachunguzi lakini kwa kadri inavyowezekana kesi hii kama kesi nyingine zozote zile imalizwe mapema iwezekanavyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo limezungumziwa na Waheshimiwa Wabunge ni suala zima la Katiba mpya. Napenda nirudie maelezo yale yaliyotolewa. Katika jambo hili niseme kama nilivyoeleza katika maelezo yangu kwenye Kamati nilipoulizwa, Serikali inatambua umuhimu wa Katiba mpya, lakini Katiba siyo kitabu hiki tu. Ziko nchi hazina katiba iliyoandikwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waingereza hawana Katiba ilioandikwa. Ukiwaliza Waingereza leo Katiba yao ni nini? Ni mila na desturi. Israel haina Katiba ilioandikwa; na kwa kuwakumbusha, Zanzibar toka mwaka 1964 baada ya Mapinduzi mpaka mwaka 1979 haikuwa na Katiba ilioandikwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo, mimi na Mheshimiwa Dkt. Harrison George Mwakyembe tutamkumbuka Mwalimu wetu wa Katiba, Profesa Srivatava aliyetuambia Katiba siyo hicho kitabu, ni ujumla wa maisha yenu yote, matamano yenu, matarajio yenu na shida zenu. Hii ambapo Waingereza wenyewe hawakuwa na Katiba ya kuandika na mpaka leo hawataki, walituandikia sisi na sijui niliseme maana yake nimekuwa Waziri, wakiamini kwamba ninyi hamna uwezo wa kuwa na mila na desturi zinazostahili kuwa Katiba. Kwa hiyo, wawaandikie. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana Katiba yetu ya uhuru ya mwaka 1961, *actually it was a schedule to an Act of Parliament which was passed by the House of Commons. The Tanganyika Order in council and accented by the Queen, not in Buckingham Palace, in St. George Chapel, Windsor.* (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, maana yake kama alivyosema dada, Mheshimiwa Riziki Shahari Mngwali, Tume ya Mabadiliko ya Katiba ilitoa siyo Rasimu tu; tuliangalia Rasimu tu na nimekutaja kwa kazi kubwa uliyofanya. Tulitoa Juzu hii, maoni ya wananchi kuhusu sera, sheria na utekelezaji, iwe sehemu ya hiyo Katiba inayoishi. Ndani ya mambo hayo, niwasomee moja tu ambalo wananchi walituambia, ni safari za viongozi, ukurasa wa 38 kwamba safari za viongozi ziwe na kikomo. (*Makof*)

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Hatujasikia Mheshimiwa.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa huyu anasafiri sana? Wakasema, malengo ya safari za nje za viongozi yawe wazi kwa wananchi. Niwaambie jambo moja walilolisema, na mimi ningetamani

liwe, matumizi ya neno mheshimiwa, mapendekezo ya wananchi. Mapendekezo ya wananchi kuhusu matumizi ya neno mheshimiwa yalikuwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, neno mheshimiwa lisitumike kwa Wabunge na viongozi wengine wa umma, badala yake neno ndugu litumike ili kuondoa matabaka na kuwakweza viongozi juu ya wananchi ambao kimsingi ndio waliowaweka madarakani. (*Makofi/Kicheko*)

MBUNGE FULANI: Tutakuwa tunaitana ndugu.

MBUNGE FULANI: Sasa unashangiliwa kila upande.

MBUNGE FULANI: Tuanzie kesho.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Iakini sehemu kubwa kama alivyosema Mheshimiwa Shahari Mngwali...

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKTI: Mheshimiwa Waziri, malizia tu.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyosema Mheshimiwa Shahari Mngwali, kitu kikubwa kilichozungumzwa na wananchi humu, ni maadili ya viongozi. Moja, wananchi walipendekeza viongozi wote wakiapishwa, waape maadili ya viongozi. Tunaapa au hatuapi?

WABUNGE FULANI: Tunaapa. (*Makofi*)

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi, mimi, mimi...

MBUNGE FULANI: Muongezee nusu saa.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kitabu hiki nitakikisha tunakipa uzito unaostahili kwa sababu ndiyo maoni ya wananchi ya Katiba inayoishi. Kwa hiyo, tayari matashi ya wananchi yameanza kutekelezwa. Ndiyo maana kwa sasa kama nilivyosema kwenye Kamati, kazi tunayoifanya ni kazi ya kuzichambua sheria, ndiyo maana haina kasma. Si ni kazi za siku zote, ndiyo maana haikutengewa fedha, kwa sababu ni kazi tunayoifanya ndani ya Serikali. Ni kazi ya kila siku, tunaangalia sheria zote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hivyo tu, nawaambia mambo makubwa kama haya hayataki shinkizo. Mambo makubwa kama haya yanataka umuombe Mwenyezi Mungu akufanye uwe mwerevu kama nyoka na mpole kama hua ili ufikie unapotaka Taifa likiwa moja. (*Makofi*)

(Hapa kengele ya pili ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi na Wabunge wametoa maoni mengi na ninataka niwahakikishie kwamba maoni yote tumeyapokea na kwa utaratibu uliopangwa na Bunge, tutahakikisha kila aliyetao hoja yake, jibu lake linapatikana kwa utaratibu uliopo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

MBUNGE FULANI: Muongezee muda.

MWENYEKITI: Ahsante. Hoja imetolewa, imeungwa mkono. Profesa tunakushukuru sana kwa mchango wako na kwa elimu uliyotoa kwa Waheshimiwa Wabunge na wananchi. Endelea hivyo. (*Makofi*)

MBUNGE FULANI: Sindano imewachoma.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaingia kwenye Kamati ya Matumizi, nachukua nafasi hii kutoa tangazo tu kwa sababu ya muda, tuna wageni hapa ambao siyo lazima wakakaa na sisi mpaka mwisho, nao ni wageni wa Mwenyekiti wa *TWPG*, Mheshimiwa Margaret Sitta ambao ni wageni kutoka Taasisi ya *Girl Guides Tanzania* wakiongozwa na Profesa Martha Qorro. Mko wapi? Msimame, simameni. Karibuni sana wageni wetu, mmejionea shughuli za Bunge la Jamhuri wa Muungano wa Tanzania. Karibuni sana. Katibu! (*Makofi*)

NDG. JOSHUA CHAMWELA – KATIBU MEZANI:

KAMATI YA MATUMIZI

MATUMIZI YA KAWAIDA

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Fungu 41 – Wizara ya Katiba na Sheria

Kif. 1001- *Admin. and HR Management...* Shs. 5,484,469,000/=

MWENYEKITI: Huo ndiyo mshahara. Ndiyo, lakini ninyi Waheshimiwa Wabunge msifikirie kwamba kwa sababu tuna utaratibu huu, eti hakuna kusimama. Shauri yenu, lazima msimame kuandika. Eeh, sawa na msije mkashangaa.

Mheshimiwa Tundu Lissu, Mheshimiwa Abdallah Ally Mtalea, Mheshimiwa Balozi Adadi Rajab, Mheshimiwa Cosato Chumi na Mheshimiwa Amina Mollel.

MHE. RICHARD P. MBOGO: Mbogo.

MWENYEKITI: Kwa uwiano wetu, kwenye eneo hili lazima nitende haki, ni matakwa ya kanuni. Tunaanza na Mheshimiwa Amina Mollel.

MHE. AMINA S. MOLLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Katika mshahara wa Mheshimiwa Waziri, mimi narejea katika Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wamezungumza mengi, vilevile Mheshimiwa Waziri amezungumza mengi pamoja na AG, lakini hili ni suala ambalo kwa kweli kwa muda mrefu Waheshimiwa Wabunge na jamii yote kwa ujumla imekuwa ikilizungumzia sana na lina madhara makubwa kwa watoto wa kike. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumemsikia Mheshimiwa Waziri jana/juzi katika mojawapo ya maswali alilielezea kwa mapana na akaelezea mengi tu. Kubwa hasa tunalotaka kujua na endapo sitaridhishwa na majibu ya Mheshimiwa Waziri nitakamata mshahara wake. Tunataka kujua ni lini sheria hii italetwa humu ndani ili iweze kufanyiwa marekebisho, kwa sababu madhara wanayopata watoto wa kike ni makubwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria hii inaruhusu mtoto aolewe chini ya miaka 18 na hapo hapo katika sheria hii tulipitisha sheria hapa mwaka 2016, inayosema kwamba ukimpa mtoto wa kike mimba chini ya miaka 18 unafungwa miaka 30 jela. Kama unafungwa miaka 30, iweje mtoto huyu aolewe chini ya miaka 14? Kwa maana hiyo, sheria hizi mbili zinakinzana. Napenda tu kutoa mfano, katika Mkao wa Shinyanga kati wa watoto 100, watoto 58 mpaka 59 wanaolewa na sheria hii hamtaki kuileta hapa. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Kwa nini umechukua Mkao wa Shinyanga? (*Kicheko*)

MHE. AMINA S. MOLLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni utafiti na pengine wewe ni mwanasheria mzuri na unatoka huko, sasa ushuhudie kwamba ni kwa jinsi gani pamoja na kwamba unatoka huko watoto 59 kati ya 100 wanaolewa. Siyo Shinyanga tu, ukienda Tabora 58 pia wanaolewa, ninaye hapa mwanasheria pia...

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante, umeeleweka.

MHE. AMINA S. MOLLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, endapo sitaridhika na majibu ya Mheshimiwa Waziri, nitatoa hoja ili basi Wabunge wote waweze kuchangia na tuweze kuomba ni lini sheria hiyo italetwa katika Bunge hili tufanyie marekebisho. Ahsante. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri au AG.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kumshukuru sana Mheshimiwa Amina Mollel, Mbunge. Na mimi kujibu maswali ya akina Amina napata shida kwa sababu mke wangu anaitwa Amina na kwa maana hiyo ni lazima nilijibu kwa heshima sana ili nitunze jina la heshima la mama wa Mtume Muhammad *Swallahahu-Alayhi Wasalam*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa kama nilivyosema jana, kama ni matashi yangu mimi ningekwenda na maoni hayo, lakini kwa utaratibu wa Serikali yako mambo muhimu ambayo lazima yachukuliwe kabla ya hayo tunayoyatamani kufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ambayo napenda kuitoa ni kwamba tayari utaratibu wa ndani wa Wizara wa Kuipitia Sheria ya Ndoa umekamilika na nimeanza kuipitia ili na mimi niweze kutoa maoni yangu kuhusu taarifa hiyo ambayo hatimaye kwa utaratibu unaotakiwa itafikishwa katika vyombo husika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda tu niseme kwamba Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971, ukiondoa huu upungufu wa hapa na pale, ni sheria ya kimapinduzi. Sheria hii ni ya kimapinduzi. Ni sheria ambayo katika Bara la Afrika Kusini mwa Sahara ilikuwa ya kwanza kuitishwa ambayo ilillenga kumkomboa mwanamke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa mifano tu michache. Moja, sheria hii ya 1971 kwa mara ya kwanza iliondoa tafsiri ya *cohabitation* yaani maana ya wanandoa kuishi pamoja kuwa na maana ya kuishi ndani ya nyumba moja na chumba kimoja. Leo hii kwa mujibu wa sheria yetu ya mwaka 1971, *cohabitation* sasa ni pamoja na *whatsapp*, mnapotumiana *whatsapp* na mkeo au mmeo, tayari mna-*cohabit* siyo lazima muwe pamoja. Kabla ya hapo ilikuwa ni lazima muishi pamoja. Matokeo yake ni nini? Wanawake wengi walishindwa kupata madaraka makubwa, kwa sababu ilikuwa ni lazima waishi walipo waume zao, leo siyo hivyo. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, linge zuri tu kabisa liliwekwa humu ndani, ni kuhusu suala zima la *presumption of marriage*. *Presumption of marriage* bahati mbaya imetafsiriwa lsivyo, maana yake siyo ndoa ipo, ila inapotokea mwanamke ameishi na mwanaume na jamii imewachukulia kuwa ni mke na mume na hawana vizuizi vya ndoa na sasa mahusiano hayo yanavunjika, Mahakama ita-*assume there was a marriage* ili mwanamke huyo na watoto hao wasiondoke mikono mitupu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata ikitokea ikionekana kwamba pana kasoro kwamba hawa walikuwa ni maharimu yaani watu wasioruhusiwa kuoana, bado sheria hiyo inasema wale watoto wapewe haki na watunzwe.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, muhimu ni *necessary of life*. Sasa kwa sababu hiyo, yapo mambo mengi ambayo tunayapitia ikiwa ni pamoja na kifungu cha umri wa mtoto ili kwa pamoja Serikali itakapoleta mabadiliko ya Sheria ya Ndoa yasiwe tu ya kipengele kimoja cha umri, bali na mambo mengine yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, muipe Serikali muda, iyapitie mapendekezo yote yaliyoletwa na hatimaye

tuone ni jinsi gani jambo hili tulileté, lakini kwa kulinda yale mazuri yaliyomo ndani ya ile sheria. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeanza na hayo kwa sababu *tendency* ni kui-*dismiss* sheria yote, inayo mazuri na inayo yaliyopungua, lakini tutafanya hiyo. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana. Mheshimiwa Mollel, baada ya *assurance* hiyo ya Serikali bado unataka tena kuongea?

MHE. AMINA S. MOLLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu hayo mazuri ya Mheshimiwa Waziri, bado nakamata mshahara wake na nina sababu za msingi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, watoto wa kike wanalitegemea Bunge hili, watoto wa kike ndio Taifa la kesho ambao tunapozungumza hapa hivi tafiti mbalimbali...

MWENYEKITI: Nenda moja kwa moja unakotaka.

MHE. AMINA S. MOLLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja ili Wabunge waweze kuzungumza, waweze kujadili na Serikali basi iweze kulifanyia kazi tuje kwamba ni lini sheria hiyo inaletwa humu ndani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja Waheshimiwa Wabunge.

MHE. ZAYNAB M. VULLU: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(Hoja ilitolewa lamuliwe)

MWENYEKITI: Haya. Tutachukua wawili tu; wawili upande huu na wawili upande huu.

MBUNGE FULANI: Huku Mwenyekiti, kushoto kwako.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Vulu, Mheshimiwa Jacqueline, Mheshimiwa Salome na Mheshimiwa Dkt. Suleiman. Tunaanza na Mheshimiwa Dkt. Suleiman.

MHE. DKT. SULEIMAN ALLY YUSSUF: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuniona. Mimi siungi mkono hoja ya Mheshimiwa Bi. Amina. Siungi mkono kabisa kwa sababu suala la ndoa linaambatana na masuala ya dini na imani. Kwa imani yetu ya kiislamu hatukuwekewa muda maalum wa mtoto wa kiume kuoa au mtoto wa kike kuolewa. Kutokana na hali hiyo...

MBUNGE FULANI: Lete aya.

MHE. DKT. SULEIMAN ALLY YUSSUF: Aya zipo nyingi, hakuna haja ya kuleta aya.

MBUNGE FULANI: Lete aya.

MHE. DKT. SULEIMAN ALLY YUSSUF: Aya zipo nyingi. Mtume *Swalallahu-Alayhi Wasalam* kwa mfano, katuambia katika mambo ambayo yanatakiwa yafanywe haraka ni mtoto wa kike kuolewa anapofikia ukubwa. (*Makofi*)

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)

MHE. DKT. SULEIMAN ALLY YUSSUF: Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na hali hiyo, naomba uchunge muda wangu...

MBUNGE FULANI: Ongea, ongea.

MWENYEKITI: Ongea Mheshimiwa.

MHE. DKT. SULEIMAN ALLY YUSSUF: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisema siungi mkono hoja hiyo na kama italetwa hapa Bungeni, basi patachimbika, kabisa kabisa.

MBUNGE FULANI: Uamsho.

MWENYEKITI: Ahsante sana. Tumekuelewa!

MBUNGE FULANI: Msiiingilie imani za dini. Msiiingilie imani za dini.

MWENYEKITI: Waheshimiwa polepole! Tulielewa. Mheshimiwa Zaynabu Vulu.

MHE. ZAYNABU M. VULU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Awali ya yote niseme Mheshimiwa Waziri amejitahidi kuelezea vizuri, lakini hoja yangu iko pale pale; ni kwamba tunapozungumzia suala la mtoto wa kike kuolewa, tunaingiza imani za dini, mila na tamaduni. Sidhani kama Serikali inashindwa kusimamia yote hayo, ikatuletea hapa bila kuathiri mila za aina yoyote ile. Naomba niishie hapo. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Salome Makamba.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia suala hili la muhimu la ndoa za utotoni. Naungana na Mheshimiwa Amina Mollel kupinga ndoa za utotoni. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mimba za utotoni siyo suala la kuleta mjadala mrefu hapa. Mahakama mara zote tukikaa hapa, suala la ndoa za utotoni tunasema tusiingilie maamuzi ya Mahakama. Mahakama ilikaa, kesi ikafunguliwa na ikafikia hatima. Kesi iliyofunguliwa mwaka 2016 imetolewa maamuzi na Jaji Kihyo pamoja na Jaji Munisi tarehe 8 Julai, 2016. Wamesema kwamba ndoa za chini ya miaka 18 ni marufuku. Jaji huyo akaenda mbali na kusema kuwa, ukisoma *judgment*, Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na Waziri wetu wa Sheria mtusaidie. (*Makof*)

Mhehsimiwa Mwenyekiti, hukumu inasema ndani ya mwaka mmoja *Attorney General*/pamoja na Waziri wa Sheria walete sheria hii Bungeni tuibadilishe. Haya ni maagizo yaliyotolewa na Mahakama. Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, wakataka ku-dilly dally hili suala la kulipeleka kule wajifanye

wanataka kukataa rufaa, wakashindwa. Tunashikilia hukumu ipi?

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ndoa za utotoni ni kinyume na katiba, miaka 18 ndiyo mtoto anatakiwa kuolewa... (*Kicheko*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Muda wako umekwisha.

Waheshimiwa Wabunge, naongeza muda usiozidi dakika 30 tufanye majukumu yetu vizuri. Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani.

(Hapa baadi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)

MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Naomba niunge mkono hoja ya Mheshimiwa Amina Mollel kwa hoja zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama unavyofahamu kwamba umri wa mtoto wa kike na wa kiume kuweza kujitegemea wakati ambapo atakuwa anajitambua kujua zuri na baya ni umri wa miaka 18. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sioni sababu wa kuwashisha shughuli, kumuozesha mtoto akiwa na miaka 14 kwa sababu akiwa na miaka 18 ndiyo atakuwa anajua barabara shughuli yenyewe namna ya kwenda. Kwa hiyo, niseme tu kumuozesha mtoto miaka 14 yaani hii ni sawasawa na mateso bila chuki. (*Kicheko/Makofi*)

Kwa hiyo, naona ni vizuri mtoto akiwa na umri wa miaka 18 ndiyo aweze kuozeshwa kwa mujibu wa sheria ambayo tunataka kuileta hapa kurekebishiwa tena ilete haraka sana ili tuikebishe na tutaisimamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Simbachawene.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mtu ye yote aliyesoma sheria, jambo hili lazima lilimpasua kichwa. Nataka niwashawishi Waheshimiwa Wabunge, tukubaliane na *position* ya Serikali. Sababu ni moja tu, kuna *conflict of interest* za jambo hili. Ili uweze kufanya uamuzi mzuri wa kuzingatia makundi yote ni lazima ukubali kuna cha kutoa na cha kuchukua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu hiyo, Serikali tumesema jambo hili tunalijadili na tunazingitia mapendelekezo mengi. Hapa kuna mgogoro wa kidini, lakini nataka niwalize, kuna mgogoro pia wa kibaiolojia, kimaumbile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi mtoto wa kike anavunja ungo akiwa na miaka kuanzia 12, 13, 14 mpaka 15. Siku hizi wanavunja ungo mpaka na miaka 10. (*Kicheko/Makofii*)

(*Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Naomba mnisikilize. Sasa kama hamnisikilizi...

MWENYEKITI: Haya, *order, order!*

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tutasema kifungu cha 13 na 17 vya Sheria ya Ndoa; kifungu cha 17 kinasema, mtoto ambaye ni chini ya umri wa miaka 18 ataoleta endapo wazazi wake wataridhia. Sasa hili linazingatia nini? Tuchukue kwamba alilingia darasa la kwanza akiwa na miaka saba, anamaliza darasa la saba akiwa na miaka 14, hahitaji kwenda hiyo sekondari yenu, hahitaji chochote yupo. Halafu sheria iseme, halafu amepata mchumba, halafu mchumba mwenyewe yuko vizuri, anataka kumuoa halafu sheria inamzuia...

MHE. KOSHUMA Z. KITETO: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria inamzuia, inamtaka toka miaka 14 mpaka afike miaka 18 au 19 au 20. Watakwenda kufungua kesi Mahakamani wapinge sheria hii...

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mwanao wa kike anakuona.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba tukubaliane na *position* ya Serikali, acha tukae na tutafakari yote haya kwa umoja tuone itakuwa katika *position* ya namna gani na itakuja Bungeni na Wabunge tutatunga sheria.

MBUNGE FULANI: Taarifa.

MWENYEKITI: Nakuelewa.

Waheshimiwa Wabunge, mnaona jinsi huu mjadala unavyonoga. Utakuja kuwa mtamu zaidi wakati Serikali itakapoleta muswada.

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Mwenyekiti, hukumu ya Mahakama haijadiliwi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mollel, hitimisha tuamue sisi.

MHE. AMINA S. MOLLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, nina imani sana na Serikali. Nina imani sana na Waziri kwa sababu ndiyo ameingia tu katika Wizara hii...

WABUNGE FULANI: Aaaaaah!

MHE. AMINA S. MOLLEL: Tulieni.

MBUNGE FULANI: *Lakumnidukum Walyadin!*

MHE. AMINA S. MOLLEL: Kwa sababu kama alivyosema ndiyo ameingia tu kwenye Wizara hii, Mheshimiwa Waziri umebeba dhamana ya watoto wa kike wa Taifa hili. Watoto wa kike wanakutegemea wewe. Pamoja na kuonesha kila mmoja anaegemea upande wake, lakini lazima tufike mahali tukubaliane wote ili kumnusuru mtoto wa kike. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Kwa kifupi.

MHE. AMINA S. MOLLEL: Kama alivyosema Mheshimiwa Waziri, mke wake ni Amina, mimi ni Amina, nakurudishia mshahara wako. Ahsante. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Balozi Adadi.

MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi nilizungumzia suala kubwa la msongamano wa mahabusu ndani ya magereza zetu. Msongamano ni mkubwa sana na unachangisha na mambo mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo mambo mengi, ni kesi ambazo upelelezi wake umemalizika, lakini mahabusu wengi wanasubiri kitu kinaitwa *High Court Session*, hasa kwa kesi za mauaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, watuhumiwa wa kesi za mauaji wengi wanasubiri *High Court Session* na wako ndani ya mahabusu zaidi ya miaka minne, mitano wakati wanasubiri *session* hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na *session* hiyo, hata kesi hizo zinaposikilizwa na hukumu ya kifo inapotolewa, utekelezaji wa adhabu hiyo haufanyiki. Tangu Awamu ya Tatu na ya Nne, karibu zaidi ya miaka 20 sasa hivi mahabusu ambaao ni *condemned* wanaotakiwa kunyonwa wanagalagala kwenye mahabusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka uthibitisho wa Serikali kwenye mambo mawili; kwanza, ni wataishauri mamlaka inayohusika ili watuhumiwa wao ambao wanasubiri adhabu hiyo aidha itekelezwe au kama inashindwa kutekelezwa basi itolewe adhabu nyingine mbadala. (*Makofî*)

Pili, Serikali iangalie utaratibu sasa hivi wa kujaribu kuboresha *High Court Sessions* ili kesi ambazo upelelezi wake umemalizika mapema ziweze kusikilizwa kuondoa mlundikano wa mahabusu iliyoko magerezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nisipopata majibu mazuri kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, nitachukua shilingi yake. Naomba kuwasilisha. (*Makofî*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Waziri, majibu.

WAZIRI WA SHERIA NA KATIBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimshukuru Mheshimiwa Adadi Rajab, Mbunge wa Muheza kwa ushauri alioutoa kwetu. Ni kweli kabisa kumekuwa na msongamano wa mahabusu na suala zima la *High Court Sessions*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya sababu imekuwa ni upungufu wa rasilimali fedha, lakini pia, inawezekana kabisa tatizo hilo linatokana pia na mfumo wenywewe. Kwa hiyo, napenda nikubali ushauri huo ili Wizara pamoja na mhimili wa Mahakama tuone ni njia gani bora zaidi inayoweza kutumika kuhakikisha kwamba mashauri haya na suala zima la *High Court Session* linafanyiwa kazi vizuri. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukichukua *spirit* ya sasa, iliyoko katika Mahakama Kuu kuhakikisha kwamba hizi *backlog* za kesi zinakwisha. Kwa kutumia hii *justice* na njia nyingine, ninaamini kabisa tukikutana tena bajeti ijayo tutakuwa tumekuja na jibu zuri kutoka mhimili wa Mahakama. Uzuri ndani ya ukumbi huu, ingawa siyo ndani ya Bunge, kule kwenye *gallery*, watu wa mhimili wa Mahakama wapo, ikiwa ni pamoja na Jaji Kiongozi ambao

nadhani kwa pamoja na Mtendaji wa Mahakama tutaona jinsi ya kulifanya jambo hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la watu waliohukumiwa adhabu ya kifo na adhabu hiyo hajatekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tunakusanya maoni ya wananchi, mimi nilikusanya maoni ya wananchi katika Gereza la Ukonga, wengine wakaenda Segerea; tulitembelea kila magareza kwa sababu wafungwa pia ni Watanzania. Kweli pale Ukonga tulikuta watu ambao wamehukumiwa kifo na adhabu hiyo hajatekelezwa. Mionganoni mwa maoni yao yanafanana kabisa na ya Mheshimiwa Adadi Rajab. Wengi waliomba wapewe adhabu mbadala na hasa vijana; na wale watu wazima kwa umri, walisema basi miaka yote imeishia humu si wanimalize tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, pia napenda kukubali ushauri huu. Labda Serikali ione utaratibu ikiwezekana hata kutumia *Law Reform Commission* kwa sababu utafiti uliofanywa na *Law Reform Commission* ulihu adhabu yenye ya kifo kuhusu nini kifanyike kwa wale waliohukumiwa. Kwa hiyo, tunalichukua na tutalipeleka huko ili tuone jinsi ya kuona nini kifanyike. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Sawa kabisa. Mheshimiwa Balozi Adadi Rajab.

MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri amejitahidi sana kujibu maswali yangu na hoja yangu. Naamini kwa sababu ya ugeni wake, ushauri huo atauchukua. Kama tusipoona mabadiliko yoyote, basi tutakutana kwenye bajeti ijayo. Nakushukuru sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante. Tutakutana tu, hata leo hii. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Cosato Chumi!

MHE. COSATO D. CHUMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi. Nimepitia kitabu hiki cha Mheshimiwa Waziri kutoka ukurasa wa kwanza mpaka wa mwisho ukurasa wa 71 na nimepitia pia kitabu cha Maoni ya Kamati, ukurasa wa 17 nadhani ni kipengele cha tatu, maoni ya Kamati yanazungumzia kuhusu suala la kurekebisha sheria kwa ajili ya Katiba Mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Katiba Mpya katika nchi nyingi duniani ni jambo ambalo limechukua miaka mingi na *resource* nyingi. Mfano mzuri ni wenzetu Kenya, walianza takribani miaka ya 1990, wakaja kupata Katiba Mpya mwaka 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika nchi yetu tumekuwa na jambo hili na limechukua gharama kubwa, *resource* kubwa kwa Taifa letu mpaka kuflikia hatua ambayo ilikuwa imebaki, kwangu mimi noana ilikuwa imebaki kazi ndogo ya kuelekea kwenye kupiga kura ya maoni. Wabunge wengi katika michango yao, wanazungumzia sana kuhusu kura ya maoni na namna gani bajeti itatengwa kwa ajili ya kura ya maoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwangu mimi pamoja na kuwa sio mwanasheria, mimi ni *political scientist*, ninafahamu kwamba sheria inayohusiana na masuala ya Katiba Mpya ilishakufa na kwa hiyo, inahitaji kuhuishwa upya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kitabu cha Mheshimiwa Waziri pamoja na maoni yaliyomo kwenye Kamati, sijaona popote ambapo panaonesha kwamba kuna dalili zozote za kuleta sheria hiyo ili kuweza kuhuishwa mchakato huu wa Katiba Mpya. Kwa sababu hiyo, napenda kupata maelezo ya kujitosheleza kwa sababu hata wananchi wana hamu ya kuona jambo hili ambalo tulitumia fedha nyingi kulifanyia kazi, kilichobaki ni kitu kidogo. Kama sitapata maelezo ya kutosha, na mimi nitaitingia kwenye mkumbo wa kutoa shilingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, maelezo tu.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa majumuisho nililieza jambo hili na bado napenda nirudie yale yale niliyoyasema; mchakato huu umefika mahali ulipofika na sheria mbalimbali zilihusika. Kwa wakati muafaka, jambo hili litakapokuwa sasa linashughulikiwa, tutatoa maelezo ya jinsi kuhuisha mchakato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme hivi, Mheshimiwa Cosato Chumi ni *political scientist* na mimi nawaheshimu ma-*political scientist* kwa sababu ilibidi miaka miwili nisome *political science*. Nasema hivi, mchakato wowote wa mabadiliko ya Katiba katika Taifa una mawanda ya aina mbalimbali. Na mimi katika hilli ningewasihi sana sisii sote tuyute subira kwa sababu hata hao Kenya walipokwama hawakujikwamua kwa njia ambayo labda tungependa na sisii tuipitie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba kusema, Wizara na Serikali inaendelea kuzipitia sheria, wakati muafaka utakapofika hayo yote yatajadiliwa. Tukitaka kuyatolea majibu sasa, tutakuwa tunatoa majibu wakati usiokuwa muafaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kusema kwamba jambo hili lisubiri. Kwa nini lisubiri? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lisubiri kidogo kwa sababu, mnapokuwa katika hali ya vumbi, siyo vizuri kuja na jambo kubwa kama hili. Linahitaji sote tutulie, tuwe wamoja; lakini wakati huu mazingira ya kutufanya tuwe na huo utulivu yanaendelea na baadhi ya mambo tunayoyahitaji yanaanza kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, muda ukifika, wala hayatakuwa na mjadala kwa sababu tayari yatakuwa

yameshatekelezwa, yamekubalika yamekuwa sehemu ya utamaduni wetu wa kisheria. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Cosato, wewe siyo tu *a political scientist*, wewe ni mwanadiplomasia, nadhani umeelewa anachokisema Mheshimiwa Waziri.

MHE. COSATO D. CHUMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naona umenivisha pia kofia ya ziada. Sioni kama naweza nikawa na nyongeza zaidi baada ya maelezo ya Mheshimiwa Waziri, lakini napenda kufahamisha Bunge kwamba wananchi wangependa jambo hili lifike wakati liweze kutendeka na kukamilika. Nashukuru. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Nakushukuru sana Mheshimiwa. Mheshimiwa Tundu Lissu.

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuzungumzia hoja ya Kaimu Jaji Mkuu na kwa sababu Mheshimiwa Waziri hawezi akaniridhisha, nitaondoa shilingi hili jambo lijadiliwe na Bunge. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemsikia Mheshimiwa Profesa Kabudi na marembo mengi. Mheshimiwa Profesa Kabudi ni msomi kweli kweli, sijawahi kuwa na shaka kabisa, lakini kwa alichokisema leo kuhusu nafasi ya Kaimu Jaji Mkuu kutokuwa ya ukomo, imenishangaza sana. Inanishangaza, naanza kufikiria alichokiandika yeye na Mlimuka kwamba kuna wataalamu wasomi ambao wanatumika ku-*justify the unjustifiable*. *A progressive rhetoric* ili ku-*justify* mambo ya hovyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katiba yetu, nilisema katika maoni yangu kuna sababu kwa nini huyu anaitwa Kaimu Jaji Mkuu, kuna sababu. Kuna sababu ya Ibara ya 118(1) inayosema Jaji Mkuu. Kuna tofauti katika Jaji Mkuu na Kaimu Jaji Mkuu. Hoja yangu ni kwamba ukishasema kaimu (*acting*), ni *interlocutory*, ni *interim*, ni ya muda. Haiwezi ikawa haina

ukomo. Haiwezi ikawa haina ukomo, ndiyo maana inaitwa kaimu, ndiyo maana inaitwa ya muda na ndiyo maana inaitwa *interim. Pending substantive appointment.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Profesa anataka kutuaminisha kwamba kunaweza kukawa na Kaimu Jaji Mkuu miaka yote, haiwezekani! Haiwezekani, siyo kwa Katiba hii. Profesa Kabudi...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Muda umekwisha.

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Nitatoa shilingi yako.

MWENYEKITI: Wewe, hakuna haja.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema...

MWENYEKITI: Tulia tu.

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Nimesema natoa shilingi tujadiliane.

MWENYEKITI: Unatulia muda tu. Profesa, hebu lielezee kwa kifupi tu. Maana umeeleza sana.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudie yale yale niliyoyasema kwamba nafasi ya Kaimu Jaji Mkuu kama ni ukomo ni pale kwa mujibu wa Ibara ya 118, Rais atakapomteua Jaji Mkuu au Jaji Mkuu atakaporejea nchini au kama alikuwa hawezি kufanya kazi anaumwa, amepona na amerudi kazini. Huo ndio ukomo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lini Rais atamteuwa Jaji mwagine ilii Kaimu Jaji Mkoo aache kuwa Jaji Mkoo, hilo ndilo niliosema halijawekewa muda. Hajaambiwa miezi sita au miezi mitano, hajawekewa, lakini mara akimteua huyo huyo au mwagine huo ndiyo ukomo wa Kaimu Jaji Mkoo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilichokisema, ukija kwenye *functions* zake, ndiyo maana ukienda kwenye Ibara ya 151 inayoeleza nani Jaji Mkoo, *functions* zake ni zile zile za Jaji Mkoo. Ana-enjoy mamlaka yote ya Jaji Mkoo na ana-enjoy security of tenure ambayo tayari ana-enjoy kwa sababu ni Jaji wa Mahakama ya Rufani. Katika maamuzi yake, yeze mwenyewe haingiliwi na yeze hawaingili Majaji wala Mahakimu wengine, hata Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, toka Kaimu Jaji Mkoo huyu ateuliwe ni takribani miezi mitatu. Sasa Mheshimiwa Tundu Lissu, mdogo wangu hakuwepo hapa nilisihi na ninaendelea kusihii, mimi naanza kuzielewa nchi ambazo suala la Mahakama na *vote* ya Mahakama haiji Bungeni. Sasa naelewa. Ziko nchi za *commonwealth*, mhimili wa Mahakama hela zake zinatolewa moja kwa moja kwenye *CF* na sasa naanza kuelewa. Kwa sababu, ni chombo ambacho nisingependa kabisa tukijadili. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua Mahakimu na Majaji wanasi mama nafasi ya Mwenyezi Mungu, ndiyo. Ni Mwenyezi Mungu peke yake mwenye hukumu ya haki na ndiyo maana hukumu hiyo ya Mwenyezi Mungu haina rufaa za sisi wote binadamu. Tunajitahidi, ndiyo maana tuna madaraja ya rufaa. Sasa watu ambaao Nabii Daudi kwenye Zaburi ya 15 anawaita ni marafiki wa Mungu kwa sababu wanafanya kazi ambayo yeze peke yake ndiyo mtoa haki, tuwaheshimu kidogo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, napenda kusema kwamba mdogo wangu nirudishie shilingi, ili jambo hili tulijadili vizuri na tuiachie mamlaka husika kutekeleza majukumu yake. Kwenye hotuba yako umenisihii nitoe ushauri,

sasa kwa njia hii itakuwa vigumu kutoa ushauri. Kwa hiyo, nisaidie kutoa ushauri kwa kurudisha shilingi. (*Makofi*)

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Mheshimiwa Mwenyekiti, shilingi yangu hairudi, hili jambo tulijadili. (*Kicheko*)

Narudia tena, hizi hoja ni nyepesi sana. Kweli Mheshimiwa Profesa Kabudi anapenda sana kusema, *The Chief Justice is primus inter pares*, maneno umenifundisha sana Mwalimu wangu na Majaji wengine. *Primus inter pares*, ana mamlaka yale yale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Spika wa Bunge na Mwenyekiti wa Bunge, wewe Mwenyekiti unapokuwa hapo, kazi zako ziko sawa na za Spika. Wewe ni Spika? (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mwalimu wangu, Mheshimiwa Profesa Kabudi anasema kwa vile kazi za *Chief Justice* zinafanana na kazi za *Acting Chief Justice, then the Acting Chief Justice is the Chief Justice*, tafadhali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kitu amekisema Mheshimiwa Profesa Kabudi kizuri sana. Nchi zinaishi kwa mila na desturi za kikatiba na kisiasa. Mila za desturi za kikatiba na kisiasa za nchi hii, kwenye suala la Jaji Mkuu tangu enzi za Philip Georges ni kwamba nafasi ya *Chief Justice* ikiwa wazi, anateuliwa *immediately a substantive Chief Justice. It happened 1964* umesema, *it happened 1973 with Philip Georges, it happened with Judge Agostino Said, it happened with Nyalali, it happened with Samata, it happened with Augustine Ramadhani*, imetokea kwa Jaji Mohamed Othmani Chande utafikiri hamkujua kwamba Chande Othman atastaafu mkajipanga. Utafikiri hamkujua. *It was well known.* (*Makofi*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini *you are breaking with our constitutional and judicial tradition?* Tumekuwa na Majaji Wakuu *substantive* miaka yote, *why now?* Kwa hiyo, hili jambo lijadiliwe, nimeondoa shilingi na hairudi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa hoja lijadiliwe.
(*Makofi*)

MWENYEKITI: Haya, tunachukua majina. Mnaelewa maana yake? Mnanielewa eeh! Nachukua wawili huku na wawili huku. Naanza na Mheshimiwa Angellah Kairuki na Mheshimiwa Kakunda Joseph, Mheshimiwa Mnyika na Mheshimiwa Ally Saleh. Tunaanza na Mheshimiwa Ally Saleh.

MHE. ALLY SALEH ALLY: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza napenda kusema kwamba naunga mkono hoja iliyoletwa mezani na Mheshimiwa Tundu Lissu. Hoja zangu ni zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tunatengeneza utamaduni mpya kabisa, utamaduni amba tunaonyesha, kama alivyosema Mheshimiwa Tundu Lissu tangu asubuhi kwamba hatuko tayari kwa kitu ambacho tulikuwa tuko tayari na tukajua kwamba kitatokezea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha pili, nataka Mheshimiwa Waziri atuelezee ni wapi katika utamaduni wa *commonwealth* tunakaa muda wa miezi kama hii hatujampata Jaji mwininge? Ingekuwa angalau tuna *system* ya kumleta mwombaji katika *panel* kuhojiwa kupitia katika mfumo kama vile Marekani au kama vile Kenya angalau tungesema imechukua muda; lakini bado tulikuwa tunajua muda wake ni muda fulani, haikutekelezwa.

Suala la tatu, inaondoa *confidence* ya utawala wa kisheria katika nchi, inaondoa *confidence* kwa wawekezaji na marafiki zetu, kwamba nchi hii haipo *stable*, tunashindwa kuamua katika jambo muhimu la nguzo ya kitaifa. Kwa hiyo, nahisi kwamba katika hili hatupendi kusema, lakini tunapenda kusema kwamba Mheshimiwa Rais hakutekeleza wajibu wake wa Kikatiba.

Kwa hiyo, naunga mkono hoja hii kwamba tuendelee kujadili na tuamue katika njia nyingine, lakini siyo kupitisha bajeti ya Waziri. Ahsante. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kariuki.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA: Mheshimiwa Mwenyeekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Niendelee kusimamia katika maelezo ya Waziri, Mheshimiwa Profesa Kabudi. Ameeleza kwa kina kabisa msingi mzima wa Ibara 118(1). Ukiangalia ibara 118(4)(a) lakini zaidi katika ibara yenye 118(5).

Mheshimiwa Mwenyeekiti, mimi sijaona lolote liliolaribika, kwa kuwa anakaimu Jaji Mkuu mpaka sasa. Tumekuwa tushuhudia ufanisi wa Mahakama. Kesi kwa kiasi kikubwa zaidi ya asilimia 85 unaona kuna *completion rate* na *disposal rate* zaidi ya asilimia 90 na wamekuwa wakifanya kazi kubwa kwa kweli tunawapongeza sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyeekiti, Ukiangalia Ibara ya 118(4)(a), nafasi ya Jaji Mkuu itakapokuwa wazi na imeeleza ni mazingira gani inaweza ikatokea ikawa wazi na mini kinafanyika na ambacho amekifanya Mheshimiwa Rais, amemteua Kaimu Jaji Mkuu anatekeleza madaraka yake mpaka hapo Mheshimiwa Rais atakapofanya uteuzi.

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Malizia.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA: Mheshimiwa Mwenyeekiti, naunga mkono maoni na maelezo ya Mheshimiwa Profesa Kabudi. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kakunda.

MHE. JOSEPH G. KAKUNDA: Mheshimiwa Mwenyeekiti, imeletwa hoja hapa ya nchi za *commonwealth*, na mimi naomba niongezee kwenye maelezo ya Mheshimiwa Waziri kwa kuongeza maelezo kumwambia mchangiaji mmoja

aliyetaka mfano kwenye nchi za *commonwealth*, Katiba ya India mwaka 1949 lbara ya 126 kuhusu *appointment of Acting Chief Justice* inasema: “*When the office of the Chief Justice of India is vacant or when the Chief Justice is by any reason or otherwise unable to perform the duties of his office, the President may appoint...*”

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasoma kipengele cha Katiba na nanukuu; “*The duties of the office shall be performed by such one of the other Judges of the Court as the President may appoint for the purpose.*” Kwa hiyo, India wana kipengele cha kuteua Kaimu Jaji Mkuu. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Sawa, Mheshimiwa Mnyika.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naunga mkono hoja illyotolewa na Mheshimiwa Tundu Lissu. Mheshimiwa Waziri Kairuki alipokuwa anazungumza hapa, amesema hahaona tatizo lolote katika kipindi hiki ambacho Jaji Mkuu amekaimu nafasi yake kwa kipindi chote hicho. Sasa kama Mheshimiwa Kairuki anaona hakujawa na tatizo lolote, kwa nini sasa asikubaliane na hoja ya Kambi ya Upinzani kwamba Rais amthibitishe huyu Kaimu Jaji Mkuu ili sasa awe Jaji Mkuu kamili ili kusiwe na utata tena? (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba sana Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ninyi ndio Washauri Wakuu wa Mheshimiwa Rais katika masuala ya sheria. Ninyi washauri wakuu wa Mheshimiwa Rais katika masuala ya sheria mkichukulia msimamo kwamba mamlaka ya Rais hayana kikomo katika kuachia nafasi ya ukaimu, ni wazi kwamba ninyi mnaongoza katika kumpotosha Mheshimiwa Rais na ili msiingie katika vitabu vya kumpotosha Mheshimiwa Rais ni vema mka... (*Makofi/Kicheko*)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Muda. Ahsante sana.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa MwenyeKITI, Bunge hili linafanya kazi na linapaswa lifanye kazi kwa kuzingatia Katiba. Kwanza, imeletwa hoja hapa ya Bunge kutaka kumshauri Mheshimiwa Rais amthibitishhe Kaimu Jaji Mkuu kitu ambacho hakipo. Kwa sababu tunayo Ibara ya 37 inasema hivi, mbali na...

MBUNGE FULANI: (*Hapa alizungumza bila kutumia kipaza sauti*).

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Sasa kwa nini mnaleta hoja hapa? Mbali na kuzingatia masharti yaliyomo katika Katiba hii na Sheria za Jamhuri ya Muungano katika utekelezaji wa kazi nashughuli zake, Rais atakuwa huru na hatalazimka kufuata ushauri atakaopewa na mtu ye yeyote isipokuwa tu pale atakapotakiwa na katiba hii au na sheria nyingine yoyote kufanya jambo lolote kulingana na ushauri anaopewa na mtu au mamlaka yoyote.

Moja, Katiba haijatoa mamlaka kwa Bunge hili kumshauri Rais kuhusu uteuzi wa Jaji Mkuu; hilo la kwanza; la pili, katiba haijaweka kiasi cha ukomo wa mtu anayeteuliwa kuwa Jaji Mkuu kukaimu. Kwa hiyo, muda wa kukaimu huyo Jaji Mkuu huwezi kusema kwamba umeisha kwamba Rais amefungwa. Tumwachie Rais atekeleze wajibu wake.

Mheshimiwa MwenyeKITI, katika hali ya kawaida, sisi tulipaswa tushangilie kwamba mwenzetu anateuliwa kuwa Kaimu ambaye ni njia ya kwenda pengine kuthibitishwa kule halafu wewe unakasirika. *How many people have been appointed on the acting positions, then let one be confirmed accordingly. (Makof/Kicheko)*

MBUNGE FULANI: Ruka baba, ruka!

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa MwenyeKITI, nilisema hapa nilipochangia mara ya mwisho, hatuwezi kuwa na tabia ya kuwasakama...

MBUNGE FULANI: *Chief Whip.*

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mmakuwa na tabia ya kuwasakama viongozi wakuu wa mahakama. Jaji Mstaafu Chande mlikuwa mniamshambulia...

MHE. PAULINE P. GEKUL: Apunguze sauti, hatumsikii kabisa.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Halafu pia na huyu mniamshambulia, *why? We can ask ourself.*

Mheshimiwa Mwenyeekiti, kwa hiyo, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri na namwomba Mheshimiwa Tundu Lissu baada ya kusoma masharti haya ya Katiba akubali kumrudishia Mheshimiwa Waziri shilingi yake. (*Makof*)

MWENYEKITU: Mheshimiwa Tundu Lissu, kwa kifupi tuhitimishe tu.

MHE. TUNDU A. LISSU: Mheshimiwa Mwenyeekiti, hapana ni dakika zangu tatu.

MWENYEKITU: Siyo lazima utumie zote.

MHE. TUNDU A. LISSU: Muda wangu wa Kibunge tafadhalil!

Mheshimiwa Mwenyeekiti, ya Masaju nitayaacha, kwa sababu sasa tuna Mwanasheria Mkuu au tuna *party apparatchik?* (*Kicheko/Makof*)

Mheshimiwa Mwenyeekiti, kuna hoja inajengwa kwamba kuhoji mambo haya ni kuidharau Mahakama. Hapana, unaidharau Mahakama kwa kutofanya Mahakama iwe na kiongozi wake kamili, hiyo ndiyo dharau ya Mahakama. Siyo hawa wanaohoji kwa nini *Judiciary* haina *Substantive Head?* Ni ninyi ambao mnasababisha haina, ndio mnaodharau. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kuna hoja kwamba halijaharibika neno. Limeharibika neno vibaya sana. *Judiciary* ni mhimili wa dola, unaongozwa na Jaji Mkuu. Katiba inasema ndiye Mkuu wa Mahakama ya Tanzania. Ukimfanya akaimu, hana uhakika kama kesho atakuwa *confirmed*, hana hakika kama kesho ataondolewa, maana yake ni namna ya kuvuruga *independence* ya *Judiciary*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na uzuri kabisa, nimesema uzuri wa walimu wangu hawa walipokuwa bado vijana na wakweli, sasa hivi wamekuwa wanatumikia tu, walizungumza vitu vya maana sana. Walizungumza vya maana sana. Samahani mwalimu wangu, samahani kaka yangu. (*Kicheko/Makofii*)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa. Muda ndiyo huo. (*Makofii*)

MBUNGE FULANI: Tumechoka pumba.

MHE. TUNDU A. LISSU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachosema ni kwamba...

MWENYEKITI: Muda wako umekwisha. Muda umekwisha Mheshimiwa.

MBUNGE FULANI: Muda wake umeisha.

MHE. TUNDU A. LISSU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba...

MBUNGE FULANI: Tumechoka pumba.

MBUNGE FULANI: Kaa chini.

MHE. TUNDU A. LISSU: Tunataka *Judiciay* iheshimiwe, Mheshimiwa Waziri amshauri Rais atuee Jaji Mkuu.

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea.

Waheshimiwa Wabunge, nawahoji wale mnaoafiki hoja ya Mheshimiwa Tundu Lissu ya kupunguza mshahara wa Waziri kwa shilingi moja waseme ndiyo na wasioafiki waseme siyo.

*(Hoja ilitolewa lamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kukataliwa)*

(Hoja ya kuondoa shilingi katika mshahara wa Waziri wa Katiba na Sheria, iliyotolewa na Mhe. Tundu A. M. Lissu ilikataliwa na Kamati ya Matumizi)

MWENYEKITI: Wasioafiki wameshinda.

Mheshimiwa Abdallah Mtolea muda haupo. Sema tu ulichonacho, tutaenda mbele. (*Kicheko/Makofi*)

MHE. ABDALLAH A. MTOLEA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Pamoja na muda haupo lakini kuna muda ule wa kanuni zetu za Kibunge, kwa hiyo, naamini huo utaheshimika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nataka kuzungumzia jambo dogo tu na lenyewe ni hili, kuzuia mikutano ya Vyama vya Siasa. Mheshimiwa Waziri kabla hujajiunga na Serikali hii yalitoka matamko ya kuzuia mikutano ya kisiasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wanasiasa unaotuona humu ndani, hatufanyi mikutano ya kisiasa. Na wewe umesema hapa kwamba unasoma sana Ibara ya nane. Kama unasoma Ibara ya nane ambayo inaitaja Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa ni nchi ya Kidemokrasia, pia utakuwa unaisoma Ibara ya 18 ambayo inatoa uhuru wa mawazo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhuru wa mawazo na kuijenga demokrasia inatutaka tuzungumze na wananchi,

inatutaka twende kwa jamii tukafanye mikutano tuwaeleze Serikali inafanya nini na Serikali haifanyi kitu gani? Ndiyo maana katika Awamu ya Nne wakati Chama cha Mapinduzi kinaelelekeea shiloni, Mheshimiwa Kinana na Mheshimiwa Nape Nnauye walizunguruka nchi nzima...*(Makof)*

MBUNGE FULANI: Kuzunguruka?

MHE. ABDALLAH A. MTOLEA: Kuelezea namna gani Serikali inatekeleza majukumu yake na ikaweza kuinusuru CCM na hatimaye ikashinda kwenye uchaguzi wa mwaka 2015.

MHE. AMINA N. MAKILAGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa!

MWENYEKITI: Muda Mheshimiwa.

MHE. AMINA N. MAKILAGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe taarifa.

MWENYEKITI: Hapana.

MHE. ABDALLAH A. MTOLEA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama sikupata maelezo ya kina kutoka kwa Waziri, kweli nitaondoa shilingi katika eneo hili.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba niweke kumbukumbu sawa. Mikutano ya vyama vya siasa haijafutwa wala haijazuwa, bali imewekewa utaratibu. Duniani kote, hiyo ndiyo *standard*; mikutano ya hadhara inawekewa utaratibu. *(Makof)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, duniani kote mikutano ya hadhara huwa inapangwa na Tume ya Uchaguzi panapokuwepo na majukumu ya masuala ya kisiasa. Hivi majuzi tulikuwa na chaguzi za marudio za Kata pamoja na

Jimbo. Vyama vyote vya siasa viliruhusiwa, vilienda kufanya kampeni popote pale walipokuwa wanataka. (*Kicheko/Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mazingira ya sasa hivi, hapa tulipo wachaguliwa wote ambao ni ninyi Waheshimiwa Wabunge mnarusiwa kufanya mikutano ya hadhara na ninyi ni wanasiasa. Hakuna Mbunge hata mmoja ambaye sio mwaniasiasa na hakuna Mbunge hata mmoja ambaye anapokuwa kwenye Jimbo lake hatokani na chama chochote siasa. Kwa maana hiyo, mikutano ya hadhara inaendelea kama kawaida, lakini kwa kuwekewa utaratibu kutumia watu ambao wana anuani ya kuweza kuitisha mikutano ya aina hii. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili limewasaidia sana ninyi wenyewe Waheshimiwa Wabunge. Na mimi namshukuru sana Mheshimiwa Rais. Nadhani kwa uzoefu wake wa kuwa Mbunge kwa zaidi ya miaka 20 ametambua kwamba ni vizuri katika nchi kuweka utaratibu wa kufanya mikutano ya hadhara ambao utakuwa unatumia watu ambao wanawajibika katika eneo ambalo wanafanya mikutano ya hadhara. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niliseme kwa uwazi kabisa na wenzetu hawa watumie mifano hata ya nchi hizo ambazo wanazitumia kwenye demokrasia, huo ndiyo utaratibu wanaoutumia.

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge kwa mamlaka niliyonayo kwa mujibu wa Kanuni 104(2) sasa tunaingia kwenye *guillotine*.

Fungu 41- Wizara ya Katiba na Sheria

Kif. 1001 - Admin.and HR Management ...	Shs. 5,033,833,000/=
Kif. 1002 - Finance and Accounts	Shs. 228,991,000/=
Kif. 1003 - Police and Information Services..	Shs. 437,718,000/=
Kif. 1004 - Internal Audit Unit.....	Shs. 122,562,000/=
Kif. 1005 - Government Comm. Unit.....	Shs. 107,736,000/=

Kif. 1006 - *Procurement Mg'nt Unit*..... Shs. 131,204,000/=
Kif. 1007 - *Management Inform. Unit*..... Shs. 141,758,000/=

*(Vifungu vilivyojatwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya
Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Fungu 12 - Tume ya Utumishi wa Mahakama

Kif. 1001 - *Admin. and HR Management*.... Shs. 916,897,595/=
Kif. 1002 - *Finance and Accounts* Shs. 24,295,000/=
Kif. 1003 - *Procurement Mg'nt Unit*.....Shs. 14,260,000/=
Kif. 1004 - *Internal Audit Unit*..... Shs. 12,440,000/=
Kif. 1005 - *Recruitment, Appointment &
Confirmation*..... Shs.102,030,000/=
Kif. 1006 - *Ethics and Discipline Section*.....Shs. 32,988,400/=

*(Vifungu vilivyojatwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya
Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Fungu 16 - Mwanasheria Mkuu wa Serikali

Kif. 1001 - *Admin. and HR Mg'nt*.....Shs. 1,915,081,000/=
Kif. 1002 - *Finance and Accounts Unit*Shs. 408,964,000/=
Kif. 1003 - *Planning Division*.....Shs. 513,080,000/=
Kif. 1004 - *Internal Audit Unit*.....Shs. 268,194,000/=
Kif. 1005 - *Government Commu. Unit*.....Shs. 98,150,000/=
Kif. 1006 - *Legal Registry Unit*..... Shs. 132,512,000/=
Kif. 1007 - *Procurement Mg'nt Unit*..... Shs. 216,304,000/=
Kif. 1008 - *Research and LibraryService Unit*. Shs.100,824,000/=
Kif. 1009 - *Information and Comm. Unit*.... Shs. 197,020,000/=
Kif. 2003 - *Legislative Drafting*.....Shs. 976,016,000/=
Kif. 3001 - *Civil Litigation & Arbitration
Division*.....Shs.1,100,573,000/=
Kif. 3002 - *Treaties and Contracts Div*..... Shs. 799,761,000/=
Kif. 4001 - *Constitutional Affairs and
Human Rights*.....Shs. 556,044,000/=

*(Vifungu vilivyojatwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya
Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Fungu 35 - MKurugenzi wa Mashitaka

Kif. 2002 - *Public Prosecutions Division*.....Shs. 4,106,416,000/=
Kif. 2004 - *Zonal Office Arusha*Shs. 855,004,000/=
Kif. 2005 - *Zonal Office Dodoma*Shs. 492,634,000/=
Kif. 2006 - *Zonal Office Dar es Salaam*.....Shs. 1,995,042,000/=
Kif. 2007 - *Zonal Office Iringa*.....Shs. 367,612,000/=
Kif. 2008 - *Zonal Office Moshi*Shs. 422,073,000/=
Kif. 2009 - *Zonal Office Kagera*.....Shs. 321,481,000/=
Kif. 2010 - *Zonal Office Mbeya*Shs. 499,729,000/=
Kif. 2011 - *Zonal Office Mtwara*Shs. 346,856,000/=
Kif. 2012 - *Zonal Office Mwanza*Shs. 891,419,000/=
Kif. 2013 - *Zonal Office Ruvuma*Shs. 300,269,000/=
Kif. 2014 - *Zonal Office Sumbawanga*Shs. 305,778,000/=
Kif. 2015 - *Zonal Office Tabora*Shs. 501,312,000/=
Kif. 2016 - *Zonal Office Tanga*Shs. 523,039,000/=
Kif. 2017 - *Zonal Office Shinyanga*Shs. 372,857,000/=
Kif. 2018 - *Zonal Office Singida*Shs. 274,746,000/=
Kif. 2019 - *Zonal Office Lindi*.....Shs. 214,558,000/=
Kif. 2020 - *Zonal Office Mara*Shs. 183,188,000/=
Kif. 2021 - *Zonal Office Manyara*Shs. 172,757,000/=
Kif. 2022 - *Zonal Office Kigoma*Shs. 224,695,000/=
Kif. 2023 - *Zonal Office Pwani*Shs. 358,741,000/=
Kif. 2024 - *Zonal Office Njombe*Shs. 283,623,000/=
Kif. 2025 - *Zonal Office Morogoro*.....Shs. 310,644,000/=
Kif. 2026 - *Zonal Office Geita*Shs. 216,451,000/=
Kif. 2027 - *Zonal Office Simiyu*Shs. 180,821,000/=
Kif. 2028 - *Zonal Office Katavi*Shs. 192,318,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Fungu 40 - Mfuko wa Mahakama

Kif. 2002 - *Court of Appeal D'Salaam*...Shs.106,959,018,000/=

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi pamoja na Marekebisho yake)

Fungu 55 – Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora

Kif. 1001 - Admin. and HR Mg'nt.....Shs. 1,539,930,400/=
Kif. 1002 - Finance and AccountsShs. 215,028,000/=
Kif. 1003 - Internal Audit UnitShs. 66,220,000/=
Kif. 1004 - Legal ServicesShs. 252,815,000/=
Kif. 1005 - Procurement Unit.....Shs. 46,840,000/=
Kif. 1006 - Mg'nt Information Syst. Unit.....Shs. 47,070,000/=
Kif. 2001 - Administrative Justice.....Shs. 650,063,000/=
Kif. 2002 - Human Rights.....Shs. 502,021,600/=
Kif. 2003 - Research and Documentation...Shs. 166,586,000/=
Kif. 2004 - Public Education and Training.....Shs. 150,488,000/=
Kif. 3001 - Zanzibar Office.....Shs. 180,912,000/=
Kif. 3002 - Mwanza OfficeShs. 45,638,000/=
Kif. 3003 - Lindi OfficeShs. 30,570,000/=

*(Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya
Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Fungu 59 – Tume ya Kurekebisha Sheria

Kif. 1001 - Admin. and HR Mg'nt.....Shs. 2,034,335,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya
Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

MIPANGO YA MAENDELEO

Fungu 16 – Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali

Kif. 1003 - Planning Division.....Shs. 0
Kif. 3002 - Treaties and Contract Division.....Shs. 0

*(Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya
Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Fungu 35 - Public Prosecutions Division

Kif. 2002 - *Public Prosecutions Division* Shs. 0

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Fungu 41 – Wizara ya Katiba na Sheria

Kif. 1003 - *Policy and Inform. Services*.....Shs. 2,806,020,000/=

(Kifungu Kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Fungu 55 – Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora

Kif. 2002 - *Human Rights*.....Shs. 2,272,796,000/=

Kif. 2003 - *Research and Documentation*..... Sh. 0

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

NDG. JOSHUA CHAMWELA - KATIBU MEZANI:
Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Matumizi imemaliza kazi yake.

MWENYEKITI: Bunge linarejea.

Waheshimiwa Wabunge, naomba utulivu. Tukae.

Mheshimiwa mtoa hoja, taarifa. (*Makofii*)

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge lako lilikaa kama Kamati ya Matumizi, limekamilisha kazi zake. Naomba taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.
(*Makofii*)

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA,
WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

MWENYEKITI: Hoja imetolewa na imeungwa mkono.
Sasa naitoa kwenu muiamue.

(Hoja *ilitolewa lamuliwe*)
(Hoja *iliamuliwa na Kuafikiwa*)

(*Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka 2017/2018 yalipitishwa na Bunge*)

MWENYEKITI: Walioafiki wameshinda. Kwa hiyo, napenda kutamka rasmi kwamba maombi ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mafungu yote ambayo yako chini ya Wizara hiyo yamepitishwa rasmi na Bunge. (*Makofii*)

Nachukua nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Profesa Kabudi, Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Serikali nzima, uongozi wa Mahakama, Jaji Kiongozi na timu yake, Katibu Mkuu na wataalam wote ambao wengine hamuwaoni ambao wako nyuma hapa, wako wengi, kwa kazi nzuri ambayo mmeifanya.

Bunge limeidhinisha maombi ya fedha kwa mwaka ujao wa fedha, matarajio yetu ni kwamba yaliyosemwa, yaliyoshauriwa, fedha hizi kwa mafungu yote zitapatikana kwa mtiririko mzuri ili muweze kutekeleza majukumu yenu. Hongereni sana. Kwangu mimi kwa Wizara hii huwa najisikia kama ni chura mnatrejesha kwenye maji, nimefurahi sana. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, kabla sijaendelea, kuna ombi moja ambalo nadhani mtanivumilia. Nilikuwa naongea na Katibu hapa Mezani, siku za usoni nadhani tuwe tuna-*anticipate*, mimi huwa sipendi kuvunja Kanuni na sidhani hata kiongozi yejote anayekaa hapa anapenda kuvunja Kanuni. Suala la muda, tutakuwa tunawahi tunapoona hali

ilivyo maana dakika 30 tunaona hatuzitendei haki shughuli ya Bunge. Kwa leo, Mheshimiwa Mdee, dakika tatu tu.

MAELEZO BINAFSI YA MBUNGE

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, mosi, nakushukuru kwa kunipa fursa hii, lakini vilevile nilitamani wakati ninasema maneno haya Mheshimiwa Spika angekuwepo, lakini ninaamini kwamba uwepo wako wewe unawakilisha Kiti cha Spika na atapata kusikia maneno ambayo nilitaka kuyasema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 4 Aprili, 2017 wakati wa uchaguzi wa *EALA* kuna matukio ambayo yalitokea yakanipelekea kuzungumza lugha ambayo kitamaduni za Bunge siyo sawa. Lugha husika ilimgusa pia Mheshimiwa Spika na Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla kwa namna moja au nyininge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Mbunge mzoefu, nilitumia jitihada kuzungumza na kuomba radhi wahusika katika *individual capacity*, lakini vilevile nikaona ni busara kwa sababu haya maneno niliyasema Bungeni, kuzungumza pia hapa na kumwomba radhi Mheshimiwa Spika. Kwa hiyo, niliomba huu muda *specifically* kumwomba radhi, kumwambia kwamba namheshimu na kwamba sitarudia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika ni kiongozi wangu, lakini Spika ni mwananchi wa Jimbo la Kawe. Kwa hiyo, nina kila sababu ya kuyazingatia haya mawili kwa umakini mkubwa. Kwa hiyo, naomba radhi kwake, naomba radhi kwa Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla, ninaomba radhi kwa Bunge na ninaomba radhi kwa wananchi wa Jimbo la Kawe ambao miongoni mwenu ninyi asilimia kubwa ni wananchi wa Jimbo la Kawe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niahidi tu na wananchi wa Tanzania najua kuna ambao nitakuwa nimewakwaza, kwa hiyo, ninaomba radhi. Naahidi tu

michango yangu ya Kibunge itaendelea kama ilivyo lakini kwa kutumia lugha za staha. (*Makofi*)

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Leo Halima kaokoka leo!
(*Kicheko/Makofi*)

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. (*Makofi*)

MBUNGE FULANI: Ameacha pombe. (*Makofi*)

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Halima ni wewe kweli Halima? (*Makofi*)

MBUNGE FULANI: Ameacha pombe? (*Makofi*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, nami namshukuru sana Mheshimiwa Halima Mdee kwa ukomavu wake aliouonesha. Huo ndiyo uongozi, hongera sana. (*Makofi*)

Tutazifikisha salamu zako na ombi lako tutalifikisha kwa Mheshimiwa Spika pamoja na kwamba imo kwenye *Hansard*.

Nifanye sahihisho la *Hansard* kwa jina la Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, nilitaja jina Mheshimiwa Angellah Kariuki, jina sahihi ni Mheshimiwa Angellah Kairuki, ikae vizuri. Ukisema hivyo, unaleta matatizo mengine.

Tangazo linatoka kwa *Chief Whip* wa Serikali Mheshimiwa Jenista Mhagama, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, kwa shughuli kubwa ya kesho ya Muungano.

Tangazo, tunaadhimisha miaka 53 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, kesho Jumatano tarehe 26 Aprili, 2017. Maadhimisho hayo kitaifa yatafanya katika Uwanja wa Jamhuri Dodoma. Mgeni Rasmi katika maadhimisho hayo, atakuwa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu

wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama. Wabunge wote wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mnaalikwa rasmi kuhuduria katika sherehe hizo. (*Makof*)

Kutakuwa na usafiri wa pamoja kwa Waheshimiwa Wabunge kuelekea Uwanja wa Jamhuri utakaoanzia katika Uwanja wa Mashujaa saa moja asubuhi, tuwahi. Usafiri huo utawarudisheni uwanja wa Mashujaa mara baada ya sherehe kumalizika. Hii ni kutokana na kutokuwepo nafasi ya kuegesha magari Uwanja wa Jamhuri. Kauli Mbiu ya Sherehe za kutimiza miaka 53 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ni Miaka 53 ya Muungano, Tuulinde na Kuuimarisha, Tupige Vita Dawa za Kulevyaa na Kufanya Kazi kwa Bidii. (*Makof*)

MBUNGE FULANI: Hakuna usalama wa magari kule.

MWENYEKITI: Hilo ndillo tangazo. Kesho Waheshimiwa Wabunge tuwahi saa moja eneo la Viwanja vyta Mashujaa.

MBUNGE FULANI: (*Hapa alizungumza bila kutumia kipaza sauti*).

MWENYEKITI: Hayo mtauliza baadaye.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, niwashukuru sana kwa kazi nzuri mliyoifanya, ndio shughuli za Bunge. Tuendelee hivyo kushikamana.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, naliahirisha Bunge hadi kesho kutwa siku ya Alhamisi tarehe 27 Aprili, 2017 saa 3.00 asubuhi.

(Saa 2.32 Usiku Bunge lilahirishwa mpaka Siku ya Alhamisi, Tarehe 27 Aprili, 2017 Saa Tatu Asubuhi)